# ITIKADI ZA KIUANA KATIKA METHALI ZA KINYANKOLE NA KISWAHILI

**YUNUSU LUBUUKA**

**C82EA/30606/2015**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU (PhD) YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**MACHI , 2023**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

SAHIHI:........................................TAREHE: 16/02/2023........

**LUBUUKA YUNUSU**

**C82EA/30606/2015**

## IDHINI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii.

SAHIHI:........................................TAREHE: 16/02/2023

**PROF. CATHERINE NDUNGO**

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

Chuo kikuu cha Kenyatta

SAHIHI:........................................TAREHE: 16/02/2023

**DKT. JESSE JOSEPH MURITHI**

Idara ya Kiswahili na Lugha Za Kiafrika

Chuo kikuu cha Kenyatta

## SHUKRANI

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa yote kwa kunipa uhai na afya njema kuweza kushughulikia na kukamilisha kazi hii. Mbawazi zake zimekuwa chachu ya kufanikisha kazi yangu. Napenda pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu; Profesa Catherine Ndungo na Dkt. Jessee Joseph Murithi ambao wamesimamia kazi hii hatua kwa hatua mpaka kukamilika kwake. Kiwango cha kazi hii kimefikiwa kutokana na mwongozo wao wa kitaaluma. Ninamuomba Maulana abariki kazi za mikono yao ikiwemo tasnifu hii. Nina wajibu wa kutoa shukurani maalum kwa familia yangu hususan mke wangu mpenzi Bi Nasasira Jackline Mariam pamoja na watoto wangu Baraka M. Lubuuka, Hashim M. Lubuuka, Fahim M. Lubuuka na Aifat M. Lubuuka kwa kunivumilia wakati wote nikiwa katika chuo kikuu cha Kenyatta, Nairobi pamoja na nyanjani. Walikosa ukaribu wangu nikiwa ninashughulika na kazi hii. Ninawashukuru kwa kunivumilia, kuniweka kwa maombi yao na kunihimiza. Namuomba Mwenyezi Mungu awafidie na awazidishie sifa za kuwa na moyo wa kuvumilia daima. Aidha, nashukuru utawala wa Chuo kikuu cha Kyambogo kunifadhili kwa programu hii ya uzamifu. Bila ufadhili huu, nisingeweza kufikia kiwango hiki. Natambua mchango muhimu niliopewa na wazazi wangu Bi. Nakimbugwe Jalia na Bw. Lubuuka Wahabu, pamoja na kuwajibika kama wazazi kwa kunisomesha na kusimamia mambo mbalimbali nyumbani bila kuchoka wakati nikiwa masomoni. Hakika ninajivunia kuwepo kwenu duniani. Ninamwomba Maulana awajalie afya njema na maisha marefu duniani ili muweze kuvuna zaidi mlichopanda bila kusahau ndugu zangu wakiwamo Asia na Mama Sulaina. Kadhalika, ninashukuru Ustadh Adul Khadir al maarufu MAU kutoka Lamu, Profesa Rocha Chimerah wa Chuo kikuu cha Pwani Kilifi, Profesa Austin Bukenya, Dkt Masood kutoka chuo kikuu cha SUZA. Natambua na kuthamini sana mchango wa kila mtu hasa wale ambao walikuwa wakinipa moyo wa kusoma na kukabiriana na changamoto za kozi, watafitiwa wote, wasailiwa maalum na wale wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine lakini haiwezekani kuwataja wote, ila wajue kuwa nawashukuru na kuthamini sana michango yao.

## TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu, mke wangu na watoto wangu pamoja na wadau wa Kiswahili nchini Uganda.

## MAANA ZA ISTILAHI MUHIMU

**Adhani:** Ni kitendo cha muadhini kuita watu ili waje kusali msikitini.

**Iqama:** Adhani fupi kabla ya kuanza kusali.

**Itikadi:** Ni mawazo yanayoakisi na kushikiliwa na kundi fulani la watu katika jamii**.**

**Jinsia**: Ni maumbile ya kibayolojia ya mtu kuwa mwanamume au mwanamke.

**Mahusiano ya kiuana:** Ni njia ambazo jamii inatumia kufasiri mwingiliano wa wanaume na wanawake kuhusu majukumu, haki na utambulishaji wao.

**Methali:** Ni usemi mfupi wa kimapokeo unaobeba fikira, amali za kawaida, maadili, na mafunzo mazito ambayo yanatokana na uzoefu wa maisha ya jamii fulani.

**Methali za Kiswahili**: Kwa mujibu wa utafiti huu ni methali ambazo zinatumika katika jamii ya Waswahili

**Msomi:** Mtu mwenye kiwango cha juu cha elimu kuhusu taaluma fulani.

**Mtaalamu:** Mtu aliyebobea na mwenye ujuzi kuhusu fani fulani.

**Nyin'eka:** Mama wa familia.

**Sheha:** Kiongozi wa kijiji katika maeneo ya Zanzibar.

**Uana**: Ni mitazamo, hisia na mienendo ambayo inahusishwa na utamaduni fulani kwa binadamu kulingana na jinsia yake.

**Ubabedume**: Ni hali ya wanaume kutawala wanawake nyumbani na maeneo ya umma.

**Ubabejike**: Uwezo wa wanawake wa kudhibiti na kuendeleza familia kama akina mama.

**Ukinzani:** Ni hali inayobainisha kutowiana kwa kauli na mawazo. Ni kupingana kwa kauli au mawazo.

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **A.M.I.N** | **:** Amani Iwe Naye |
| **KRH** | **:** Kiruhura |
| **Hm** | : Hakuna mwaka |
| **LMU** | : Lamu |
| **MSA** | : Mombasa |
| **SHM** | : Sheema |
| **Whr** | : Wahariri |
| **ZNB** | : Zanzibar |

# YALIYOMO

**UNGAMO** .......... **ii**

**SHUKRANI** .......... **ii**

**TABARUKU** .......... **iv**

**MAANA ZA ISTILAHI MUHIMU** .......... **v**

**YALIYOMO** .......... **vii**

**IKISIRI** .......... **xii**

**ABSTRACT** .......... **xiii**

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

**MSINGI WA UTAFITI** .......... **1**

1.0 Utangulizi .......... 1
1.1 Usuli wa utafiti .......... 1
1.2 Suala la utafiti .......... 4
1.3 Madhumuni ya utafiti .......... 5
1.4 Maswali ya utafiti .......... 5
1.5 Sababu za kuchagua mada .......... 6
1.6 Upeo na mipaka ya utafiti .......... 9
1.7 Hitimisho .......... 10

**SURA YA PILI** .......... **12**

**YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA NA MISINGI YA NADHARIA** .......... **12**

2.0 Utangulizi .......... 12
2.1 Itikadi za kiuana .......... 12
2.2 Methali za kiuana .......... 35
2.3 Usawa wa kiuana .......... 43
2.4 Misingi ya nadharia .......... 56
2.4.1 Nadharia ya Itikadi .......... 57
2.4.2 Nadharia ya Ufeministi .......... 65
2.4.3 Nadharia ya Udenguzi .......... 73
2.5 Hitimisho .......... 82

**SURA YA TATU**......84

**MBINU ZA UTAFITI**......84

3.0 Utangulizi......84
3.1 Muundo wa Utafiti......85
3.2 Eneo la Utafiti......86
3.3 Sampuli Lengwa......88
3.4 Mbinu za Usampulishaji......90
3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data......93
3.6 Uchanganuzi wa Data......94
3.7 Vifaa vya Utafiti......96
3.8 Uwasilishaji wa Matokeo......96
3.9 Uzingativu wa Maadili ya Utafiti......97
3.10 Hitimisho......98

**SURA YA NNE**......99

**MATOKEO YA UTAFITI**......99

**ITIKADI ZA KIUANA**......99

4.0 Utangulizi......99
4.1 Itikadi za kiuana na Suala la Ndoa......100
4.1.1 Itikadi za kiuana na suala la utiifu wa mke katika ndoa.......108
4.1.2 Itikadi za kiuana na suala la mitala......112
4.1.3 Itikadi za kiuana na suala la ukewenza......115
4.1.4 Itikadi za kiauna na suala la uzazi......118
4.1.5 Itikadi ya kiuana na suala la malezi......124
4.1.6 Itikadi za kiuana na suala la uongozi katika jamii......130
4.1.7 Itikadi za kiuana na suala la ujasiriamali......137
4.1.8 Itikadi ya uwezo wa kufanya kazi......142
4.1.9 Itikadi na suala la urembo wa wanawake......145
4.2 Itikadi za kiuana katika methali za Kiswahili......147
4.2.1 Itikadi za kiuana na ndoa......148
4.2.2 Itikadi za kiuana na suala la uzazi......162
4.2.3 Itikadi za kiuana na malezi ya watoto......163

4.2.4 Itikadi na urembo ........ 167
4.2.5 Itikadi kuhusu wakwe ........ 169
4.2.6 Itikadi ya udhalilishaji ........ 171
4.2.7 Itikadi za kiuana na suala la heshima ........ 173
4.3 Hitimisho ........ 175

**SURA YA TANO ........ 176**

**ITIKADI NA MAHUSIANO YA KIUANA KATIKA METHALI ZA KINYANKOLE NA KISWAHILI ........ 176**

5.0 Utangulizi ........ 176
5.1 Itikadi na mahusiano ya ndoa katika methali za Kinyankole ........ 176
5.1.1 Itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya ukewenza ........ 184
5.1.2 Itikadi na mahusiano ya utawa wa mwanamke ........ 186
5.1.3 Itikadi na mahusiano ya uzazi katika methali za Kinyankole ........ 188
5.1.4 Itikadi na mahusiano ya malezi ........ 192
5.1.5 Itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya uongozi ........ 196
5.1.6 Itikadi za kiuana kuhusu kazi ........ 202
5.1.7 Itikadi za kiuana kuhusu mahusiano na wakwe ........ 205
5.1.8 Itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya mjane ........ 209
5.1.9 Itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya udhalilishaji ........ 212
5.2 Itikadi na mahusiano ya kiuana katika methali za Kiswahili ........ 215
5.2.1 Itikadi na mahusiano ya ndoa ........ 216
5.2.2 Itikadi kuhusu ushirikiano wa mume na mke katika ndoa ........ 221
5.2.3 Itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya ndoa za mitala ........ 224
5.2.4 Itikadi za kiuana na mahusiano ya kiuana kuhusu uzazi ........ 226
5.2.5 Itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya malezi ya watoto ........ 227
5.2.6 Itikadi kuhusu mahusiano ya nguvu, mamlaka na uongozi ........ 232
5.2.7 Itikadi kuhusu mahusiano na wakwe ........ 236
5.2.8 Itikadi za kiuana kuhusu mgawanyo wa majukumu ........ 237
5.3 Hitimisho ........ 239

**SURA YA SITA ............................................................................................241**

**UKINZANI WA ITIKADI ZA KIUANA NA ATHARI ZAKE KATIKA METHALI ZA KINYANKOLE NA KISWAHILI ....................................241**

6.0 Utangulizi ............................................................................................241

6.1 Ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake katika methali za Kinyankole ............................................................................................241

6.1.1 Suala la ndoa............................................................................................243

6.1.2 Suala la ndoa za mitala ............................................................................246

6.1.3 Suala la mke kumtii mume ......................................................................250

6.1.4 Suala la uzazi ............................................................................................252

6.1.5 Suala la malezi ..........................................................................................257

6.1.6 Suala la uongozi na mamlaka ..................................................................259

6.1.7 Suala la kazi..............................................................................................263

6.1.8 Suala la mahusiano na wakwe ..................................................................265

6.1.9 Suala la ujane............................................................................................267

6.1.10 Suala la udhalilishaji..............................................................................269

6.2 Ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake katika methali za Kiswahili271

6.2.1 Suala la ndoa............................................................................................271

6.2.2 Suala la ukewenza na wazazi wa kambo ..................................................275

6.2.3 Suala la uzazi ............................................................................................276

6.2.4 Suala la malezi ..........................................................................................277

6.2.5 Suala la uongozi na mamlaka ..................................................................280

6.2.6 Suala la maslahi ........................................................................................282

6.2.7 Suala la wakwe ..........................................................................................284

6.2.8 Suala la uwajibikiaji wa majukumu..........................................................285

6.3 Hitimisho ............................................................................................287

**SURA YA SABA ............................................................................................289**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ....................................289**

7.0 Utangulizi ............................................................................................289

7.1 Muhtasari wa tasnifu..................................................................................289

7.2 Matokeo na mchango wa utafiti ................................................................292

7.3 Changamoto za utafiti ........ 296
7.4 Mapendekezo ........ 298
7.5 Hitimisho ........ 302

**MAREJELEO ........ 304**

**VIAMBATISHO ........ 318**

A.Mwongozo wa maswali kwa wahojiwa ........ 318

B.Oradha ya majedwali ........ 320

C.Orodha ya methali za kinyankole zilizotumika. ........ 322

D.Orodha ya methali za kiswahili zilizotumika ........ 329

E.Cheti cha ruhusu kufanya utafiti ........ 332

F.Barua ya ruhusa wa kufanya utafiti ........ 333

# IKISIRI

Utafiti huu umechunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Utafiti umedhamiria kubainisha itikadi za kiuana na vile zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi kati ya wanaume na wanawake. Itikadi kama imani za watu zina nguvu za kuwashawishi na kuwafanya wakubali nafasi zao na majukumu kwa misingi ya maumbile yao. Fikira na mielekeo katika mahusiano yao ya kawaida huganda akilini mwao na kuchukulia mambo kuwa ya kawaida. Imani hizi kuhusu mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake zinaendelezwa kwa ukubalifu na ushawishi ulio na msingi katika utamaduni wa jamii zinazotawaliwa kwa mfumodume. Jambo hili limeafikiwa kwa kuchunguza mahusiano ya kiuana yanayodhihirishwa na itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Aidha, utafiti umehakiki methali zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kuhusu usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Kadri ajuavyo mtafiti, uhakiki na utafiti wa kina umekuwa haujafanywa kubainisha itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi kati ya wanaume na wanawake. Vitabu vinne vya methali za Kinyankole na Kiswahili vimeteuliwa kuhusu itikadi za uana kwa njia ya kusudio. Vitabu hivi ni; Enfumu z'Omurunyankore Rukiga (Saite: 1989), Kamusi ya methali za Kiswahili (King'ei na Ndalu: 1989), Kamusi ya Methali (Wamitila: 2001) na Dafina Hazina ya Kiswahili (Al Haj Al Habsy, 2012). Data ambayo imekusanywa inahusu methali ambazo zinawasilisha itikadi za kiuana katika jamii ya Wanyankole na Waswahili. Nadharia za Itikadi Gramsci (1971), Ufeministi wa Kiafrika ya Steady (1981) na Udenguzi ya Derrida (1960) zimetumika. Nadharia ya Itikadi imetufaa katika kuwasilisha na kuchanganua itikadi mbalimbali zilizomo katika methali za Kinyankole na Kiswahili pamoja na kutathmini jinsi itikadi hizo zinazoendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kimsingi inalenga kuendeleza usawa wa kiuana bila ubaguzi wa binadamu katika misingi ya maumbile yao kijinsia pamoja na kuchunguza tofauti za kiuana zilizopo, na ambazo zinajikita katika amali za kijamii, kisiasa na kitamaduni. Mtazamo huu wa kinadharia umetumiwa kuelewa bayana itikadi za kiuana, mahusiano yake kimajukumu na jinsi itikadi hizo zinavyoathiri usawa wa kiuana kupitia methali za Kinyankole na Kiswahili.Vilevile, tumetumia nadharia ya Udenguzi kama inavyoendelezwa na Abrams na Harpham (2014). Nadharia hii imelenga kuhakiki methali ili kubainisha ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana. Nadharia hii imetuwezesha kufafanua methali kwa kina kwa kuibua fasili mbalimbali ambazo zimetubainishia itikadi zinazokinzana. Mbinu za utafiti ambazo zimetumika ni za maktabani na nyanjani. Maktabani, data imekusanywa kutokana na uchambuzi wa vitabu vya methali kutoka kwenye maktaba na makavazi ya Ankole, maktaba ya umma iliyoko Mombasa, maktaba ya ngome ya Fort Jesus na maktaba ya Lamu Fort. Data kutoka nyanjani inahusu maoni ya wasailiwa juu ya itikadi za kiuana katika methali kwa muktadha wa tamaduni za jamii za Wanyankole na Waswahili pamoja na methali. Utafiti umetumia mwongozo wa maswali na vinasa sauti kupata data pamoja majadiliano na wahojiwa. Wilaya za Kiruhura, Sheema nchini Uganda na miji ya pwani ya Mombasa, Lamu na Zanzibar zimehusishwa katika utafiti huu. Sampuli ya kusudio imetumiwa katika kutambua na kuwahoji wasailiwa ambao ni wanaume na wanawake wataalamu pamoja na wasomi wenye umri wa makamo. Data imechanganuliwa kwa mtindo wa kimaelezo na kuwasilishwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti kwa kuongozwa na nadharia lengwa. Hatimaye itikadi za kiuana zimebainishwa na vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu. Aidha, methali za Kinyankole na Kiswahili zimeonyeshwa namna zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kuhusu usawa wa kiuna.

# ABSTRACT

This research examines gender ideologies in Ankole and Swahili proverbs. The study intended to demonstrate how gender ideologies present gender relations through consent and persuasion between men and women. Ideological beliefs among people, have power of persuasion which makes them to consent to their positions and gender roles on the basis of their sex. Beliefs and attitudes in their day today relations clog in their minds and take things for granted. These beliefs about gender relations which are influenced by consent and persuasion, are rooted in society that is male dominated. This has been arrived at by studying gender relations and how they manifest in gender ideologies. Also, the researcher has critically analyzed proverbs to bring out ideological contradictions and their effects on gender equality through Ankole and Swahili proverbs. To the best of the researcher's knowlege, there was no in-depth scholary analysis that had been done before that showed gender ideologies present gender relations through consent and persuasion between men and women. This research sought to fill this gap. Proverbs presenting gender ideologies written in four selected Ankole and Swahili anthropology books purposively to satisfy the aim of the study were selected and analyzed. These books are; *Enfumu z'omurunyankore Rukiga* by Saite (1989), *Kamusi ya Methali za Kiswahili* by King'ei na Ndaru (1989), *Kamusi ya Methali* by Wamitila (2001) na Dafina Hazina ya Kiswahili (Seif Al Habsy, 2012). Library data has been collected from books of anthropoloies. Collected data included proverbs presenting gender ideologies in Ankole and Swahili communities. This study has been both a library and a field one. The theories of Ideology, African based Feminism and Deconstructionism have been used. The Ideological theory guided this study as a major theory to analyze different gender ideologies in Ankole and Swahili proverbs and to assess how ideologies influence gender relations by consent and through persuasion. This theoretical perspective has been used to understand clearly the gender ideologies, gender relations, and gendered roles and how those gender ideologies impact on gender equality in Ankole and Swahili proverbs. African based Feminism theory (Steady 1981) has been used. The theory basically focuses on gender equality without discrimination of human beings on the basis of their biological creation. Also, the theory delves into the existing gender differences which are a creation of social practices socially, politically and culturally. This theoretical approach has been used to study clearly gender ideologies, gender relations in relation to roles carried out, rights of women and how those ideologies impact on gender equality through Ankole and Swahili proverbs. The Deconstructionism theory (Abrams na Harpham 2014) has guided this study to analyse the contradictions in proverbs and their impact on gender equality presented in Ankole and Swahili proverbs depicting gender ideologies. This theory has helped in a thorough analysis of proverbs in presenting various meanings which present gender contradictions. Interview guide and recording gadgets were used to collect data from individual respondents and focus groups in the districts of Kiruhura and Sheema in western Uganda and the coastal towns of Mombasa, Lamu, and Zanzibar. Purposive sampling has been used to identify and interview the respondents who are scholars and experts, women and men of average age. Data has been analysed qualitatively and then presented in accordance with the objectives of the study guided by the adopted theories. Eventually, the study has demonstrated how gender ideologies present gender relations through consent and persuasion that exist between men and women. Also, the study has been able to bring out gender ideology contradictions and their impact on gender equality in Ankole and Swahili proverbs.

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inahusu usuli wa utafiti. Imejadili kuhusu dhana za msingi, yaani itikadi, uana na methali. Sura hii pia inashughulikia suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada pamoja na upeo na mipaka ya utafiti.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Wataalamu anuwai wameeleza maana ya itikadi. Miongoni mwao ni Gerring (1997), Nelson (1993) na Martin, (2015). Yako masuala ambayo wataalamu hawa na wengineo wanakubaliana kuhusu maana ya itikadi lakini kwa ujumla wanakubaliana kuwa itikadi ni mfumo wa mawazo fulani ambayo ni msingi wa mwelekeo wa kiuchumi, kisiasa au kijamii. Inaweza kuelezwa kuwa itikadi ni mielekeo inayofanya jamii kukubaliana katika masuala ya kila siku na kuyaona kuwa ni ya kawaida au ndivyo yanavyopaswa kuwa.

Nayo dhana ya uana imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo Connell (2009), Damon na wenzake (2006). Kulingana na Connell (2009) uana ni hali ya kuwa kiumbe cha kike au kiumbe cha kiume. Uana wa mtu unajengeka kijamii na kiutamaduni ilhali jinsia ya mtu inaamuliwa kibayolojia ( Damon na wenzake, 2006) . Kwa mujibu wa Gentile (1993) jinsia ni dhana iliyo na dhima ya kibayolojia na uana kama sifa au hali zinazohusishwa kwa mtu kuwa mume au mke. Itikadi za kiuana ni uthibitisho wa hadhi za kiuana hasa kutokana na tathmini za tofauti zake (Lorber, 1994). Lorber anatambua kwamba, itikadi zenye

nguvu huelekea kukandamiza ukosoaji wake kwa kufanya tofauti za kiuana kuonekana za kimaumbile. Kulingana na mawazo yake Lorber kwa hivyo, itikadi za wanaume kuwa wenye nguvu na mamlaka huku wanawake kuwa dhaifu na watiifu zinaendelezwa na mahusiano ya ukubalifu wao ulio na misingi katika amali za kiutamaduni.

Methali  kwa upande wake ni usemi mfupi wa kimapokeo unaodokeza fikira au mafunzo mazito kwa muhtasari. Mieder (2004:3) anasema:

> ‘Methali ni kauli fupi ambayo inawasilisha ukweli wa kimsingi’

Fasili hii inaungwa mkono na Mieder (1989) anayesema kwamba methali ni kauli fupi ya kijamii inayobeba maarifa ya busara, ukweli, maadili na maoni ya kiutamaduni kwa mtindo wa kiistiari ambao haubadiliki. Kauli hii inapokezana kizazi baada ya kizazi kwa njia ya kimapokezi. Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba methali ni kauli yenye ukweli ulio na msingi katika utamaduni wa jamii fulani ambayo inawasilishwa kimapokezi kwa njia ya mafumbo kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Methali kama kipera cha fasihi simulizi, ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii yoyote ile. Miongoni mwa dhima za methali ni pamoja na ya kihistoria kwani kupitia sanaa hii, mila, desturi, kazi mawazo na utamaduni wa watu wa kale hufahamika miongoni mwa kizazi kipya.

Yeye Mulokozi (2017) anasema kwamba methali ni usemi mfupi wa kimapokeo unaodokeza fikira au mafunzo mazito kwa muhtasari. Mulokozi anaendelea kusema kwamba mafunzo haya yanatokana na uzoefu wa maisha ya jamii fulani. Aidha, Mulokozi anadai kwamba methali ni chombo cha itikadi na hekima inayopatikana katika methali inaweza kuwa chanya au hasi kutegemea muktadha

wa kijamii na kihistoria. Methali zinabeba maisha ya wanajamii, matarajio, amali za kawaida na maadili ya watu katika jamii. Jambo la muhimu zaidi, methali zinawasilisha ukweli wa pamoja unaokubalika na wanajamii kwa njia ya kimafumbo (Kochman-Haładyj, 2020). Methali ziko na nafasi kubwa na dhima ya kubeba utamaduni na kuwasilisha itikadi ya jamii (Oyaro, 2019). Aidha, methali zinaumba na kuunda sheria za utamaduni au kuelezea kila imani na kuonyesha tabia kwa njia ya kifasihi iliyo ya moja kwa moja (Finnegan, 1970). Isitoshe, katika methali, tajriba za binadamu zinabainika, zinaelezwa, zinachanganuliwa na kutoa mawazo ya jumla na kanuni za jamii kwa njia ya mkato. Kwa hivyo, kwa kuegemea maoni hayo itikadi za kiuana kama mawazo yanayowasilishwa katika methali zimebainika na kuweza kudhihirisha namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Aidha, utafiti umeweza kuibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Mieder (2004) anatambua kwamba methali zinawasilisha taswira kadhaa katika miktadha tofauti. Kwa kuegemea maoni yake Mieder, utafiti umeweza kuibua ukinzani wa itikadi za kiuana ambao unadhihirishwa na methali katika miktadha tofauti.

Kutokana na mawazo haya, inabainika kuwa Itikadi ni muhimu katika kubainisha mahusiano ya kiuana. Pia, methali ni kipengele muhimu cha fasihi simulizi ambacho kimedhihirika kuwa na dhima ya kuwasilisha itikadi za jamii fulani (Ndulute, 1974). Ilikuwa muhimu kuchunguza jambo hili kwa kina ili kubainisha itikadi za kiuana zinavyojitokeza na kuendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Itikadi hizo za kiuana

zimejidhihirisha katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Jambo hili kadri ya ufahamu wa mtafiti limekuwa halijafanyiwa utafiti wa kina.

**1.2 Suala la utafiti**

Itikadi ni njia za kimakusudi za kufafanua na kupatia maana, ulimwengu wa kundi fulani la watu katika jamii wanamoishi. Njia hizi za kimakusudi zinabainisha mawazo yanayoakisi kundi fulani katika jamii. Itikadi ni jambo la msingi katika kusababisha ugawaji wa binadamu wa jamii fulani katika makundi. Wanaume na wanawake wanarejelewa kama makundi ambayo yameumbwa na kugawanywa kwa misingi ya amali za kijamii. Methali zinawasilisha itikadi za kiuana. Itikadi hizo, ziko na athari kubwa kwa maisha ya binadamu katika mahusiano ya wanaume na wanawake kama makundi ambayo yamegawanyika kwa misingi ya utamaduni katika jamii. Baadhi ya watafiti wameshughulikia usawiri wa wanawake na wanaume katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na hata katika methali za jamii mbalimbali. Miongoni mwa hao ni (Ndungo, 1998; Kobia, 2008; Wandera, 1996; Lee, 2015 pamoja na Diabah na Appia, 2015). Katika tafiti hizo haibainiki namna itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana katika methali kwa njia ya ukubalifu na ushawishi. Aidha, haidhihiriki katika tafiti hizo kuwa mahusiano ya kiuana yanayochukuliwa kama ya kawaida na wanawake kama kundi linalotawaliwa wanaathiriwa na ung'amuzi potoshi (Althusser, 1981). Pia, watafiti wa awali hufikiria kwamba mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake kwa kuwatenganisha katika matabaka ni itikadi ambayo huendelezwa kwa kutumia nguvu au vyombo vya kiitikadi kwa kulazimisha kama anavyodai Althusser (1981). Utafiti huu, umebainisha kwamba, itikadi za kiuana zinaendeleza mahusiano ya kiuana kati ya wanaume

na wanawake kwa njia ya ukubalifu na ushawishi, na wala sio kwa matumizi ya nguvu kama inavyoshadidiwa na wahakiki wengine. Wanawake wanakubali nafasi yao kama raia wa daraja la pili na kuwajibikia majukumu ambayo yanaashiria wanaume kuwa wenye mamlaka, uwezo na hadhi ya juu pamoja na kupewa kipaumbele. Utafiti ulilenga kufanya hivi kwa kuchunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia za Itikadi, Ufeministi wa Kiafrika na Udenguzi. Pamoja na hayo, utafiti huu pia umehakiki methali na kuibua mikinzano ya kimaana na kudhihirisha athari zake kwa usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili kwa mujibu wa Nadharia ya Udenguzi.

### 1.3 Madhumuni ya utafiti

Utafiti huu umelenga kuchunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Malengo mahususi ya utafiti huu ni kama ifuatavyo:

i. Kubainisha itikadi za kiuana zinazojitokeza katika methali za Kinyankole na Kiswahili.
ii. Kuchunguza itikadi za kiuana zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu katika methali za Kinyankole na Kiswahili.
iii. Kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana.

### 1.4 Maswali ya utafiti

i. Itikadi gani za kiuana zinazojitokeza katika methali za Kinyankole na Kiswahili?
ii. Itikadi za kiuana zinadhihirisha namna gani ukubalifu wa mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume katika methali za Kinyankole na Kiswahili?

iii. Ni vipi methali za Kinyankole na Kiswahili zinaibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili?

**1.5 Sababu za kuchagua mada**

Watafiti wengi kama Hussein (2005), Ezeifeka (2017), Lomotey (2019) pamoja na Gyan na Wenzake (2020) wametafiti kuhusu itikadi za kiuana katika methali. Wanakubaliana kwamba wanaume wanatweza wanawake kwa kuchunguza jinsia moja ama kutumia wanaume kuchunguza wanawake au kuwaangalia wanawake pekee. Hawaoneshi namna mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake yanavyodhihirishwa na itikadi kwa njia ya ukubalifu na ushawishi kuwajibikia majukumu yao na kubainika katika nafasi zao.

Aidha, mada hii imeteuliwa ili kuweza kuonesha methali zinazoeleza kuhusu suala la uana zinavyobainisha itikadi za kiuana na namna itikadi hizo zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Uchunguzi kuhusu uana na mahusiano yake unaendelea katika ngazi tofauti katika jamii mbalimbali duniani (Lovenduski na Norris, 1996). Lovenduski na Norris wanatumia analojia ya kitunguu ambacho kinatokwa maganda makavu na kutokezea mengine mabichi. Masuala ya Uana yanaendelea kupata sura anuwai kila wakati. Jamii za Wanyankole na Waswahili zinakua kimaendeleo, zinabadilika na kupata sura za usasa. Kwa hivyo, mahusiano ya kiuana yanapata sura tofauti, mahitaji ya kiuana yanakuwa tofauti na kuzua changamoto tofauti.

Waswahili na Wanyankole pamoja na kuwa asili yao ni ya Kibantu, tamaduni na amali zao ni tofauti. Mfano, utamaduni wa Waswahili umeathiriwa na tamaduni za wageni, dini ya Kiislamu na amali mpya za kijamii (Mbaabu, 1985; Swaleh, 2009). Aidha, jamii hizi mbili zina usuli tofauti. Akibainisha utofauti uliopo kati ya jamii, Sengo (1992) anadai kuwa kila jumuia ya watu ni huru na ni tofauti na nyingine. Mawazo haya yamesababisha kuchagua mada hii ili kubainisha itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Fasihi simulizi ni sehemu ya maisha na tamaduni za jamii mbalimbali. Mbali na jamii kukua na kubadilika katika nyanja mbalimbali, tamaduni zao hazitupiliwi mbali. Kadri jamii zinavyobadilika ndivyo tamaduni zao zinavyozua athari fulani. Hali hii inasababisha kuwepo kwa mahusiano mbalimbali ya kiuana kulingana na mabadiliko hayo katika jamii. Kutokana na sababu hii, mada hii imechaguliwa ili kuweza kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili kuonyesha namna zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana kitamaduni na kutathmini jinsi ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili unavyoathiri usawa wa kiuana.

Sababu nyingine ya kuchagua mada imetokana na uamilifu wa kipera cha methali. Methali ni kipengele cha fasihi simulizi ambacho kina dhima yake katika kupitisha ujumbe, kusheheni amali za jamii na kubeba hekima (Mtesigwa, 2013). Uchaguzi wa mada hii umefaa ili kuweza kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili kutokana na uamilifu wake wa kusheheni maarifa ya jamii na amali zake katika kubainisha itikadi za kiuana. Methali ni chombo cha itikadi, na

kwamba, hekima inayopatikana katika methali inaweza kuwa chanya au hasi kutegemea muktadha wa kijamii na kihistoria (Mulokozi, 2017).

Utafiti huu pia umechochewa na tafiti za awali ambazo zimechunguza sura anuwai za mwanamke na mwanaume katika utengano. Tafiti hizo zilichunguza taswira na hadhi za au mwanamke ama mwanamume na kuzitolea uchanganuzi (Ndungo,1998; Momanyi, 1998; Simala, 2000; Kobia, 2008 na Wandera 1996) lakini itikadi za kiuana hazikuwa lengo katika tafiti zao na hazibainishi namna mahusiano ya kiuana yanaendelezwa kwa ukubalifu na ushawishi. Pia, namna methali zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili ni suala ambalo halizingatiwi katika tafiti hizo.

Watafiti wengine wametumia kipera cha methali kutafitia masuala mengine (Maitaria, 2012). Tafiti hizo hazikulenga kubainisha itikadi za kiuana zinavyotokea katika kudhihirisha mahusiano ya kiuana. Aidha, tafiti hizo hazikulenga kuchunguzai tikadi za kiuana zinavyoathiri mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Pia, namna methali zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana zijulikanazo za kiutamaduni za Kinyankole na Kiswahili ni suala ambalo lilikuwa halijashughulikiwa kitaaluma kabla ya utafiti huu.

Kulingana na sababu hizi, inadhihirika kwamba kumekuwa kunakosekana utafiti wa fasihi ya Kiswahili ambao unachunguza itikadi za kiuana zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi katika methali na namna

methali zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali hizo na vilevile jinsi ukinzani wa itikadi za kiuana unaathiri usawa wa kiuana. Isitoshe, kadri ya uelewa wa mtafiti hakuna utafiti wa fasihi ya Kiswahili ambao umeshughulikia itikadi za kiuana katika methali kwa kurejelea mikabala ya itikadi ya ( Gramsci, 1985;  Althusser, 1981).

**1.6 Upeo na mipaka ya utafiti**

Utafiti huu umelenga  utanzu wa fasihi simulizi na umejikita kwenye kipera cha methali. Umejikita katika kuchunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Utafiti umehusisha methali 174, yaani methali 92 za Kinyankole na methali 82 za Kiswahili kutoka kwenye vitabu vya methali pamoja na nyanjani zinazohusu itikadi za kiuana. Tofauti kuhusu usawa wa idadi ya methali za Kinyankole na Kiswahili umejitokeza kwa sababu methali za Kinyankole zinazofafanua kuhusu masuala ya Uana zimekuwa nyingi kuliko za Kiswahili. Methali ambazo hazizungumzii wanawake na wanaume mfano zile zinazotumia jinsia ya kike au ya kiume kama njia ya kuwasilisha ujumbe unaolenga mambo mengine yasiyohusiana na suala la uana, hazijashughulikiwa. Methali za Kinyankole na Kiswahili zimeteuliwa  kwa sababu methali zina dhima kuu ya kuwasilisha falsafa na itikadi za jamii (Finnegan, 1970). Kwa hivyo itikadi za kiuana na amali muhimu za jamii hizi mbili pamoja na sifa za kiuana zinawasilishwa moja kwa moja katika methali.

Utafiti huu umefanyika nchini Uganda katika kata ndogo ya Kitongore, kata ya Engari wilayani Kiruhura pamoja na Kabwohe na Bugongi wilayani Sheema nchini Uganda. Maeneo haya yamechaguliwa kwa sababu utamaduni wa

Wanyankole katika maeneo haya haujaathiriwa na amali za tamaduni za jamii nyingine (Kirindi 2008). Pia, utafiti huu umelenga pwani ya Afrika Mashariki katika maeneo ya Kiembeni na Mombasa mjini katika kaunti ya Mombasa; Mitaa ya Mtamuini na Mkunguni katika kaunti ya Lamu nchini Kenya pamoja na Bububu na Kiembe samaki, Zanzibar nchini Tanzania. Maeneo haya yameteuliwa kutokana na mchango wake katika kufanikisha utafiti huu kama ifuatavyo: Lamu na Mombasa ni maeneo ambayo yametoa mchango kuhusu utamaduni asilia wa Waswahili. Ghaidan (1974) anaeleza kwamba mji wa Mombasa ni eneo mwafaka la kihistoria kwa sababu unahifadhi historia yake asilia ukilinganishwa na maeneo mengine ya Uswahilini. Pia, amali za Waswahili na mahusiano yao ya kijamii yanapatikana sehemu hizo. Utafiti huu umepata data ya msingi kuhusu itikadi za kiuana za Waswahili katika maeneo hayo. Maarifa muhimu kuhusu historia na utamaduni wa Waswahili pia yamepatikana katika eneo la Lamu. Eneo hili limeteuliwa kwa sababu ya maarifa ya msingi yanayopatikana kwenye makavazi ya Waswahili kuhusu elimu pana ya historia na utamaduni wa Waswahili. Eneo la Zanzibar limechangia utafiti huu kwa kupata maoni kuhusu methali za Kiswahili katika Kiswahili sanifu kutokana na historia yake ya kuchaguliwa kwa Kiunguja kusanifishia lugha ya Kiswahili (Mbaabu, 2007). Kwa hivyo, mtafiti amepata ufafanuzi wa methali za Kiswahili.

## 1.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia usuli wa mada. Moja ya vipengele mahususi katika sura hii ni suala la utafiti. Imedhihirishwa kuwa suala la itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana katika methali kwa njia ya ukubalifu na kuchukuliwa kama za kawaida, wanawake kubainika kama kundi linalotawaliwa

ni ung’amuzi potoshi. Pamoja na hayo, kumeonyeshwa malengo ya utafiti. Malengo hayo ni: Kubainisha itikadi za kiuana zinazojitokeza katika methali za Kinyankole na Kiswahili, kuchunguza mahusiano ya kiuana yanayodhihirishwa na itikadi za kiuana kwa ukubalifu katika methali za Kinyankole na Kiswahili na kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana. Aidha, maswali ya utafiti yameshughulikiwa na sababu za kuchagua mada. Imeonyeshwa kwamba methali kama kipengele cha fasihi simulizi zinabeba itikadi za jamii. Methali zinakuwa na uamilifu wa kupitisha amali na hekima katika jamii. Ijulikanavyo, hakuna utafiti ambao ulikuwa umefanywa kuhusu itikadi za kiuana namna zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na kuchukuliwa kama za kawaida na kubainisha kuwa wanawake kama kundi linalotawaliwa wanaathiriwa na ung’amuzi potoshi. Mwisho, upeo na mipaka ya utafiti imeshughulikiwa.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inapitia na kuhakiki kazi za wataalamu mbalimbali pamoja na tafiti zilizofanywa kuhusu mada. Mtafiti ameangalia tafiti, makala na vitabu mbalimbali vinavyozungumzia itikadi za kiuana, mahusiano ya kiuana, pamoja na maandishi kuhusu methali kwa mujibu wa mipaka ya mada ili kuweza kubainisha pengo la utafiti. Sura hii imeshughulikia pia nadharia na mihimili yake iliyoongoza utafiti. Nadharia zilizotuongoza ni zifuatazo: Nadharia ya Itikadi kwa mujibu wa ( Gramsci, 1971), (Althusser, 1971) na (Bressler, 2007); Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika (Steady, 1981) pamoja na nadharia ya Udenguzi (Derrida, 1976).

## 2.1 Itikadi za kiuana

Watafiti wamechunguza kuhusu itikadi za kiuana, wengi wao wameshughulikia itikadi za kiuana kwa kuchunguza usawiri na hadhi ama ya wanaume au wanawake katika methali (Ndungo, 1998); (Schipper, 1991); (Sarwet, 2015); (Mubarok, 2017); (Zheng, X 2018); (Kochman-Haładyj, 2020). Wengine wameshughulikia itikadi za kiuana katika tanzu nyingine za fasihi (Ogunsina, 1996), (Kobia, 2008), (Handayani, 2017), (Murithi, 2018), (Allagbe, 2020), ( Ogutu na wenzake, 2020) na (Ikeke, 2021).

Kutawaliwa kwa kundi fulani mara nyingi kunaendelezwa na kuhalalisha mielekeo na itikadi ya tabaka tawala (Gramsci, 1971). Itikadi hiyo inapatikana

kwa kuendeleza ukubalifu wa nguvu za kijamii ambayo ni shughuli endelevu. Itikadi inaibua imani za binadamu tunazobeba akilini kama fikra zetu juu ya mambo mbalimbali na jinsi tunavyoyatumia kuendeleza maisha tunayofikiria ndiyo yanafaa. Gerring (1997) anafafanua matumizi mbalimbali ya dhana ya itikadi kama mkusanyiko wa mawazo fulani yenye maudhui fulani. Fauka ya hayo, Gerring anatambua kwamba itikadi zinabainisha mawazo vile watu wanaingiliana kijamii. Itikadi hizo zinahusu thamani na imani katika kuibua mahusiano ya kitabaka na kuficha migongano. Yeye Heywood (1994) anatambua na kuunga mkono mawazo ya Karl Marx, (1975) kwamba mfumo wa ubepari uliimarishwa na itikadi za tabaka tawala, hali iliyoibua mawazo ya ung'amuzi potoshi ambayo yaliwafanya wafanyakazi kutotambua na kupinga kudhulumiwa kwao.

Itikadi fulani ina uwezo wa kufanya mtu au kundi fulani la watu kutambua mapungufu ya mwingine au kundi lingine na kushindwa kutambua mapungufu yaliyo kwa upande wao (Nelson, 1993). Maoni ya Nelson yanajikita katika itikadi iliyoshikiliwa na (Napoleon 1769-1821) akiwakashifu na kuwalaumu wanaharakati waliojaribu kuendeleza haki za kimsingi za binadamu, kudai uhuru na harakati za uzinduzi wa watawaliwa. Alidai kuwa upande wake ndio sahihi na upande wa wanaharakati kudhihirika kutokuwa sahihi.

Lorber (1994) anatambua kwamba, itikadi zenye nguvu huelekea kukandamiza ukosoaji wake kwa kufanya tofauti za kiuana kuonekana za kimaumbile. Kulingana na mawazo ya Lorber, itikadi za wanaume kuwa wenye nguvu na mamlaka huku wanawake kuwa dhaifu na watiifu zinaendelezwa na mahusiano

ya ukubalifu wao ulio na misingi katika amali za kitamaduni. Kila jamii inatengeneza na kuendeleza itikadi zake za kiuana. Itikadi hizo zinatenganisha wanaume na wanawake kwa kuwaweka katika nafasi tofauti zinazokinzana. Tofauti hizo zinaibua matarajio tofauti kati ya wanaume na wanawake kama anavyotambua Kochman-Haładyj (2020). Kochman-Haładyj anaendelea kusema kwamba katika kila utamaduni, wanaume wanachukuliwa kuwa wakakamavu huku wanawake wanachukuliwa kama viumbe dhaifu. Mtazamo huu wa kiitikadi unaendeleza utofauti wa mahusiano ya kiuana katika maisha ya wanaume na wanawake katika jamii.

Kulingana na Connell (2009), uana ni hali ya kuwa kiumbe cha kike au kiumbe cha kiume. Uana wa mtu unajengeka kijamii na kiutamaduni ilhali jinsia ya mtu inaamuliwa kibayolojia (Ridgeway na Correll 2004). Jinsia ni dhana iliyo na dhima ya kibayolojia na uana kama sifa au hali zinazohusishwa kwa mtu kuwa mume au mke. Msingi wake ni wa kijamii kuliko wa kibayolojia (Gentile, 1993). Kulingana na Gentile, fasili hizi zingeweza kupunguza hali ya kuchanganyikiwa katika matumizi ya dhana hizi mbili ambazo zinaonekana kuwa zinaingiliana. Utata huu huenda unaakisiwa katika fasihi simulizi kuhusu itikadi za kiuana zinavyobainika katika methali kwa mfano jukumu la kulea watoto ni la wanawake kama mama kwa sababu ya hali ya kibayolojia ya mama kumnyonyesha mtoto. Ufafanuzi huu unathibitisha maoni ya (Ogundipe, 1987) ambaye anasema kwamba maumbile ya kibayolojia ya mwanamke ndiyo yamekuwa majaliwa kwake kutoka mwanzoni. Maumbile hayo yalisababisha kuchipuka na kuimarika kwa majukumu, taswira na hali yake. Kutokana na

maoni ya Ogundipe mwanamume anachukua mwanamke kulingana na hali ya maumbile yake.

Kroska (2007) amefafanua dhana ya itikadi za kiuana kama mitazamo inayohusu majukumu na haki za wanaume na wanawake katika jamii. Itikadi za kiuana kwa misingi ya utamaduni, zinasisitiza dhima ya kutenganisha majukumu kwa wanawake na wanaume. Wanaume wanatekeleza majukumu yao muhimu ya kutafutia familia riziki. Wanawake kwa upande mwingine wanatekeleza majukumu yao ya kutunza watoto, kutunza nyumba pamoja na shughuli za malezi.

Mahusiano ya kiuana ni juhudi za kuelewa nafasi ya wanawake na wanaume kwa kuhusisha majukumu ya kiuana, uwezo na mamlaka pamoja na nafasi za kiume na za kike katika jamii (Schalkwyk, 2000). Ni njia zinazowekwa na utamaduni kuhusu mahusiano kati ya wanaume na wanawake ambapo wanaume wanabainika kuwa kwenye nafasi ya mbele na kupendelewa kuliko wanawake. Mahusiano ya kiuana yenye mfumo wa kutenganisha majukumu ya kiuana yanatokana na utamaduni wa binadamu kuwa kiumbe cha kike au kiume. Itikadi hii inadhihirika katika ugawaji wa kazi kiuana. Mawazo haya yanathibitishwa na (Schalkwyk, 2000) kwamba, katika jamii nyingi kuna kazi za nyumbani na za umma zijulikanazo kuwa za wanawake na wanaume ambapo, nafasi na matarajio kuhusu hulka, sifa na tabia faafu kwa wanawake au wanaume pamoja na uhusiano kati yao zinajengwa na utamaduni. Vitambulisho vya uana na mahusiano yake ni vipengele muhimu vya utamaduni kwa sababu vinaathiri maisha ya kila siku katika familia, katika jamii na maeneo ya kazi. Kwa hivyo,

itikadi za kiuana ziko na mchango mkubwa katika kuathari mahusiano ya kiuana katika kutekeleza majukumu yanayochukuliwa kuwa ama ya kike au ya kiume kwa misingi ya kiutamaduni.

Uana ni matokeo ya jamii katika utambulisho wa jinsia ilhali jinsia inatokana na hali ya kimaumbile au kibayolojia (Lovenduski & Norris, 1996), (Abrams, 2012) na (Kaveh na wenzake 2021). Kulingana na Lovenduski & Norris, (1996), uana ni suala ambalo lina mjadala mkubwa duniani kote katika karne hii ya ishirini na moja. Suala hili linaathiri moja kwa moja usawa wa kiuana, suala ambalo ni nyeti duniani. Zaidi ya haya, Lovenduski & Norris (1996) wanaendelea kusema kwamba Afrika bado iko nyuma katika takwimu za kilimwengu za utetezi wa usawa wa kiuana na inaongoza katika takwimu kuhusu mizozo ya kifamilia iliyo na misingi katika kasumba za kiume. Tukirejelea maoni ya Lovenduski & Norris kwa hivyo, itikadi za kiuana kama zinavyobainika katika methali za Kinyankole na Kiswahili zimechunguzwa kuonyesha mahusiano ya kiuana ili kutathmini mchango wake katika kuendeleza suala la usawa wa kiuana na haki za msingi za binadamu, katika jamii ya Wanyankole na Waswahili.

Utafiti huu umechunguza suala hili kwa kuzingatia kwamba, mwanamke na mwanamume ni viumbe ambao wameishi pamoja tangu kuwepo kwa binadamu kwa kushirikiana, kugawana majukumu na kuaminiana (Etchezahar na Ungaretti, 2014). Vilevile Abrams (2012) anasema kwamba, itikadi za kiuana zinaathiri namna binadamu wanavyoingiliana katika mazingira yao, namna wanavyofanya maamuzi katika familia, uhusiano kati ya mume na mke, malezi, uamuzi binafsi, matamanio, mafanikio na mienendo ya binadamu kwa jumla. Kulingana na

mawazo ya wataalamu hawa, utafiti huu umedhamiria kuchunguza itikadi za kiuana zinavyodhihirisha mahusiano kati ya wanaume na wanawake kwa ukubalifu na ushawishi. Utafiti huu umefanywa kwa kubaini kwamba wanaume na wanawake wanaishi pamoja na itikadi za kiuana zinaathiri namna wanavyoingiliana. Fauka ya hayo, uchunguzi kuhusu mahusiano ya kiuana yanaendelea katika ngazi tofauti kama wanavyotambua (Lovenduski na Norris, 1996). Wakirejelea mahusiano ya kiuana kati ya wanawake na wanaume, Lovenduski na Norris (1996:4) wanatumia analojia ya kitunguu ambacho kinatokwa maganda makavu na kutokezea mengine mabichi:

> " ganda linapoambuka jingine linatokezea. Kwa njia hiyo, vile kitunguu kina rusu zake,ndivyo rusu za mahusiano ya kiuana yalivyo kati ya mwanamke na mwanamume katika jamii za kisasa" .

Maoni haya yanadhihirisha kuwa, jamii zinapoendelea kubadilika, mahusiano ya kiuana yanapata sura tofauti na mahitaji ya kiuana yanakuwa tofauti. Vile vile, kuzungumzia wanawake bila kuzungumzia wanaume ni kama kupiga makofi kwa mkono mmoja, jambo ambalo haliwezekani kama anavyotambua (Nira, 1997). Kulingana na maoni ya Nira, tafiti ambazo zimeshughulikia suala la uana, nyingi zimeangalia sana sura anuai za mwanamke na uchanganuzi wake ukatolewa na kubainisha jinsi mwanamke huyo anavyokandamizwa na kutoshiriki katika nyanja mbalimbali za kijamii katika jamii zao. Itikadi za kiuana zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu kulingana na utafiti huu si nia ya tafiti hizo.

Yulanesta (2014) amechunguza jinsi itikadi za kiuana zinavyowasilishwa katika riwaya za Indonesia. Amelenga mchango wa utambulishaji wa kiuana, harakati za wanawake na mahusiano yao na wahusika wengine pamoja na kuainisha itikadi na tofauti za kiuana. Yulanesta amechunguza suala hili katika riwaya sita za waandishi wa Indonesia. Anasema kwamba riwaya za Kiindonesia zinawasilisha itikadi za ubabe dume, itikadi za utawala wa wanaume, itikadi za umame, tofauti za kiuana, na utekelezaji wa majukumu ya nyumbani kwa wanawake na kutawishwa kwao kwenye mazingira ya nyumbani. Anabainisha kwamba kuwepo kwa itikadi za kiuana kunashadidiwa na sifa za kitamaduni za uanaume na uanawake. Utafiti wake ni muhimu kwa utafiti huu kwa kutoa mwanga kuhusu itikadi za kiuana mbalimbali. Hata hivyo, katika utafiti wake haonyeshi namna itikadi za kiuana zinavyoendelezwa kwa njia ya ukubalifu na ushawishi, suala ambalo limechunguzwa katika utafiti huu. Isitoshe, katika utafiti huu itikadi za kiuana zimechunguzwa kwa undani zaidi kwa kuzingatia methali. Pia, utafiti umezingatia mahusiano ya kiuana yanayodhihirishwa na itikadi za kiuana kwa ukubalifu na kudhihirisha ukubalifu huo unavyochukuliwa kama jambo la kawaida. Suala hili halichunguzwi katika kazi ya Yulanesta.

Copenhaver (2002) ameshughulikia usawiri wa uana na kueleza majukumu ya kiuana katika tamthilia teule za kisasa za Kimarekani. Katika kazi yake anatambua kwamba wahusika wa kike wanatekeleza majukumu ya kiuana kulingana na matarajio ya utamaduni. Utekelezaji huo wa majukumu unasababishwa na wanawake kuwa katika nafasi ya mke au mama na wanaume kushikilia nafasi ya mume au baba. Ingawa Copenhaver anashughulikia utanzu

wa tamthilia, utafiti huu umevutiwa na kazi yake kwa sababu anaeleza masuala ya uana na majukumu ya kiuana. Utafiti huu unafaidika na kazi yake ambapo anabainisha majukumu ya kiuana kwa mfano wanaume kuwajibika katika kutafutia familia zao riziki kwa upande mmoja na wanawake kuwajibikia majukumu ya nyumbani. Hata hivyo, katika kazi yake Copenhaver haonyeshi itikadi za kiuana kwa kina na kwa mapana yake namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifi. Vile vile haonyeshi kuwa mahusiano kati ya wanaume na wanawake yanayoendelezwa kwa njia ya kawaida yanaathiriwa na ung'amuzi potoshi. Isitoshe, utafiti wake unahusika na tamthilia ilhali utafiti huu unachunguza methali katika kubainisha itikadi za kiuana zinavyoendelezwa kwa ukubalifu.

Handayani (2017) ameshughulikia itikadi za kiuana katika riwaya ya 'The story of Zaha' of Asy-Syaikh (1945). Anabainisha itikadi za kiuana katika riwaya hiyo ambazo zinahusu ukuaji wa utambulishaji wa kiuana, umbo la wanawake na ubikira. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kwamba waandishi wa kike wanawafafanua wanawake kuwakilisha suala la uana ili kuweza kutetea hali zinazowazunguka kwa ubainifu. Katika maoni yake kuhusu itikadi za kiuana, anajikita kwa hali ya kuwa mwanamke, umbo la mwanamke na ubikira katika jamii ya Lebanon. Anazingatia mitazamo iliyo na misingi katika amali za itikadi za mfumodume. Utafiti wa Handayani umeongoza utafiti huu kwa kubainisha baadhi ya itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na utafiti wa Handayani kwa sababu tulicutafiti huu unachunguza itikadi za kiuana zinazotokea katika methali kwa kuzingatia jinsia

zote mbili yaani wanaume na wanawake, tofauti na yeye anayeegemea upande mmoja wa wanawake.

Sultana (2010) amechunguza ubabedume na ukandamizaji wa wanawake. Amelenga kuchanganua namna itikadi ya ubabedume inavyoathiri maendeleo ya wanawake na kudhihirisha mfumo unaofanya wanawake kukandamizwa na kutopata maendeleo. Sultana anabaini kwamba, hali ya kibayolojia ya wanawake inaathiri namna wanavyofikiria, uwezo wao na namna wanavyotekeleza majukumu yao. Utafiti huu umebainisha itikadi za kiuana vile zinatokea katika methali za Kinyankole na Kiswahili kwa ukubalifu, jambo ambalo halijitokezi katika utafiti wa Sultana. Aidha, utafiti huu haulengi ukandamizaji wa wanawake kwa misingi ya ubabedume kama suala la msingi, kama vile inavyosisitizwa katika utafiti wa Sultana. Isitoshe, utafiti wake haushughulikii mahusiano ya kiuana vile yanavyodhihirishwa na itikadi za kiuana.

Malicke (2013) amechunguza kuhusu athari za kusisitiza tofauti za kiuana kwa upande mmoja na kupuuza tofauti za kiuana kwa upande mwingine. Anazingatia aina mbili za itikadi pamoja na kutathmini sifa za kike na za kiume ambazo ni kuepuka kutenganisha binadamu katika makundi kwa sababu ya maumbile yao. Malicke anapendekeza kwamba utambuzi wa kiuana ni mfumo mwafaka kuondoa ubaguzi wa kiuana kwa wanawake katika maeneo ya kazi. Utafiti wa Malicke umefaidi utafiti huu kwa sababu katika kazi yake anadokeza kuhusu athari za itikadi za kiuana kuhusu usawa wa kiuana, jambo ambalo pia limeshughulikiwa kwa kina katika utafiti huu. Tofauti na kazi yake, utafiti huu unatathmini namna ukinzani wa kiuana unavyoathiri usawa wa kiuana.

Davis na wenzake (2010) katika utafiti wao wa athari kuhusu itikadi za akina mama ambao hawajaolewa kuhusu kuzaa watoto, wanatambua kwamba kuzaa na kuwa na watoto kunasababisha kuendeleza na kudumisha imani za kiutamaduni kuhusu uana. Davis na wenzake wanasema kwamba kuwa mzazi ni suala linaloathiriwa na itikadi za kiuana. Katika utafiti wao, wanachunguza maisha ya wanawake ambao ni akina mama wakiwa wajawazito na kipindi cha kujifungua. Wanalenga akina mama ambao hawajaolewa huko Marekani. Wanabainisha iwapo kubeba mimba na kujifungua mtoto kunachangia ujengaji wa itikadi za kiuana, na ni kwa jinsi gani hali hizo zinavyochangia ujengaji wa itikadi za kiuana. Wanagundua kwamba, kubeba mimba na kuzaa mtoto hakuna athari za kiitikadi kwa akina mama ambao wanazaa mara ya kwanza na hawajaolewa. Matokeo ya utafiti wao yanachangia utafiti huu kwa kudokeza kuhusu mahusiano ya kiuana, hata kama wanajikita kwa kuchunguza athari za itikadi za kiuana kwa akina mama wasio katika ndoa kuhusu kuzaa watoto. Kwa upande mwingine, tofauti na kiini cha uchunguzi wao, utafiti huu tumechunguza itikadi za kiuana na namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili na tumebainisha jinsi methali hizo zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana zijulikanazo kiutamaduni.

Smith-Hefner (2009) katika utafiti wake kuhusu mabadiliko ya lugha, uana na itikadi za usasa katika eneo la kati kisiwani Java nchini Indonesia, anagundua kwamba wanawake wanadhihirisha wasiwasi na ugumu kuhusu upatikanaji wa wachumba wa kuwaoa. Wanawake wanapoendelea kukua kiumri na kusoma sana, inakuwa vigumu kupata wachumba. Wanaume wa Kijava wanapendelea

kuoa wanawake wenye umri mdogo na wenye elimu ndogo kuliko wao. Pamoja na hayo, wanawake wa Kijava wameathiriwa na mahitaji ya Kiislamu ya ndoa mseto. Wana imani kwamba idadi ya wanawake ni kubwa wakilinganishwa na ya wanaume. Smith-Hefner anadhihirisha kwamba wanawake wanatambua sheria za dini ya Kiislamu kama njia muhimu ya kupata mume mzuri kuliko masuala ya kitamaduni. Utafiti wa Smith-Hefner kuhusu mahusiano ya kindoa katika jamii ya Wajava ulifaa utafiti huu kuweza kubainisha itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana. Utafiti wa Smith-Hefner hata hivyo ni tofauti na huu kwa sababu yeye Smith-Hefner anaangazia suala la uana na itikadi za kisasa ilhali utafiti huu unachunguza itikadi za kiuana vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Katika utafiti wa (Etchezahar & Ungaretti, 2014), wanaeleza umuhimu wa muktadha wa amali za utamaduni ambazo zinapitisha sifa zenye vitendo kwa wanaume na sifa hisi kwa wanawake. Wanagundua katika utafiti wao kwamba, sifa za uana zinatengenezwa na utamaduni. Wanaendelea kutambua kwamba tofauti za kibayolojia haziendelezi ubaguzi wa kiuana kati ya wanaume na wanawake katika jamii ya kisasa. Wanaume wanakuwa na sifa za mamlaka na uongozi kwa jumla. Wao wanawake wanawekewa mipaka ya kubaki katika mazingira ya kifamilia, kuchukua majukumu ya kike, akina mama, akina dada na mabinti, yaani wanafamilia ambao ni wategemezi. Ingawa katika utafiti wao wanashughulikia uana, walijikita katika dhana gande na hisia kinzani kuhusu ubaguzi wa kijinsia kwa wanawake katika jamii ya Buenos Aires.

Katika utafiti wake kuhusu uhusiano kati ya itikadi za kiuana na mgao wa kazi za nyumbani kwa wanaume na wanawake, Parveen (2012) anaangazia utaratibu unaozingatiwa kugawana kazi na kutekeleza majukumu ya kiuana kati ya wanaume na wanawake nyumbani. Utekelezaji wa majukumu hayo unahusisha itikadi za dini na utamaduni pamoja na uchaguzi na utekelezi wa majukumu ya kijinsia. Ugawaji wa kazi za nyumbani aidha unaegemea itikadi ya mfumodume ama itikadi ya usawa kulingana na dini au utamaduni. Parveen anagundua kwamba mabadiliko ya usawa katika itikadi ya kidini na kitamaduni wa Kisikh unachangia mtazamo wa usawa wa kidini na kiutamaduni wa Wasikh. Ilibainika pia usawa wa kidini na kiutamaduni katika jamii ya Waskh haujachangia sana usawa katika majukumu ya kiuana kama yanavyobainika katika uchaguzi wa majukumu ya kijinsia. Utafiti wake Parveen ni muhimu kwa sababu unadokeza kuhusu dhana ya itikadi namna inavyoweza kuathiri mtazamo wa usawa. Suala hili linahusiana na itikadi za kiuana namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana ambalo utafiti huu unachunguza. Kwa upande mwingine, utafiti wa Parveen anaangazia juu ya kugawana kazi na kutekeleza majukumu ya kiuana kati ya wanaume na wanawake nyumbani tofauti na utafiti huu ambao unachunguza itikadi za kiuana zinavyoendelezwa kwa ukubalifu katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Connell (2009) anachunguza itikadi za kiuana zenye misingi ya ubabedume ambapo anatambua amali za kijamii zinazompa mwanamume nafasi muhimu na kuonyesha namna mwanamume huyo anashikilia nafasi hizo ilihali mwanamke ana nafasi duni. Connell anaeleza kuhusu majukumu muhimu ya kifahari ambayo mwanamume hujirundikia dhidi ya mwanamke ambaye majukumu yake ni ya

kiutwana. Katika baadhi ya jamii hasa za Kiafrika, ubwana wa mwanamume umemshinda nguvu mwanamke mpaka akakubali hali yake duni. Katika kazi yake Connell hata hivyo hachunguzi mahusiano ya kiuana na kuonyesha ukinzani wa itikadi za kiuana unaoibuka katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Ni katika muktadha huu utafiti huu umetafitia itikadi za kiuana kuhusu amali za kijamii katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Cuddy wa wenzake (2010), wao wameshughulikia namna utamaduni unavyoendeleza dhana gande kuhusu uana. Cuddy wa wenzake wanatambua kwamba, dhana gande za kiuana si za kilimwengu bali zinadhibitiwa na utamaduni wa jamii mahsusi. Inaaminiwa wanaume wana sifa ambazo zinathaminiwa sana na utamaduni. Hali hii inatokana na jamii za Kiafrika ambazo zimejengeka kwenye msingi wa mfumo dume. Maoni haya yanawekea utafiti huu msingi wa kuchunguza itikadi za kiuana ili kubainisha mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake kupitia methali za Kinyankole na Kiswahili. Ingawa, kazi yao inajihusisha na dhana gande za kiuana. Kazi yao ni tofauti na utafiti huu unaojikita kwenye itikadi za kiuana. Kunabainika pengo la kitaaluma kwa sababu dhana za itikadi za kiuana na dhana gande za kiuana kimsingi ni tofauti. Pengo hilo linazibwa na utafiti huu.

Jonathan (2009) katika uchunguzi wake kuhusu suala la itikadi za kiuana, anachunguza jinsi mabadiliko ya maisha katika ndoa, malezi na kazi, yanavyosababisha mabadiliko ya itikadi za kiuana za mtu binafsi. Katika utafiti wake wa kisoroveya anagundua kwamba, ndoa, malezi, kazi, mingoni mwa mambo mengine yanaathiri itikadi za kiuana. Utafiti wake unadhihirisha zaidi

kwamba itikadi za kiuana zinabadilika, na maisha ya mtu anayopitia, ni chanzo muhimu cha mabadiliko. Mabadiliko hayo yanategemea maisha ya mtu. Katika utafiti wake anafafanua jinsi mkabala dhanishi unavyosaidia kuelewa ujengaji wa itikadi za kiuana kwa kudhihirisha tofauti muhimu ambazo hazikushughulikiwa na tafiti za awali. Jonathan analenga uhusiano uliopo kati ya mabadiliko katika tajriba za maisha na mabadiliko ya mtu binafsi ya itikadi za kiuana. Jonathan anaendelea kusema kwamba, itikadi za kiuana zinabadilika baada ya muda fulani. Mabadiliko haya, watu binafsi wanapitia mazingira mapya ya kijamii kupitia ndoa, malezi na kutunza watoto pamoja na kutekeleza majukumu, ambayo yanawaelekeza kwa matarajio ya kiuana. Maoni yake yanaongoza utafiti huu katika kuainisha itikadi za kiuana zinazotokea na namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa wanawake na wanaume katika methali, suala ambalo halishughulikiwi na tafiti za awali. Mbali na maoni yake Jonathan kuelekeza utafiti huu, katika kazi yake hazingatii imani na mitazamo ambayo ni kiini cha itikadi za kiuana. Utafiti huu unajikita katika imani za Wanyankole na Waswahili pamoja na mitazamo yao, jamii ambazo zina amali, imani na mitazamo tofauti kiitikadi kuhusu uana na jamii ya Kimarekani aliyotafitia.

Theodore (1996) amechunguza kuhusu kushiriki kwa wanaume katika kazi za nyumbani na athari zake za kiuana. Katika utafiti wake anaangazia mtagusano wa wake na waume zao ili kuweza kuelewa namna ugawaji wa kazi unavyoibuka. Theodore alidadisi zaidi iwapo itikadi za kiuana za wanawake na wanaume zinachangia kugawa majukumu ya kiuana kwa wanandoa kiutamaduni. Anagundua kwamba namna mtu anavyotekeleza majukumu yake ya kindoa na kifamilia kiutamaduni, yana uhusiano na mgao wa kazi za nyumbani. Kazi yake

ni muhimu kwa kazi hii kwa kuwa inaelekeza katika kufahamu zaidi itikadi za kiuana zinavyoathiri mahusiano ya wanaume na wanawake. Pamoja na kushughulikia suala la itikadi za kiuana katika utafiti wake, anajikita kwenye mitazamo ya waume kuhusu kushiriki kwao katika kazi za nyumbani kuwa kunaathiriwa na itikadi za kiuana za mwingiliano wa wake na waume. Anapuuza mahusiano mapana ya wanaume na wanawake, suala ambalo linachunguzwa katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Utafiti mwingine kuhusu itikadi za kiuana, umefanywa katika uwanja wa dini, imani kuhusu majukumu ya kiuana na utamaduni wa kundi la Waislamu wa kiume wenye usuli tofauti wa kiutamaduni huko Marekani. Utafiti huo umetathmini jambo hili kuhusu itikadi za kiuana za wanaume wa kiislamu wa Kimarekani (Bagheri, 2012). Washiriki katika utafiti huu walikuwa Waislamu wa kiume wenye umri kati ya 21 na 49. Bagheri aligundua kwamba, wanaume wa Kiislamu wanaamini mafundisho ya dini kuhusu suala la uana. Ingawa hawangeweza kufasiri maoni yao juu ya suala la uana katika misingi ya Qurani lakini walikiri kwamba imani zao kuhusu uana zinaungwa mkono na mafundisho ya kiislamu. Itikadi zao kuhusu uana zimebainika kwamba, wanawake ni viumbe dhaifu wa kimwili wakilinganishwa na wanaume; wanawake wana uwezo mkubwa katika malezi na utunzaji wa watoto. Utafiti unapendekeza kwamba wanaume na wanawake wapate elimu sawa. Ili kuweza kuruhusu mwingiliano huru kati ya wanawake na wanaume, majukumu ya mwanamke yasifungiwe kwa kazi za nyumbani; Uisilamu unakataza ukandamizaji wa mwanamke na wanafaa kuheshimiwa; kazi za nyumbani zigawanywe kati ya wanaume na wanawake. Utafiti wa Bagheri unatutolea mwanga kuhusu namna itikadi zinavyoelekeza

mgao wa majukumu ya kiuana, suala ambalo ni sehemu mojawapo ya mahusiano ya kiuana yanayoshughulikiwa katika utafiti huu. Utafiti wake unajikita kwa itikadi kuhusu majukumu ya kiuana na utamaduni wa Waislamu tofauti na utafiti huu unaochunguza kwa kina na mapana suala la itikadi za kiuana katika methali. Isitoshe, Bagheri anashughulikia imani zinazohusisha itikadi za kiuana kulingana na mila za  Kimarekani ambazo zinaoana na sharia za Marekani na mtafiti wa kazi hii anajikita kwa methali za utamaduni wa Kiafrika.

Katika kazi ya Allagbe na Amoussou (2020) wamebainisha jinsi nguvu za asasi za kijamii zinavyotumika kukubali itikadi za kiuana kama maarifa ya kawaida katika riwaya ya kifeministi ya kisasa ya. Allagbe na Amoussou wanaendelea kuonyesha namna  wanawake wanavyopinga kanuni za kiutamaduni na itikadi za kiuana zijulikanazo katika jamii kuhusu uana, ugawaji wa majukumu na mamlaka. Wanaonyesha kwamba mahusiano ya kiuana yenye usawa wa mamlaka kati ya wanaume na wanawake yanaweza kuhakikisha haki na amani katika jamii. Vilevile unathibitisha namna asasi za kijamii zinavyotumiwa katika kukubali  itikadi za kiuana. Kupitia matumizi ya lugha, wanaonyesha namna itikadi za ubabedume zinavyohakikiwa katika kazi za kinathari. Utafiti wa Allagbe na Amoussou ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu umetuelekeza kuhusu itikadi za kiuana zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana lakini katika kazi yao hawalengi suala la ukubalifu wa itikadi na vile zinachukulia mahusiano ya kiuana kama maarifa ya kawaida. Pia, katika kazi yao hawalengi suala la ukinzani wa itikadi za kiuana unavyotokea na vile ukinzani huo unavyoathiri usawa wa kiuana, suala ambalo tunalishughulikia katika utafiti huu.

Ikeke (2021) amechunguza kuhusu usawiri wa uana katika muziki wa kitamaduni wa Urhobo. Ikeke anagundua kwamba mitazamo na maisha ya wanawake hayatambuliki katika mijadala ya kifeministi. Ikeke anaendelea kusema kwamba, kuna tofauti za kimamlaka katika utamaduni wa kubagua wanawake, na wanaume wanakuwa katika nafasi zenye hadhi, kuwa na upendeleo wa haki kwa wanaume dhidi ya wanawake. Mahusiano yaliyopo kati ya wanaume na wanawake yanadhihirika karibu katika nyanja zote za amali za kiutamaduni. Katika utafiti wake anaonyesha kwamba nguvu za mfumodume zinasawiri wanawake kama viumbe wanyonge wakilinganishwa na wanaume. Kwamba, wanawake wanastahili kutii wanaume wakati wa kutoa na kutekeleza maamuzi katika jamii. Utafiti wake Ikeke haubainishi mahusiano ya kiuana kwa uwazi. Anaangazia itikadi za kiuana kwa kuongozwa na nadharia ya ufeministi iliyo na upendeleo katika kutetea maslahi ya wanawake na kutozingatia kwa makusudi itikadi kuhusu wanaume.

Ogunsina (1996) ametathmini usawiri wa wanawake katika ushairi wa Kiyoruba. Anasema kwamaba wanawake wananyanyaswa, wanateswa, na kudunishwa na utamaduni unaothamini utawala wa mfumodume katika fasihi simulizi. Anabainisha ubaguzi wa wanawake kwenye maeneo ya kazi kupitia fasihi simulizi. Kwamba, itikadi za kiuana zimejikita sana katika ngazi mbalimbali katika jamii pamoja na kuwa na athari hasi. Kazi yake Ogunsina imefaidi utafiti huu kwa sababu anatudokezea kuhusu itikadi za kiuana zinazobainika kwenye ngazi tofauti katika jamii. Hata hivyo, utafiti wa Ogunsina ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa haonyeshi kwa kina itikadi hizo ambazo zinabainika katika ngazi mbalimbali katika jamii na itikadi hizo vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana

kwa ukubalifu halikuwa lengo lake. Pia, anashughulikia itikadi za kiuana kuwa kuhusisha wanawake katika kubainisha jinsi wanavyonyanyaswa na kubaguliwa. Isitoshe, katika uchanganuzi wake halengi itikadi za kiuana namna zinavyoathiri usawa wa kiuana kwa kuchunguza wanaume na wanawake moja kwa moja. Vilevile anajikita kwa udhalilishaji wa wanawake, suala linalodhihirisha tofauti kati ya kazi yake na utafiti huu.

Hassan (2015) amechunguza mabadiliko katika majukumu ya kiuana miongoni mwa wanawake mkoani Garissa nchini Somalia. Katika kazi yake Hassan anatambua kwamba majukumu ya kiuana ni matarajio ya kitamaduni ya wanaume na wanawake katika jamii kuhusu uwezo wa ‘kimaumbile’ wa wanaume na wanawake, kazi zinazochukuliwa kuwa mwafaka kwa wanaume na wanawake pamoja na tofauti za sifa na tabia kati ya wanaume na wanawake. Ameonyesha kwamba, kuna mabadiliko na uhuru wa utekelezaji wa majukumu ambayo yana mizizi yake katika mabadiliko ya jamii. Pia, Hassan ameonyesha kwamba katika familia kulikuwa na utenganishaji wa majukumu, wanawake wakishughulikia majukumu ya nyumbani na wanaume wakitoka nje kushughulikia utafutaji wa riziki. Anahitimisha kwamba mabadiliko ya kimajukumu ni jambo la kawaida. Wanawake wanachukua majukumu muhimu katika kufanya maamuzi nyumbani na kufanya kazi za kuongeza kipato cha familia. Utafiti wa Hassan umechangia utafiti huu katika kuelewa majukumu ya kiuana vile yanavyotokea katika kazi nyingine na namna yanavyobadilika. Huu umekuwa mwongozo wa kuchunguza methali za kiuana zinazoibua ukinzani wa itikadi za kiuana zijulikanazo kitamaduni kati wanaume na wanawake ili kubainisha mabadiliko hayo. Hata hivyo, kazi yake Abdi ni tofauti kwa sababu

kazi hii inachunguza itikadi za kiuana vile zinavyotokea na kuendeleza mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Murithi, (2017) amechunguza dhana ya itikadi katika riwaya za S. A Mohamed. Anasema kwamba itikadi ni dhana inayobadilika na ina mielekeo tofauti. Anaendelea kusema kwamba, itikadi kama imani za watu zina nguvu za kuwashawishi na kupata fikira na mielekeo katika uzoefu wa tabia na matendo yao ya kawaida na hatimaye kuganda akilini mwao. Mambo haya huchukuliwa kuwa ya kawaida. Mawazo ya Murithi yanapatia mwanga utafiti huu kuchunguza vipi mahusiano ya kiuana yanaendelezwa na hali ya ukubalifu na ushawishi na kuchukulia mahusiano hayo kuwa sehemu ya maumbile yao na ya kawaida katika jamii. Isitoshe, katika uchunguzi wake Murithi anatambua aina mbalimbali za itikadi; Itikadi kuhusu dini, itikadi kuhusu ndoa, itikadi za mfumo dume na kudunishwa kwa mwanamke katika riwaya. Kazi yake ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu inatoa mdokezo kuhusu aina za itikadi. Kwa njia hiyo, kazi yake inaongoza kuhusu ubainishaji wa itikadi mbalimbali za kiuana kulingana na mazingira yanayozunguka wanaume na wanawake na vile zinavyoathiri usawa wa kiuana. Fauka ya hayo, utafiti wake umefaidi kazi hii katika kubainisha mahusiano ya kiuana yanavyoathiriwa na hali ya ukubalifu na kushawishika kwa njia tofauti na kudhihirisha jinsi mahusiano hayo yanavyochukuliwa kuwa sehemu ya maumbile na ya kawaida katika jamii. Hata hivyo, kazi hii inatofautiana na kazi ya Murithi kwa sababu yeye halengi itikadi za kiuana katika kazi yake, suala ambalo ni kiini cha utafiti huu. Pia, ameshughulikia itikadi za kiuana kwa kuangazia itikadi ya mfumodume kama mojawapo ya itikadi inayobainishwa na mtunzi wa *Riwaya Za Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi*

*Yangu* (2013), kwa kuangazia mwanamke kuchorwa kwa uzuri na ubaya na pia kudunishwa kwa mwanamke, ilhali utafiti huu unachunguza kwa kina itikadi za kiuana zinazotokea na kuendelezwa kwa njia ya ukubalifu na kuonyesha ung'amuzi potofu wake katika methali.

Ogutu na wenzake, (2020) wamehakiki itikadi na uwezo wa kijinsia katika nyimbo za Taarab za Daktari wa Mapenzi na VIP zilizoimbwa na Mzee Yusuf katika bendi ya Jahazi Modern Taarab nchini Tanzania. Wamelenga ufafanuzi wa matumizi ya lugha katika nyimbo hizo kuonyesha mahusiano ya uwezo kati ya mwanamke na mwanamume katika jamii.Wamejadili namna itikadi inavyonyima mwanamke uwezo wa kutekeleza majukumu sawa na mwanamume. Ogutu na wenzake wanaonyesha kwamba itikadi inaathiri binadamu jinsi anavyotumia lugha katika kuonyesha mahusiano ya mamlaka. Utafiti wao umekuwa na mchango kwa utafiti huu katika kuelewa mahusiano ya uwezo kati ya mwanamke na mwanamume katika jamii. Hata hivyo, utafiti huu ulishughulikia itikadi za kiuana jinsi zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa kina kwa njia ya ukubalifu katika methali za Kinyankole na Kiswahili, tofauti na utafiti wa Ogutu na wenzake ambao wanachunguza matumizi ya lugha katika kuonyesha usawiri wa mwanamke.

Katika utafiti wake Murithi (2018) anaonyesha kwamba itikadi huwa tofauti kulingana na vipindi tofauti. Anagundua haya katika utafiti wake wa uhusiano wa itikadi na mtazamo wa mtunzi. Mawazo ya utafiti wake yalifaidi utafiti huu kwa kutuwezesha kugundua itikadi za kiuana mbalimbali zinazotokea katika methali za Kinyankole na Kiswahili kuhusu mahusiano kati ya wanaume na wanawake.

Ingawa kazi yake ni tofauti na hii. Murithi amelenga kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na mtazamo wa mtunzi kwa kurejelea riwaya za Said A. Mohamed na utafiti huu unashughulikia itikadi za kiuana vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Lukamika na wenzake (2019) wamechunguza tamathali za semi zinazosawiri ubabedume katika majigambo ya miviga ya shilembe na mchezasili wa mayo ya Waisukha, nchini Kenya kwa mtazamo wa semantiki. Wamejadili ubabedume katika majigambo ya miviga ya Shilembe na mchezasili wa Mayo katika jamii ya Waisukha. Wamehakiki tamathali mbalimbali za semi ambazo ni pamoja na chuku, jazanda na majazi ili kudhihirisha namna zinavyosawiri ubabedume. Wanaonyesha kuwa lugha ya majigambo inayoghaniwa na fanani hubeba tamathali za semi zinazosawiri ubabedume. Pia wanatambua kuwa, lugha hutumiwa kwa njia isiyo sahihi katika jamii kuwatukuza wanaume na kuwapa uwezo na mamlaka dhidi ya wanawake. Kwamba ubabedume umejengwa katika mila, itikadi na utamaduni wa jamii. Utafiti wake Lukamika na wenzake umemfaa mtafiti katika kuelewa baadhi ya itikadi za kiuana, vile lugha inaweza kutumwa kwa njia isiyo sahihi na kutudokezea jinsi itikadi tofauti zinajengwa katika mila na tamaduni. Kwa upande mwingine tofauti na utafiti huu, Lukamika na wenzake wao wanashughulikia itikadi ya ubabedume katika majigambo ya miviga na halengi itikadi za kiuana mbalimbali. Mtafiti katika kazi hii amechunguza itikadi za kiuana katika methali na namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa njia ya ukubalifu. Isitoshe utafiti wake unalenga tamathali mbalimbali za semi katika kudhihirisha ubabedume, tofauti na utafiti huu ambao umelenga kipengele cha methali katika kudhihirisha itikadi za kiuana.

Sengo (1988) kaika utafiti wake kuhusu itikadi na maendeleo ya jamii, anaainisha itikadi kuu za Waswahili. Itikadi hizo zinajumuisha dini na imani kuhusu maadili miongoni mwa nyingine. Katika kazi yake, anahitimisha kwamba, itikadi na imani za watu zina nafasi kubwa katika kuathiri maisha na maendeleo yao. Itikadi hizi ni taashira za utamaduni wao na ishara za nafsi zao wakitarajia upendo, furaha, amani, subira na nidhamu huria. Utafiti huu umenufaika kutokana na utafiti wa Sengo hasa kwa kuainisha baadhi ya itikadi kuu za Waswahili na msingi wa itikadi hizo. Pamoja na hayo, Sengo anadokeza kuhusu mchango wa itikadi katika kuathiri maisha ya watu. Mawazo haya yanafaa zaidi katika utafiti huu kuweza kubainisha itikadi za kiuana vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake. Utafiti wa Sengo kwa upande mwingine ni tofauti na huu kwa sababu katika utafiti huu kunashughulikiwa itikadi za kiuana na namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana pamoja na ukinzani wa itikadi za kiuana unavyoathiri usawa wa kiuana. Nia ya utafiti wake Sengo ni kujaribu kuonyesha itikadi zilizo hai na umuhimu wa itikadi hizo katika maisha ya kila siku ya Mswahili. Isitoshe, utafiti wa Sengo umekuwa wa kiujumla sana na amechunguza jamii moja ya Waswahili, tofauti na utafiti huu ambao umejikita katika kipengele cha itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili katika jamii za Wanyankole na Waswahili.

Wanyenya (2020) amechunguza kuhusu matumizi ya lugha za Kiafrika kuelekeza wasichana katika masuala ya ndoa. Yeye Wanyenya anasema kuwa lugha za Kiafrika huwa zinafanya kazi kubwa sana ya kuelimisha wasichana mambo ya ndoa. Wanyenya ameeleza jinsi wazazi wanavyotumia lugha katika shughuli ya

kuelekeza watoto wa kike katika kudumisha ndoa zao. Amerejelea ndoa za kijadi katika jamii ya Wamasaaba nchini Uganda. Katika kazi yake, Wanyenya anazingatia matumizi ya semi mbalimbali. Anasema kwamba matumizi ya lugha yalidhamiria kukuza watoto wa kike ambao wangevumilia katika ndoa. Ndoa katika mazingira ya Waafrika inathaminiwa kwa sababu ya kuwa mojawapo ya njia za utajiri kutokana na mahari yanayokuwa yakitolewa kwa wazazi. Kazi hii imefaidika na utafiti wa Wanyenya kwa kutoa mwanga vile matumizi ya lugha inavyoathiri mahusiano ya kiuana kupitia asasi ya ndoa. Aidha, kazi yake inaelekeza katika utambuzi wa itikadi mbalimbali zilizo na misingi yake katika jamii ya Kiafrika kuhusu mahusiano ya kiuana. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa sababu unachunguza itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana ndoa ikiwemo, jambo ambalo halengi na habainishi katika utafiti wake. Isitoshe, matumizi ya lugha/semi katika kudumisha ndoa halirejelei kama suala la itikadi inayokubaliwa kutokana na ushawishi katika jamii.

Katika utafiti wake Momanyi, (1998) ameshughulikia usawiri wa mwanamke Mwislamu katika jamii ya Waswahili, alilenga kuhakiki tungo za Washairi teule ili kutambua usawiri wa mwanamke kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi – nafsia katika mtazamo wa kike. Utafiti huo unabainisha udhalilishaji wa mwanamke kama kifaa, kutumikia mwanamume, nafasi ya utegemezi, kutoshiriki katika kuzalisha mali miongoni mwa mengine. Utafiti wa Momanyi umechangia kazi hii katika kubainisha amali na utamaduni wa Waswahili kuhusu suala la uana. Hata hivyo, utafiti huu haudhamirii kuchunguza usawiri wa mwanamke. Utafiti umejikita kwa kuchunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili katika kubainisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu, kutathmini

ukinzani wa kiuana na jinsi ukinzani huo unavyoathiri ugawaji wa majukumu ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Kobia, (2008) amefanya utafiti kuhusu taswira za kiuana katika nyimbo za Tohara za Wanaume miongoni mwa Waigembe. Kobia amechunguza wanaume wa Waigembe katika nyimbo zao za jando, Itikadi za kiuana zimefafanuliwa katika muktadha wa kurejelea jinsia ya kike. Ingawa utafiti wake unachunguza suala la uana, anajikita kwa kipengele cha taswira za kiuana katika nyimbo za tohara za wanaume kutathmini usawiri wa mwanamke kwa kutumia nadharia ya uana. Tofauti iliyopo kati ya kazi yake na na kazi hii ni kwamba utafiti huu umechunguza itikadi za kiuana kama zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana na kudhihirisha kuwa mahusino hayo yanayoendelezwa kwa ukubalifu ni ung'amuzi potoshi katika methali za Kinyankole na Kiswahili tofauti na taswira za kiuana katika nyimbo za tohara za wanaume miongoni mwa Waigembe.

## 2.2 Methali za kiuana

Methali ni usemi mfupi wa kimapokeo unaodokeza fikira au mafunzo mazito kwa muhtasari. Methali kama kipera cha fasihi simulizi, ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii yoyote ile. Miongoni mwa dhima za methali ni pamoja na ya kihistoria kwani kupitia sanaa hii, mila, desturi, kazi mawazo na utamaduni wa watu wa kale hufahamika miongoni mwa kizazi kipya. Mafunzo haya yanatokana na uzoefu wa maisha ya jamii fulani (Mulokozi, 2017). Mulokozi anadai kwamba, methali ni chombo cha itikadi. Anasema kwamba, hekima inayopatikana katika methali inaweza kuwa chanya au hasi kutegemea muktadha wa kijamii na kihistoria. Kipengele cha methali ni muhimu kuhusu uchunguzi wa

itikadi za kiuana. Methali ni kipera cha fasihi ambacho kinabeba itikadi za jamii fulani. Madai haya yanaungwa mkono na Lomotey (2019:327) ambaye anasema:

> 'Methali ziko na mchango mkubwa wa kuweza kuwasilisha na kuendeleza itikadi muhimu katika jamii'.

Methali zinabeba maisha ya wanajamii, matarajio, amali za kawaida na maadili ya watu katika jamii. Jambo la muhimu zaidi, methali zinawasilisha ukweli wa pamoja unaokubalika na wanajamii kwa njia ya kimafumbo (Kochman, 2020). Kwa hivyo, uhusiano huo wa karibu sana kati ya methali na amali za utamaduni wa jamii fulani ni jambo ambalo halipingiki. Methali ziko na nafasi kubwa na dhima ya kubeba utamaduni na kuwasilisha itikadi ya jamii (Oyaro, 2019). Methali zinaumba na kuunda sheria za utamaduni au kuelezea kila imani na kuonyesha tabia kwa njia ya kifasihi iliyo ya moja kwa moja (Finnegan, 1970). Isitoshe, katika methali, tajriba za binadamu zinabainika, zinaelezwa, zinachanganuliwa na kutoa mawazo ya jumla na kanuni za jamii kwa njia ya mkato.

Utafiti huu umelenga kutafiti itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Imedhamiriwa kubainisha itikadi za kiuana namna zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu kama Gramsci (1971 ) anavyodai. Wanawake wanakubali mahusiano yao ya kutawaliwa na wanaume, kutengwa na kudhalilishwa kama raia wa daraja la pili na kuwajibikia majukumu yao ya kike. Wanaume kwa upande mwingine, wanaendeleza mahusiano ya kimamlaka, kiuwezo, hadhi ya juu, kupewa kipaumbele pamoja na kuwajibikia majukumu yao ya kiume. Mahusiano hayo kati ya wanawake na wanaume yanachukuliwa kama ya kawaida kwa njia ya ukubalifu na kudhihirisha kuwa wanawake kama

kundi linalotawaliwa na wanaume wanaathiriwa na ung'amuzi potoshi (Althusser 1971). Suala hili limekuwa halijabainishwa wazi na tafiti za awali. Pia, methali za Kinyankole na Kiswahili zimehakikiwa kuonyesha namna zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana na kubaini iwapo ukinzani huu unabainisha mabadiliko katika mahusiano ya kiuana kati ya wanawake na wanaume kama Stock-Morton (1991) anavyodai. Aidha, imechunguzwa ni kwa namna gani ukinzani wa itikadi za kiuana unavyoathiri usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Methali kama kipengele cha fasihi na lugha zinatumiwa katika mawasiliano ya kila siku na mawasiliano hayo yanabeba itikadi tofauti za jamii (Haji, 2018). Katika utafiti wake Haji anaeleza kwamba methali zinawasilisha itikadi zinazodhihirisha mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke. Anabainisha mawazo haya katika utafiti wake kuhusu methali za jamii ya wamakunduchi akishughulikia vipengele vya dhamira, fani, miktadha ya matumizi na dhima. Mawazo haya yanachangia utafiti huu kwa kuwa utafiti wa Haji unatudokezea kuhusu mojawapo ya dhima ya methali ya kutumiwa katika mawasiliano ya kila siku na mawasiliano hayo yanabeba itikadi ambazo zinadhihirisha mahusiano ya kiuana. Kwa upande mwingine, utafiti wake ni tofauti kwani yeye alilenga kuchunguza dhamira, fani, miktadha ya matumizi na dhima ya methali za Kimakunduchi kwa jumla ili kubaini nafasi yake katika jamii ya Wamakunduchi na katika utafiti huu kunachunguzwa itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Schipper (1991) amewasilisha methali zinazowahusu wanawake. Katika utafiti wake anarejelea jamii mbalimbali za Kiafrika katika lugha zao asilia na nyingine zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiingereza. Anajaribu kuwasilisha picha kwamba, wanawake wanasawiriwa kwa njia hasi katika fasihi simulizi ya Afrika. Kazi yake ina utangulizi mfupi na haina uchanganuzi wa methali hizo. Katika methali zake anajikita kwa sura hasi za mwanamke na habainishi mahusiano ya kiuana kati ya mwanamke na mwanamume. Isitoshe kazi yake haizungumzii ukinzani wa itikadi za kiuana unaoibuliwa na methali za Kinyankole na Kiswahili. Tofauti na Schipper anayeangazia Afrika kwa jumla na anayewasilisha methali za jamii mbalimbali, utafiti huu umelenga methali za Wanyankole na Waswahili jinsi itikadi za kiuana zinavyobainika kwa uchanganuzi wa kina na kujikita katika upeo mdogo wa kieneo.

Kochman-Haładyj (2020) katika utafiti wake amechunguza dhanagande za kiuana katika methali za kiulimwengu. Anasema kwamba taswira za wanawake zinabainika wazi wazi katika methali. Anadhihirisha kwamba dhamira za hadhi na majukumu ya wanawake zinachukua nafasi muhimu katika methali nyingi za kiuana katika kuonyesha taswira za wanawake. Kochman-Haładyj anaendelea kusema kwamba, methali hizo zinawasawiri wanawake kwa mtazamo hasi ulimwenguni. Pia, anachunguza na kutambua kundi la methali zinazothamini wanawake na kuwasawiri kwa njia iliyo chanya kwa mfano wanawake kama akina mama. Anatutolea mfano wa methali;

‘Mungu hangeweza kuwa kila mahali, kwa hivyo akaumba akina mama. UK.77

Methali za kiulimwengu ambazo zinasawiri wanawake wenye sifa ambazo wanaume wanataka na kutamani kwa mfano methali;

Mke mzuri na afya njema ndio utajiri bora wa mwanamume. UK. 78.

Utafiti wake Kochman-Haładyj umeongoza utafiti huu kwa kuchunguza suala la uana katika methali. Isitoshe, anashughulikia methali zinazothamini wanawake na kuwasawiri kwa njia iliyo chanya, suala ambalo tunaangazia pia katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa sababu unachunguza itikadi za kiuana katika methali wala si dhanagande. Pia, utafiti huu unachunguza ukinzani wa itikadi katika methali kwa kuangalia wanaume na wanawake tofauti na Kochman-Haładyj ambaye anashughulikia methali zinazothamini wanawake na kuwasawiri kwa njia iliyo chanya.

Rasul (2015) amehakiki namna mahusiano ya kiuana kuhusu mamlaka kati ya jinsia tofauti yanavyoendelezwa katika methali za Kiingereza na Kiurdu kwa kuonyesha jinsi wanawake wanavyosawiriwa. Anaendelea kulinganisha kama taswira za dhanagande kuhusu wanawake zinafanana katika methali za Kiingereza na Kiurdu. Kazi yake imenufaisha utafiti huu katika kuchunguza mahusiano ya kiuana. Utafiti wake kwa upande mwingine ni tofauti na huu. Katika kushughulikia suala la mahusiano, Rasul anaangazia dhanagande katika kuhakiki mahusiano ya kimamlaka tu ilhali katika utafiti huu kunachunguzwa itikadi za kiuana katika methali. Anaendelea kulinganisha kama taswira za dhanagande zinafanana katika methali za Kiingereza na Kiurdu na utafiti huu haulinganishi bali unabainisha itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Katika utafiti wake Mubarok (2017) ameangazia usawiri wa wanawake katika methali za jamii ya Wasundane magharibi mwa Java nchini Indonesia. Amelenga kuchunguza maoni ya kitamaduni kuhusu mitazamo na majukumu ya wanawake pamoja na kugundua uhusiano uliopo kati ya lugha, uana na utamaduni. Ifahamike kwamba, maoni ya kitamaduni yanajikita katika dhana pana ya itikadi, ambayo tunachunguza. Kwa hivyo, ni muhimu kuchunguza maoni ya kitamaduni kwa undani ili kuweza kubainisha itikadi halisi zinazoelezwa katika methali za Kinyankole na Kiswahili vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana. Mubarok ameweza kuongozwa na nadharia ya Uchanganuzi usemi wa Kifeministi katika kufikia malengo ya utafiti wake. Anabainisha kwamba wanawake wanasawiriwa katika methali za Kisundane kama wanaoendeleza utiifu na kuwa vyombo vya mapenzi. Anahitimisha kwamba, methali za Kisundane zinasawiri wanawake kwa njia maalumu kimaksudi ambazo si sahihi, njia zinazoweza kufasiriwa kama dhalilishi. Utafiti huu kwa upande mwingine unachunguza mahusiano ya kiuana kama yanavyoendelezwa na itikadi kwa kuzingatia methali za wanawake na wanaume.

Zheng (2018) ameshughulikia chanzo cha ujinsia katika methali za Kiingereza. Anasema kwamba, methali ni kipengele muhimu cha lugha ya Kiingereza katika muktadha wa kiutamaduni na kijamii. Anachunguza vipengele vya tabia, ndoa, hadhi ya kijamii miongoni mwa vingine ili kubainisha ubaguzi wa kiuana dhidi ya wanawake katika matumizi ya lugha. Anagundua kwamba, ubaguzi wa kiuana kwa misingi ya kijinsia upo katika methali za Kiingereza. Vile vile anasema kwamba maoni ya kitamaduni kuhusu wanawake yanabadilika, hali

inayosababishwa na ustaarabu katika jamii. Hadhi ya wanawake imeinuliwa kwa njia iliyo chanya na baadhi ya mitazamo hasi kuhusu wanawake inakufa. Utafiti wa Zheng umetufaa katika utafiti wetu kwa kuonyesha itikadi za kiuana zinavyobadilika katika jamii ikilinganishwa na vile zinaelezwa katika methali, hata ingawa Zheng anajikita kwenye mabadiliko yanatokea kuhusu hadhi na nafasi ya wanawake katika jamii. Utafiti huu unashughulikia ukinzaini wa kiitikadi katika methali na vile ukinzani huo unavyoathiri usawa wa kiuana, suala ambalo halishughulikiwi kwa kina kuhusu wanaume na wanawake.

Ndungo (1998) amechunguza usawiri wa mwanamke katika methali za Kikuyu na Kiswahili. Katika utafiti wake amezingatia wanawake na usawiri wao kimajukumu, kitaswira katika maeneo ya Mombasa, Malindi, Lamu na Zanzibar pamoja na maeneo ya Kikuyu. Katika utafiti wake Ndungo anaonyesha kwamba mwanamke ana majukumu zaidi yanayomkandamiza na kumnyima hazi zake za msingi. Nafasi hii ambayo mwanamke anashikilia inachangia udhalilishaji wake. Ndungo anafikia matokeo hayo kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika. Utafiti wa Ndungo ulinufaisha kazi hii katika kuchunguza namna methali zinavyoendeleza majukumu kama sehemu ya mahusiano mapana ya kiuana kwa wanawake na wanaume. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kidhamira kwa sababu umechunguza itikadi za kiuana vile zinatokea na kudhihirisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na kuonyesha mahusiano hayo kuwa ni ya ung’amuzi potoshi. Utafiti umetekeleza suala hili kwa kuangazia methali za wanaume na wanawake za Kinyankole na Kiswahili. Vile vile utafiti huu umetathmini jinsi ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili unavyoathiri usawa wa kiuana, tofauti na Ndungo aliyetafitia taswira za

wanawake huku akionyesha majukumu maalumu wanayoshikilia katika jamii ambayo yanachangia udhalilishaji wao. Taswira za wanawake katika utafiti wa ndungo haziwezi kukamilisha suala zima la itikadi za uana kwa kuacha nje wanaume, suala ambalo linashughulikiwa kwa kina.

Webster (1982) amechunguza kuhusu masuala ya wanawake na ndoa katika methali za Morocco ambapo utamaduni wao umeshikana na dini ya Kiislamu. Katika utafiti wake anashughulikia upande wa kiume katika jamii ya Wamorocco. Anagundua kwamba mbali na methali kuwa na dhima ya kuakisi maisha, ziko na mchango mkubwa katika maisha ya jamii. Anasisitiza umuhimu wa kipengele cha muktadha katika kutafitia methali. Mawazo yake yanatufaa katika utafiti huu katika kuchunguza itikadi za kiuana katika jamii za Wanyankole na Waswahili kwa kuzingatia muktadha wa tamaduni kupitia methali zao na kubainisha mahusiano ya kiuana.

Katika utafiti wake Maitaria (2012) akishughulikia dhima ya methali katika kuainisha ushairi wa Kiswahili, anatambua kwamba methali hudhihirisha tajriba, mielekeo, itikadi na uhalisi wa maisha ya jamii. Maitaria anaendelea kwa kusema kwamba methali ambazo zinatumiwa katika mawasiliano ya jamii hujenga uhalisi wa mandhari ya kitamaduni katika jamii mahsusi. Hivyo, mielekeo mbalimbali ya kiuana imebainika hasa kuhusu mahusiano ya kiuana, tabia na itikadi za kiuana na jinsi itikadi hizo zinavyoathiri usawa wa kiuana. Hata hivyo, ingawa Maitaria alishughulikia kipera cha methali, utafiti wake ulichunguza uainishaji wa ushairi wa Kiswahili akizingatia dhima ya methali, tofauti na utafiti huu

ambao umetafitia itikadi za kiuana kama zinavyobainika katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

**2.3 Usawa wa kiuana**

Kwa mujibu wa Garrett (1987), tofauti za kiuana zinazojitokeza katika jamii nyingi, kimsingi zinasababishwa na utangamano wa kijamii ukiegemea tofauti za kiuana. Kulingana na Garret, tofauti za kiuana zinaigwa kuliko kurithishwa. Anaendelea kusema kwamba Uana ni sifa ambazo zinajitokeza kijamii na kisaikolojia. Sifa hizo zinahusishwa na ama kuwa mwanaume au mwanamke, yaani hali ya kiume na kike. Mawazo haya yamesaidia utafiti huu kuchunguza mahusiano ya kiuana yanayohusishwa na itikadi za kuwa ama wanaume au wanawake katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Akishughulikia utafiti wake kuhusu uana wa Kimarekani Traci (2008) anatambua kwamba wasomi duniani wanakubali kwamba utafiti kuhusu uana unaweza kuzalisha matokeo ya msingi kwa kutojifunga kwenye mawazo ya uana ya kimagharibi bali kwa kuzingatia mabadiliko na tofauti za tamaduni katika jamii mbalimbali. Utafiti wake unajikita kwa uana wa Kimarekani kwa kuchunguza uana katika elimukale. Kulingana na maoni haya, ni dhahiri kwamba hakuna uana wa kiulimwengu. Kila jamii ina mitazamo yake tofauti na nyingine kuhusu suala la uana. Kwa hivyo, mtafiti aliweza kuchunguza itikadi za kiuana na namna zinavyoathiri mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili katika jamii ya Wanyankole na Waswahili tofauti na utafiti wake Traci.

Abrams (2012) katika utafiti wake juu ya mitazamo ya wanawake wa Kimarekani wenye asili ya Kiafrika kuhusu athari za utamaduni kwa majukumu ya kiuana, ametathmini mitazamo ya kisasa ya wanawake kuhusu utekelezaji wa majukumu ya wanaume na wanawake. Amegundua kwamba maisha ya utotoni na utu uzima ya mwanamke yanaathiri na kuathiriwa na mitazamo ya kiuana katika njia mbalimbali kwa mfano katika kufanya maamuzi ndani na nje ya nyumbani, kazi, mafanikio na kufanya maamuzi kwa kujitegemea. Hata ingawa katika utafiti wake anashughulikia wanawake wa Kimarekani wenye asili ya Afrika kuhusu sula la usawa wa kiuana, maarifa haya yameelekeza utafiti huu kwa sababu athari za utamaduni wa Kiafrika zinaakisiwa kwa wanawake hawa. Pamoja na hayo, mitazamo kuhusu majukumu ni sehemu mojawapo ya mahusiano mapana ya mwanamke na mwanamume. Mahusiano ya kiuana yameendelea kudhihirika namna yanavyoakisi jinsi binadamu wanavyoingiliana katika mazingira yao, wanavyofanya maamuzi katika familia, uhusiano kati ya mume na mke, malezi, uamuzi binafsi, matamanio, mafanikio, tabia za kujamiana na mienendo ya binadamu kwa jumla.

Gower na wenzake (1996) wameangazia wanawake wa Waswahili kwenye mwambao wa Afrika mashariki. Katika utafiti wao wameeleza kwamba hadhi ya mwanamke katika jamii ya Waswahili inategemea nafasi yake katika jamii. Katika utafiti wao, wanaonyesha kuwa wanawake walikuwa na hadhi isiyobainika katika maeneo ya Uswahilini kwenye mwambao wa Afrika ya Mashariki katika karne ya kumi na tisa. Wanasema kwamba kuna wanawake waliodunishwa katika karne ya 19 na waliokuwa huru.  Wanawake kutoka tabaka lililotukuka walikuwa na mamlaka kuhusu mali ya nyumbani na walipata mali

kupitia ndoa, tofauti na wanawake kutoka katika miji midogo na vijijini. Ilikuwa ni kutokana na majukumu yao ya kuzaa na kupanua ukoo ambapo wanawake wenye tabaka la juu waliweza kupata mali kupitia kwa waume zao na kudhibiti shughuli za kila siku za nyumbani. Katika hali nyingine walikuwa na mamlaka hata kuliko waume zao katika masuala/ shughuli za nyumbani. Pia, anatuonyesha jinsi Emily Reute, binti Sayyid Said bin Sultan, alivyodhihirisha nguvu na mamlaka. Alitekeleza maamuzi muhimu kuhusu masuala ya utawala. Mbali na nafasi hii, wanawake wa tabaka hili walibaguliwa ndani ya familia zao na walikuwa wanajisitiri katika maeneo ya umma. Utafiti wa Gower na wenzake ulifaa huu katika kuchunguza ukinzani wa itikadi za kiuana pamoja na kuonyesha namna ukinzani huo unavyoathiri uaswa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Kelly (1999) katika utafiti wake kuhusu mabadiliko ya kiuana miongoni mwa wanaume na wanawake kwenye mwambao wa Waswahili anabaisha kwamba mahusiano ya kiuana kati ya mwanamke na mwanamume ni ya utengano kwa sababu ya utamaduni wenye usuli wa dini ya Kiislamu. Wanawake wana shughuli zao tofauti na za wanaume. Anatoa mifano ya shughuli za ngoma maalumu zinazochezwa na wanawake zinazotambulika kama ngoma za wanawake na ngoma za wanaume. Shughuli za wanaume ni kuwa msikitini, kuwa kwenye baraza wakinywa kahawa. Utafiti wake Kelly ni muhimu kwa kazi hii kwa sababu umeweza kubainisha mahusiano ya kiuana vile yanaendelezwa katika methali. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa vile mtafiti katika utafiti wake huu ameshughulikia ukinzani wa itikadi za kiuana namna unavyoathiri usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Utafiti wa Angella (2018) unahusu usawiri wa mwanamke katika kazi teule za fasihi na jinsi maandiko ya kidini yanavyomwangalia mwanamke katika jamii. Anachunguza kama kuna manufaa katika kukuza na kuujenga uhusiano madhubuti katika ndoa. Anachunguza suala hili kwa kurejelea Utendi wa Mwanakupona (1858), Utendi wa (Ayubu, 1723) na maandiko ya kidini ya 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' katika Biblia Takatifu, Agano la kale (1921). Katika utafiti wake, Angella analinganisha mwanamke anavyosawiriwa katika kazi hizi mbili za fasihi na maandiko matakatifu yanavyotarajia tabia na uhusiano wa mwanamke na mwanamume kuwa katika ndoa. Anaonyesha kwamba mwanamke kusimamia nafasi yake katika ndoa sio ukandamizaji bali ni utekelezaji wa majukumu yake katika ndoa. Utafiti wake una manufaa kwa utafiti huu vile suala la usawa wa kiuana linavyosawiriwa, kwamba mwanamke na mwanamume wanastahili kuishi pamoja licha ya changamoto na matatizo ya maisha. Angella anadhihirisha kuwa wosia katika Utendi wa Mwanakupona, taswira ya mwanamke katika Utendi wa Ayubu na matini ya kidini si ukandamizaji wa mwanamke bali ni njia ya kuujenga uhusiano mwema katika ndoa, jambo linaloafikiana na ukubalifu unaochunguzwa katika utafiti huu. Ingawa, utafiti wake ni tofauti kwa sababu hadhamirii kuchunguza itikadi za kiuana namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa mwanamke na mwanamume. Isitoshe, utafiti wa Angella haushughulikii ukinzani wa kiuana namna unavyoathiri usawa wa kiuana, suala linalozingatiwa katika utafiti huu.

Kimondiu (2019) ameshughulikia usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za jamii ya Wakamba. Amechunguza suala hilo katika nyimbo za Ngungu na

Muoi (Tasa na mchawi) wimbo wa Kakai Kilonzo, Nyinyina wa Ndetei (Mama wa Ndetei) wimbo wa Kijana Mumo, Kavola Kamengele (Polepole Kamengele) wimbo wa Ancent Munyambu, Nyinyia Wa Syana (Mama Watoto) wimbo wa Dickson Mulwa, Mother (Mama) na Kana Nzula (Mpenzi Nzula) za Bosco Mulwa, Aka (Wanawake) Justus Myello, Aka ma town (Wanawake wa mjini) Danny Mutuku, Aka ni ma mithemba (Aina mbalimbali za wanawake), Wanginga na Syoka mami (Rudi mama), John Muasa wala si methali. Kimondiu amelenga kuchunguza kama mwanamke anadunishwa katika nyimbo hizo ama anatetewa katika jamii dhidi ya imani dhalilishi za ubabedume. Anasema kwamba kudunishwa kwa mwanamke kunasababishwa na jinsia yake. Kimodu anatambua kwamba imani ya kudhalilisha mwanamke inajikita kwenye itikadi na tamaduni zinazosisitizwa na mfumo dume ambao unampa thamini mwanamume na kumdhalilisha mwanamke. Tofauti na utafiti wake, utafiti huu unaonyesha vipi itikadi za kiuana zinafanya mwanamke na mwanamume wanavyotwaa nafasi zao katika jamii kimahusiano kwa ukubalifu.

Katrina (2011) akitafitia wanawake wa Kizanzibari kuhusu suala la mapenzi, anagundua kwamba bibi arusi hana usemi wowote. Bibi arusi anakuwa tayari wakati wowote kutimiza haja za mume wake kimapenzi lakini hana nafasi ya kuzungumzia hisia zake kuhusiana na mapenzi. Katrina anaeleza zaidi kwamba wanawake wanatumia kanga kuwasilisha hisia zao za kimapenzi na ngono bila kuvunja maadili ya mwanamke katika uhusiano na suala la mapenzi. Kwa hivyo, wanawake hawako huru kuwasilisha hisia zao za mapenzi. Mume ndiye anayewekewa msisitizo kuwa na haki za kuridhishwa kimapenzi kwa upande mmoja na mke kuwa na jukumu la kuridhisha mume wake. Hakuna makubaliano

kati ya mume na mke kuhusu suala hili. Wanaume hawawekewi kanuni jinsi ya kufurahisha wake zao kimapenzi. Kwa hivyo, mazungumzo na mafunzo ya Waswahili kuhusu mapenzi na ngono yanalenga kutimiza haja za mume na kuegemea upande wake kuliko wa mwanamke. Utafiti wa Katrina umekuwa na mchango kwa utafiti huu katika kuchunguza usawa wa kiuana vile unaendelezwa katika jamii ya Kizanzibari. Ingawa utafiti huu unashughulikia suala la usawa kwa njia tofauti. Unachunguza suala la usawa kwa kuangalia namna ukinzani wa itikadi za kiuana unavyoathiri usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Thompson (2011) ameshughulikia utafiti wake kuhusu mchango wa wanawake katika kutoa mafunzo ya Kiislamu kwa bibi arusi kuhusu mapenzi ya ndoa za kisasa. Katika utafiti wake Thompson anaonyesha wanawake walio na mchango katika kuendeleza familia na jamii zao ambazo zimeathiriwa na mfumodume. Anaeleza kwamba wanawake wana mchango mkubwa kama walimu wenye taaluma, wanaotoa maarifa kwa misingi ya dini ya Kiislamu. Mawazo yake yanatofautiana na itikadi ambazo zimekuwepo kwamba wanawake wanatengwa katika nafasi za mamlaka katika dini ya Kiislamu (Momanyi 2001). Utafiti wake Thompson unadhihirisha nafasi ya mwanamke kama mtoaji wa maarifa yanayotegemewa na jamii. Utafiti wa Thompson umefaa utafiti huu katika kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili namna zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana kitamaduni pamoja na kutathmini jinsi ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili unavyoathiri usawa wa kiuana. Hata hivyo, utafiti wake haushughulikii ukinzani wa kiuana kwa kina. Anachunguza tu uwezo wa mwanamke wa kutoa mafunzo kwa bibi arusi

Stoeltje (2000) katika utafiti wake, amechunguza mabadiliko ya kiuana na uamilifu wa majadiliano katika mfumo wa kisheria katika jamii ya Asante. Stoeltje amebainisha kuwa wanawake wana mamlaka ya kuendeleza mashtaka mahakamani. Katika jamii ya Asante nchini Ghana, kesi zililetwa katika mahakama ya Malkia na uamuzi kufanyiwa humo. Mara nyingi kesi hizo zilisikilizwa na wanawake wawili. Katika utafiti wake Stoeltje anaeleza kwamba, mwanamke wa Asante anapopeleka mwanamume mahakamani, anamshtaki kirasmi na kueleza mashtaka yake wazi wazi. Mwanamke anapofanya hivyo, anapinga itikadi za kiuana zinazowapa hadhi wanaume. Anabadilisha uzoefu wa kuwadhalilisha wanawake na kubainisha mahusiano ya kimamlaka katika hali zao kama wanawake. Mawazo yake yamechangia uendelezaji wa utafiti huu katika kubainisha ukinzani wa itikadi za kiuana za kitamaduni ambazo zinatawaza wanaume kama wao ndio wanastahili kuwa viongozi.

Mwanamke ni kiumbe ambaye hawezi kujitegemea katika kufanya maamuzi akilinganishwa na mwanamume (Webster, 1982). Hali hii inaendelezwa na dhana ya uana katika jamii ya Morocco. Webster anadhihirisha hali hii katika utafiti wake kuhusu methali za wanawake katika jamii ya Morocco. Mwanamke inaaminiwa kwamba, akijikuta peke yake mahali fulani na mwanaume hataweza kujizuia kuingia katika hali ya kimapenzi. Mwanamke amekuzwa akiamini kutoka utotoni kwamba kumwona mwanamke hivi tu inatosha kumbadilishia hali mwanaume kimapenzi isipokuwa kama kunatokea vizuizi vya nje ambavyo vinavyoweza kumkataza kutimiza lengo lake. Hata ingawa Webster alikuwa anachunguza masuala ya kiuana katika methali za jamii ya Morocco, utafiti wa

kazi hii umenufaika na utafiti wa Webster kwa kurejelea mawazo yake kutafitia itikadi za kiuana kama zinavyobainika katika methali za Wanyankole na Waswahili.

Chanzo cha tofauti za kiuana katika jamii kinachochewa na migawanyiko ya kitabaka. Wanajamii walikuwa wakiishi maisha ya ujamaa. Mabadiliko yalipotokea kukazuka mfumo wa ubabedume ulioanza kutawala mahusiano yote ya jamii (Engles, 1975). Mfumo huu uliimarika wakati kazi za wanaume kama ufugaji zilianza kuleta faida kuliko za wanawake za nyumbani. Huu ulikuwa mwanzo wa mwanamke kutegemea mwanamume katika mahusiano yote ya kijamii hasa ya kiuchumi. Kwa kuhusisha maoni haya, mtafiti ameweza kuchunguza namna wanawake na wanaume wanavyoendeleza mahusiano ya kiuana na namna majukumu ya wanawake na wanaume yanavyoathiri usawa wa kiuana. Kwa upande mwingine, utafiti wa Engles haugusii suala la ukinzani wa itikadi za kiuana linavyoathiri usawa wa kiuana, suala ambalo pia linashughulikiwa katika utafiti huu katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Kelly (1999) katika kazi yake kuhusu mabadiliko ya kiuana kwenye mwambao wa Afrika ya mashariki na visiwa vya Kenya na Tanzania anaeleza kwamba, maandishi kuhusu wanawake wa Kiswahili yanaonesha nafasi yao ya kupeleka ajenda yao mbele miongoni mwa mazingira ya mfumo dume. Kauli kwamba wanaume mara nyingi wanashikilia nafasi ya hadhi kuliko wanawake, inawapa jukwaa wanawake kuungana na kupinga ubaguzi wao. Kelly anaendelea kutambua kwamba mahusiano ya kiuana ya Waswahili yamepitia mabadiliko mengi. Ni vigumu kukubali kwamba ubaguzi wa kiuana unaakisi mahusiano ya

kiuana ya kipindi kilichopita. Mtafiti ameweza kurejelea maoni ya Kelly katika utafiti wake katika kudhihirisha namna methali za Kinyankole na Kiswahili zinavyoibua mabadiliko ya itikadi za kiuana kwa njia ya ukinzani na jinsi mabadiliko hayo yanavyoathiri usawa wa kiuana.

Sengo (1985) anaeleza kwamba, majukumu ya wanawake kama yanavyowasilishwa katika hadithi ni ishara halisi ya maisha yao ya kila siku. Wanawake wanafanya kazi nyingi na nzito karibu katika jamii zote za Afrika. Msisitizo wa uchunguzi wake wa hadithi na muktadha wake wa jamii ya Unguja ni kiwakilisho mwafaka cha jamii ya Waswahili. Vile vile masuala anayogusia katika uhakiki wake yanahusu jamii nyingine za Afrika wakiwemo Wanyankole ambao wamechunguzwa katika utafiti huu. Maoni ya Sengo yamenufaisha utafiti huu kwa kushughulikia itikadi za kiuana katika kuangazia mahusiano ya kiuana kupitia methali za Kinyankole na Kiswahili.

Okpewho (1992), anaonyesha kwamba dhamana ya maisha ya mwanamke katika ndoa ni kuishi na mume na kuzaa watoto wengi. Anaeleza kwamba baadhi ya nyimbo za arusi zimetungwa kwa mtindo wa kushadidia nafasi ya mbele ya mwanaume dhidi ya mwanamke. Mila za kitamaduni za Kiafrika kama nyingine zozote, ziko kwenye msingi wa taasubi za kiume. Ingawa Okpewho anahakiki nyimbo za arusi za Kigisu, Wagisu, Wanyankole na Waswahili ni jamii za eneo kubwa la ukanda wa Afrika Mashariki. Tamaduni za jamii hizi zina ukuruba mkubwa kwa hivyo, utafiti wake umechangia utafiti huu katika kuchunguza jinsi itikadi za kiuana zinavyobainisha mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Hata hivyo, utafiti wa Okpewho ni tofauti na huu kwa

sababu utafiti huu unalenga kubainisha namna methali zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana zijulikanazo za kitamaduni na vile vile jinsi ukinzani huo wa itikadi za kiuana unavyoathiri usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Kirindi (2008), anaeleza kwamba mwanamke mwari katika ukoo wa Bahima miongoni mwa jamii ya Wanyankole kulingana na utamaduni wa Wanyankole, alikuwa anastahili kuwa mrembo sana; mwenye meno meupe, mwenye rangi yake asilia nyeusi, awe na nafasi ndogo kati ya meno yake ya mbele, ufizi wa meno mweusi, awe na miguu mikubwa, makalio makubwa na mwenye kimo kirefu. Kucha zote za vidole vya miguu ziwemo. Hastahili kuwa na kovu lolote kwenye mwili wake. Maelezo ya Kirindi yanaonyesha kwamba jamii ina imani kwamba mwanamke wa jamii ya Wanyankole anafaa kupendeza na kufurahisha mume atakayemuoa. Ingawa Kirindi anazungumzia sifa za mke aula kwa mume, itikadi kama hizi za kiuana zimekuwa hazibainiki namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana katika methali za Wanyankole na za Waswahili.

Wanaume na wanawake wanatengewa majukumu tofauti ambayo wanayakubali kwa sababu ya jinsia zao (Kirindi, 2008; Elam 1979; King’ei, 2000). Kwa hivyo limekuwa jambo muhimu kuchunguza itikadi za kiuana pamoja na mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Katika jamii ya Wanyankole na Waswahili, wanawake wana majukumu ya aina ya kipekee yakilinganishwa na ya wanaume. Hali hii inatokana na tamaduni za jamii hizi tangu zamani. Majukumu haya wanayahusisha na tofauti za kimaumbile (jinsia) jambo ambalo si sahihi. Majukumu hayo yanatengwa toka utotoni. Mfano “mwanamke ni jiko”

na ‘mwanamume ni kazi’ ni semi ambazo zimo katika jamii tayari. Kutokana na falsafa iliyomo katika maoni ya kutokana na matumizi ya lugha, mtoto wa kike anakua akijua kwamba miongoni mwa majukumu anayostahili kutekeleza ni pamoja na ya jikoni. Itikadi inayowasilishwa ni kwamba mtoto wa kiume naye atakuwa na majukumu yake ambayo jamii imemtengea. Bila shaka majukumu haya yamejitokeza kwa sababu ya tofauti za kiuana.

Mtajwa (2005), anatambua sifa zinazomtambulisha mwanamume. Mwanamume anatambulishwa na sifa ambazo ziko na msingi wa itikadi za kitamaduni. Sifa hizo hubainisha ubora, uwezo, nguvu, uhodari na uhayawani wa mwanamume, kielelezo chake cha mamlaka, utendakazi wa viungo vya uzazi, upenyezi wa dhakari, kuwa na uhusiano wa kingono na zaidi ya mke mmoja nje ya ndoa, ushari wa kimapenzi, sauti nzito miongoni mwa sifa zingine. Sifa hizi huchukuliwa kama sifa mwafaka zenye kumtambulisha mwanamume. Mtajwa anazidi kufafanua kuwa, dhakari hutumika kama chombo cha kumshusha hadhi mwanamke. Kwa sababu hii, dhakari ni asili ya “uanaume,” silaha ya kumwezesha mwanamume kuwa mshindi katika ushindani wa kijinsia. Itikadi hizi za kitamaduni kama anavyoeleza Mtajwa, zimetoa mwanga katika kuchunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili katika kubainisha namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana na kuonyesha vile itikadi hizo zinachukuliwa na jamii kwa ukubalifu na za kawaida.

Yitah, (2009) katika uchunguzi wake ameshughulikia mabadiliko ya kiuana katika methali za Kaskazini mwa nchi ya Ghana. Amelenga kuhakiki mitazamo ya kiuana, sifa na tabia za wanawake zinavyoendelezwa na wanawake wenyewe

wa kisasa katika methali za kitamaduni. Amechunguza kama wanawake hao wanabadilisha maana asilia katika methali za kitamaduni au wanatumia methali hizo kupinga na kuumbua itikadi za kiuana ambazo zinabagua wanawake katika methali za Kasena. Matokeo ya utafiti wake yanadhihirisha kwamba wanawake katika methali za Kasena wanapinga na kuasi matumizi ya kitamaduni ya methali zinazowadhalilisha. Pia, wanawake wanaibua maana mpya katika methali hizo za kitamaduni kwa kupinga maana asili za kitamaduni zinazoelekea kuwadhalilisha. Yitah anagundua kwamba, wanawake wanafasiri methali za kiuana kwa kuzipatia maana mpya. Maana hizo mpya zinapinga udhalilishaji na unyamazishaji wa wanawake ambao unabainika katika matumizi ya methali hizo hizo na wanawake. Utafiti wake Yitah umetoa mdokezo katika utafiti huu kwa vile amechunguza ukinzani katika methali. Hata hivyo, ukinzani anaoshughulikia katika utafiti wake unajikita kwa maana za methali zinazoibuliwa na wanawake katika kupinga udhalilishaji na unyamazishaji wao katika methali za kitamaduni zinazotawaza wanaume. Utafiti huu umeshughulikia methali namna zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana zijulikanazo kitamaduni katika jamii ya Wanyankole na Waswahili.

Kiyimba, (2005) ameshughulikia usawiri wa watoto wa kike na watoto wa kiume katika fasihi simulizi ya Baganda. Katika uchunguzi wake anajikita kwa vile mitazamo inavyoendeleza sheria za kitamaduni katika jamii ambazo zinasababisha watoto wa kiume na watoto wa kike kujiangalia kama waume na wake, wazazi, viongozi wa kisiasa na wamilikaji wa mali wakishakua. Kiyimba anatambua kwamba utofauti uliopo kuhusu mahusiano ya kiuana miongoni mwa jamii ya Baganda unajikita katika maisha ya awali ya watoto. Anashughulikia

suala hili kwa kuhakiki methali za Baganda kuonyesha imani mbalimbali zinazoendeleza utofauti wa mahusiano ya kiuana kati ya mtoto wa kike na mtoto wa kiume katika jamii. Katika kazi yake anahitimisha kwamba matatizo kuhusu dhanagande za kiuana kama zinavyobainika katika fasihi simulizi ya Baganda inatokana na maisha ya utotoni. Utafiti wa Kiyimba unafaidi utafiti huu katika kuchunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili vile anagusia imani kuhusu uana. Hata hivyo, kwa upande mwingine kazi hii ni tofauti na yake kwa sababu yeye anajikita kwenye utofauti wa mahusiano ya kiuana katika maisha ya awali ya mtoto wa kike na mtoto wa kiume ilhali utafiti huu unachunguza itikadi za kiuana kwa kina vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana kati ya wanawake na wanaume katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Hussein (2009) katika uchunguzi wake ameshughulikia namna itikadi za kiuana zinawasilishwa katika methali teule za Ethiopia, Kenya na Sudan. Anaonyesha kwamba kuna mwingiliano matini wa methali zinazosawiri wanawake. Anatambua kwamba, methali zinawasilisha dhanagande ambazo ziko na msingi wa mfumo dume katika kujenga suala la uana. Utafiti wake umemfaa mtafiti katika kuchunguza itikadi za kiuana jinsi zinavyobainika. Ingawa utafiti wa Hussein ni tofauti na huu kwa sababu suala la itikadi analiendeleza katika muktadha wa dhanagande na mtafiti katika kazi hii anachunguza itikadi za kiuana kama imani zinazokubalika na kuendelezwa katika jamii ya Wanyankole na Waswahili vile zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana.

Uchambuzi wa yaliyoandikwa yenye uhusiano na mada ya utafiti, umedhihirisha pengo ambalo linashughulikiwa katika utafiti huu. Kupitia uhakiki huu imebainika kuwa itikadi za kiuana katika kudhihirisha mahusiano ya kiuana kati ya wanawake na wanaume kwa ukubalifu na ushawishikaji ni jambo ambalo limekuwa halijashughulikiwa moja kwa moja. Nyingi ya tafiti hizi zimeshughulikia usawiri wa ama wa mwanamke au wa mwanamume katika methali za jamii za watafiti. Tafiti nyingine zimeshughulikia usawiri huo katika tanzu mbalimbali za fasihi kama vile riwaya, tamthilia, nyimbo na tenzi. Utafiti huu umejikita kwa kuchunguza itikadi za kiuana na kuonyesha jinsi itikadi hizo zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ashawishi. Aidha, utafiti huu umehakiki methali na kuibua mikinzano ya kimaana na athari zake kwa usawa wa kiuana katika methali Kinyankole na Kiswahili. Mtafiti amefanya hivyo kwa kuibua maana mbalimbali za kiitikadi kulingana na nadharia ya udenguzi.

## 2.4 Misingi ya nadharia

Nadharia ambazo zimeongoza utafiti huu ni zifuatazo: Nadharia ya Itikadi kwa mujibu wa Gramsci (1971) na Althusser (1981); Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa kuongozwa na mawazo ya Steady (1981) pamoja na Nadharia ya Udenguzi (Derrida, 1976). Hivyo, utafiti huu umeongozwa na nadharia tatu. Nadharia hizo zimeelekeza utafiti huu katika kupitia maandishi yenye uhusiano na mada, ukusanyaji na uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo na hatimaye kuhitimisha utafiti. Pia, zilituongoza katika kutimiza malengo ya utafiti.

### 2.4.1 Nadharia ya Itikadi

Kwa mujibu wa Kennedy (1979) dhana ya itikadi ilianzishwa na Antoine Destutt de Tracy (1796). Mtaalamu huyu alijaribu kudhihirisha jinsi ya kutambua mawazo kutokana na ufahamu na mtazamo wa mtu binafsi (Oxford, 2021). Alianzisha sayansi ya mawazo ambayo hatimaye yaliibuka kuwa itikadi. Dhana hii baadaye iliendelezwa na Karl Marx (1818 – 1883), ambaye aliipatia dhana hii maana mpya na kuanza kutumiwa kuchunguza mitazamo kinzani ya kisiasa, maoni na fikra za makundi ya jamii. Mawazo yake yalipata upya kwa kushughulikiwa na wasomi wa Shule ya Frankfurt hasa Antonio Gramsci (1985) na Louis Althusser (1981). Mawazo yao yalisababisha nadharia hii kupata sura mpya na uamilifu katika masula kadhaa yakiwemo na masuala ya uana kulingana na mpito wa wakati.

Nadharia ya Itikadi inalenga kubainisha utawala unaojikita kwenye ugawaji wa jamii kwa matabaka. Uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii. Wanaitikadi wanasema kwamba kugawanyika kwa tabaka tawala na wanaotawaliwa ni matokeo ya imani zinazotengenezwa na watu. Imani hizi zinalenga kukidhi mahitaji ya mfumo wa kiuchumi kwa kuyachukulia mawazo ya kiitikadi kuonekana ya kimaumbile. Wanaotawaliwa wanakubali hali ya kutengwa, hali ambayo wanaichukulia kuwa ya kawaida. Kwa hivyo, itikadi ni sehemu muhimu ya mwingiliano wa kijamii na lengo lake ni ushawishi.

Crehan (2011) anasema kwamba tabaka tawala linalaumu tabaka tawaliwa na kulirejelea kama kundi la watu ambao hawafai kuwasilisha mawazo yao.

Anaendelea kusema, siyo kwamba watu wa kawaida hawawezi kuelewa au kutoa mawazo kwa urazini bali kundi tawala linadai mawazo ya tabaka tawala hayahitajiki kuwa falsafa ya binadamu. Hivyo ni dhahiri kwamba tabaka tawala linakandamiza watu wa kawaida. Utamaduni wa tabaka hili hautambui hisia na haja za watu wa kawaida. Tabaka tawala linaendeleza ubaguzi kati yao na watawaliwa; huwachukulia kama wasio na uwezo na ni watu wa hadhi ya chini na wanaoishi mashambani. Itikadi hii ya ubaguzi inafanya kundi la tabaka tawala kutojali maslahi ya watawaliwa. Kate analinganisha uhusiano uliopo kati ya watawala na watu wa hadhi ya chini na wanahistoria wanaofuata na kuathiriwa na mkondo wa kifalsafa ambao wanaandika juzuu na juzuu kuhusu uzalendo na juhudi za ujenzi wa taifa bila hata kutaja mchango wa wafanyakazi viwandani au wafanya kazi mashambani. Katika utafiti wetu, wanaume wanawakilisha tabaka tawala na wanawake wanawakilisha watu wa kawaida ambao wanadhulumiwa. Mawazo haya yameongoza utafiti huu kwa kubainisha itikadi za kiuana zinavyowasilisha mahusiano ya kiuana yanayowanufaisha wanaume na kutotambua haja na maslahi ya wanawake.

Kwa mujibu wa Gramsci (1985), watawala wanaendeleza imani ya utawala kwa ukubalifu kwa kutumia itikadi kuliko nguvu na kulazimisha. Ukubalifu na ushawishi unaibua mitazamo na kaida. Kaida hizo hatimaye zinachukuliwa kuwa ukweli unaokubalika na watu wote wa kawaida na kuendeleza hali ilivyo bila kuibadilisha. Gramsci anadai kwamba watu wanashawishika kwa itikadi mbalimbali zinazopatikana katika jamii kama za kimaumbile na kuchukuliwa kama ni ukweli usiopingika. Mawazo ya Gramsci yanaendelezwa na Patnaik (1988:2) ambaye anasema:

> 'watu wanakumbana na imani kadhaa ambazo wanakuta kama tayari zipo na kuzichukulia kama ukweli unaojidhihirisha bila kutafakari na kuzihoji'.

Mawazo ya Gramsci kuhusu itikadi, yanaelezwa katika mawanda mbalimbali, kwa mfano mawanda ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Pia, Gramsci (1985) anasema kwamba binadamu hatawaliwi kwa nguvu na mamlaka tu lakini pia kwa kutumia mawazo; utawala wa kisiasa unaegemea ukubalifu wa watawaliwa. Ukubalifu huu unapatikana kutokana na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala. Kulingana na mawazo ya Gramsci, mfumo huu wa kunyamazisha na kutawala wanawake kwa ukubalifu unatokana na ushawishi wa itikadi za wanaume kama tabaka tawala. Utawala huu unalenga kujitolea na kutumika kwa tabaka tawaliwa wakitumikia wanaume. Mawazo yake yaliongoza utafiti huu kwa kuchunguza namna mahusiano ya kiuana yanavyoendelezwa kati ya wanawake na wanaume katika methali za Kinyankole na Kiswahili kwa ukubalifu na kushawishika. Mtafiti amebainisha vile wanawake wanavyoshawishika kiitikadi katika kuendeleza mahusiano ya kutawaliwa bila kulazimishwa katika methali za Kinyankole na Kiswahili pamoja na kuonyesha jinsi wanawake wanavyojitolea, kukubali kutumika na kutumikia wanaume.

Bates (1975) anazungumzia dhana nyingine ya itikadi kwamba, fikira za kiitikadi ni matokeo ya mahusiano miongoni mwa watu binafsi katika jamii. Mfumo wa mahusiano na upatikanaji wa mabadiliko katika jamii yanategemea uwezeshaji wa watu binafsi katika kujiendeleza. Kwa hivyo ni muhimu kuchunguza jinsi mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake kama watu binafsi

yanavyoendelezwa na itikadi za kiuana ili kuwezesha mabadiliko katika jamii. Mawazo haya yamenufaisha utafiti huu kwa kuchunguza mahusiano ya kiuana kwa kuzingatia kuwa athari za itikadi za kiuana ni matokeo ya mahusiano kati ya wanaume na wanawake kama watu binafsi. Mahusiano hayo ambayo yanatengeneza itikadi zinazoshikiliwa na jamii kwa jumla.

Althusser (1981) anasema kwamba wanaotawaliwa na kudhulumiwa wanaathiriwa na ung'amuzi potoshi. Hizi ni imani zinazozuia mtu kufasiri hali halisi ya maisha yake aidha kijamii au kiuchumi. Imani hizo zinaumbwa na watu katika jamii ambapo wanajamii wanafanywa kuelewa maisha ya kijamii kwa njia tofauti na kuyafasiri kwa njia isiyo sahihi. Imani hizi zinafanya watu kutofahamu nguvu zinazoathiri kufikiria kwao hatimaye kuwapotosha. Pamoja na hayo, imani hizo zinaficha hali ya unyonyaji wa watawala na dhuluma kwa watawaliwa kisha kusababisha kugawanyika kwao katika matabaka; tabaka tawala na la watawaliwa. Imani hizi zinalenga kukidhi mahitaji ya mfumo wa kiuchumi kwa kuyachukulia mawazo ya kiitikadi kuonekana ya kimaumbile.

Althusser (1981) anasema kwamba binadamu wanachukulia fikra ambazo siyo za kweli na kuzifanya kuwa za kweli. Kuhusu mali ya kibinafsi na mamlaka kuhusu njia za uzalishaji mali, kunatokeza kundi fulani la watu linalomiliki mali nyingi kuliko lingine. Tofauti hii inazua mkinzano na kutoleta usawa. Anazungumzia kuhusu kumiliki mali hasa ardhi vile kunazua na kuendeleza tofauti za kiuana na mvutano. Mawazo yake Althusser yalifaa kwa kuchunguza itikadi za kiuana kuhusu umiliki wa mali namna unavyoathiri mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake katika methali za Wanyankole na Waswahili. Althusser

anaendelea kusema kwamba itikadi ni zao la amali za kijamii. Hii ni nguzo muhimu katika utafiti huu. Vile utafiti huu unashughulikia itikadi za kiuana, imani, fikira na mitazamo ya Wanyankole na Waswahili kuhusu mahusiano ya kiuana imedhihirika kupitia methali za jamii zao.

Bressler (2007) anazungumzia itikadi za unyanyasaji na ukubalifu ulio na misingi yake katika kutawaliwa bila kupinga kwa kundi linalotawaliwa pamoja na kuchangia kutawaliwa kwao kuliko kutumia mabavu. Bressler alipanua mawazo ya Gramsci kuhusu dhana ya itikadi kwa kuhusisha 'maarifa ya kawaida' kurejelea mitazamo ya kawaida kutoka tabaka tawala yaani mitazamo hii inaonekana kuwa ya kawaida ilhali ilibuniwa kwa azma ya kufaidi kundi mahsusi la kijamii. Wanaitikadi wanazungumzia itikadi katika miktadha mingine lakini utafiti huu umeshughulikia itikadi kwa muktadha wa uana hasa zilizo na misingi katika ukubalifu, upotoshaji na unyanyasaji wa kiuana.

Mihimili ya Nadharia ya Itikadi ni kama ifuatayo:

a) Binadamu hatawaliwi kwa nguvu na kutumia mamlaka peke yake lakini pia kwa kutumia maarifa; utawala wa kisiasa unaegemea ukubalifu (hejimonia) wa watawaliwa. Watawala wanaendeleza imani ya utawala kwa ukubalifu kwa kutumia itikadi kuliko nguvu na kulazimisha.
b) Ukubalifu unapatikana kutokana na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala. Utawala unalenga kujitolea na kutumika kwa tabaka tawaliwa wakitumikia kundi dogo watawaliwa.

c) Mchakato wa kiitikadi unapotosha watu wa tabaka la chini katika jamii kwa kuficha masuala ya msingi kuhusu unyonyaji na unyanyasaji katika mahusiano ya kijamii kati ya matabaka.

d) Uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii yaani utawala unaathiriwa na ung'amuzi potoshi. Binadamu wanachukulia fikira ambazo siyo za kweli na kuzifanya zionekane kuwa za kweli. Wanaodhulumiwa wanaathiriwa na ung'amuzi potoshi na kukubali hali ya kutengwa. Imani hizi zinazotengenezwa na watu, ambapo watu hawafahamu nguvu zinazoathiri kufikiria kwao. Imani hizi zinasababisha kugawanyika kwao katika matabaka. Ung'amuzi potoshi unalenga kukidhi mahitaji ya mfumo wa kiuchumi kwa kuyachukulia mawazo ya kiitikadi kuonekana ya kimaumbile. Mchakato huu wa kiitikadi unapotosha watu wa tabaka la chini katika jamii kuficha masuala ya msingi kuhusu unyonyaji na unyanyasaji katika mahusiano ya kijamii kati ya matabaka.

e) Mafikirio ya kiitikadi ni matokeo ya mahusiano miongoni mwa watu binafsi katika jamii. Upatikanaji wa mabadiliko katika jamii na mfumo wa mahusiano yanategemea uwezeshaji wa watu binafsi katika kujiendeleza.

f) Utamaduni wa tabaka tawala hautambui hisia na haja za watu wa kawaida. Wanaendeleza ubaguzi kati yao na watawaliwa/wa kawaida, kuwachukulia kama wasio na uwezo na ni watu wa hadhi ya chini wanaoishi vijijini. Itikadi hii ya ubaguzi inafanya kundi la tabaka tawala kutojali maslahi ya watawaliwa.

g) Matumizi ya vyombo vya dola huendeleza ukubalifu wa watawaliwa kama anavyodai Althusser (1981).

Mihimili hii ya nadharia ya Itikadi imefaa utafiti huu kama ifuatavyo;

Binadamu hatawaliwi kwa nguvu na kutumia mamlaka peke yake lakini pia kwa kutumia maarifa. Mhimili huu umeelekeza utafiti huu kwa kubainisha itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya wanaume na wanawake kwa kushawishika kukubali majukumu na hadhi yao. Utawala wa kisiasa unaegemea ukubalifu na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala. Ukubalifu unapatikana kutokana na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala ambapo utawala unalenga tabaka tawaliwa kujitolea na kutumikia kundi dogo la watawaliwa.

Uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii yaani utawala unaathiriwa na ung'amuzi potoshi. Mhimili huu unarejelea watawaliwa/watu wa kawaida kutokuwa na uwezo wa kutambua ubaguzi, unyanyasaji na unyonyaji wao. Hali hii inasababishwa kuwepo kwa itikadi kandamizi zinazoruhusu na kuhalalisha matabaka katika jamii. Mhimili huu umetumiwa kubainisha itikadi za kiuana zinazoendeleza mahusiano ya kiuana ya utawala wa wanaume. Utawala huu unatekelezwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii yaani mahusiano yanaathiriwa na ung'amuzi potoshi. Itikadi zinazotokea zinalenga kufaidi wanaume wanaowakilisha kundi tawala kwa upande mmoja; unyanyasaji na unyamazishaji wa wanawake ambao wanawakilisha tabaka tawaliwa kwa upande mwingine.

Mchakato wa kiitikadi unapotosha watu wa tabaka la chini katika jamii kwa kuficha masuala ya msingi kuhusu unyonyaji na unyanyasaji katika mahusiano ya kijamii kati ya matabaka. Aidha, matumizi ya vyombo vya dola huendeleza ukubalifu wa watawaliwa kama anavyodai Althusser (1981). Mhimili huu

umeongoza utafiti huu kwa kudhihirisha taratibu za kiitikadi zinavyopotosha wanawake kama watu wa tabaka la chini katika jamii. Mchakato huu unaficha masuala ya msingi kuhusu unyonyaji na unyanyasaji wa wanawake katika mahusiano ya kijamii kati yao na wanaume. Katika utafiti huu itikadi mbalimbali zimebainishwa vile zinaendeleza mahusiano kati ya wanaume na wanawake kwa hiari. Pamoja na hayo, utafiti huu umetathmini asasi mbalimbali kama vile ndoa na kitengo cha familia kama moja wapo ya vyombo vya dola na taratibu za kijamii kufanya wanawake kutii, kunyenyekea na kutawaliwa na wanaume. Yaani ndoa huwapa mamlaka wanaume dhidi ya wanawake kama watawala.

Kwa ujumla, nadharia hii imeelekeza utafiti huu kwa kuchanganua itikadi za kiuana ambazo ni sehemu ya jamii ili kueleza jinsi methali za Wanyankole na Waswahili zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana. Jambo hili limetimizwa kwa: Kuchunguza itikadi za kiuana zinazotokea katika methali za Kinyankole na Kiswahili; Kuchunguza mahusiano ya kiuana yanayodhihirishwa na itikadi za kiuana katika methali za jamii hizo: Kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana kitamaduni, kutathmini jinsi ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali za jamii teule unavyoathiri usawa wa kiuana.

#### 2.4.1.1 Upungufu wa Nadharia ya Itikadi

Nadharia ya Itikadi haipambanui ipasavyo mahusiano ya kiuana katika methali licha ya kubainisha itikadi mbalimbali za kiuana na kudhihirisha ushawishi na ukubalifu katika methali hizo. Aidha, suala la usawa wa kiuana kama

linavyojitokeza katika methali za Kinyankole na Kiswahili halipambanuliwi vizuri na nadharia ya Itikadi.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika (Steady, 1981) imeteuliwa kufidia upungufu huo wa nadharia ya Itikadi. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imefaa zaidi utafiti huu katika kujadili itikadi za kiuana vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana. Nadharia hii ni muhimu hasa katika kuendeleza juhudi za kukomboa na kutetea mwanamke. Ni imani ya mtafiti kuwa mahusiano ya kiuana na usawa wa kiuana vinabainika waziwazi kwa kurejelea nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika (Steady, 1981). Kwa hivyo, mtafiti hakuwa na budi kurejelea mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo inapambanua suala hili kwa njia iliyo wazi. Mtafiti amezingatia mawazo ya Steady (1981) katika kujadili itikadi mbalimbali zinazobainika katika methali za Kinyankole na Kiswahili katika muktadha wa uana, kuchunguza vipi itikadi hizo za kiuana zinavyoendeleza mahusiano kati ya wanaume na wanawake kwa ukubalifu na ushawishi kwa kuzingatia majukumu na hadhi, na kuhakiki ukinzani unaoibuka kuhusu usawa wa kiuana kati ya mwanamume na mwanamke katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa hivyo, ilisaidia kufidia na nadharia ya Itikadi.

### 2.4.2 Nadharia ya Ufeministi

Ufeministi ni miongoni mwa nadharia za kisasa ambazo zinalenga kutatua matatizo yanayowakumba wanawake katika jamii inayotawaliwa wanaume (Wafula na Njogu, 2007). Matatizo wanayokumbana nayo chanzo chake ni maumbile yao. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu, Ufeministi ni nadharia

ambayo inapigania ukombozi wa wanawake ambao wamefungwa kwenye minyororo ya kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Masuala ya Ufeministi yalianza kunadharishwa katika Karne ya 19 na kuvuma katika miaka ya 1960. Kipindi hicho, wanawake wa Kimagharibi walizungumzia matatizo yaliyowakumba kwenye majukwaa tofauti pamoja na kwenye maandishi. Miongoni mwa wanaharakati waliozungumzia masuala ya wanawake wakati huo walikuwa Mary Wollstonecraft (1792) na Virginia Woolf (1929). Masuala ya Ufeministi yaliendelezwa zaidi na Simone de Beauvoir (Tidd, 2004). Tidd anasema kwamba Beauvoir alidhihirisha na kupinga amali na asasi za kijamii zilizomchukulia mwanamke kama binadamu wa daraja la pili huku zikimuinua mwananamume katika jamii. Miongoni mwa asasi alizobainisha ni utamaduni, ndoa na dini.

Tidd (2004) akimrejelea Beauvoir (1949) anasema kwamba mtu hazaliwi mwanamke bali anakuwa mwanamke. Anafafanua zaidi kwamba siyo jambo la kimaumbile kumuumba mwanamke au mwanamume vile alivyo katika jamii bali ni jamii yenyewe au utamaduni. Mifumo ya kijamii inahusisha matabaka na asasi mbalimbali kuhusu mitazamo ya jinsi mambo yanavyopaswa kutekelezwa. Mawazo haya ni ya msingi na yalitufaa katika utafiti huu ili kuweza kuangazia jinsi itikadi zinazoumbwa na jamii zinavyoibua mahusiano ya kiuana yenye utofauti kati ya wanaume na wanawake. Mwingine ni Greer (1971) ambaye katika andiko lake anawahimiza wanawake kutounga mkono ndoa kwa sababu inawafanya kuwa miliki ya wanaume na hatimaye kukosa uhuru wao. Wataalamu wengine m waliondeleza nadharia hii ni Golombok na Robyn

(1994), Nira (1997), Beasley (2005), Holmes (2007) na (Connell, 2009) miongoni mwa wengine.

Holmes (2007) anasema kwamba binadamu walipata changamoto kuhusu suala la uana ambapo tofauti za kimaumbile na za kisaikolojia ziliibuka kati ya wanawake na wanaume. Majukumu maalumu ya wanaume na wanawake yalizingatiwa na kushughulikiwa katika kuendeleza mahusiano ya kiuana. Hali hii ilipelekea kugawanya kazi katika jamii kwa misingi ya uana. Kwa mujibu wa Sydie (1987) nafasi za kijamii za utegemezi wa mwanamke zinaamuliwa na uwezo mkubwa wa kimwili wa kiume. Kwa hivyo, maoni haya yaliwezesha mtafiti kuonesha masuala ya kiuana ya kijamii ambayo yanaathiri usawa wa kiuana kwa kuyachukulia kama ya kimaumbile.

Golombok na Robyn (1994) wanabainisha chanzo cha kuibuka kwa tofauti za kiuana. Ufafanuzi wao unajikita kwa mawazo ya Sigmund Freud.  Mawazo ya Freud kuhusu ukuaji wa kijinsia ulihalalishwa na kuchukuliwa kuwa wa kawaida kuhusu tofauti kati ya wanaume na wanawake. Golombok na Robyn wanasema kwamba uainishaji wa Freud ulichukulia kuwa, tofauti za kisaikolojia kati ya jinsia ziliibuka kutokana na tofauti za kibiolojia. Majukumu ya wanawake kama watengenezaji wa nyumbani na kulea watoto, na wanaume kama watafutaji wa mahitaji ya familia hayakupingwa. Haikuaminika kwamba kuwepo kwa baba na mama kama wazazi ni jambo muhimu kwa ukuaji wa watoto kiuana. Wanawake walianza kufanya kazi katika miaka ya 1940 ili kusaidia uendelezaji wa familia. Hivyo, kupinga fikira kwamba tofauti za kiuana ni majaliwa ya kibiolojia.

Golombok anafafanua zaidi kwamba majukumu ya kimaumbile yasiangaliwe na kusisitizwa kama kiini cha kutenga majukumu ya kiuana. Wanawake kuwa na uwezo wa kubeba mimba na kuzaa watoto, haimaanishi kwamba maisha yao yafungwe kwenye kazi za nyumbani na kulea watoto. Wanaume kwa upande mwingine, kutokuwa na uwezo wa kujifungua haimaanishi kwamba hawawezi kutekeleza majukumu ya kutunza watoto. Katika miaka ya 1960 na1970 aina mpya za familia zilibainika huko Uingereza ambapo wanaume na wanawake kama wazazi walianza kushughulikia majukumu kwa kutozingatia ama ni ya wanawake au wanaume. Mabadiliko ya kimsingi katika muundo wa familia yalitokea ambapo wanaume walihusika katika majukumu ya nyumbani na kutunza watoto. Maoni haya yalikuwa faafu kwa utafiti huu uliochunguza jinsi mahusiano ya kiuana yanavyoendelezwa kati ya wanawake na wanaume kwa misingi ya itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Aidha, maoni haya yaliwezesha mtafiti kuangazia namna itikadi za kiuana zinavyoathiri mgao wa majukumu ya kiuana katika methali katika jamii za Wanyankole na Waswahili.

Plaskow (2007) kama mmoja wa watetezi wa Nadharia ya Ufeministi anasema kwamba uana si suala la kimaumbile bali ni matokeo ya mchakato changamani wa kijamii ambapo binadamu wanatengewa majukumu. Alifafanua uana katika jamii yake ya Yiddishi kwamba wanaume waliweza kuwa katika nafasi ya wanawake kimajukumu na wakati mwingine wanawake wangeweza kuwa katika nafasi za wanaume. Kwa kurejelea maoni yake ni dhahiri kwamba uana unatokea kulingana na jinsi wanaume kwa wanawake wanavyotangamana katika jamii. Utangamano huu hatimaye unaathiri utekelezaji wa majukumu kwa kuyatenga

kulingana na misingi ya uana. Majukumu hayo ya kiuana yanatengwa kulingana na itikadi za kijamii. Kwa hivyo, mwelekeo huu ni faafu kwa kubainishia jinsi methali za Kinyankole na Kiswahili zinavyobadilisha itikadi za kiuana ambazo zinashikiliwa kitamaduni.

McElhinny (2003) anaendeleza dhana ya uana kwamba, tabia za wanawake na wanaume ambazo zinaonekana kutobadilika zitathminiwe kila mara kwa muktadha wa kijamii bali si kama suala la kimaumbile. McElhinny anaendelea kusema kwamba mwanamume alijitengenezea mahusiano ya kimamlaka dhidi ya mwanamke na kumwangalia mwanamke kama aliye tofauti na yeye, hali ambayo wanawake waliikubali. Kulingana na maoni hayo wanawake wakakubali hali na nafasi yao kwa kupotoshwa. Maoni ya McElhinny yalifaa katika utafiti huu ili kuweza kubainisha sifa za wanawake na wanaume hususani jinsi wanaume wanavyojitengenezea mahusiano ya kimamlaka dhidi ya wanawake na namna wanawake wanavyoikubali hali hiyo ya kudunishwa. Mawazo hayo yalikuwa kuntu kwa utafiti huu kwa kuongoza uchunguzi wa masuala ya wanawake hususani namna wanavyochukuliwa kama viumbe duni huku wanaume wanathaminiwa na kuheshimiwa. Maoni haya yanajikita pia katika mawazo ya Foucault (1978) anayepinga kuwa mamlaka ya kijamii na kisiasa ni nguzo zinazotokea upande mmoja wa wanaume.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kwamba Nadharia ya Ufeministi inabainishwa katika matapo mawili. Tapo la kwanza ni la kimaeneo ambapo wanawake kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu wanazungumzia na kusisitiza masuala mbalimbali kuhuku ukombozi wao. Njogu na Chimerah

wanatambua sehemu za ulimwengu zilizohusishwa na tapo hili kama Eneo la Kifaransa, Eneo la Kimarekani, Eneo la Kiingereza na Eneo la Kiafrika. Tapo la pili ni lile ambalo linazungumzia mielekeo maalumu na mahususi katika Nadharia ya Ufeministi. Kwa mujibu wa utafiti wetu, tapo la kimaeneo ndilo linazingatiwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Ufeministi katika muktadha wa Kiafrika.

#### 2.4.2.1 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

Nadharia hii iliasisiwa na Steady (1981) na inahusu ushirikishaji wa mwanamke kwenye shughuli mbalimbali za kijamii bila kuzingatia utawala wa ubabedume. Nadharia hii ya Ufeministi mkabala wa Kiafrika asili yake ni Bara la Afrika. Steady anasema kuwa Ufeministi wa Kiafrika unajikita katika misingi inayoangalia majukumu tofauti ya kijinsia yanategemeana na kukamilishana, yenye usawa katika kuendeleza jamii. Aidha, anaeleza kuwa Ufeministi wa Kiafrika huweka pamoja masuala ya kijinsia, ubaguzi, utabaka na mielekeo tofauti ya kiutamaduni ili kuibua aina ya Ufeministi unaomwangalia mwanamke kama binadamu badala ya kurejelewa kama kiumbe kinachoamriwa na jinsia yake. Steady anaongezea kuwa Ufeministi wa Kiafrika huchunguza masuala ya kitamaduni yanayomlenga mwanamke. Isitoshe, hushughulikia masuala ya kijinsia kwa kujikita katika muktadha wa Kiafrika. Nadharia hii ya Ufeministi wa Kiafrika inanuia kuleta usawa wa wanadamu kijinsia na kiutamaduni. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za binadamu Pamoja na kukuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

Juhudi za Steady (1981) zinachochewa na haja ya kumkomboa mwanamke wa Kiafrika kutokana na ubaguzi wa kitamaduni na kidini. Njogu na Chimera (1999) wanafafanua mihimili ya msingi ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kama ifuatavyo: moja, ufeministi wa Kiafrika ni jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali anamojipata mwanamke wa Kiafrika ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo. Pili, mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika hujaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na ambao hawawategemei wanaume ili kujitambulisha na ambao kisaikolojia wanaojitambua na kujiamini na wasio na hisia kuwa wana udhaifu kwa sababu tu ni wanawake.

Kwa muhtasari, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ilifaa utafiti huu kwa kuongozwa na mihimili ifuatayo:

a) Binadamu wanapaswa kuwa sawa katika masuala ya utamaduni na uana. Mkabala huu unalenga jamii ambayo inaendelezwa kwenye misingi ya amali za kibinadamu kama vile upendo, ushirikiano na umama bila kuzingatia maumbile.

b) Fasihi hutumiwa kama jukwaa la kuelezea hali halisi mwanamke anayokumbana nayo ili iweze kueleweka kwa binadamu wengine. Methali kama kipera cha fasihi katika utafiti wetu zimetufaa katika kuchunguza na kudhihirisha nafasi ya mwanamke kupitia kwa mahusiano yake na mwanamume katika jamii.

c) Wanawake wanapaswa kukuza na kuendeleza umoja wao kama kundi linalodhurumiwa. Jambo hili linaendelezwa kwa ajili ya kupeana nguvu za kujitetea badala ya kutazamwa kama kundi linaloendeleza utawala

wao kwa kupingana wao kwa wao. Aidha, wanawake wazinduke na kubadili mielekeo vile wanavyojiona katika uhusiano na wanaume.

d) Tabia za uana ambazo zinaonekana kutobadilika zitathminiwe kila mara kwa muktadha wa kijamii bali si kama suala la kimaumbile.

e) Wanaume na wanawake washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana bila kuathiriwa na majukumu ya kimaumbile.

Hivyo, kwa kifupi, mkabala wa Ufeministi wa Kiafrika unapigania kutobaguliwa kwa wanawake, hadhi chanya ya wanawake, haki na ukombozi wa mwanamke. Nadharia hii imeelekeza utafiti huu kujadili itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano kati ya wanaume na wanawake kwa ukubalifu na ushawishi. Mjadala wa utafiti huu umezingatia majukumu na hadhi ya wanawake na wanaume. Aidha, utafiti umehakiki ukinzani unaoibuka vile unaathiri usawa wa kiuana kati yao katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Mihimili ifuatayo ya Nadharia hii ndiyo imeongoza utafiti huu;

Binadamu wanapaswa kuwa sawa katika masuala ya utamaduni na uana. Jamii inafaa kuendelezwa kwenye misingi ya amali za kibinadamu kama vile upendo, ushirikiano na umama bila kuzingatia maumbile. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imedhihirisha tofauti za kiuana kati ya wanawake na wanaume. Tofauti hizi zimeoneshwa kuwa zinashawishi wanawake kukubali kushughulikia majukumu mazito na kuwa katika nafasi ya kutawaliwa na wanaume. Itikadi hizi kama zinavyobainisha wanawake zinalenga kukidhi malengo ya wanaume ya kuendelea kudhihirika kama wenye mamlaka na watawala. Wanawake wao

wanabainishwa kama raia wa daraja la pili katika jamii. Hali hii si sahihi kwa misingi ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

Pamoja na hayo, nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imenufaisha utafiti huu katika kuchunguza tabia, sifa na mitazamo ya kiuana. Uchunguzi huu umejikita kwa misingi ya amali za kiutamaduni katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Hatimaye imesaidia kubainisha jinsi itikadi za kiuana zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana kati ya wanawake na wanaume kupitia methali za Kinyankole na Kiswahili.

#### 2.4.2.1.1 Upungufu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imeweza kuongoza utathmini wa mahusiano yenye ubaguzi wa kiuana na athari za itikadi kwa usawa wa kiuana katika hatua mbalimbali za jamii ya Wanyankole na Waswahili. Hata hivyo, nadharia hii haiongozi kuibua mikinzano ya kimaana kwa kuhakiki methali kwa jicho la kiupekuzi. Nadharia ya Udenguzi iliyoasisiwa na Derrida (1960) imeweza kufidia mwanya huu.

### 2.4.3 Nadharia ya Udenguzi

Abrams na Harpham (2014) wanatambua kuwa nadharia ya udenguzi iliasisiwa na mwanafalsafa Jacques Derrida katika miaka ya 1960. Nadharia hii iliendelezwa na Miller (2009) miongoni mwa waitifaki wengine. Udenguzi ni mkabala wa kuelewa uhusiano uliopo kati ya matini na maana. Kwa hivyo, udenguzi ni nadharia inayolenga kuelewa ujuzi na maarifa. Kulingana na nadharia hii kuna utata wa kuelewa ujuzi na maarifa bayana. Maana ya kazi ya fasihi kulingana na nadharia hii ina utelezi na inajikita kwenye ukinzani wa

lugha. Yaani, lugha huwa na maana zinazokinzana na kujidengua. Nadharia ya udenguzi inaelekeza mhakiki kufafanua matini ya kifasihi kwa kina kwa kuibomoa matini hiyo ili kufikia maana halisi kuhusu jamii.

Derrida (1960) anasema kwamba lugha ina utelezi kwa sababu kiashiria chochote kinaweza kuibua maana kadhaa za kiashiriwa wakati wowote na kuifanya lugha kuwa na maana husishi. Wahakiki wa kiudenguzi wanatambua namna matini inavyojenga maana za maneno na kupinga uwezekano wa matini kubainisha maana moja. Derrida anadai kwamba, watu hufikiria na kueleza mawazo yao katika jozi kinzani . Derrida anapendekeza kwamba ukinzani huu una dhana chanya au dhana yenye hadhi na kwa upande mwingine dhana hasi au duni. Kwa hivyo, lugha ina uamilifu wake katika njia kinzani

Derrida, alidai kuwa lugha, kama ishara, ina uwezo wa kujifafanua tukiitazama kwa undani. Udenguzi husisitiza jinsi lugha inavyoingiliana na maana kwa uamilifu wake. Udenguzi ni mkabala unaolenga katika kuingilia matini kati, kuihakiki ndani kwa kuipeperusha, kuipindapinda. Kulingana na Derrida, matini ni muhimu katika kubainisha maana na dhana ambazo huwa zinaingiliana. Kwa hivyo maoni ya Derrida yanaafiki na kuongoza utafiti wetu kwa kuchunguza kauli za methali katika kuibua maana mpya kuhusu itikadi za kiuana namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kati ya mwanamke na mwanamume. Kwa hivyo, nadharia hii ya Udenguzi ilifaa utafiti huu katika kutekeleza lengo la tatu ambalo limedhamiria kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili ili kuweza kuibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana. Watetezi wengine wa udenguzi kama vile Bloom, Miller, Hartman na

Abrams,wanasema kwamba huenda kukatokea maingiliano ya tafsiri mbili za kazi ya fasihi zisizolingana na tafsiri zote mbili huenda zikakubalika.

Udenguzi ni uhakiki unaojikita na kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana bila kurejelea muktadha. Sifa kubwa ya udenguzi ni uzingatifu wa lugha na matini. Hupasua matini katika vipengele vyake vyote ili kuweka wazi kilichofichika. Nadharia hii iliweza kutumika katika kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili kwa kuzingatia maana zinazoibuliwa na maneno katika methali na matumizi yake kwa njia ya ukinzani.

Stock-Morton (1991) anasema kwamba, Derrida katika uchunguzi wake, neno mwanamke kama linavyowekwa katika nafasi ya pili baada ya neno mwanamume, alionyesha uwezekano wa kukinzana na uainishaji huu. Kwa kuongozwa na mhimili huu mtafiti alionyesha kuwa mwanamke kama anavyorejelewa katika tafiti za awali kama kiumbe wa daraja la pili na kudhalilishwa, maana hii inadenguliwa na kuibua maana mpya iliyo chanya ya mwanamke katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Udenguzi unatumia dhana ya uwili ambapo dhana moja inapewa hadhi kuliko nyingine yaani zuri/baya, upendo/chuki, eupe/eusi na mwanamume/mwanamke. Katika matini, dhana hizi zenye jozi kinzani zinaunda dhamira ya kinachesemwa. Hata hivyo, nadharia ya udenguzi inalenga kuchunguza jinsi lugha ya matini inavyofaa kwa jozi moja ya maneno. Nadharia ya udenguzi inapendelea kinyume lakini si lazima iwe jozi inayopendelewa. Nadharia hii, inasaidia uhakiki wa kibinafsi kuhusu matarajio ya kimapokeo hasa kuhusu maneno duni kwenye jozi yanavyoendeleza

maana katika jamii. Nadharia ya udenguzi inahusisha usomaji wa matini kwa makini ili kuonyesha kwamba matini yoyote ile ina maana kinzani.

Miller (2009) mmojawapo wa waendelezaji wa nadharia ya udenguzi wa Kimarekani anaeleza kwamba, udenguzi si ubomoaji wa muundo wa matini lakini ni udhihirishaji kuwa matini imeshajimomoa tayari. Yeye Barthes (1977) anasema kwamba, mhakiki asome matini za kifasihi ili aweze kutoa maana kulingana na welewa wake kwa njia ya kimantiki na muktadha wa jamii yake. Anatoa maelezo yake kwa madai kwamba, fasihi inabainisha maana anwai. Utafiti huu unaafikiana na Barthes kuhusu kauli yake ya kwamba fasihi hasa methali kama kauli za kimapokeo zinaibua maana nyingi kulingana fasili ya mhakiki na muktadha wa matumizi yake katika jamii. Kupitia uchambuzi, matini za kifasihi zinabainisha ukinzani wa ujuzi unaofichama kwenye miundo ya lugha.

Njogu na Chimerah  (1999) wanaeleza kuwa udenguzi unapinga mgawo mkali wa hali mbili au zaidi zinazokinzana, na kuonyesha uwezekano wa hali kama hizo kuwa pamoja na kuchangiana kimaana. Njogu anaendelea kusema kuwa udenguzi ni juhudi ya kufikia nguvu na uwezo wa matini kama chombo kinachojifafanua.

Angela (2018) anadai kuwa, udenguzi ni kusoma upya na kutazama kila neno katika matini kwa jicho la kiupekuzi. Nadharia ya udenguzi inadai kuwa matini za fasihi huzungumzia mambo yasiyodhamiriwa. Madhumuni ya nadharia hii ni kujenga maana kwa njia ya kubomoa maana. Nadharia hii ilifaa kazi hii kwa kuibua maana zinazokinzana na maana zinazoonekana kuwa ndizo

zinadhamiriwa katika methali za Kinyankole na Kiswahili kuhusu itikadi za kiuana. Kwa hivyo, mtafiti alinuia kupata maana mpya ya itikadi za kiuana vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana kati ya mwanamume na mwanamke kupitia maana kinzani. Utafiti huu ulifaidika na nadharia hii kwa uchambuzi wa data zilizokusanywa kuhusu ukinzani wa itikadi za kiuana vile unaibuka katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Mtafiti amehakiki methali za Kinyankole na Kiswahili kwa jicho la kiupekuzi ili kuweza kubainisha namna itikadi za kiuana zinavyoibua ukinzani kuhusu mahusiano ya mwanamume na mwanamke. Udenguzi ni ukinzani wa matarajio ya kawaida ya matini. Kwa hivyo, nadharia hii inabainisha ule ukinzani wa kauli za kawaida za methali vile zinaeleza mahusiano ya kiuana ya mwanamume na mwanamke. Ukinzani huu unalenga kuwasilisha ujumbe ulio kinyume na ujumbe uliozoeleka. Maoni haya kama yanavyoendelezwa na (Abrams, 2014) yalisaidia mtafiti kuibua maana mpya ya itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya kiuana.

Aidha, udenguzi huonyesha kuwa ukinzani unaweza kutokea wakati maana ambazo hazikukusudiwa zinaingiliana na zile zilizokusudiwa. Hoja hii imeelekeza utafiti huu kwa kudhihirisha kuwa fasihi simulizi zimejaa utata ambao hutokea wakati wa uchambuzi. Hii ni kwa sababu msikilizaji anaweza kutafsiri maana ya utanzu unaohusika kwa njia tofauti kabisa na ile iliyokusudiwa na mzungumzaji. Hapa mtafiti anasisitiza umuhimu wa kujua muktadha na mazingira ya utendaji wakati wa uchanganuzi. Katika uchaganuzi, udenguzi hutafuta utata ulioko katika matini mpaka kupatikana.

Nadharia hii husisitiza uwezekano wa kuwa na maana zaidi ya moja katika matini. Imebainishwa hapa kuwa kuna na uwezekano wa kutafsiri fani hiyo kinyume kabisa na vile inavyotarajiwa na mwingine kwa sababu maana inayojitokeza katika matini si timilifu. Mtafiti anasisitiza kuwa kuna utata katika uhakiki na maana ya tanzu za fasihi simulizi kwa vile istiara tofauti hutumiwa kutoa maana tofauti kulingana na jamii. Maoni hayo yameelekeza utafiti huu kwanza kukubali kuwa methali kama kazi ya kifasihi, kuna uwezekano wa kuzifasili na kuibua maana iliyo kinyume na inayotarajiwa. Pia kwa mujibu wa nadharia hii, inasisitizwa kwamba methali, kwa mfano, hazina umbo maalum kinyume cha mawazo ya wasomi kama vile Finnegan (1970) wanaoamini kuwa methali ni usemi mfupi. Mawazo yao yanadhihirisha kama kwamba, kauli hizi fupi zinawasilisha maana kwa upeo mdogo kulingana na fasili hiyo. Kwa hakika methali moja inaweza kuchambuliwa na kupata maana nyingi Zaidi.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba katika udenguzi, hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Hii ndiyo inayofanya wahakiki kutoa fasili tofauti tofauti za jambo moja. Fasili hizo zaweza kufanana au kutofautiana. Kwa hiyo udenguzi unaweza kuboresha matini au kuumba upya kwa lengo la kukidhi upya mahitaji ya jamii. Mawazo haya yameelekeza utafiti katika kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili ili kuibua ukinzani wa itikadi za kiuana na kutathmini vile itikadi za kiuana zinavyoathiri usawa wa kiuana. Ukinzani huu unatufanya kugundua kwamba, mwanamke na mwanamume ni viumbe wanaotegemeana katika kutekeleza majukumu yao, mwanamke anaheshimiwa sana kama mama, kama mke, uongozi na mwenye mamlaka. Mahusiano ya mwanamke na mwanamume yanapaswa kuwa ya kimlishano.

Nadharia ya Udenguzi imechangia utafiti huu kwa kurejelea methali za Kinyankole na Kiswahili upya na kuzichunguza kwa jicho la ndani ili kubainisha maana iliyokusudiwa kuhusu itikadi za kiuana. Ifuatayo ni mihimili mihimili ya nadharia ya udenguzi kwa jumla:

(a) Nadharia hii inashikilia kuwa maandishi yoyote hayana maana moja anayoweza kutegemea msomaji bali ni maana nyingi za matini katika lugha kulingana na kiashiria na kiashiriwa.

(b) Udenguzi ni kile kinachotokea katika maana wakati lugha inaeleweka kama maandishi. Maana ya lugha hivyo haitokani na dhana ya mtumiaji wa lugha binafsi kwa sababu dhana husika tayari zinatendeka katika lugha isiyotokana na dhana hizo.

(c) Uibuaji wa mikinzano na mikanganyo ya kimaana katika matini ya fasihi una uhusiano wa karibu na udenguzi.

(d) Maana za matini hubadilika na hivyo maneno na dhana hazina maana thabiti hivyo ni telezi.

(e) Uainishaji wa dhana zote kiulimwengu kwa kuzingatia uwili, mke/mume, kizuri/kibaya, kilicho hai/kisicho hai kwa hivyo dhana zinazokinzana zinakaribiana kimaana.

(f) Matini huwa na mielekeo mingi ya maana ambayo huibua fasili nyingi. Hii hutokana na maana za lugha kupingana zenyewe

Nadharia ya udenguzi imeongoza utafiti huu kwa kuzingatia mihimili ifuatayo:

Matini huwa na mielekeo mingi ya maana ambayo huibua fasili nyingi. Hii hutokana na maana za lugha kupingana zenyewe. Mhimili huu umeongoza mtafiti katika kueleza maana za itikadi za kiuana mbalimbali katika methali za

Kinyankole na Kiswahili. Pamoja na hayo, mhimili huu umewezesha utafiti huu kuibua itikadi tofauti katika methali za Kinyankole na Kiswahili tofauti na zile zilizochunguzwa kabla ya utafiti huu.

Maana za matini hubadilika na hivyo maneno na dhana hazina maana thabiti hivyo ni telezi. Mhimili huu umetumika kubainisha itikadi kadhaa kuhusu mahusiano ya mwanamume na mwanamke kuwa ni telezi siyo ile maana moja inayobainika na kujulikana kama inavyoshikiliwa katika methali. Imebainika kuwa itikadi za kiuana zinabadilika katika methali za Kinyankole na Kiswahili bali hazichukui mkondo ule mmoja wa kudhalilisha wanawake na kukweza wanaume. Aidha, kwa kutumia mhimili huu wa udenguzi, maana za itikadi mbalimbali namna zinavyobainisha mahusiano ya kiuana kati ya mwanamke na mwanamume zimedhihirika.

Uibuaji wa mikinzano na mikanganyo ya kimaana katika matini ya fasihi una uhusiano wa karibu na udenguzi. Mhimili huu umeongoza utafiti huu kuonyesha kwamba itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili zinakinzana na kubainisha unyume wa itikadi, tofauti na vile inashikiliwa na tafiti za awali. Baadhi ya maana katika matini zinapingana kwa hivyo utafiti huu umeweza kuonyesha namna itikadi zinavyoibua unyume na itikadi za mfumodume. Isitoshe, inadhihirishwa kuwa itikadi za kiuana zinabadilika ambapo mwanamume na mwanamke wamebainisha haja ya kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yao ya kiuana bila kuathiriwa na itikadi za kiutamaduni. Vilevile, imedhihirishwa kuwa itikadi za kiuana zinabadilikabadilika katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Nadharia ya udenguzi huondoa mipaka kati ya uwili wa maneno yenye jozi sawia. Udenguzi unazingatia uainishaji wa dhana zote kiulimwengu kwa uwili; mke/mume, kizuri/kibaya, kilicho hai/kisicho hai. Kwa hivyo, dhana zinazokinzana zinakaribiana kimaana. Katika muktadha wa utafiti huu, udenguzi umebainisha kuwa mwanamume na mwanamke ni jozi ambayo imetangamana. Inakuwa vigumu kuelewa upande mmoja bila mwingine. Utafiti huu umeweza kuchunguza itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kati ya mwanamke na mwanamume. Imekuwa rahisi kuelewa mwanamke kwa undani kupitia kwa mahusiano yake na mwanamume.

Udenguzi hushughulikia maneno yanayokinzana na kubainisha itikadi kuu zinazojitokeza na zinazostahili kusailiwa upya. Kupitia uchanganuzi wa kiudenguzi wa matini, wadenguzi hudhihirisha ukinzani wa matini hizo. Mhimili huu umeongoza mtafiti kuweza kudhihirisha itikadi za kiuana katika methali. Mtafiti ameweza kudengua itikadi kinzani zilizomo katika lugha ya methali za Kinyankole na Kiswahili kutokana na ukweli huo kwamba lugha inajengeka kama mfumo wenye ukinzani na unaotofautisha maana.

Nadharia ya Udenguzi imesaidia mtafiti kupata mitazamo mipya kuhusu itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Kwa kuhakiki upya methali hizi ambazo zimehusishwa katika utafiti huu, imebainika wazi kwamba wanawake na wanaume wanadhihirisha haja ya kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, wanapaswa kuwa na haki na hadhi sawa katika mahusiano yao. Nadharia hii imebainisha wazi mahusiano ya wanaume na wanawake katika masuala ya kuzaa, kulea ndoa, kazi na uongozi. Kwa ujumla,

nadharia hii ya Udenguzi imedhihirisha mitazamo mipya kuhusu wanawake katika jamii na uhusiano wao na wanaume. Itikadi zinazopendekeza wanaume kuwa mbele kimamlaka na kihadhi zinadhihirika kuwa na athari za ubabedume ambao unafanya mahusiano ya kiuana kuonekana ya kawaida ilhali si sahihi kwa misingi ya nadharia ya itikadi  na hazisababishi kuwepo kwa usawa wa kiuana kati ya wanawake na wanaume.

## 2.5 Hitimisho

Sura hii, imeshughulikia yaliyoandikwa yenye uhusiano na mada ya utafiti. Mtafiti aliweza kupitia na kuhakiki kazi za wataalamu mbalimbali pamoja na tafiti zilizofanywa ambazo zinahusiana na utafiti huu. Katika kazi mbalimbali mtafiti amehusisha tafiti, makala na vitabu mbalimbali vinavyozungumzia itikadi za kiuana, mahusiano ya kiuana, ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana ili kuweza kubainisha suala la utafiti. Maandishi haya yamefaa sana utafiti huu sana sana kwa kumulika tafiti kadhaa kuhusu methali na suala la itikadi za uana. Katika utafiti huu imeonyeshwa kwamba watafiti kadhaa ambao wamechunguza kuhusu itikadi za kiuana, wengi wao wameshughulikia itikadi za kiuana kwa kuchunguza usawiri na hadhi au ya wanaume ama ya wanawake katika methali. Mapitio hayo yamebainisha kwamba itikadi za kiuana vile zinaendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi ni suala ambalo halidhihiriki. Isitoshe, katika tafiti hizo ukinzani wa itikadi za kiuana haushughulikiwi. Wengine wameshughulikia itikadi kwa kuchunguza mambo mengine. Sura hii pia imeshughulikia nadharia zilizotumika katika utafiti huu. Hizi ni: Nadharia ya Itikadi kwa mujibu wa Gramsci, (1971) na Althusser,

(1981), Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika Steady, (1981) pamoja na nadharia ya Udenguzi Abrams na Harpham (2014).

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Tafiti za awali kuhusu masuala ya uana na methali zimejikita kwa kubainisha ubaguzi na unyanyasaji wa wanawake na kuonyesha wanaume kama wenye uwezo na mamlaka wakichukua nafasi ya mbele katika jamii. Tafiti chache zimechunguza mahusiano ya kiuana na itikadi za kiuana (Malenya, 2020) lakini itikadi za kiuana namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi ni suala ambalo limekuwa halijashughulikiwa. Wanawake na wanaume wanashawishika kutwaa nafasi zao na kushughulikia majukumu yao, wanawake wakiwa kwenye nafasi ya kutumikia wanaume. Wanaume wao hubainika kuwa wenye mamlaka. Mahusiano hayo yanadhihirishwa katika utafiti huu kuwa ni ung'amuzi potoshi. Aidha, ni tafiti chache sana ambazo zimeshughulikia ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake vile unaibuka katika methali. Basi, utafiti huu umelenga kuziba pengo hili kwa kuteua mbinu zinazoongoza kujadili mahusiano ya kiuana kati ya wanawake na wanaume.

Sura hii inashughulikia mbinu ambazo zimetumiwa katika kufikia malengo ya utafiti huu kwa kukusanya, kuchanganua, kufasili na kuwasilisha matokeo ili kuweza kubainisha itikadi  mbalimbali za kiuana pamoja na kudhihirisha namna itikadi hizo zinaendeleza mahusiano ya kiuana kwa njia ya ukubalifu na ushawishi na kuonesha kuwa mahusiano hayo ni ya kiung'amuzi potoshi. Sehemu zifuatazo za sura hii zinafafanuliwa kwa kina: muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli lengwa, mbinu za usampulishaji jinsi data ilivyokusanywa, vifaa

vya utafiti vilivyotumiwa katika ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa Data, uzingativu wa maadili na hitimisho.

### 3.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni mpangilio kuhusu namna data inavyokusanywa na kuchanganuliwa. Unaonesha sababu ya kushughulikia mada na lengo la utafiti kwa utaratibu; yaani ni mfumo ambamo utafiti unaendelezwa (Kothari, 2004). Huu ni mpango ambao unabainisha maeneo na aina ya data inayohusiana na suala la utafiti. Muundo wa utafiti pia ni mkakati ambao unaonesha mfumo unaotumiwa katika kukusanya na kuchanganua data. Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo. Kulingana na Mugenda na Mugenda (1999), muundo wa kimaelezo ni utaratibu wa kukusanya data ili kuweza kujibu maswali kuhusu hali ya dhana zinazochunguzwa. Muundo huu hudhamiria kuelekeza mtafiti kufahamu mazingira ya wahojiwa kwa kushiriki binafsi katika ukusanyaji wa data. Utafiti wa aina hii hutegemea maoni ya wahojiwa kuhusu tatizo linalochunguzwa kwa kusikiliza na kurekodi kwa makini maoni ya watoa taarifa, hatimaye mtafiti kuweza kuibua maana kutoka kwa data aliyokusanya (Cresswell, 2014). Katika utafiti huu washiriki walihojiwa na kujadiliana nao huku maoni yao yakirekodiwa. Itikadi mbalimbali za kiuana zimechunguzwa na kudhihirisha vipi itikadi hizo zinaendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi pamoja na kuonyesha kuwa itikadi hizo zinachukuliwa kiung’amuzi potoshi katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Data ambazo zimepatikana kulingana na uhakiki wa methali na kutoka kwa watoa taarifa, zimeweza kubainisha itikadi za kiuana zinazoelezwa katika methali

za Kinyankole na Kiswahili na kudhihirisha kuwa zinaendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu pamoja na kuonesha methali namna zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuna. Hatimaye, hitimisho baada ya kila maudhui muhimu yanayotokana na uchanganuzi wa data katika uhusiano na malengo ya utafiti linaelezwa kwa kina. Pia muundo huu wa kimaelezo umetoa ufafanuzi wa tabia, mitazamo, maadili na sifa za wanaume na wanawake katika jamii tafitiwa. Kwa hivyo, muundo huu umeweza kuongoza utafiti huu katika kuchunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

**3.2 Eneo la Utafiti**

Ukusanyaji wa methali na maoni ya wahojiwa yamehusisha maeneo ya maktabani na nyanjani. Hivyo, utafiti huu umefanyiwa maktabani na nyanjani. Maktabani, mtafiti ameweza kudurusu majarida vitabu na makala yenye uhusiano na utafiti huu. Mbinu hizi mbili za kukusanya data zinaelezwa hapa chini. Katika kutekeleza usomaji huu, mtafiti amehusisha maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta nchini Kenya, maktaba na makavazi ya Waswahili ya Fort Jesus, Maktaba ya Taifa iliyoko Mombasa, makavazi ya Lamu na maktaba ya Lamu, maktaba ya Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda na Makavazi ya Ankole.

Fauka ya hayo, tafiti ambazo zimeshughulikia masuala ya itikadi, uana na methali pamoja na utamaduni zimerejelewa. Utafiti wa maktabani umelenga kutupatia mwongozo zaidi kuhusu itikadi za kiuana katika methali. Aidha, utafiti wa maktabani umesaidia mtafiti kusoma vitabu, tasnifu na makala mbalimbali kuhusu mada ya utafiti, uamilifu wa nadharia na maandishi ya kimsingi kuhusu mada tafitiwa. Maandishi, hususani tasnifu, majarida na machapisho mengine

yamedurusiwa. Makala pia yamesomwa pamoja na vitabu na majarida kwenye mtandao ili kuelekeza utafiti huu zaidi, kuhusiana na nadharia ya Itikadi, Ufeministi wa Kiafrika na nadharia ya Udenguzi katika uhusiano na utafiti huu kwa lengo la kufahamu na kuhusisha uamilifu wa mihimili ya nadharia lengwa.

Nyanjani, maoni mbalimbali yamepatikana kuhusu amali za kiutamaduni za jamii tafitiwa na itikadi za kiuana. Ili kufanikisha shughuli hii, maeneo yafuatayo yametembelewa: nchini Uganda, utafiti huu umefanyiwa magharibi mwa Uganda kwenye Kata ndogo ya Engari, kata ya Kitongore wilayani Kiruhura; Kabwohe na Bisharara- Bugongi wilayani Sheema. Kwa upande wa pwani ya Afrika Mashariki tumelenga na kushirikisha Waswahili katika maeneo ya Kiembeni na Mombasa mjini katika Kaunti ya Mombasa, Mitaa ya Mtamuini na Mkunguni, katika Kaunti ya Lamu nchini Kenya na Bububu, Zanzibar nchini Tanzania. Wasailiwa waliweza kuchaguliwa katika maeneo haya kimaksudi kwa kutumia viongozi wao. Maeneo haya yamekuwa na mchango muhimu katika kufanikisha utafiti huu.

Maoni ya wahojiwa kuhusu itikadi za kiuana katika jamii za Wanyankole na Waswahili yameweza kupatikana katika sehemu hizo pamoja na uteuzi wa baadhi ya methali za kiuana. Wasailiwa wamehojiwa na kujadiliana nao kwa ajili ya kubainisha itikadi za kiuana, mahusiano ya kiuana yanayoendelezwa na itikadi za kiuana katika methali za jamii zao na namna ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana katika methali. Mahojiano yamekuwa ya moja kwa moja kwa kutangamana na wasailiwa. Mwongozo wa maswali umetumiwa kwa ajili ya kufanikisha mahojiano hayo pamoja na majadiliano. Mtafiti

ameweza kupata data ya utafiti huu kuhusu itikadi za kiuana za Wanyankole na Waswahili pamoja na baadhi ya methali zinazohusu uana. Lamu ni eneo ambalo limenufaisha utafiti huu kwa kupatikana kwa maarifa muhimu yanayohusiana na historia na utamaduni wa Waswahili. Kuna maandishi mengi ya kihistoria ambayo yamehifadhiwa kwenye makavazi ya Lamu. Maarifa ya msingi yamepatikana kwenye makavazi ya Lamu kuhusu elimu pana ya historia na utamaduni wa Waswahili kwa sababu mji unahifadhi historia yake asili ukilinganishwa na maeneo mengine ya Uswahilini (Ghaidan, 1974). Kwa hivyo, amali za Waswahili na mahusiano yao ya kijamii yamepatikana sehemu hizo. Data ya utafiti huu imefafanuliwa kwa misingi ya Kiswahili sanifu.

### 3.3 Sampuli Lengwa

Mtafiti ameteua na kudurusu vitabu vyenye methali za Kinyankole na Kiswahili kuhusu itikadi za uana kwa njia ya kimakusudi. Vitabu hivi ni Enfumu z'omurunyankore Rukiga ( Saite, 1989), Kamusi ya methali za Kiswahili ( King'ei na Ndalu, 1989), Kamusi ya methali Wamitila (2001) na Dafina Hazina ya Kiswahili (Al Habsy, 2012). Vitabu hivi vimesomwa kwa makini zaidi kwa kurejelea maana inayoibuliwa katika uhusiano na itikadi za kiuana, data ya msingi ambayo imelengwa kuhusu utafiti huu. Pamoja na hayo, utafiti huu umelenga na kushirikisha wahojiwa katika jamii ya Wanyankole kwenye Kata ndogo ya Engari, Kata ya Kitongore, wilayani Kiruhura; Kabwohe na Bisharara Bugongi wilayani Sheema. Kwa upande wa pwani ya Afrika Mashariki utafiti umelenga na kushirikisha Waswahili katika maeneo ya Kiembeni na Mombasa mjini katika Kaunti ya Mombasa, Mitaa ya Mtamuini na Mkunguni, katika Kaunti ya Lamu nchini Kenya na Bububu, Zanzibar nchini Tanzania. Wahojiwa

hawa wamelengwa kutoa maoni yao kuhusu itikadi mbalimbali katika methali za jamii husika katika muktadha wa tamaduni zao. Maeneo haya yamehusishwa na kuchagua wahojiwa 40 kimaksudi kwa njia ya sampuli mkufu ili kuendeleza mahojiano na majadiliano.

Suala la uteuzi wa idadi ya wahojiwa ni muhimu. Mbinu teule ambazo zinatumiwa kukusanyia data na aina ya wahojiwa wanaolengwa kushirikisha, inasaidia kuteua idadi maalumu ya wahojiwa (Creswell, 20014). Utafiti huu, umefikia idadi ya 40 kutokana na kujirudia kwa mawazo ya wahojiwa walioshirikishwa wakati wa mahojiano. Yeye Kothari (2004) anasema kwamba katika utafiti wa kimaelezo kwa kutumia usampulishaji wa kimaksudi kwa njia ya sampuli mkufu, idadi ya wahojiwa inaamuliwa na uradidi wa mawazo wakati wa kuendeleza mahojiano. Kwa maoni hayo, mtafiti amefikia idadi ya wahojiwa 40 pale ambapo mawazo ya wahojiwa yaliweza kujirudia wakati wa mahojiano. Hatimaye, mtafiti aliweza kubaini kuwa hakuna mawazo mapya yaliyoweza kuongezeka. Warren (2002) anapendekeza kwamba idadi ya wahojiwa inatakiwa kuwa kati ya 20 na 30. Utafiti huu umelenga ufahamu wa kina wa Itikadi za kiuana namna zinavyobainika na namna zinaendelezwa kwa ushawishi na ukubalifu na maarifa haya tumetegemea wahojiwa. Kimsingi, katika utafiti kunahitajika data ya kutosha kuthibitisha matokeo ya utafiti na kutolaumiwa kuwa matokeo ya utafiti yanaegemea maoni ya wahojiwa wachache (Kothari, (2004). Pamoja na hayo, data ya methali imekusanywa na kuchambuliwa maktabani. Data hii imechangiana na data ya nyanjani kupitia kwa mahojiano. Kwa hivyo, wahojiwa 40 walitosha kuchunguza itikadi za kiuana katika methali. Mahojiano na majadiliano yanatumiwa kama mbinu za msingi za kukusanya data

nyanjani kwa sababu ya uwezo wake wa kuzalisha taarifa ya kina kutoka kwa wahojiwa kuhusu maoni yao juu ya mada fulani (Creswell, 20014). Cresswell anaendelea kueleza kuwa mbinu hasa ya mahojiano kwa muda mrefu inahusishwa na utafiti wa kimaelezo ambao unalenga ufafanuzi wa maana, maoni na tajriba juu ya jambo fulani linalochunguzwa. Kwa hivyo, maoni ya wahojiwa yameweza kukusanywa kwa kina kuhusu itikadi za kiuana, mahusiano ya kiuana na methali za kiuana kwa kuongozwa na mbinu ya mahojiano. Watafiti wasaidizi pia wameweza kuteuliwa sana sana wa kike katika maeneo ya Mombasa, Lamu na Zanzibar ambao wamesaidia kupata data kutoka kwa wahojiwa wa kike katika maeneo hayo. Data ilikusanywa wakati wa kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani. Mtafiti angepata ugumu kuhoji wahojiwa wa kike moja kwa moja kwa sababu ya kutoonekana kwa maeneo ya umma kama mila ya Waswahili iliyoathiriwa na dini ya Kiislamu inavyowataka.

### 3.4 Mbinu za Usampulishaji

Utaratibu wa uteuzi wa sampuli uliongozwa na madhumuni ya utafiti. Madhumuni ya utafiti yamelenga kuchunguza itikadi za kiuana na kubainisha mahusiano ya kiuana yanavyoendelezwa na itikadi za kiuana kwa ukubalifu katika methali za Kinyankole na Kiswahili na kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili namna zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana. Mkakati wa uteuzi wa sampuli lengwa katika utafiti huu ni wa kimaksudi. Mtafiti ameweza kuteua vitabu vya methali na uchaguzi wa methali za kiuana kwa njia ya kimaksudi.

Kulingana na mwongozo huo wa kimaksudi wa uteuzi wa vitabu vya methali, uchambuzi na uhakiki wa makini wa methali umefanywa na kuibuka na methali 80 za Kinyankole na methali 70 za Kiswahili za kiuana katika vitabu teule. Vitabu vya methali ambavyo vimezingatiwa ni; 'Enfumu z'omurunyankore Rukiga' Saite (1989). Kitabu hiki ni marejeleo ya msingi kwa sababu kimekusanya methali nyingi za Kinyankole na ndicho kikubwa zaidi. Kamusi ya Methali za Kiswahili ( King'ei na Ndalu , 1989) na Kamusi ya Methali (Wamitila, 2001) zimerejelewa kwa upande wa methali za Kiswahili kutupatia data ya msingi. Vitabu hivi pia hadi sasa ndivyo vinatoa urejezi mzuri wa methali za Kiswahili. Imekuwa rahisi kuchagua methali za kiuana katika vitabu hivi kwa sababu ya mpangilio wa methali katika mtindo wa kiabjadi. Pamoja na vitabu hivi muhimu vya methali, kitabu cha Dafina Hazina ya Kiswahili kitabu cha Al Haj Al Habsy (2012) kimerejelewa kuongeza methali zaidi za kiuana. Utafiti huu umeweza pia kukusanya methali 12 za Kinyankole na methali 10 za Kiswahili kutoka nyanjani kwa njia ya mahojiano. Methali hizo hazipatikani katika machapisho yoyote ya awali na zinabainisha itikadi muhimu katika jamii husika. Jumla ya methali 174 zinazohusu uana katika vitabu vya methali pamoja na nyanjani kutoka kwa wahojiwa zimehakikiwa.

Uchanganuzi wa methali za Kinyankole na Kiswahili kuhusu itikadi za kiuana umetegemea maudhui muhimu ambayo yameibuliwa kulingana na malengo ya utafiti huu. Methali hizo zimeweza kubainisha Itikadi za kiuna zinazoendeleza mahusiano ya kiuana kwa njia ya ushawishi na Ukubalifu pamoja na kudhihirisha ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana. Isitoshe mbinu ya kimaksudi imetumiwa kuteua na kusaili wahojiwa 40 nyanjani

kutokana na tajriba na umahiri wao kuhusu methali za jamii pamoja na uzoefu wao wa tamaduni, desturi na mila za jamii zao.

Nyanjani, mtafiti amelenga kupata data kuhusu maoni ya wahojiwa kuhusu amali za kijamii, itikadi mbalimbali za kiuana pamoja. Aidha, mtafiti amelenga kupata data zaidi ya methali ambazo hazipatikani kwenye vitabu vya methali kwa sababu waandishi wa vitabu ambavyo vimerejelewa nia yao ilikuwa ni kukusanya methali kwa ujumla wala hawakulenga methali za kiuana tu. Mtafiti ameweka wahojiwa katika vikundi viwili ili kufanikiwa kupata data kutoka kwao. Kikundi cha kwanza ni cha wahojiwa 20 wataalamu kuhusu masuala ya uana, mila na tamaduni za jamii zao wenye umri wa kimo wa kiume na wa kike kwa kuzingatia kigezo cha umri na sifa ya kijinsia. Kikundi cha pili ni cha wasomi 20 ambao ni wabobezi katika taaluma ya fasihi simulizi na masuala ya uana. Wasomi hawa wamechaguliwa wanne katika kila eneo kwa kuzingatia jinsia ambao wameweza kutoa ufafanuzi wa amali za kijamii, mila, tamaduni na kutoa maoni yao kuhusu itikadi za kiuana katika methali za kiuana kitaaluma. Wahojiwa wanane wameteuliwa katika kila eneo, wanne wa kiume na wanne wa kike kwa kila kikundi. Hao wameteuliwa kwa sababu ya uzoefu wao wa muda mrefu na tajriba kuhusu tamaduni na amali za kijamii wanamoishi kuhusu masuala ya itikadi na uana. Mtafiti amemteua kiongozi mmoja katika kila eneo la utafiti kwa njia ya kimaksudi baada ya kuelekezwa kwao na kiongozi wa kituo cha polisi. Viongozi wamepatikana kupitia kwa vituo vya polisi. Viongozi hao wamekuwa nguzo muhimu katika kutambua wahojiwa wenye umri wa kimo walio na maarifa kuhusu lugha, historia, utamaduni na amali za kijamii kwa jumla. Baadaye, viongozi walisaidia mtafiti kutambua wahojiwa wengine kwa ajili ya mahojiano.

Ukusanyaji na uchanganuzi wa data umetegemea mwongozo wa maswali ambayo yameteuliwa**.** Uchanganuzi wa kila methali umeegemezwa maoni ya wasailiwa tofauti kwa kuzingatia malengo ya utafiti na nadharia teule. Kupitia njia ya kutangamana na kuwahoji Wanyankole wenyeji wa Kiruhura na Sheema, pamoja na Waswahili wa Mombasa, Lamu na Zanzibar, mtafiti amechunguza na kufahamu zaidi misingi ya kitamaduni na amali ambazo methali zimejikita. Mielekeo, tabia, mila na desturi za jamii hizo zimeweza pia kufahamika; Itikadi zao na mtazamo wao kuhusu mahusiano ya mwanamke na mwanamume katika jamii kwa kuzingatia Uzazi na Malezi; Ndoa; Uongozi na mamlaka; Uzalishaji wa mali pamoja na ukuzaji wa jamii kwa misingi ya kijamii. Taarifa ambazo zimepatikana zimechangia kubainisha suala la utafiti kuhusu Itikadi za kiuana zinazoendeleza mahusiano ya kiuana kwa ushawishi na ukubalifu katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Wasailiwa wameweza kutoa maoni yao kuhusu itikadi za kiuana katika muktadha wa jamii za Wanyankole na Waswahili, data ambayo imefaidi katika uchanganuzi wa methali kuhusu suala tafitiwa. Pia, kutoka kwa wahojiwa tumeweza kupata methali za ziada kuhusu suala la uana na methali hizi hazipatikani katika vitabu hivi vya methali.

### 3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu umelenga kukusanya aina mbili za data. Data ya kwanza imekuwa ni ukusanyaji wa methali katika vitabu vya methali pamoja na baadhi ya methali nyanjani. Data ya pili ni maoni ya wahojiwa kuhusu amali za kiutamaduni na mila pamoja na itikadi za kiuana kati wa wanawake na wanaume. Data ya utafiti huu imekusanywa kutoka maktabani kwa kudurusu na kuhakiki kwa makini data kutoka katika vitabu teule vya methali ambavyo ni: Enfumu z’omurunyankore

Rukiga (Saite, 1989), Kamusi ya Methali za Kiswahili ( King'ei na Ndalu, 1989) Kamusi ya Methali (Wamitila, 2001) na Dafina Hazina ya Kiswahili (Al Haj Al Habsy 2012) kwenye maktaba za Ankole (Ankole Cultural Trust Centre), maktaba na makavazi ya Waswahili (Lamu Museum, Lamu Library na Malindi). Utaratibu ufuatao wa kuteua methali za kiuana umetumiwa. Methali za kiuana ambazo zinazungumzia wanaume na wanawake ziliandikwa kwenye daftari. Pamoja na kuandika methali hizo, itikadi tofauti zilinukuliwa kama zinavyoelezwa katika kila methali na maudhui yanayoibuliwa na methali. Methali hizo zimeweza kuonyesha itikadi za kiuana, mahusiano ya kiuana na ukinzani wa itikadi za kiuna na athari zake kwa usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Mbinu hii imepewa kipaumbele kwa sababu mtafiti ameweza kupata na kuchanganua methali za kutosha kama data ya msingi ambayo imetegemewa katika utafiti huu. Nyanjani, pamoja na kupata maoni ya watoa taarifa kuhusu itikadi za kiuana methali za ziada zimepatikana ambazo zinakosekana katika vitabu vya methali maktabani. Data imepatikana kutoka kwa wasailiwa moja kwa moja. Mtafiti ametumia vinasa sauti ili kufanikiwa kupata data hii. Maoni ya wahojiwa yamekuwa na mchango katika kufafanua juu ya itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili kwa muktadha wa utamaduni wa jamii husika.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Data ambayo imechanganuliwa ni methali pamoja na maoni ya wahojiwa kuhusu itikadi za kiuana. Data hii imewezesha mtafiti kuchunguza itikadi za kiuana na kudhihirisha mahusiano ya kiuana namna yanaendelezwa kwa njia ya ukubalifu na ushawishi katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Pia, mtafiti ameweza

kuhakiki methali kudhihirisha namna ukinzani wa itikadi za kiuana unavyoibuliwa na athiri zake kwa usawa wa kiuana. Katika matayarisho ya uchanganuzi wa data, muundo maalumu umezingatiwa ambao umesaidia katika mchakato wa uchanganuzi. Kwanza, methali za Kinyankole zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu utafiti huu umehusisha lugha mbili tofauti yaani lugha ya Kinyankole na lugha ya Kiswahili. Baada ya kutafsiri methali hizo, zimeainishwa pamoja na zile za Kiswahili na kuziibulia maudhui. Methali zimechanganuliwa kulingana na itikadi za kijamii, kiuchumi na uongozi katika utaratibu huo kwa kuzingatia malengo ya utafiti na kuongozwa na nadharia za itikadi na Uana. Uchanganuzi huu umelenga kujibu maswali ya utafiti yaliyoibuliwa kulingana na malengo ya utafiti kuhusu itikadi za kiuana kama zinavyobainika katika methali za Kinyankole na Kiswahili na hatimaye kutoa muhtasari. Imedhamiriwa kuonyesha itikadi za kiuana, kudhihirisha namna mahusiano yanayoendelezwa na itikadi za kiuana kati ya wanaume na wanawake na kubainisha kwamba mahusiano hayo yanatokea kwa ukubalifu na ushawishi. Fauka ya hayo, uchanganuzi huu umedhihirisha namna ukinzani wa itikadi za kiuana unavyotokea na athari zake kwa usawa wa kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

Aidha, nadharia ya itikadi imetumika katika uchanganuzi wa data kuonyesha jinsi itikadi zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake kwa ukubalifu na kushawishika, Pia, nadharia ya itikadi imeongoza utafiti huu kudhihirisha uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala kuwa unatimizwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii yaani utawala unaathiriwa na ung’amuzi potoshi. Mchakato huu wa kiitikadi unapotosha watu wa tabaka la chini katika

jamii na kuficha masuala ya msingi kuhusu unyonyaji na unyanyasaji katika mahusiano ya kijamii kati ya matabaka. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa upande mwingine imefaa utafiti huu kuonyesha athari za uana katika hatua mbalimbali za maisha yetu kwa kushirikisha wanawake na wanaume kwa pamoja. Pia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imeweza kudhihirisha kwamba uana si suala la kimaumbile bali ni matokeo ya mchakato wa kijamii ambapo binadamu wanatengewa majukumu. Vilevile, utafiti umeonyesha haja ya wanaume na wanawake kushughulikia majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana. Ushirikiano huu haupaswi kuangalia na kusisitiza majukumu ya kimaumbile kama kiini cha kutenga majukumu ya kiuana. Mwisho, nadharia ya Udenguzi imeongoza utafiti huu kwa kuhakiki methali ili kuibua ukinzani na athari zake kwa usawa wa kiuana.

### 3.7 Vifaa vya Utafiti

Vifaa tofauti vimetumika ili kuweza kutekeleza utafiti huu. Daftari na kalamu vimetumika ili kuweza kunukuu methali na hoja muhimu maktabani na nyanjani kuhusu utafiti. Pia mtafiti ametumia talakilishi kuchakata data ya utafiti. Nyanjani, mwongozo wa maswali umetumika kwa ajili ya kuwahoji wasailiwa. Pamoja na hayo, mtafiti ameweza kutumia vinasa sauti ili kuweza kurekodi washiriki na kuhifadhi maoni yao. Simu imetumiwa pia kuendeleza mahojiano pale ambapo usafiri umekuwa haupo kwa sababu ya ugonjwa wa UVIKO 19.

### 3.8 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti kwa kuzingatia nadharia ya Itikadi na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika pamoja na Nadharia ya Udenguzi kwa njia ya kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu

yamewasilishwa kwa njia ya kimaelezo kwa kuwa sehemu kubwa ya utafiti imekuwa ni uchambuzi wa maudhui ya kiitikadi maktabani. Maudhui yameweza kuchambuliwa katika methali za Kinyankole na Kiswahili.

### 3.9 Uzingativu wa Maadili ya Utafiti

Sehemu hii inafafanua namna tumezingatia suala la maadili ya utafiti. Katika matayarisho ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data, utafiti huu umeweza kuendelezwa kwa uzingativu wa maadili yake kwa hali ya juu sana. Mtafiti amefanya hivi kwa kuhifadhi utambulisho wa wahojiwa, haki zao na ufaragha wao. Mtafiti amepata kwanza kuidhihishwa na chuo mwezi wa Mei 2018 kutoka Shule ya mafunzo ya juu, chuo kikuu cha Kenyatta ili kumuwezesha kupata ruhusa na cheti cha NACOSTI kuruhusiwa kwenda nyanjani. Nchini Uganda, mtafiti alipata wepesi wa kufikia wahojiwa na kutangamana nao kwa sababu ya uzoefu na mazingira ya nyumbani na baadhi ya masuala ya itikadi za kiuana katika jamii ya Wanyankole. Katika maeneo ya Uswahilini mtafiti hakuwa na uzoefu wa maeneo hayo kwa hivyo, ilibidi ajitambulishe kwa viongozi wa mitaa ambao walituelekeza kwa wahojiwa kirasmi. Nyanjani, aliomba idhini ya kila mhojiwa amkubalie kumhoji kuhusu mada baada ya kumfahamisha kuhusu lengo la utafiti, masuala muhimu ya kujadili, uhuru wao wa kushiriki yaani zoezi la mahojiano halikuwa la lazima. Pia wahojiwa walifahamishwa kuwa kujibu maswali ilikuwa ni hiari yao. Walihakikishiwa kwamba utambulisho wao hautatolewa hadharani bila idhini yao pamoja na kuhifadhi data zilizotoka kwao kwa mfano taarifa zilizonaswa na kuhifadhiwa walihakikishiwa kuwa zingetumiwa kwa lengo la utafiti huu wa kiakademia tu.

### 3.10 Hitimisho

Katika sura hii, mbinu zilizotumiwa katika utafiti zimeshughulikiwa. Hatua na taratibu mbalimbali zimeonyeshwa ambazo mtafiti alipitia kuweza kufanikisha utafiti. Ameeleza muundo wa utafiti kwamba utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo. Mtafiti ameweza kuhoji wahojiwa na kurikodi maoni yao kwa kina ili kuchunguza namna itikadi za kiuana zinaendeleza mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu na ushawishi, ambao ni ung'amuzi potoshi. Eneo la utafiti limeonyeshwa kuwa ni maktabani na nyanjani ambapo maktabani vitabu kadhaa, machapisho, vitabu maalumu vya methali vilivyosomwa. Vilevile mtafiti ameonesha maeneo aliyohusisha kwenye utafiti. Katika maeneo haya mtafiti aliweza kupata maoni ya wahojiwa kuhusu itikadi za kiuana pamoja na kunukuu baadhi ya methali za kiuana nyanjani. Aidha, ameonesha sampuli lengwa kuwa ni vitabu vinne vya methali. Mbinu ya usampulishaji ya kimaksudi imeelezwa namna ilivyotumiwa katika utafiti kwa kutumia sampuli mkufu. Mtafiti aliweza kutumia vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuhoji na kuhifadhi maoni ya wahojiwa, kunukuu methali na hoja muhimu maktabani na nyanjani. Aidha mtafiti ameweza kuonesha namna alivyotekeleza uchanganuzi wa data kwa mujibu wa malengo ya utafiti kwa kuongozwa na nadharia teule. Hatimaye mtafiti ameonyesha namna alivyoweza kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa njia ya kimaelezo.

# SURA YA NNE

# MATOKEO YA UTAFITI ITIKADI ZA KIUANA

## 4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia inahusu mbinu ambazo zilitumika katika utafiti. Sura hii inahusu matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo ya utafiti na inajikita katika lengo la kwanza kwa kubainisha itikadi za kiuana. Mtafiti katika sura hii ya nne anajadili na kubainisha itikadi mbalimbali za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Mjadala na uhakiki kuhusu methali za kiuana umezingatia upeo wa ubainishaji wa itikadi za kiuana katika kila methali. Suala la idadi mahsusi ya methali katika kila jedwali halijazingatiwa katika kuhakiki hizo methali. Hii ni kwa sababu itikadi fulani zimebainika kupitia methali kadhaa ilhali itikadi zingine zimeshahidiwa kwa methali chache. Methali hizi zimefafanuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya Nadharia za Itikadi na Ufeministi wa Kiafrika ili kuweza kudhihirisha itikadi hizo. Majukumu, haki na hadhi ya wanawake na wanaume katika jamii za Wanyankole na Waswahili vimezingatiwa katika kudhihirisha namna itikadi za kiuana zinavyoendelezwa kwa njia ya ushawishi na ukubalifu. Kwa ujumla, sura hii inabainisha methali zinazohusu itikadi za kiuna na maudhui kuhusu masuala ya ndoa, uzazi, malezi na utunzaji wa watoto, wazazi wa kambo, uongozi, uzalishaji wa mali, uhuru, ukuzaji na maendeleo ya jamii.

Methali zinatumiwa katika mawasiliano ya kawaida katika maeneo kadhaa (Karwemera, 1994). Vile methali zinatumika sana katika mawasiliano ya kila siku ya Wanyankole mawazo, amali na sifa za kiuana zinajidhihirisha na

kuwasilishwa moja kwa moja katika methali za Kinyankole. Ilimuia rahisi mtafiti kurejelea methali za Kinyankole ili kubainisha itikadi zao za kiuana. Kuwepo kwa wingi wa methali katika jamii za Wanyankole ni dhahiri kwamba methali ni utanzu wa fasihi simulizi ambao uko karibu sana na wanajamii. Matumizi yake katika lugha yanawawia rahisi kwa sababu ya uwamilifu wake na upatikanaji wake wa karibu. Kwa hivyo, itikadi za kiuana zimeweza kudhihirika waziwazi katika methali hizo kutokana na ukweli kwamba methali za Wanyankole ni sehemu muhimu ya jamii zinazowasilisha utamaduni wao. Itikadi za kiuana namna zinavyobainisha, mahusiano ya kiuana, amali za Wanyankole misimamo yao ilitambulika na kutathiminiwa kwa urahisi.

Mwanamke akiolewa kulingana na mila ya Kinyankole anatarajiwa kuzaa watoto wengi ili kuendeleza familia. Imani hii ya kuzaa watoto wengi pamoja na kupatia kipaumbele watoto wa kiume inaelezwa na (Kirindi, 2008). Imani hii inashikiliwa kwa madai ya kuendeleza familia na ukoo wa upande wa mwanamume. Kwa hivyo, wanaume wanajitahidi kutafuta wake kutoka katika familia ambazo inaaminika kuwa na wake wenye uwezo wa kuzaa ili waweze kupata watoto wengi. Zipo methali anuwai za Kinyankole ambazo zinawasilisha itikadi za kiuana kuhusu ndoa. Itikadi za kiuana kuhusu suala hili katika methali za Kinyankole zinajadiliwa kama ifuatavyo:

### 4.1 Itikadi za Kiuana na Suala la Ndoa

Ndoa inachukuliwa kuwa chanzo cha uendelezaji wa jamii. Ukomavu wa wanaohusika katika ndoa pamoja na kuwajibikia majukumu yao ni mambo muhimu. Katika jamii ya Wanyankole mwanamke anarejelewa sana katika

kuendeleza ndoa na anachunguzwa tabia zake kama zinafaa au hazifai kwa kuzingatia viwango vya utamaduni wa Wanyankole. Kuna sifa ambazo zinatambulika na kukubalika kulingana na mila za Wanyankole kwa binti ambaye anafaa kuolewa. Kulingana na maoni ya Kirindi (2008), sifa hizi ni kama vile utiifu, heshima, ukimya, utulivu na kutokuwa mzururaji. Nyingine ni uwezo wa kutunza nyumba na kushughulikia maslahi ya mume wake. Imani hii inamfanya mwanamume kushawishika kuwa makini kuchagua mke wa kuoa ambaye anakidhi sifa tajwa. Angela (2018) anaeleza kwamba mwanamume anatarajiwa kuwa makini wakati anachagua mke wa kuoa kwa sababu mke ana nafasi muhimu ya kudumisha ndoa. Katika mahojiano yaliyofanyika wilayani Kiruhura tarehe 18 Aprili, 2018 mhojiwa wa kiume KRH 2, alieleza kuwa katika jamii ya Wanyankole, wazazi wa kiume pamoja na ndugu zao huzingatia misingi ya kitamaduni. Hivyo, mwanamume anahisi kuwa ni yeye anapaswa kuwa na haki ya kuchunguza na kuchagua mke wa kuoa. Mwanamume huchukua muda mrefu kuchunguza aina ya msichana ambaye ataolewa na mtoto wao. Itikadi hii inaelezwa katika Jedwali Na.1 kama ifuatavyo:

**Jedwali 1: Methali kuhusu Itikadi za Ndoa**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Owashwera abuuza.* | Atakaye kuoa hudadisi. |
| 2. | *Omwishiki ku akura ashwerwa.* | Msichana akishakua huolewa. |
| 3. | *Enyamwonyo ku ekura eribwa omwishiki ku akura ashwerwa.* | Ndizi ikiwa tayari huliwa msichana akikua huolewa. |
| 4. | *Nkunda taata na maawe hona tashwerwa nabo.* | Nawapenda baba na mama haolewi nao. |
| 5 | *Emwe y'owibanye nekira igana ry'owa tata.* | Ng'ombe mmoja wa mume wangu ni bora kuliko mia wa baba. |

Methali ya (1) inadhihirisha itikadi ya mwanamume kuwa na usemi na uamuzi kuhusu aina ya mke anayetaka kumuoa. Itikadi hii inaoneshwa na uwezo wa kudadisi anaopewa mwanamume kuhusu mke anayetarajia kuoa. Matarajio ya jamii pamoja na mwanamume ni kuweza kutambua na kugundua sifa na tabia zinazokubalika na zile zisizokubalika za mwanamke ili kuepukana na matatizo ya kudumu ya ndoa. Mhojiwa KRH 3 kutoka wilayani Kiruhura tarehe 17 April, 2018 alieleza kwamba, Wanyankole walikuwa na tabia ya kuchunguza mke wa kuoa. Maoni ya mhojiwa yalilenga kueleza kuhusu amali hiyo kama inavyofafanuliwa katika methali (1). KRH alifafanua kwamba, uchunguzi kuhusu mke wa kuoa ulifanyika ili familia ya mwanamume wapate habari kuhusu mienendo ya familia wanakotarajia kuoa hasa tabia za msichana. Walifanya uchunguzi huu kwa kuogopa magonjwa na tabia mbaya kama vile uchawi na umalaya. Udadisi huu ulikuwa unafanywa kabla ya kuonesha nia ya kutaka kuoa.

Itikadi ya kufanya udadisi, hadi sasa inachochea wanaume wanaotarajia kuoa, kutaka kumfahamu zaidi mke mtarajiwa. Kulingana na Nadharia ya Itikadi, mhimili kuwa, uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unaotimizwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii unaafikiana na mawazo katika methali. Itikadi hii inaonesha kwamba wanaume wanakuwa na mamlaka ya kuchagua mke wa kuoa. Mwanamke anapoolewa anakuwa chini ya mwanamume ambaye alimchagua. Hii ni mojawapo ya njia na mikakati mbalimbali ya utawala wa mfumo dume inayoendelezwa na wanaume kwa njia ya kumdunisha mwanamke. Hali hii inaendeleza mahusiano ya kiuana ya mwanamume kuwa na usemi kuhusu suala la ndoa. Ndoa hatimaye inabainika kushadidia ukubalifu wa mfumodume. Mawazo haya yanaungwa mkono zaidi na Muniu (2013)

anayeeleza kwamba ndoa hushadidia utawala wa mfumodume. Mwanamke ananyimwa nafasi ya kuonesha hisia zake kwa uhuru na kufikia makubaliano mwafaka ya kindoa kwa kumchunguza mwanamume ili aweze kufanya uamuzi sahihi wa mume mtarajiwa.

Mwanamke kuolewa na kuishi na mume katika ndoa ni itikadi inayothaminiwa sana katika jamii za Kiafrika. Msichana anayetimiza umri wa kuolewa anapaswa kutafutiwa mume ili aweze kuolewa. Msichana anaposhindwa kupata mume wa kumuoa ni aibu kwake, ndugu zake hasa wa kike na wazazi wake. Itikadi hii ina chanzo katika tamaduni nyingi za Kiafrika zinazotawaliwa na mfumodume ambapo mtoto wa kike anapovunja ungo aozwe haraka. Itikadi hii inaelezwa katika methali ya (2) na (3). Msichana katika mila za Kinyankole anapovunja ungo huanza kufunzwa jinsi ya kuishi na mume na namna ya kutekeleza majukumu anuwai atakapoolewa. Itikadi hii ilikuwa maarufu na kuendelezwa katika rika tofautitofauti, kuanzia utotoni hadi utu uzima (Kiyimba, 2005). Maelezo ya kiitikadi yanayopatikana katika methali hii yanaafikiana na mhimili wa Nadharia ya Itikadi ya kwamba watawala wanaendeleza imani ya utawala wa ukubalifu kwa kutumia itikadi kuliko mamlaka ya kulazimishwa. Msichana anaridhia kuolewa kwa kushawishika na itikadi ya kimfumo dume ili kutimiza jukumu lake la kijamii kulingana na muono-ulimwengu wa Wanyankole.

Itikadi hii ya ndoa kama jambo la msingi katika maisha ya mwanamke inabainishwa katika methali ya (3).  Mwanamke analinganishwa na mkungu wa ndizi ambapo taswira ya haja ya kuolewa inaibuliwa. Ndizi inapokuwa tayari inavunwa; vivyo hivyo, msichana anapokua, huolewa. Itikadi hii haibainishi tu

haja ya kuolewa lakini msichana anapaswa kuharakisha kuolewa. Ndizi zisipoliwa zitakuwa mbivu na hatimaye mbovu na binti ambaye amefikisha umri wa kuolewa hivyo ndivyo anachukuliwa katika jamii. Itikadi ya Kinyankole kiutamaduni, inadhihirisha ndoa kama jambo la haraka kwa binti akishatimiza umri stahiki. Itikadi hii haimruhusu kufanya uchaguzi na uamuzi kati ya ndoa na mambo mengine yanayoweza kumjenga zaidi. Kwa hivyo, maisha yake hayatazamwi nje ya mipaka ya ndoa. Hilo ndilo analolilenga kutokana na ushawishi anaopata katika jamii; ndilo wanalolitarajia wazazi na jamii kwa ujumla. Chanzo cha itikadi hii ni wazazi wa binti kushawishika na itikadi ya kutazama mtoto wa kike katika lenzi za bidhaa itakayowasaidia kwa kulipwa mahari kama malipo ya juhudi zao za malezi. Hivyo, mtoto wa kike alichukuliwa kama chanzo cha kutajirika (Sanauddin, 2015). Pamoja na hayo, wazazi walitaka kumuoza binti yao ili wapate heshima katika jamii kwamba binti yao hakukawia nyumbani. Mzazi wa kiume ndiye aliyekuwa anachochea sana suala hili ili aweze kupokea mahari. Itikadi hii ilikuwa inajulikana na kuendelezwa katika rika tofauti, kuanzia utotoni hadi utu uzima.

Itikadi hii ya kiutamaduni kama inavyobainika katika methali hii, inaafikiana na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaosema kwamba mchakato wa kiitikadi unapotosha watu wa tabaka la chini katika jamii kwa kuficha masuala ya msingi kuhusu unyonyaji na unyanyasaji katika mahusiano ya kijamii kati ya matabaka. Aidha, matumizi ya vyombo vya dola huendeleza ukubalifu wa watawaliwa kama anavyodai Althusser (1981). Ndoa kama mojawapo ya asasi za vyombo vya dola ni ushawishi mkubwa wa ukubalifu wa itikadi ya msichana kuona ndoa kama kimbilio. Itikadi hii pia inaathiri wanaume pamoja na kanuni za jamii za

msichana kuolewa kwa haraka ili aishi na mume katika ndoa. Itikadi hii haimruhusu mtoto wa kike kuwa huru kufanya uchaguzi na uamuzi wa mambo mengine yanayoweza kumjenga kuliko ndoa. Suala la ndoa ndilo pekee analolilenga; ndilo linalotarajiwa na wazazi pamoja na jamii. Katika mahojiano yaliyofanyika wilayani Sheema tarehe 20/04/2018, kulingana na mhojiwa SHM 3, mwanamke katika methali hii anakuwa na jukumu la kuolewa kama sehemu kuu ya maisha yake.

Kirindi (2008) katika kuelezea matayarisho ya kuoza binti, anasema kwamba, maandalizi huanzia akiwa katika umri mdogo. Baba yake mume mtarajiwa hupeleka ng'ombe wawili kwa familia ya msichana. Mmoja kati ya hao ni ng'ombe jike ambaye hajazaa, anayeitwa "enkwatarugo." Methali nyingi za Kinyankole zinazoashiria asasi ya ndoa pia zinaeleza maoni juu ya maisha tete kwa ujumla. Katika muktadha huu, umuhimu wa methali hizi hujitokeza katika uwezo wake wa kumfasiri mwanamke kama mke. Katika mchakato huu, uchanganuzi unawasilisha mgogoro wa ndani kwa ndani katika methali hizi kutokana na uzoefu wa jamii ya Wanyankole kuhusu methali hizi na amali za jamii yenyewe na maeneo mbalimbali ulimwenguni kote. Katika kuendeleza uchanganuzi huu wa itikadi za kiuana kuhusu ndoa na jinsi zinavyobainisha mahusiano ya kiuana, mwanamke wa Kinyankole anadhihirika akiendeleza itikadi ya kuthamini, kuamini na kuipatia ndoa kipaumbele. Katika jamii ya Wanyankole ndoa ni suala la msingi katika maisha ya binti. Mwanamwari kuolewa ni jambo muhimu na ni sehemu kuu ya maisha yake. Katika methali ya (4), mtoto wa kike anapotimiza umri wa kuolewa, lazima aishi na mume wake. Methali inaeleza kwamba, mbali na mtoto wa kike kulelewa na wazazi wake na

mapenzi ya dhati yaliyopo kati yake na wazazi wake ‘nkunda taata na mawe’, yaani hawezi kuolewa nao muda wa kuolewa ukiwadia. Msichana anatengana nao na kuishi kwa mume wake.

Kulingana na itikadi katika methali hii, ni wajibu kwa mtoto wa kike kuolewa afikishapo umri wa kuolewa. Msichana anashawishika kuondoka kwao, anatengana na wazazi wake awapendao na kuanza maisha yake ya kindoa. Kiutamaduni, kwa upande wa mume wake, mtoto huyo wa kike anafanyiwa sherehe ya kumkaribisha na kumuunganisha na familia ya mume wake na kukata uhusiano na familia ya wazazi wake. Mume wake anampa jina jingine kama njia ya kuhakikisha kwamba sasa mke wake ni mmoja wa wanafamilia yake (Elam, 1973). Mhimili mmojawapo wa Nadharia ya Itikadi unasema kwamba ukubalifu unatokana na ushawishi wa kundi tawala; utawala unalenga kujitolea na kutumika kwa watawaliwa wakitumikia watawala. Itikadi katika methali hii inaafikiana na mhimili huu ambapo inadhihirisha ndoa kama chombo kinachotumia nguvu za kiitikadi na kuendeleza ukubalifu wa majukumu ya kindoa kiasi cha mwanamke kushawishika na kukatisha uhusiano na wazazi wake na kuunganishwa na familia ya mume wake.  Itikadi hii ndiyo inayosababisha mtoto wa kike na wazazi kuliangalia suala la ndoa kama jambo la dharura au la haraka mara msichana akishatimiza umri stahiki. Itikadi hii inaendelezwa zaidi katika methali ya (5).

Methali ya (5) inabainisha mwanamke kama kiumbe anayeweka matumaini ya ufanisi wake kwa mume wake. Kumiliki ng’ombe katika jamii ya Wanyankole ni ishara ya utajiri. Methali hii inamrejelea mtoto wa kike ambaye anathamini

ng'ombe mmoja anayemilikiwa na mume wake mtarajiwa kuliko mamia wanaopatikana kwa wazazi wake. Katika methali hii, itikadi ya mtoto wa kike kuamini kwamba mali yake inapatikana kwa upande wa atakayekuwa mume wake siku za usoni inawasilishwa. Hii ni itikadi anayomshawishi kuukubali utamaduni huu. Hata kama nyumbani kwao wana mali nyingi, kwanza, kiutamaduni hatarajiwi kurithi kutoka kwa wazazi wake na hana mgao anakozaliwa. Pili, itikadi hii inamfanya msichana kutazamia utajiri wake kwa mume wake. Jambo hili hatimaye linachangia pia kuharakisha kuolewa ili msichana huyo aweze kuchangia maendeleo ya familia yake na mume wake. Mtoto wa kike anashawishiwa na itikadi hii kuanza kupangia maisha yake kwa mume wake mtarajiwa ambaye hajajulikana kwake. Imani hii inamfanya kukua na itikadi hii na kuweka fikra zake na kuthamini atakakoolewa hata kama mume wake si tajiri, yaani ni wa 'ng'ombe mmoja'**.** Matumaini yake yote yako kwa mumewe kwa sababu nyumbani anakozaliwa hana fursa ya kurithi mali. Kwa hivyo, itikadi hii ya utamaduni wa msichana kurithi kwa mume wake inamshawishi kupendelea na kutamani kufunga ndoa mapema ili naye aweze kumiliki angalau mali kutoka kwa mume wake. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mhimili unaosema kwamba mila za kiutamaduni ambazo zinaonekana kutobadilika zitathminiwe kila mara kwa muktadha wa kijamii, unatuelekeza kudhihirisha kuwa, mtoto wa kike kukimbimbilia ndoa kwa ajili ya mirathi ni itikadi ambayo inamnyima uhuru wa uchaguzi na kutekeleza uamuzi sahihi.

### 4.1.1 Itikadi za Kiuana na Suala la Utiifu wa Mke katika ndoa.

Ndoa ni mojawapo ya asasi za kijamii zinazoshadidia utawala wa wanaume juu ya wanawake. Ogutu (2020) anaeleza kwamba, ndoa inatumiwa na wanaume kuwatawala wanawake kwa vishawishi vinavyowafanya wakubali nafasi zao katika jamii. Mwanamke anakuwa kwenye nafasi yake ya kuwa mtiifu kwa mume wake ili adumishe amani kati yake na mume wake na ndoa kwa ujumla. Maoni haya yanasisitizwa pia katika utenzi wa Mwanakupona (King'ei, 2000:99) ambapo Mwanakupona anamhusia binti yake kumheshimu na kumtii mume wake bila kubishana naye. Anamweleza kama ifuatavyo:

> Fuata yake idhini,
> Awe radhi kwa yakini,
> Wala sikae ndiani,
> Saa yane kasia. (ubeti wa 45).

Angella (2018:85) anaendelea kusema kwamba heshima na utiifu anaokuwa nao mwanamke unamfanya aishi na mume wake bila ugomvi. Kwamba:

> mwanamke anafanya uamuzi wake bila
> kushurutishwa kumheshimu mumewe
> kumtendea mema.

Kuna amali ambazo mwanamke anastahili kuzitekeleza na sifa anazostahili kuonesha ili kuweza kudumisha amani na ndoa kiitikadi. Hizi ni pamoja na utiifu, heshima pamoja na kumhudumia mume wake. Momanyi (2001) anaeleza kwamba utiifu ni Itikadi ambayo inamshawishi mwanamke kukubali nafasi yake ya kunyenyekea mume ndani ya asasi ya ndoa huku mwanamume naye akibainika kuendeleza itikadi za mfumo dume zinazohalalisha mamlaka yake kwa ukubalifu na mila za kitamaduni za kunyenyekewa na wanawake. Katika

jamii ya Wanyankole, methali zinazodhihirisha itikadi hizi zipo na zinajadiliwa katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali 2: Methali kuhusu Itikadi ya Utiifu wa Mke katika Ndoa**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omukazi wamaryo tahungurwa* | Mke mwenye ubishi harithiwi. |
| 2. | *Omukazi aba empene esibikwa heihi namatojo.* | Mwanamke ni mbuzi, afungwa karibu na majani yenye miiba |
| 3. | *Omukazi wo'muhuuru tagira matu* | Mke mtarajiwa wa kapera hawi na masikio. |

Methali ya (1) inaeleza kwamba mke mwenye ubishi harithiwi. Kiutamaduni katika jamii ya Wanyankole mke mwenye umri mdogo alipofiwa mume wake, alirithiwa na ndugu zake marehemu. Mke aliyekuwa na tabia nzuri aliweza kupata nafasi ya kuolewa tena na ndugu za aliyekuwa mume wake. Mke mbishi alishindwa kupata mume wa kumuoa tena kwa kuwa tabia hizo hazistahamiliki.

Methali hii inabainisha itikadi kwamba, mke anapaswa kuwa mnyenyekevu na aoneshe tabia ambazo zitamfanya kutamaniwa kuolewa. Pili, itikadi hii inadhihirisha kuwa kuolewa tena kwa mjane na ndugu za marehemu ni uhisani anaofanyiwa. Itikadi hii haishawishi mwanamke kukubali utiifu kwa mume tu bali inadhihirisha kuwa yuko chini ya huruma za mwanamume ambaye anadhibiti maisha yake. Hali hii inaafikiana na mhimili wa nadharia ya itikadi wa unyamazishaji wa watawaliwa ambapo mwanamke anabainika kukubali kutii na kunyenyekea mwanamume ili apate fursa ya kuolewa na ndugu ya aliyekuwa mume wake kwa kuweza kuhimiliwa. Itikadi hii kama inavyoendeleza mahusiano haya, inabadilika katika utamaduni wa Wanyankole.

Zaidi ya hayo, methali ya (2) inalinganisha mwanamke na mbuzi kwa tabia. Methali hii inamaanisha kwamba mbuzi ni mnyama ambaye si rahisi kumtunza kwa sababu ya sifa zake za ukaidi. Njia mojawapo ya kumdhibiti mbuzi ni kumfunga kwenye majani yenye miiba. Mwanamke naye anapaswa kuwekwa karibu na zana za kumlainisha kwa sababu ya ukaidi wake. Itikadi katika methali hii inamchukulia mwanamke kuwa mkaidi na mwenye kiburi, anayepaswa kuchapwa; na hayo majani ni kama njia ya kumtuliza. Itikadi hii inaonyesha kuwa ili mwanamke arekebishwe, anahitaji matumizi ya nguvu. Majadiliano na KRH 1 yaliyofanyika tarehe 17/04/2018 alieleza kuhusu itikadi ya methali hii kwamba, tabia hii ya ukaidi inatokea sana kwa wakewenza. Wakewenza wanapogombana vita vyao haviishi, mmea wenye majani ya miiba ‘amatojo’ ndio unaweza kukomesha vita hivyo kwa kuwatenganisha.

Kulingana na utamaduni wa Wanyankole, ni mwiko kupigwa ‘amatojo’. Mhojiwa SHM 2 katika mahojiano naye ya tarehe 20/04/2018, alidai kuwa wanawake wakianzisha ugomvi au kulemewa na jambo fulani si rahisi kuwatenganisha au kuwabadili nia. Mhojiwa anashikilia madai yake kuhusu sifa muhimu zinazotambulisha hadhi ya mwanamke na mwanamume katika jamii yake. Wanawake aghalabu hawatapata mwafaka haraka mpaka ‘amatojo’ yatumiwe kuwatenganisha. Mwanamke katika methali hii anabainishwa na itikadi ya kwamba ni kiumbe ambaye ni mkaidi na asiye mwepesi wa kubadilisha nia. Njia faafu ya kumrekebisha ni kutumia nguvu. Mwanamume ndiye anadhihirika kuwa na uwezo wa kuleta mwafaka kati ya wake ambao wanagombana na wanawake wenyewe hawawezi kusuluhisha migogoro kati yao. Kwa kuongozwa na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema

kwamba wanawake wazinduke na kubadili mielekeo vile wanajiona katika uhusiano na wanaume, tunagundua kuwa itikadi hii haipatii fursa wanawake kusuluhisha changamoto zinazowakabili. Wanaume ndio wanaopaswa kuingilia kati ili kuleta amani na utulivu kati ya wanawake paoja na kuwarekebisha kitabia pindi wanapoenda kombo.

Vilevile, itikadi ya mamlaka ya mwanamume dhidi ya mwanamke inabainishwa na methali ya (3). Methali hii inaeleza kuhusu mke mtarajiwa wa kapera ambaye anajengea taswira. Kapera ni kijana wa kiume ambaye hajaoa. Kapera, kijana wa kiutamaduni akiwa miongoni mwa rika yake huwa anasema kwamba angekuwa na mke aliye na tabia ambazo hazifai kulingana na matarajio ya jamii, angemuadhibu daima hata kwa kumkata masikio. Methali hii inaeleza kwamba mke wa kijana huyo ambaye hajaoa kitaswira, ni yule ambaye hana masikio. Methali hii inabainisha jinsi itikadi ya ubabedume inavyoendelezwa katika jamii. Imani ya kapera inaakisi itikadi ya kiuana ya kuwa, mwanamume kuridhia kuishi naye sharti mwanamke amtii. Utiifu, unyamavu na kutawaliwa kwa mwanamke ni mambo ambayo yanabainisha tabia nzuri anazostahili kuwa nazo mbele ya mwanamume. Itikadi hii inawaathiri mwanamke na mwanamume ambapo mwanamke anajiona kuwa mtawaliwa na mwanamume hujiona mwenye mamlaka na anayepaswa kumtawala mwanamke. Mke anaposhindwa kutekeleza majukumu yake anavutwa masikio au pengine ‘kuyakata’. Mke kuvutwa masikio ni ishara ya ukaidi wake kwa mujibu wa mfumodume na hiyo ndiyo njia inayotumiwa kumrekebisha. Katika methali hii, mamlaka kumtawala mwanamke yanaonekana ndiyo njia mwafaka kutumiwa na mwanamume. Kwa hivyo,

kulingana na methali hii, itikadi inayobainika ni ya ubwana wa mwanamume dhidi ya kutawaliwa kwa mwanamke.

### 4.1.2 Itikadi za Kiuana na Suala la Mitala

Methali za Kinyankole kuhusu ndoa za mitala, ukewenza na uzazi wa kambo zinaendelezwa kwa msingi unaodumisha mfumo unaokweza na kumnufaisha mwanamume. Mwanamke hubainika kuwa anaathirika kutokana na mahusiano hayo ya kumtumikia mwanamume. Baloyi (2013) anadai kuwa ndoa za mitala ni hali inayojulikana sana katika jamii za Kiafrika. Katika jamii hizi kwa ujumla, kitendo cha kuoa wake zaidi ya mmoja kinaruhusiwa. Baloyi anaendela kusema kwamba, watoto wakiwa wengi, ambao aghalabu hutokana na wake wengi, humwezesha mwanamume kuendeleza ukoo wake. Mawazo haya yanaelezwa zaidi na Ssetuba (2002) ambaye anadai kwamba ndoa za mitala katika jamii ni suala la kawaida, linalofaa na halilalamikiwi. Ssetuba anaongeza kwamba, kuwepo kwa wakewenza na mama wa kambo kuna asili yake kwenye ndoa hizo za mitala. Kuoa wake zaidi ya mmoja katika jamii za Kiafrika kunahusishwa na hadhi ya mwanamume. Mwanamke anatumikia nafasi yake kwa kushawishika na kukubali kuwa ni wajibu na hadhi yake katika jamii. Katika jamii ya Wanyankole, methali ya (1) katika Jedwali Na. 3 inazungumzia suala hili la kuoa wanawake zaidi ya mmoja au ndoa ya mseto:

**Jedwali 3: Methali kuhusu Ndoa za Mitala.**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omukazi omwe ni nyoko* | Mwanamke mmoja ni mama yako |
| 2. | *Owamaka abiri tararakwo* | Mwenye boma mbili halali njaa |

Methali ya (1) inamaanisha kwamba mwanamke ambaye ni mmoja katika uhusiano na mwanamume ni mama yake. Mhojiwa KRH 4 katika wilaya ya Kiruhura tarehe 18/04/2018, alieleza kwamba, mtu (mwanamume) hawezi kuzaliwa na wanawake zaidi ya mmoja, ni lazima awe na mama mmoja lakini kimila mwanamume ana uhuru wa kuwa na wake wengi kwa sababu si maharimu kwake. Kwa mahusiano ya mume na mke kwa mujibu wa itikadi hii, si tatizo mume kuwa na wake zaidi ya mmoja. Itikadi inayodhihirika katika methali hii ni ya uhuru wa wanaume kuoa wake zaidi ya mmoja. Itikadi hii ina nguvu za ushawishi mkubwa kutoka kwa wanaume kama kundi tawala kuwa mwanamume anapaswa kuwa na wake zaidi ya mmoja.

Katika methali ya (2) inaendeleza itikadi ya mwanamume kuwa na wake zaidi ya mmoja kwa ajili ya manufaa yake, kufaidika kutokana na kuhudumiwa na wake zake. Itikadi hii inaendeleza kufaidika kwa mwanaume bila kuzingatia upande wa wanawake ambao wanampatia huduma. Dipio (2019) anatoa maoni yake kwamba wanaume ndio wanafaidika kutokana na mahusiano haya ya wakewenza. Methali (2) inaonyesha itikadi ya mwanaume kuoa wake wengi ni kwa ajili ya kunufaika dhidi ya wanawake anaowaoa. Stock-Morton (1991) akirejelea dhana ya uwili ya Derrida anafafanua kwamba utumiaji wa dhana ya uwili kuna dhana moja ambayo inapewa hadhi kuliko nyingine. Nadharia ya Udenguzi inabainisha matumizi ya dhana ya uwili ambapo dhana moja inapewa hadhi kuliko nyingine

yaani mwanamume/mwanamke. Abrams na Harpham (2014) wanafafaua kwamba katika matini, dhana zenye jozi kinzani zinaunda dhamira ya kinachesemwa. Hata hivyo, nadharia ya udenguzi inalenga kuchunguza jinsi lugha ya matini inavyofaa kwa jozi moja ya maneno. Mhimili huu wa nadharia ya Udenguzi unatuelekeza kutambua na kutubainishia nafasi ya mbele ya mwanamume ya kutaka kuhudumiwa na mwanamke. Nafasi hii inatokana na kuoa wake zaidi ya mmoja. Mwanamke anaolewa kwa ajili ya kutumikia mwanamume ambaye hajali maslahi ya wake anaowaoa.

Methali hii ya (2) inamrejelea mwanamume ambaye ana familia mbili kuwa hawezi kulala njaa. Akikosa chakula kwa mke wake mmoja, anaenda kwenye boma nyingine kuhudumiwa. Methali hii inadhihirisha itikadi ya mwanamume kuwa na boma mbili au zaidi, yaani kuoa mke zaidi ya mmoja kwa sababu ya kutaka kuhudumiwa na wake zake. Wake hawa ambao wameolewa na mume mmoja, wanajikuta wanashindana kuhakikisha kwamba kila mmoja ndiye anapata umaarufu mbele ya mume wao. Wanafanya hivi kwa kutoa huduma nzuri kudhihirisha utunzaji wa juu kwa mume ili mmoja apendwe zaidi kuliko mwenzake. Kwa kutathmini kwa undani maelezo haya, mwanamke wa Kinyankole anawajibika kutafuta chakula cha kulisha familia na mume wake. Mume akikosa chakula kwenye boma lake moja, hatakosa chakula kwenye boma la pili. Kwa hivyo, methali hii inashadidia lengo la mwanamume kuoa wake ka ajili ya haja ya kuhudumiwa na wake zake. Kulingana na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba, tabia za uana ambazo zinaonekana kutobadilika zitathminiwe kwa muktadha wa kijamii wala si kuyashughulikia kwa muktadha wa kimaumbile.

Itikadi ya mke kutumikia mume kimila, inathibitishwa katika methali yah apo juu (2). Jukumu hili la mume kuhudumiwa na wake zake kwenye boma tofauti, linamfanya mwanamume kuwa kwenye nafasi ya kutumikiwa na wake zake. Wanawake wanachukua na kutekeleza jukumu hilo kama la kimaumbile. Ushindani unaoibuka kati ya wake hao wawili au zaidi kuhusu kumhudumia mume wao unaendeleza itikadi ya ndoa za mitala na hatimaye kuimarisha itikadi ya ukewenza. Ukewenza ni itikadi ambayo inabainishwa na methali kadhaa za Kinyankole. Itikadi hizi zinajadiliwa katika 4.2.1.3

### 4.1.3 Itikadi za Kiuana na Suala la Ukewenza

Methali za ukewenza zinamwonesha mwanamke kama mwenye wivu kwa wake wenzake. Mkemwenza anaendeleza mabishano na ushindani mkali ili aweze kupata umaarufu mbele ya mume wao. Itikadi inayobainishwa katika methali kuhusu ukewenza inadhihirisha ukosefu wa utulivu na amani miongoni mwa wakewenza, watoto wao na mume wao. Dipio (2019) anasema kwamba hata kama wanaume wanafaidika kutokana na ndoa za mitala nao hawana furaha kwenye ndoa za aina hii. Chanzo cha uhasama kati ya wakewenza ni ugawanaji wa mali kati ya wakewenza lakini zaidi ni upendo wa mume wao na kuweza kuzaa watoto kwa mume, suala ambalo haliwezekani kutekelezwa.

Katika jamii ya Wanyankole, wakewenza wanaelezewa katika methali zao kama watu wanaoendeleza upinzani wa wao kwa wao; wanaozozana na kuoneana wivu wakishindania mume. Mila hii inaendeleza itikadi kwamba hakuna ushirikiano na kuonesha nia ya kuendeleza shughuli za kujenga familia pamoja na kuishi kwa amani kati ya wakewenza. Methali za Kinyankole zinadhihirisha waziwazi itikadi

hizi zenye uonevu na tuhuma kati ya wakewenza hata katika hali ngumu ambazo zingehitaji kushirikiana pamoja. Methali nyingine zinajaribu kuwasawiri wanawake ambao wameolewa pamoja kwa njia iliyo chanya. Methali zinaonesha kijuujuu kwamba mwanamke mmoja anaweza kuishi na mke mwenzie kwa amani lakini zinaendelea kuonya daima kuwa wanawake walioolewa pamoja wawe waangalifu. Mwanamke amebainishwa na methali kuwa na wasiwasi wa kuolewa na mwenzake kwa mume mmoja. Mwanamke anapinga vikali mwanamume kuoa na kutoa huduma yoyote kwa mkemwenza na anatumia mbinu anuwai kuhakikisha mwanamume anammiliki peke yake. Methali zifuatazo za Kinyankole zinazoeleza itikadi kuhusu wakewenza ni ithibati inayoeleza hoja hii:

**Jedwali 4: Methali kuhusu Itikadi ya Ukewenza**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Abakazi bashweirwe hamwe nigo mahari.* | Wanawake waolewao pamoja hawakosi wivu. |
| 2. | *Eihari ringi rikujumisa ekituuro.* | Wivu mwingi hukufanya kutusi kaburi. |

Methali hii ya (1) katika Jedwali Na. 4 inamaanisha kwamba wakewenza au wanawake ambao wanaolewa na mume mmoja hawakosi wivu. Chanzo cha migogoro na chuki kati ya wakewenza katika jamii ya Wanyankole ni ugawanyaji wa mapenzi na vitu vya matumizi nyumbani kwa usawa kati ya wanawake kutoka kwa mume wao ambaye anaegemea upande fulani. Wakewenza hutafuta umaarufu mbele ya mume wao. Kusudi lao ni kuona nani anapendwa zaidi. Kadhalika, wakewenza wanashindania nafasi, yaani mke wa kwanza hujiona mwenye hadhi kuliko mke wa pili. Mke wa pili naye hujiona kuwa ni mdogo na

anastahili kupendelewa zaidi. Jankowiak na wenzake (2005) wanaeleza kwamba ushindani mkubwa na uhasama kati ya wakewenza daima utaendelea kutokea. Aidha, mwanamume anaoneshwa kuwa ndiye anafaidika kutokana na ndoa hizi za mitala zinazoibua ukewenza.

Kwa upande wa wakewenza, wao wanaonekana kushindania mume na hatimaye kumweka kwenye nafasi muhimu kwao. Itikadi hii inachukuliwa kuwa ya kawaida kati ya wakewenza na kati yao na mume wao kutokana na ushawishi na ukubalifu wa nafasi hii ya wanawake katika jamii. Kulingana na mhimili wa Nadharia ya Itikadi, ukubalifu unapatikana kutokana na ushawishi wa wanaume kama kundi tawala kuwafanya wanawake kujitolea kuwatumikia na hatimaye kuonekana kuwa watawala. Kwa mujibu wa mhimili mwingine unaosema kwamba utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi. Inadhihirika kwamba suala la wakewenza kushindania mume, linawafarakanisha kuliko kuwaletea amani. Aidha, ushindani na kuoneana wivu kuliendelezwa hata katika jamii, kwa mfano kuhusu upatikaji wa mtoto wa kiume. Wivu huu katika baadhi ya methali unaelezwa katika methali ya 2.

Methali ya (2) Jedwali Na. 4 inafafanuliwa kwa mujibu wa mhimili wa Nadharia ya Udenguzi. Maana ya matumizi ya neno ‘eihari’ kumaanisha wivu, ambapo wakewenza wanajulikana kwa kuoneana wivu katika jamii. Mawazo haya yanaungwa mkono na Dipio, (2019 Ssetuba (2002). Matumizi ya methali hii katika jamii ya Wanyankole yamewekwa kwa muktadha wa ukewenza. Katika mahojiano yaliyofanyika wilayani Kiruhura tarehe 17/04/ 2018, Mhojiwa KRH 3 alisema kwamba methali hii inatumiwa kuonesha uhasama kati ya wakewenza.

Kwa hivyo, methali hii inawasilisha mwanamke mwenye wivu, hasira na chuki. Huduma kwa familia zinapungua kwa kuzigawanya kati ya familia. Kupungua ama ukosefu wa huduma hizo ndiyo chanzo cha kuzuka kwa uhasama kati ya wakewenza. Mke wa kwanza ndiye chanzo cha uhasama huo na ugomvi wa mara kwa mara ambao unasababisha kuwepo kwa wivu kiasi kwamba mke akiona kaburi la mkemwenza aliyefariki analitusi. Kugawana mapenzi na mali baina ya mwenzake ni mambo ya msingi yanayoibua mifarakano. Kifo ni suala ambalo lingefanya watu kuridhiana na kuwa katika majonzi lakini mkemwenza anabainika kuwa bado ana kisirani na mke mwenzake kiasi kwamba anatusi kaburi la mwezie aliyefariki.

### 4.1.4 Itikadi za Kiauna na Suala la Uzazi

Kwa desturi za kiutamaduni katika jamii za Kiafrika, ndoa inakuwa na maana zaidi pale mwanamke anapopata mimba na kuzaa watoto. Mbiti (1969) anathibitisha hoja hii kwamba watoto wanaozaliwa wanakuwa furaha ya muungano wa ndoa kati ya mwanamume na mwanamke. Tafiti kadhaa kuhusu methali za kiuana zimedhihirisha kuwa mwanamke akiolewa anapaswa kuzaa watoto wengi. Sanauddin (2015) anatambua kwamba pamoja na kupatikana kwa watoto wengi kipaumbele ni kwa watoto wa kiume. Itikadi hii inabainika kutokana na mila za tamaduni nyingi katika jamii za Kiafrika na ulimwengu kwa ujumla (Kiyimba, 2005), kama inavyodhihirika katika methali zifuatazo:

**Jedwali 5: Methali kuhusu Itikadi za Uzazi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Nyina omwe niwe nyina busha.* | Mama wa mtoto mmoja ni sawa na mama asiye na mtoto. |
| 2. | *Omwana omwe tamara nyina obugumba.* | Mtoto mmoja haondolei mamake utasa. |
| 3. | *Omwana omwe n'oruhu rutakuhikire.* | Mtoto mmoja ni ngozi ndogo isiyokufaa. |
| 4. | *Okuzaara kwita abakazi.* | Kuzaa huua wanawake. |
| 5 | *Ou otazaire omutuma orotami.* | Mtoto usiyemzaa unatuma ukiwa umeotama. |

Katika methali ya (1) mama wa mtoto mmoja analinganishwa na mwanamke ambaye hana mtoto hata mmoja. Kulingana na utamaduni wa Wanyankole, ili mwanamke aweze kutambulika kama mama na kupata heshima anapaswa kuzaa watoto wengi. Mwanamume wa Kinyankole anapata heshima zaidi katika jamii kulingana na idadi ya watoto alio nao. Itikadi hii ya kuzaa watoto wengi inawashawishi wanamume na wanawake katika jamii ya Wanyankole kukubali na kuthamini jukumu la kuzaa watoto wengi. Dhana ya itikadi inashadidiwa na Gramcsi (1971) katika Bates (1975) kwamba itikadi ni matokeo ya mahusiano miongoni mwa watu binafsi katika jamii na ukubalifu wao. Wanawake kwa wanaume wanashawishika na kukubali kwamba ili mama aweze kutulia, kuwa na amani pamoja na kuheshimika kwenye ndoa yake anapaswa kuzaa watoto wengi.

Mhojiwa KRH 1 tarehe 17/04/2018 alibainisha kuwa, kuzaa mtoto mmoja au wachache kunazua wasiwasi kwa mke na mume. Mwanamke anajihisi kuwa asipozaa au akizaa mtoto mmoja, hawezi kuheshimiwa; na anaweza hata kupewa talaka. Jamii inachukulia suala la kuzaa watoto wengi ni jukumu la mwanamke kwenye ndoa. Itikadi hii inamnyima mwanamke uhuru wa kuishi kwa amani kwenye ndoa.

Maoni haya yanaungwa mkono na Elam (1973) ambaye anaeleza kwamba wanawake tasa katika jamii ya Wanyankole walikuwa wanarudishwa kwa wazazi wao na waume zao. Walikuwa hawathaminiwi na walichukuliwa kuwa ni ‘hasara’ kwa familia. Katika methali hii uwezo wa mwanamume wa kutozaa hautajwi na mwanamke ndiye anaonekana kuwa na jukumu la kumzalia mume watoto wengi. Itikadi ya ubabedume inabainika kumshawishi mwanamke kukubali jukumu hili la kuzaa watoto wengi. Suala hili la uwezo na haja ya mwanamke kuzaa watoto wengi katika jamii hiyo linathibitishwa na baba mkwe ambaye wakati wa kugawa mirathi (ng’ombe) kwa watoto wake wa kiume, anamgeukia mkaza mwana wake tasa na kumwambia kuwa amemfanyia kazi bure na anaweza kurudi nyumbani kwa baba yake (Elam, 1973).

Itikadi ya wanawake kuwazalia wanaume watoto wengi inaendelezwa katika methali ya (2) ambapo mwanamke mwenye mtoto mmoja analinganishwa na mke tasa. Itikadi inamshawishi na kumfanya mwanamke kuamini na kukubali kwamba kuzaa mtoto mmoja au wachache ni sawa na kuwa tasa. Itikadi hii inaungwa mkono na Wasike (2020) anayesema kwamba, uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio unaolengwa. Mwanamke anakuwa wa kwanza kulaumiwa kama kunatokea changamoto ya uzazi katika familia kati yake na mume wake na wala si mwanamume. Mawazo haya yanajikita katika mhimili wa Nadharia ya Itikadi ambao unasema kwamba, tabaka tawala linakandamiza tabaka tawaliwa ambapo imani za tabaka tawala hazitambui hisia na haja za watawaliwa. Kwa hivyo, haja ya kuzaa watoto wengi inawapendelea wanaume bila kujali hali ya wanawake wanaoleta watoto hao duniani. Kulingana na maoni ya mhojiwa SHM 2, tarehe 20/04/2018, itikadi ya mke kuzaa watoto wengi inaambatana na gharama yake.

Kila mtoto anayezaliwa anahitaji kupatiwa malezi bora ambayo yanahitaji kujipanga kiuchumi ili kuweza kumudu na kuwatunza watoto. Kulingana na Salem (2013) mwanamke hapewi nafasi ya kupanga idadi ya watoto atakaozaa. Suala la kuzaa watoto pia, linategemea uwezo wa kiuchumi wa jamii, hususani wa familia, kwa sababu kuna mabadiliko yanatokea katika jamii, kiuchumi na kijamii, hali inayoathiri namna ya kuishi. Itikadi hii inaendelezwa zaidi na methali namba (3):

Methali ya (3) inarejelea kipindi cha kihistotia katika jamii ya Wanyankole. Wanyankole walikuwa wanavaa ngozi kama vazi. Ngozi ndogo ilikuwa inampa shida mvaaji kwa kukaa kwa wasiwasi. Ngozi inawakilisha nguo za kisasa. Kuzaa mtoto mmoja kunalinganishwa na kuvaa nguo ambayo haikufai. Kuwa na mtoto mmoja hakumpatii raha yoyote mzazi. Kulingana na Michalos (2014), wanaume au wanawake ambao hawajaliwi angalau mtoto zaidi ya mmoja, wanadharauliwa na kurejelewa kama wasio na watoto. Davis na Moore (2010) nao wanasema kwamba, mke kuzaa watoto wachache ilihofiwa kwa kuwa wangeweza kufariki na wakaachwa bila watoto. Itikadi hii iliwashawishi kuzaa watoto wengi ili waweze kunusuru baadhi yao lakini itikadi inabainika kurejelea wanawake kuwa ndio wanawajibishwa kwa jukumu hilo. Uwezo wa kuzaa watoto ni kwa wazazi wa pande zote mbili, yaani mume na mke. Methali hii haitofautishi kati ya mume na mke ni nani anawajibika katika suala la kuzaa watoto wengi. Katika mahojiano yaliyofanyika wilayani Kiruhura tarehe 18/04/2018, mhojiwa KRH 2 alieleza kwamba, mwanamume ndiye hurejelewa kuzaa na kuhesabiwa watoto. Itikadi hii kama inavyojulikana katika jamii ya Wanyankole inatofautiana na vile inavyowasilishwa katika methali hii. Methali

haibainishi kama ni mume anayekuwa na wasiwasi kwa kutozaa watoto wengi au ni mke.

Utamaduni umewafanya wanawake kwa wanaume kushawishika na kukubali kuwa mwanamume ndiye ana uwezo wa kuzaa katika jamii. Kwa hivyo, ni yeye anayerejelewa kulingana na maelezo ya wahojiwa lakini ni tofauti katika itikadi ya methali. Jamii inayotawaliwa kwa msingi wa ubabedume inatambua kuwa wanaume ndio wenye haki ya kumiliki watoto. Hata kama ni wanawake ndiyo wanaohisi uchungu wa uzazi, wanaozaa ni wanamume. Itikadi hii inadhihirika kupotosha hali halisi katika jamii kama mhimili wa wa Nadharia ya Itikadi unavyobainisha kuwa, uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unatekelezwa kwa ung'amuzi potoshi. Wanawake kwa wanaume wanashawishika kukubali fikira zisizo za kweli na kuzifanya zionekane kuwa za kweli na kukubali mahusiano hayo kati yao. Kwa hivyo, wanaume kama kundi linalorejelewa kuwa na usemi, linafunika ukweli na kuonesha upande unaowanufaisha.

Methali ya (4) inadhihirisha itikadi ya ugumu na matatizo ambayo akinamama wanapitia wakati wa kujifungua na utaratibu mzima wa upatikanaji wa watoto. Wanawake wanavumilia matatizo yanayotokana na ujauzito. Kubeba mimba na kuzaa ni kitendo ambacho hudhoofisha afya za akinamama. Pia, husababisha msongo wa mawazo na hata kupoteza maisha. Itikadi ya mwanamke kuzaa watoto wengi kama inavyodhihirishwa katika methali ya (1) hadi ya (4) ni hali ya hatari kwa maisha yao. Itikadi hii ya ugumu na matatizo ya mwanamke anayopitia ili watoto wengi wapatikane inadhihirishwa kupitia methali hii. Itikadi hii inabainishwa kupitia kwa mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

unaosema kwamba fasihi hutumiwa kama jukwaa la kuelezea hali halisi ya mwanamke anayokumbana nayo ili iweze kueleweka. Vilevile, kuna haja ya kutunza na kuwajali akinamama wajawazito kwa ajili ya usalama wa maisha yao. Jamii inapaswa kuwajali na kuwaunga mkono ili kuweza kupitia kipindi kigumu cha ujauzito mpaka wakati wa kujifungua.

Methali nyingine inayowasilisha itikadi kuhusu kuzaa na kuwa na watoto ni ya (5). Methali hii inamaanisha kwamba mtoto ambaye hujamzaa unamtuma kama umechuchumaa. Ina maana kwamba unakuwa na wasiwasi unapomtuma. Wasiwasi huu unabainishwa na hali ya ‘kuotama’ yaani kukaa kwa kutumia miguu bila ya makalio kugusa chini. Hii inawasilisha taswira ya mzazi kutokuwa na utulivu. Mzazi anapomtuma na kushughulisha mtoto ambaye si wake hapati raha na utulivu. Maana yake ni kuwa mwanamume au mwanamke asiyezaa aghalabu anakuwa na wasiwasi. Methali hii inawasilisha itikadi ya haja ya ama mwanamume au mwanamke kuzaa, kwa kuwa watoto ni furaha ya kila mzazi. Kwa hivyo, mwanamke na mwanamume wanalazimika kuzaa ili kuwa na watoto wa kuwafariji na kuwapa raha. Kulingana na itikadi hii, mwanamume na mwanamke katika jamii ya Wanyankole wanapaswa kuzaa watoto wao ambao watawafaa kuliko kutegemea watoto wa wengine. Katika mahojiano yaliyofanyika wilayani Sheema tarehe 21/04/2018, mhojiwa SHM 4 alisema kwamba katika jamii ya Wanyankole mwanamke ndiye anapaswa kuzaa, yaani kuwa na watoto ambao wataweza kumfaa katika kutekeleza kazi na majukumu yake ya nyumbani. Watoto hao watamfariji na kumfanya atulie ndani ya ndoa yake. Aidha, watamsaidia kazi za nyumbani. Mwanamke anakuwa na faraja zaidi akiwa amezaa watoto wa kiume, kama jamii inavyopendelea na kutarajia.

Katika kipengele hiki, itikadi za kiuana kuhusu suala la uzazi zimejadiliwa. Imebainika kuwa itikadi ya wanawake kuzaa watoto wengi kwa wanaume ni jukumu ambalo wanawake wanashawishiwa na itikadi hii na kuikubali. Itikadi hii ya ubabedume inaendeleza ushawishi na ukubalifu wa jukumu hili kati ya wanaume na wanawake. Pamoja na itikadi ya wanawake kubainika kuzaa idadi kubwa ya watoto, wanawajibika pia kwa malezi yao. Itikadi hii inachanganuliwa hapa chini.

### 4.1.5 Itikadi ya Kiuana na Suala la Malezi

Desturi za kitamaduni kuhusu malezi zina mchango mkubwa katika kuunda na kuendeleza itikadi kuhusu wanawake na wanaume (Ndungo, 1998). Craig na wenzake (2006) pamoja na Stephens (2009) wamejadili suala hili na kubaini kwamba kuna tofauti ya mtazamo kati ya wanaume na wanawake kuhusu suala la malezi. Wanawake wanaweza kutimiza jukumu la malezi na kutunza watoto pamoja na kushughulika na kazi nyingine. Malezi ya watoto ni sehemu ya itikadi zalishi ambazo zinahusu majukumu, uhusiano na shughuli muhimu ambazo zinahitajika ili kuendeleza maisha ya binadamu ya kila siku na kumwezesha kuishi (Barbara & Johanna, 1989). Itikadi zalishi kwa misingi ya kijamii, zinahusu malezi na utunzaji wa watoto miongoni mwa mambo mengine. Itikadi za kiuana kuhusu suala la malezi ya watoto katika methali za Kinyankole zinajadiliwa katika Jedwali Na. 6:

**Jedwali 6: Methali kuhusu Itikadi ya Malezi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Egabo yabaana eigusya banyinabo.* | Mlo wa watoto hushibisha mama zao. |
| 2. | *Enaku yotagambiire nyoko tetuuba.* | Shida usizomwambia mama yako hazipunguki. |
| 3. | *Ku ota nyoko endugu totayo rumuri.* | Ukimkabidhi mama yako dhamana, usiwe na wasiwasi. |

Itikadi ya kiuana kuhusu suala la malezi na utunzaji wa watoto, inawataka wanawake kutoa huduma na kuwajibikia masilahi ya watoto. Masilahi ya watoto yanabainishwa na matumizi ya neno ‘egabo/mlo’ katika methali ya (1). Mwanamke anadhihirika kwa kujinyima ili watoto wake waweze kula na kushiba vizuri. Itikadi hii inatokana na ukubalifu wa jukumu la malezi na utunzaji kuchukuliwa kuwa la wanawake. Aidha, kujinyima kwa akinamama kwa ajili ya watoto wao kunasababishwa na itikadi ya umama inayohusishwa na upendo pamoja na ufungamano wa karibu sana wa mama kwa watoto anaowazaa. Itikadi hii inajikita katika historia ya Wanyankole ambapo nyakati fulani walikuwa wanakumbwa na janga la njaa na uhaba wa chakula. Katika hali kama hizi akinamama walihiari kukosa kula chakula mradi watoto wao wapate chakula cha kuwashibisha. Watoto waliposhiba na kuwa katika hali njema ya afya, mama zao walifarijika hata kama hawakupata chakula au walipata kidogo. Chakula kinaashiria huduma na maslahi mengine ya msingi ambayo watoto wanatakiwa kupata. Watoto wakipata huduma nzuri na wakiwa na afya njema, akinamama huwa furaha. Mhojiwa SHM 1 katika mahojiano yaliyofanyika wilayani Sheema tarehe 19/04/2018, alielezea kama ifuatavyo:

> ‘Mwanamke anawatafutia na kuwaandalia watoto chakula, kuwafulia nguo na huduma nyinginezo mtoto yeyote anazostahili. Mtoto akiwa katika hali nzuri ya kiafya mama yake anakuwa na amani’

Yeye mhojiwa SHM 1 wa kike, katika mahojiano ya tarehe 19/04/2018, anadai kwamba, wanawake wanajitolea na kujinyima kwa ajili ya usalama na maisha bora ya watoto. Pamoja na hayo, itikadi hii inadhihirisha mapenzi ya mama kwa watoto, ambayo huwafanya kuvumilia hali za mateso yanayotokana na vurugu za kiuana. Itikadi hii inawatenga wanaume kuhusu utunzaji wa watoto.

Aidha, upendo wa mwana na mama unatokana na ukaribu uliopo kati ya mtoto na mama. Upendo huu unamfanya mtoto kuwa na imani kwa mama yake. Kunapotokea jambo ambalo linahitaji kushauriana na wazazi, ni rahisi kwa mtoto kumuelezea mama kuliko baba. Itikadi hii inadhihirishwa na methali ya (2). Methali hii inazungumzia itikadi ya mama kama mtoa nasaha na ushauri kwa watoto wake. Mwanamke kama mama anadhihirisha utangamano huru na watoto wake. Hali hii inatokana na mapenzi na ukaribu ambao unaziba mwanya kati yao. Kutokana na itikadi hii, mama anakubali kuchukua dhamana ya kutoa nasaha na ushauri kwa watoto kama jukumu analopaswa kuwajibikia kwa matarajio ya jamii. Dhamana hiyo inatokana na imani inayojengwa na watoto kwa upande mwingine ya uaminifu kwa mama zao. Kwa hivyo, itikadi ya methali hii inamweka mwanamume katika kundi jingine tofauti na kundi hili la utunzaji wa watoto.

Pia, katika methali ya (3) itikadi ya uaminifu wa mama inabainika. Katika methali hii, mama anabainishwa kama mwaminifu na jasiri kwa watoto wake.

'Endugu' ni ndani ya chumba ambamo mna giza. 'Orumuri' ni kurunzi ambayo inatoa mwanga. Kwa hivyo, unapomweka mama yako katika chumba chenye giza, hakuna haja ya kuweka kurunzi. Kwa sababu ya uaminifu wa mama, hakuna haja tena ya kufuatilia mali ambayo imewekwa chini ya dhamana yake. Inamaanisha kwamba mama anawajibikia mali ya mwanawe. Itikadi zilizomo katika methali hii kwa muhtasari ni kwamba mama anaoneshwa kama msiri, jasiri, mwaminifu, mwajibikaji na mwenye upendo wa dhati na anayejitolea kwa heri ya watoto wake.

#### 4.1.5.1 Itikadi za Kiuana na Suala la Mama wa Kambo

Mama wa kambo ni mojawapo ya masuala muhimu yanayoendelezwa katika methali za jamii nyingi ulimwenguni (Deka hm,) hususani katika tamaduni za Kiafrika. Mama wa kambo anarejelewa kama mwanamke anayependelea watoto wake aliowazaa kuliko watoto wa kambo. Suala hili la mama wa kambo mara nyingi huibuka wakati watoto wamepoteza mama zao kwa kufariki au kutalikiwa kutokana na changamoto za ndoa. Mawazo haya yanaungwa mkono na Sarma (2008) anayeeleza kwamba suala la mama wa kambo linasababishwa na ndoa za mseto ambazo zinaishia kwenye talaka. Katika jamii ya Wanyankole suala hili linabainika katika methali zao. Katika jamii hiyo mama wa kambo anachukuliwa kama asiyependa watoto wa kambo, asiye na upendo, mwenye hila na katili. Kwa ujumla, mama wa kambo hudhaniwa kuwa mbaya kwa mtoto asiyemzaa. Methali zifuatazo katika Jedwali Na. 7 zinadhihirisha itikadi hii:

**Jedwali 7: Methali kuhusu Itikadi ya Mama wa Kambo**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omwana aine mukaishe tahwa bunaku.* | Mtoto anayeishi na mama wa kambo haachi kulia. |
| 2. | *Oteekyerwa muka ishe niwe arya munonga.* | Apikiwaye na mama wa kambo ndiye hula sana. |
| 3. | *Ku ogaya obukono bukye bwa nyoko ebikono ebihango bya mukasho bikweshumba ohendeka.* | Unapodharau mikono midogo ya mamako, mikubwa ya mama wa kambo itakuhepa na utaanguka chini. |
| 4 | *Omwana ayonka mukeishe buri aba abuzire nyina.* | Titi la mama litamu hata likiwa la mbwa. |
| 5 | *Ebihande ni nyoko obunono ni mukasho.* | Unga wa chenga chenga ni mamako unga safi ni mama wa kambo. |

Katika methali hii ya (1), katika Jedwali Na. 7 mtoto anayeishi na mama wa kambo haishiwi na majonzi. Itikadi inayodhihirika katika methali hii ni kwamba mama wa kambo anamtesa mtoto wa kambo ambaye anaonekana kuwa hana raha. Mama huyu hana mapenzi kwa mtoto asiyemzaa akilinganishwa na mama mzazi. Itikadi hii inaendeleza dhana ya umuhimu wa mama kulea watoto wake aliowazaaa na mapenzi yake kwa watoto wake ni ya kweli. Jambo hilo linampa nafasi na hadhi kubwa katika malezi ya watoto. Aidha, methali ya (2) inaendeleza chuki na visingizio vya mama wa kambo kwa mtoto wa kambo kuwa anakula sana. Mtoto huyo kama ni wake anatamani ale sana ili apate nguvu za kukua. Miongoni mwa watoto anaowatunza, mtoto wa mke mwenzake ndiye analaumiwa daima kuwa na tabia mbaya kwa kusingiziwa. Itikadi hii ya mama wa kambo inadhihirisha chuki kwa mtoto wa mke mwenza. Kila kosa hata kama si mtoto wa kambo kalitenda, ndiye analaumiwa. Itikadi hii kama inavyobainika katika methali za Kinyankole inaakisi desturi ya jamii ya Wanyankole na chanzo chake ni wanaume kukubali kuendeleza ndoa za mitala.

Methali hii ya (3) inabainisha imani ya mama kwa watoto wake. Mama anaweza kuwa na uwezo mdogo kama unavyoashiriwa na mikono midogo lakini uwezo huo ni wa kweli. Kwake mama wa kambo, uwezo wake mkubwa hauwezi kuaminika, hatimaye, mama wa kambo atamkwepa mtoto huyo bila huruma na ataanguka chini. Methali inabainisha itikadi ya usaliti wa mama wa kambo, kutokuwa mwaminifu na anayejisingizia kuwa ni uaminifu kwa mtoto wa mke mwenzake. Itikadi katika methali hii inamhadharisha mtoto kutodanganywa na upendo wa mama wa kambo ambao unaweza kumfanya kupata matatizo. ‘Bikweshumba’/‘inakuepa’ ni neno linalothibitisha kutoaminika kwa mama wa kambo. Methali hii inawasilisha tofauti iliyopo kati ya thamani ya mama mzazi kwa mwanawe na mama wa kambo. Nadharia ya Ufeministi, mhimili unaosema kuwa wanawake wanapaswa kukuza na kuendeleza umoja wao kama kundi linalodhulumiwa kwa kupeana nguvu. Vitendo hivi vya chuki na kutuhumiana kwa wakewenza vinaendeleza utengano kati yao. Utengano huu hauwezi kuwakomboa wanawake kama kundi linalodhulumiwa na wanaume.

Pamoja na hayo, methali ya (5) inaendelea zaidi kubainisha ubaya wa mama wa kambo. Mtoto anapaswa kunyonya maziwa ya mama yake mzazi wala si ya mama wa kambo. Mtoto anapofikia kiwango cha kunyonya maziwa ya mama wa kambo, atakuwa amekosa mama mzazi. Itikadi hii inamweka mama wa kambo katika nafasi ya mbali sana na utunzaji wa watoto wa kambo. Utunzaji huu unawakilishwa na unyonyaji wa maziwa. Haya yote yana chanzo chake katika uhasama unaoibuka kwa sababu ya kuwepo kwa ndoa za mseto.

### 4.1.6 Itikadi za Kiuana na Suala la Uongozi katika jamii

Mwanamume anashikilia nafasi ya uongozi katika jamiiitika jamii ya Wanyankole ambapo wanaume walikuwa na dhamana ya kulinda familia zao na kuzielekeza. Imani hii inaelezwa zaidi na Opunde na wenzake (2018) kwamba katika jamii nyingi za Kiafrikaa mwanamume alihitajika kuiongoza jamii kupitia uzalishaji mali, kuilinda kutokana na adui na kuipatia mwelekeo.

Mwanamume anapaswa kuwa kiongozi wa familia, hakimu, mwenye msimamo na anayetarajiwa kuheshimiwa kwa sababu ya uwezo wake mkubwa. Mwamzandi (2016) ana hoja yake kwamba, mwanamume ana umaarufu na kubainika kupewa mamlaka katika jamii. Mwanamume anashawishika kukubali kuwa na uwezo mkubwa kuliko mwanamke kama wanavyosema Malenya na wenzake (2020:57):

> Mwanamume anadai kwamba amepewa uwezo mkubwa
> na Mungu wa kumtawala mwanamke.

Methali za Kinyankole zimedhihirisha majukumu ambayo yanampa nafasi ya kusimamia shughuli za familia tofauti na mwanamke. Jamii huyachukulia majukumu hayo kuwa ni ya kiume. Mosha (2016) anadai kuwa mwanamume katika jamii zinazotawaliwa na mfumodume anabainika kuwa mwenye msimamo. Itikadi inayombainisha mwanamume katika nafasi hii ya uongozi na mamlaka kuliko mwanamke inaendelezwa na desturi ya kitamaduni. Itikadi hii ipo na inathibitishwa katika methali za Kinyankole zifuatazo kuhusu majukumu, haki na hadhi yake katika jamii ya Wanyankole:

**Jedwali 8: Methali kuhusu Itikadi ya Uongozi**

| **Na.** | **Methali ya Kinyankole** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|---|
| 1. | *Nyineka ku aba atagiire mukisibo, eze ziitwa engoha.* | Mwenye boma asipoenda zizini, ng'ombe wake humalizwa na kupe. |
| 2. | *Nyineeka yaba atarimu zibyamira eshaabo.* | Mwenye boma asipokuwepo ng'ombe hulala pachafu |
| 3. | *Nyineeka ku ashitamira orurimi entaama zirara omushondi.* | Mwenye boma akikalia ulimi, kondoo hulala pachafu |
| 4. | *Nyineeka ku ainika amabega eka emarwa amayonza.* | Mwenye boma akiinamisha mabega familia humalizwa na vibyongo. |

Methali namba (1), (2) na (3) katika Jedwali Na. 8: matumizi ya neno 'Nyineeka' linamaanisha mkuu wa familia na 'Mkuu wa familia ni mwanamume' kwa madai ya mhojiwa SHM 4 21/04/2018. Methali ya (2) inamaanisha kwamba mkuu wa familia asipofuatilia ng'ombe wake zizini kuwakagua, watashambuliwa na kupe. Inadhihirika kwamba jukumu la usimamizi wa mali katika methali hii mwanamume anawajibishwa kama mkuu wa familia. Mwanamke anabainika kutoshughulika na jukumu hili maana si lake. Hata kama mke yupo nyumbani wakati mume wake hayupo usimamizi hautekelezeki. Mwanamke hashughulishwi na usimamizi kwa sababu si jukumu lake analopaswa kulitekeleza kulingana na itikadi katika methali hiyo. Mtafiti alimhoji KRH 2, mwezi wa 18/04/2018 kuhusu mamlaka ya mwanamke nyumbani, alieleza kwamba mwanamke anakuwa na majukumu yake ambayo anapaswa kuyatekeleza, kwa mfano awasimamie na kuelekeza watoto wake wa kike katika mapishi na kazi nyingize za nyumbani za kike. Anafaa kuhakikisha kwamba watoto wa kike wanatekeleza majukumu yao ipasavyo.

Aidha, itikadi katika methali ya (2) inadhihirisha kuwa mali inayosimamiwa ni ya mwanamume kulingana na matumizi ya kimilikishi ‘eze’/wake. Mwanamume akiwepo hakuna haja ya mwanamke kuwajibikia majukumu hayo. Isitoshe, methali hiyo ya (2) inasisitiza itikadi ya mwanamume kuwa msimamizi kwa ajili ya kuratibu masuala ya nyumbani. Methali inaeleza kwamba mkuu wa familia asipokuwepo ng’ombe wake watalala pahali pachafu. Itikadi hii inabainisha ushawishi wa mwanamke kukubali kwamba jukumu la usimamizi wa mali, mwanamume ndiye anapaswa kuutekeleza kwa sababu hata na mali ni yake. Ukubalifu wa wanawake kuchukulia jukumu la usimamizi kuwa la wanaume ni utawaliwa unalenga kujitolea kwao kwa njia ya ushawishi kuendelea kutumikia wanaume. Mawazo haya yanaendelezwa na mhimili wa nadharia ya Itikadi kwamba ukubalifu unapatikana kutokana na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala. Utawala huo unalenga kujitolea na kutumika kwa tabaka tawaliwa wakitumikia kundi dogo la watawala.

Aidha, methali ya (3) inasisitiza itikadi ya mamlaka ya wanaume ya usimamizi wa familia na kutowajibika kwa wanawake kuhusu jukumu hili. Methali hii inamaanisha kwamba mkuu wa nyumba asipotoa sauti na maelekezo hakutakuwa na utaratibu nyumbani. Mwanamume ndani ya nyumba hapaswi kunyamaza au kubweteka kwa sababu akifanya hivyo mambo yatasambaratika. Matumizi ya nahau ya ‘Kukalia ulimi’ katika methali hii kunaashiria mwanamume ambaye anakuwa mkimya. Mwanamume wa aina hii atasababisha kuharibika kwa mambo kwenye familia. Itikadi hii ya mwanamume kuwa msimamizi na mwelekezi wa shughuli za nyumbani, inadhihirisha jukumu na nafasi ya mwanamume ya kutokaa kimya kama kutakuwepo utaratibu kwa familia yake. ‘Nyineeka’ ni neno

linaloundwa pamoja na kimilikishi cha nafsi ya kwanza cha umoja – (nyine - Ninamiliki, eka - nyumba). Katika utamaduni wa Wanyankole, mwanamume ndiye mwenye boma au mwenye nyumba. Itikadi hii inawatenga wanawake kuhusu suala hili la usimamizi. Hata kama kuna mwanamke, ni wajibu wa mwanamume kuhakikisha kila jambo linakuwa katika utaratibu wake. Kwa mujibu wa mhojiwa SHM 1 katika mahojiano na yeye yaliyofanyika tarehe 19/04/2018 wilayani Sheema , alishikilia kwamba mume anafaa kuwa msimamizi wa shughuli za mke pamoja na maelekezo ya watoto. Pamoja na hayo, mume anawajibishwa kwa mambo yote nyumbani pamoja na maelekezo bora ya watoto. Itikadi inayoendelezwa ni ya utawala wa mwanamume kumtawala mwanamke.

Vilevile, katika methali ya (4) mkuu wa nyumba anaelezwa kwamba, anapotembea kwa mtindo wa kuinamisha mabega, wanafamilia wanaiga mwendo wake kwa kutembea kama yeye na hatimaye familia nzima kuambukizwa vibyongo. Itikadi inayobainika katika methali hii ni ya kwamba mwanamume anapaswa kuwa kielelezo na kiongozi bora katika familia. Mwanamume anakuwa kielelezo bora kwa kutoa maelekezo sahihi na wanafamilia wengine kumuiga. Mhojiwa SHM 3 katika mahojiano yaliyofanyika tarehe 21/04/2018 wilayani Sheema alieleza kuwa mwanamume anapaswa kuwa makini na mienendo au tabia zake kwa kuwa aghalabu watoto huiga kwake. Hivyo, kiongozi wa familia ambaye ni mwanamume anapaswa kuwa mfano bora kitabia, la sivyo, wafuasi wake, yaani wanafamilia wanaweza kuiga mienendo yake mibaya.

Methali hizi zinadhihirisha kwamba wanaume wanaendeleza itikadi shawishi na kuwafanya wanawake kukubali mamlaka ya wanaume. Wanawake kuwasilishwa

kama viumbe wasio na mamlaka na wanaotegemea kuongozwa na wanaume ni itikadi inayotokana na  amali za kifamilia na kijamii kwa jumla kwa njia ya ukubalifu. Shah na wenzake (2018) wanathibitisha hoja hii kwamba utawala wa kundi lenye mamlaka dhidi ya kundi tawaliwa unaendeleza mamlaka yake kwa kuwashawishi watawaliwa kuamini kwamba mahusiano yanayoendelezwa kati yao ni kwa manufaa yao, jambo ambalo si la ukweli. Itikadi hii inabainisha namna wanaume wanavyotekeleza na kuhalalisha mamlaka yao juu ya wanawake na vile wanavyoweza kuendeleza nafasi yao katika jamii kupitia kwa ukubalifu wa wanawake katika methali za Kinyankole.

#### 4.1.6.1 Itikadi za Kiuana na Suala la Uhuru wa Mwanamume

Mwanamume anachukuliwa kuwa kiumbe mwenye uhuru wa kufanya uchaguzi anaotaka na aliye na nguvu. Malenya (2020) anafafanua kwamba, mwanamume anadhihirisha nguvu za kimwili, shujaa na anayejitakia makuu. Methali za Kinyankole ambazo zinabainisha itikadi hii zipo na zinaiendeleza itikadi hii kama ifuatavyo:

**Jedwali 9: Methali kuhusu Itikadi ya Kuashiria na Uhuru wa Mwanamume**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Nyineeka ateera enanga yarikwenda* | Mkuu wa familia hucheza kinanda atakacho. |
| 2. | *Omushaija omuhango ayeha ekitebe kihango* | Mwanamume mnene hujipatia kiti kikubwa |
| 3. | *Akashaija kakye okagaira nseeri* | Mwanamume mdogo unamdharau akiwa mbali |

Methali ya (1) inamaanisha kwamba mwanamume ni mkuu katika familia yake na ana uhuru wa kucheza kinanda anachotaka. Kinanda ni chombo cha muziki

kinachotoa sauti kwa kubonyezwa na kuvutwa kwa mikono. Methali hii inaonesha itikadi ya uhuru wa mwanamume kufanya lolote analotaka kwa hiari yake bila kikwazo. Katika mahojiano yaliyofanyika wilayani Kiruhura yaliyoendelezwa tarehe 18/04/2018, katika kutaka kubaini mamlaka na uhuru wa mwanamume , Mhojiwa KRH 4, alisema kwamba mwanamume kama kiongozi katika familia yake, hakuna anayemkataza kufanya jambo lolote kwa uamuzi wake na hiari. Itikadi hii kama inavyobainika katika methali na kwa kutathmini maoni ya mhojiwa inadhihirisha ubabe wa mwanamume wa kufanya uchaguzi atakao na unyamazishaji wa mwanamke. Itikadi hii inashawishi wanawake kukubali kuwa mwanamume ana uwezo maalumu. Kwa upande mwingine, mwanamke hana uhuru na fursa ya kufanya uchaguzi anaotaka. Itikadi kama inavyowasilishwa katika methali hii haidhihirishi fursa ya uamuzi wenye misingi ya makubaliano na maelewano kati ya mwanamke na mwanamume. Kulingana na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, itikadi hii haikidhi matarajio ya usawa wa kiuana katika jamii ya Wanyankole ambapo mwanamume na mwanamke kimsingi wanastahili kuelewana na kufanya uamuzi kwa pamoja kama mume na mke.

Pamoja na uhuru wa mwanamume wa kufanya uchaguzi anaotaka unaoendelezwa kwa njia ya ukubalifu na ushawishi, methali ya (2) inawasilisha itikadi ya kujiashiria kwa mwanamume. Mwanamume, anajihisi kuwa na nguvu za kimwili na kujitakia makuu. Kulingana na maoni ya mhojiwa SHM 3, kwenye mahojiano ya tarehe 20/04/2018, mwanamume, hasa ambaye ni mkubwa kimwili anahusishwa na utawala, nguvu na heshima. Mhojiwa aliendelea kusema kwamba, kwa mfano kwenye sherehe, mwanamume wa aina hiyo anaweza

kupewa hata viti viwili bila kuomba. Hii inaonesha itikadi kwamba mwanamume anatambulishwa kuwa mbabe anayepaswa kuheshimiwa kwa matarajio ya jamii ya Wanyankole. Heshima hiyo huambatana na nguvu za kimwili na kujiashiria, huku mwanamke akidhihirika kuwa ni dhaifu. Itikadi hii inathibitishwa na Kobia na Mung'ahu (2017) wakiwarejelea Chafetz (1974) na Doyle (1985) ambao wanatambua kwamba ubabedume unajitokeza katika desturi kwa jumla kupitia maumbile na nguvu za kimwili. Mwanamume hushawishika kwa itikadi ya kwamba ni mwenye nguvu na mwenye mamlaka. Ushawishi huu unabainishwa na jinsi anavyojitakia makuu na kujiashiria. Uwezo huu wa kujiashiria unamfanya pia mwanamke kukubali nafasi yake ya kumtambua na kumheshimu mwanamume kama mwenye nguvu na anayestahili kuwa mbele. Ukubwa wa mwili wa mwanamume kuhusishwa na mamlaka, utawala, busara na heshima si kigezo cha kuwabagua binadamu kwa misingi ya kiuana. Mawazo haya yanaungwa mkono na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa mhimili wake unaofafanua kwamba wanawake wazinduke na kubadili mielekeo vile wanavyojiona katika uhusiano na wanaume. Aidha, itikadi ya methali hii inadhihirisha mwelekeo wa Gramsci (1985) kuhusu matumizi ya ushawishi na ukubalifu ili kuendeleza itikadi ya ubwana. Murithi (2017) anadhihirisha hoja hii kwamba mwanamume anabainika kama mwenye haki ya kutenda lolote lile mradi atimize haja zake.

Itikadi ya mamlaka ya mwanamume, kujiashiria kwa mwanamume, ubabe wa mwanamume, mwanamke kumheshimu mwanamume kwenye asasi ya ndoa inaendelezwa zaidi na methali ya (3). Methali hii inamaanisha kwamba mwanamume hudharauliwa akiwa mbali lakini anaposogelea anakuwa na sifa

zote zinazotambulisha mume kulingana na utamaduni wa jamii. Mume kama anatekeleza majukumu yake ya kiume, anastahili kuheshimiwa. Hata kama majukumu yake hayatekelezi sawasawa, mume hatakiwi kudharauliwa na mke wake. Itikadi hii inadhihirisha kuwa mwanamume ni kiumbe anayestahili kuheshimiwa na kutiiwa na mwanamke faraghani na hadharani hata kama ni gumegume kwa masuala ya faraghani na kutomridhisha mke wake kimapenzi. Mume wa aina hiyo anaposhindwa kutekeleza shughuli hiyo ipasavyo haimuondolei sifa ya kuwa mwanamume mwenye mamlaka. Mume na mke wakiwa hadharani, mke wake hapaswi kumdharau kwa sababu hali hiyo haiondoi ukweli kuwa ndiye mume wake anayefaa kuheshimiwa.

### 4.1.7 Itikadi za Kiuana na Suala la Ujasiriamali

**Jedwali 10: Methali za Itikadi za Kiuana na Suala la Ujasiriamali**

| **Na.** | **Methali ya Kinyankole** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|---|
| 1. | *Ebibahingire baine enda nibyo barya bazaire.* | Chakula wanacholima wakiwa wajawazito ndicho huliwa wajifunguapo. |
| 2. | *Omukazi taba mugyenyi* | Mwanamke hawi mgeni |
| 3. | *Omukazi omuhingi atega eiguru entabire.* | Mwanamke mkulima hugema shamba mbingu. |
| 4. | *Omukazi oine iba taba mworo* | Mwanamke aliye na mume hawi maskini. |
| 5. | *Omukazi omugara ayesiima yaazaara.* | Mwanamke mvivu hufurahi anapozaa watoto**.** |

Methali hii ya (1) katika jedwali la 10 inaeleza kuwa wanawake wakiwa wajawazito wanapaswa kufanya kazi kwa bidii kama njia ya kujihami ili wanapojifungua, waweze kuwa na chakula cha kutosha. Itikadi katika methali hii inaonesha kuwa wanaume wako tayari kuwanyonya na kuwanyanyasa wanawake kwa kuwafanya wakubali kufanya kazi ngumu hata wakiwa wajawazito.

Mhojiwa SHM 4 kwenye mahojiano ya tarehe 21/04/2018 alisema kuwa, baada ya kujifungua, mwanamke anakaa muda mrefu bila kufanya kazi na ndiyo sababu anashauriwa kujihami mapema. Kwa hivyo, kazi ambayo angefanya wakati huo wa kupumzika anapaswa kuishughulikia akiwa mjamzito. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mhimili unaoeleza kwamba jamii iendelezwe kwenye misingi ya amali za kibinadamu, hauafikiani na mawazo ya mhojiwa SHM 4 hapo juu. Mwanamke mjamzito huwa anastahili kupewa muda wa kupumzika na kuhimiliwa lakini katika methali hii, anabainika kutopewa fursa na haki ya kulea mimba bali anatarajiwa kuchapa kazi kwa bidii. Salem (2013: 86) anasema:

> Mwanamke anapokuwa katika hali ya ujauzito, hapati matunzo yanayostahili ili aweze kupata afya, ila anaishi kwa kunyanyasika mpaka atakapojifungua…afya hasa ya uzazi mwanaume hajihusishi.

Itikadi kama inavyobainika katika methali hii haiafikiani na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kuhusu ushirikiano wa wanaume na wanawake ili kuweza kuwahimili wake zao wakiwa wajawazito na hata baada ya kujifungua.

Itikadi kuhusu unyonyaji wa nguvu za mwanamke kwenye kazi inaendelezwa zaidi na methali ya (2). Mgeni katika jamii ya Wanyankole kama ilivyo ada ya Waafrika, anapokelewa kwa heshima kubwa na kupewa huduma nzuri lakini kulingana na maana ya methali hii, mwanamke ambaye yuko ugenini hapokei sifa za mgeni anazostahili kama vile kuandaliwa chakula na kuhudumiwa ipasavyo. Mwanamke anapokuwa ugenini hasubiri kupewa heshima hii na huduma za mgeni anazostahiki. Mwanamke anashawishika kwa itikadi hii ya sifa yake ya kufanya kazi za jikoni na kuziendeleza kwa ukubalifu kuwa ni jukumu lake. Hakai na kusubiri kuhudumiwa hata kama ni mgeni. Mara moja

anajishirikisha na kujibidiisha katika kufanya kazi za jikoni kama maandalizi ya chakula, kuosha vyombo miongoni mwa shughuli nyingine. Mwanamke anafanya hivi kwa sababu anaamini kuwa hii ni kazi yake anayopaswa kuitekeleza kama inavyoaminiwa na jamii. Tofauti na mwanamume ambaye anakaa na kuhudumiwa kama mgeni. Mhimili wa nadharia ya Itikadi unaodai kwamba uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii. Utawala huu unachukulia fikira ambazo si za kweli na kuzifnya zionekane kuwa za kweli. Kulingana na mhimili huu tunadhihirisha vile itikadi hii inavyoshawishi wanawake kukubali jukumu hili kuwa wanapaswa kulitekeleza. Shughuli hizi zote na juhudi zake zinaisha kwa kunyonywa bila kuwekwa kwenye mizani ya thamani ya pesa.

Nguvu za mwanamke kuhusu uzalishaji wa mali zinaendelea kubainika katika methali ya (3). Methali hii inamaanisha kwamba mwanamke anayejibidiisha na kazi, anapaswa kutayarisha mapema shamba lake ili mvua inaponyesha anatangulia kupanda. Mwanamke wa Kinyankole alikuwa na jukumu la kufanya kazi ili apate chakula cha kutosha cha kulisha familia yake. Kirindi (2008) anasema kwamba wanawake walikuwa wanafanya kazi za ukulima katika mashamba yao siku nzima. Mwanamume naye wakati wa kuoa, alitakiwa kutafuta mke mwenye uwezo wa kufanya kazi. Kulingana na maoni ya mhojiwa SHM 3, tarehe 20/04/2018, anaeleza kwamba hadi sasa, mke anayependelewa kuolewa katika jamii ya Wanyankole ni yule mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa bidii. Itikadi inayoelezwa katika methali hii ya mwanamke kufanya kazi kwa bidii ili kukimu familia, kunaonesha kuwa ni nguzo muhimu katika maendeleo ya jamii. Juhudi za mwanamke anaziendeleza kwa ukubalifu, hali inayoafikiana na

Nadharia ya Itikadi kwa mhimili unaosema kwamba tabaka tawaliwa hushughulikia kazi zinazohimili maendeleo ya jamii lakini juhudi zao zinalinufaisha tabaka tawala. Kwa hivyo, wanawake wanawakilisha tabaka la wafanyakazi ambapo shughuli za uzalishaji mali kupitia ukulima zinabainika kuwa mikononi mwao. Kazi hizi ndogondogo ndizo zinasaidia uzalishaji wa mali na hivyo kuweza kuhimili familia na jamii kwa ujumla.

Methali ya (4**)** inaeleza kwamba mwanamke anayeishi na mume hawi maskini. Ufafanuzi wake ni kwamba mafanikio ya mwanamke yanategemea uwepo wa mume. Hivyo, methali inaonyesha kuwa mume ni nguzo muhimu katika maisha ya mwanamke. Itikadi inayobainishwa katika methali hii ni ya mwanamke kumtegemea mwanamume kwa ufanisi wake. Itikadi hii inaendelezwa kwa misingi ya ushawishi kati ya wanaume na wanawake. Wanaume kama kundi tawala wanalishawishi kundi la wanawake kujitambua kuwa hawawezi kujitegemea na kufaulu maishani. Mhojiwa KRH 1 tarehe 17/04/2018 alisema kwamba, ili mwanamke aweze kufanikiwa kiuchumi ni lazima awe na mume ambaye ataweza kufanikisha maendeleo yake. Itikadi hii inaendeleza ugandishaji wa mawazo kwamba mwanamke hawezi kufanya na kuendeleza shughuli ambazo zinaweza kumuinua na kumfanya ajitegemee bila juhudi za mwanamume. Itikadi hii inadhihirisha utawala wa wanaume kwa kupotosha hali halisi kwa sababu inaendelezwa kwa ushawishi ili kubainika kuwa ya kweli na kufanya wanawake kukubali nafasi ya utegemezi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, wanawake wanapaswa kuzinduka na kupinga mielekeo ya namna hii vile wanavyojiona katika uhusiano na wanaume.

Aidha, itikadi ya haja ya mwanamke kuwajibikia kazi inaendelezwa na methali ya (5). Maana ya methali hii ni kwamba mwanamke mvivu anafurahi anapozaa watoto. Kulingana na itikadi hii, kimsingi mwanamke anatarajiwa kufanya kazi nyumbani kwa mume wake kama mojawapo ya majukumu muhimu. Kwa hivyo, watoto watamsaidia kazi zake ambazo anapaswa kufanya. Kwa mujibu wa mhojiwa KRH 3 tarehe 17/04/2018, mwanamke anaposhindwa kufanya kazi zake anaingia katika mgogoro na mume wake. Mwanamke wa aina hiyo anadharauliwa na pengine hata kutalikiwa. Maoni ya mhojiwa yanatubainishia kuwa thamani ya mwanamke inaangaliwa katika muktadha wa kufanya kazi na kuzalisha mali. Hii ndiyo sababu mwanamke anashawishika na kukubali jukumu hili kama lake kiasi kwamba anapozaa anaona amepata bahati ya kusaidiwa na watoto kwa kazi zake anazotarajia kuwajibikia. Itikadi hii inashadidiwa na mhimili wa Nadharia ya Itikadi ya kwamba, ukubalifu unapatikana kutokana na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala. Utawala unalenga kujitolea na kutumika kwa tabaka tawaliwa wakitumikia kundi dogo la watawala.

Kwa mtazamo mwingine, mwanamke mvivu anapozaa watoto, wanakuwa kishikio madhubuti cha ndoa yake hata kama hataweza kufanya kazi kama inavyotarajiwa. Itikadi hii inaonyesha mwanamke kimsingi kama anayetarajiwa kufanya kazi kwa bidii. Mwanamke anapouwa mvivu lakini kama ataweza kuzaa watoto kwa mume wake, watoto hao watakuwa kiungo na kibali cha kutulia kwenye ndoa. Kwa hivyo, itikadi ya kiuana kuhusu kazi inashawishi mwanamke kukubali kutarajiwa kufanya kazi kwa bidii na utegemezi wake kwa mwanamume katika kufanya kazi.

### 4.1.8 Itikadi ya Uwezo wa Kufanya Kazi

Wanawake wa Kiafrika wanadhalilishwa katika methali za jamii zao na itikadi za kiuana ambazo zinachukua mkondo wa ubabedume ambapo wanawake wanaangaliwa kama wenye uwezo mdogo wa kuzalisha mali. Methali hizo huwatofautisha wanawake na wanaume kwa misingi ya udhaifu wao na nguvu za wanaume. Wanawake pia wanashawishika na kukubali udhaifu wao huku wakikiona kiumbe cha kiume kama chenye nguvu. Itikadi ya unyonge wa wanawake kwa misingi ya kiuana inafafanuliwa na mhimili wa Nadharia ya Itikadi wa ukubalifu na ushawishi. Ukubalifu na ushawishi unadhihirika pale ambapo tabaka tawaliwa hujitolea kutumikia kundi dogo la watawala. Hussein (2009) anafafanua kwamba wanawake wanapotambulika kuwa wao ni viumbe dhaifu, wanyonge na wategemezi, wanashawishika na hali yao hiyo ya unyonge na utegemezi kiitikadi. Methali zifuatazo zinabainisha itikadi hiyo.

**Jedwali 11: Methali kuhusu Uwezo wa Kufanya Kazi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1.<br><br>2.<br>3. | *Omukazi kuayikarira tayimuka.*<br>*Omukazi ku aita takurura*<br>*Emburabure yamukazi ati kuri*<br>*nabeire omushaija* | Mwanamke anapompiga (vizia) mwenzake mweleka hainuki<br>Mwanamke anapoua havuti mzoga.<br>Mwanamke mzembe, laiti ningekuwa mwanamume. |

Itikadi ya unyonge wa mwanamke inaendelezwa katika methali ya (1) katika Jedwali la 11. Methali hii inabainisha kuwa wanawake wakiwa wanapigana, mmoja akimzidi mwenzake nguvu na kumtupa chini, aliyetupwa chini naye hawezi kuinuka. Methali hii inabainisha itikadi ya unyonge wa mwanamke. Hata

hivyo, shindano la kutupa mweleka ni la wanaume kwa sababu linahusisha matumizi ya nguvu nyingi kama anavyoeleza mhojiwa SHM 1 tarehe 19/04/2018. Mwanamke akishiriki katika mashindano hayo na akitupwa mweleka, itakuwa vigumu kupata nguvu za kuinuka. Mwanamke anaposhughulikia jambo hilo, anapata ugumu wa kulikamilisha. Vilevile, methali ya (2) inaonesha unyonge wa mwanamke ambapo kama ameweza kuua mnyama fulani, hawezi kuendelea hatua zaidi ya kuvuta mzoga wa mnyama huyo. Pamoja na itikadi ya udhaifu wa mwanamke inayodhihirika, kuna itikadi ya uvivu wa mwanamke katika methali hizi. Mawazo haya ya kiitikadi kama yanavyodhihirika ni ukweli usio sahihi. Mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unapendekeza kwamba tabia za uana ambazo zinaonekana kutobadilika zitathminiwe kila mara kwa muktadha wa kijamii bali si kama suala la kimaumbile. Itikadi inayobainishwa katika methali hii inalenga kuendeleza uwezo wa mwanamume na mwanamke kama asiyeweza kuchangia maendeleo ya jamii. Mwanamke anashawishika kukubali uvivu na udhaifu wake. Hali hii inapoendelezwa hivi inadhihirisha utofauti wenye misingi ya kiuana kati ya wanawake na wanaume ambao wanawake pia wanaukubali.

Jamii ambazo zinaendelezwa kwa misingi ya mfumodume zinadai kuwa wanawake wanapaswa kuhimiliwa na wanaume. Wanaume wanachukuliwa kuwa wenye uwezo wa kuwasaidia wanawake ambao hawajiwezi. Hussein (2009) anaeleza kwamba wanawake wanaendelea kusawiriwa kama wenye uwezo mdogo na wanatarajiwa kuongozwa na wanaume. Itikadi hii ipo katika methali ya (3) ya Kinyankole. Methali hii inaeleza itikadi inayojikita katika mila na desturi za Wanyankole kwamba, wanaume ndio wanaothaminiwa na wanaopewa kipaumbele. Methali hii inamwonesha mwanamke ambaye anatamani kuwa

mwanamume. Kiyimba (2001) anadai kwamba mwanamke kuzaliwa kama kiumbe wa kike, analalamikia uwezo wake na jinsi yake kuwa ndiyo chanzo za kutojiweza kama mwanamke huku akitamani nafasi ya uwezo anaokuwa nao mwanamume katika jamii. Kulingana na mawazo ya Kiyimba, methali hii inawafanya wanawake kujutia kwa nini waliumbwa hivyo.

Aidha, itikadi hii ya kutojiamini kwa wanawake na mamlaka ya wanaume inaendelezwa zaidi na Ssetuba (2002) akirejelea misemo ya Kiganda kuashiria uwezo wao. Mwanamume ‘Omusajja’ anajiashiria kwa kudai kuwa *'Nze eyajja omu sajja* (Mimi niliyekuja peke yangu, sikufika!) na kwa upande wa mwanamke ‘*omukazi*’ analalamika, ‘*omukazi’* (Maskini, kumbe mimi niliyekuja peke yangu!) kwa matumizi ya neno ‘kazzi’ kuonesha majuto na kilio cha mwanamke pamoja na kujihurumia. Itikadi hii inawafanya wanawake kuamini kwamba majukumu mengine yanawashinda kwa sababu ya maumbile yao. Wanawake wanashawishika na kukubali kwamba kuna kazi ambazo zinapaswa kufanywa na wanaume na wao hawaziwezi. Itikadi hii inaendelezwa na Nadharia ya Itikadi, ambapo wanawake wanashawishika na kukubali jinsi yao kuwa ni dhaifu, na hivyo wanaopaswa kuwa chini ya wanaume. Itikadi hii inaendeleza utenganishaji wa kazi kati ya wanawake na wanaume. ‘Emburabure’ inamrejelea mwanamke ambaye hata kazi zake za kike zinamshinda na anatoa kisingizio cha kuwa yeye ni kiumbe wa kike. Kulingana na itikadi katika methali hii ya (3), wanawake kwa mujibu wa Nadharia ya Itikadi unaosema kwamba uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii, anawake wanakubali kuchukulia fikira ambazo si za kweli kuhusu uwezo wao wa kufanya

kazi na kuzifanya kuwa za kweli kiasi cha kuona kazi nyingine hawaziwezi na kuzichukulia kuwa ni za kiume.

### 4.1.9 Itikadi na Suala la Urembo wa Wanawake

Wanawake katika jamii tofauti za Kiafrika wanatarajiwa kuvutia kwa kujiremba. Ndungo (1998) anatambua kwamba wanawake jukumu wanalolikubali kutokana na matarajio ya jamii ni kujiremba kwa ajili ya kuvutia wanaume. Dhana hii ya urembo inaendelezwa katika methali zifuatazo za Kinyankore:

**Jedwali 12: Methali kuhusu Mahusiano ya Uzuri**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omukazi mubi n'otajwaire.* | Mwanamke asovutia ni yule asiyejikwatuwa |
| 2. | *Omukazi aba amate ayerinda ebitakoozi.* | Mwanamke ni maziwa, anajihadhari na uchafu |
| 3. | *Omukazi omurofa bamureebera ahabyokuzwara.* | Mwanamke mchafu hutambulika kwa mavazi yake. |

Itikadi ya usafi na urembo wa wanawake inaendelezwa katika methali ya (1) katika Jedwali Na. 12. Methali hii inamaanasha kwamba mwanamke ambaye havutii ni yule asiyevaa vizuri. Kuvaa vizuri katika muktadha huu kunahusisha mambo kama vile kuvaa nguo zinazopendeza, kujipamba, kuchega nywele, kujipaka mafuta yenye uturi. Kulingana na utamaduni wa Wanyankole ni jukumu la wanawake kujiremba kwa kuvaa vizuri ili wapendeze. Itikadi hii ya usafi wa wanawake na kuonekana vizuri kulingana na maoni ya mhojiwa KRH 4 tarehe 18/04/2018 ni  kwa sababu wanawake ni utambulisho wa jamii. Mhojiwa aliendelea kueleza kwamba, wanawake ambao hawajali usafi wa miili, mavazi na mwonekano wao hawathaminiwi na jamii. Hivyo, ni jukumu la mke daima kuhakikisha kwamba anakuwa katika hali ya mvuto na kupendeza. Itikadi ya

kumtarajia mwanamke kujirembesha kwa ajili ya kuvutia mwanamume inamfanya kama chombo cha kuvutia wanaume. Mwanamke anashawishika na itikadi hiyo na kukubali thamani ya kujirembesha kwa ajili ya mwanamume. Ingawa wanawake wanapaswa kujirembesha, jukumu hili wanalokubali linawashushia hadhi na kuchukuliwa kama chombo cha kuvutia wanaume. Itikadi hii ya uzuri unaendelezwa zaidi katika methali ya 2.

Methali ya (2) katika Jedwali la 12 inalinganisha utunzaji wa uzuri wa wanawake na maziwa. Maziwa ni kimiminika ambacho kinapaswa kutunzwa kwa umakini ili kisiingie uchafu na hatimaye kuharibika. Istiari ya wanawake kulinganishwa na maziwa ‘omukazi aba amate’ inatubainishia itikadi ya wanawake kuwa makini katika utunzaji wa uzuri wao ili usije ukaharibika na hatimaye kutelekezwa. Urembo na usafi wa wanawake ni dafina ambayo wanapaswa kuilinda.

Wanawake wasiojitunza ni muhali kutamaniwa. Mhojiwa SHM 2 tarehe 20/04/2018 alieleza kuwa urembo wa mwanamke na kutunza usafi wake ni mambo ambayo yanasisitizwa na mwanamume hata wakati wa kuchagua mke wa kuoa. Methali hii inapohakikiwa kwa kuongozwa na mhimili wa Nadharia ya Udenguzi unaodai kwamba matini huwa na mielekeo mingi ya maana ambayo huibua fasili nyingi, itikadi kwamba, ili mwanamke aweze kuvutia yapasa mwanamume kujali maslahi yake inaibuliwa. Kimiminika ambacho kinarejelewa (maziwa) kinahitaji mtu wa kukitunza ili kisiharibike na kwamba hakiwezi kikajitunza chenyewe. Hivyo, hii ni tofauti na maelezo ya methali ambayo inamtaka mwanamke kujijali. Mwanamume ana wajibu kuhakikisha kwamba mke wake amevaa maridadi na anavutia.

Pia, methali ya (3) inafafanua zaidi itikadi ya unadhifu wa wanawake. Methali hii inaeleza kuwa mwanamke mchafu anatambulika kwa nguo zake anazovaa. Nguo zimetumiwa kimetonomia kumfafanua mwanamke mchafu. Nguo za mwanamke zikiwa chafu zinafafanua sifa yake ya uchafu. Hivyo, anapaswa kudumisha usafi ambao unatambulishwa na mavazi yake kwa ajili ya kupendezesha. Kwa hivyo, thamani ya wanawake inashushwa kuchukuliwa kuwa kwenye nafasi ya kupendeza macho ya wanaume. Wanawake wanashawishika na itikadi hii ya kujikwatua kwa ajili ya kupendezesha macho ya wanaume na hatimaye kukubali hadhi hii katika jamii.

## 4.2 Itikadi za Kiuana katika Methali za Kiswahili

Katika sehemu hii itikadi za kiuana zinabainishwa na kuchanganuliwa katika methali za Kiswahili. Itikadi ya haja ya wanawake kutamani kuolewa ili wawe na nafasi ya kutekeleza maamuzi, kuwa na sauti, uwezo wa kumiliki na kudhibitiwa na mume zinadhihirika. Itikadi zinaendelea kudhihirisha kuwa wanaume hawako kwenye nafasi ya kujitegemea bila wake zao. Itikadi hizi na nyingine kama wanawake kutowajibishwa kuwahudumia wanaume kama inavyotarajiwa na kujulikana kimila katika jamii ya Waswahili, itikadi ya  wa kutegemeana na kusaidiana kati ya wanaume na wanawake zinajadiliwa hapa Pia, zipo itikadi zenye mwelekeo wa upendeleo kwa misingi ya uana kama zinavyobainishwa katika methali za Kiswahili.

Waswahili wanatumia methali tofautitofauti kulingana na amali zao za kila siku. Asili ya methali za Kiswahili kama ilivyo katika jamii mbalimbali za Kiafrika

zinatokana na tajriba ya maisha ya kawaida ya Waswahili. Pia, falsafa ya Waswahili inafahamika zaidi kupitia methali za jamii yao.

### 4.2.1 Itikadi za Kiuana na Ndoa

Katika jamii ya Waswahili, ndoa ni kiungo cha mwanamume na mwanamke. Hii ni nguzo muhimu katika kubainisha itikadi za kiuana katika jamii. Sengo (1992) anaeleza kwamba ndoa na harusi ni asasi ya msingi na yenye thamani katika misha ya kila Mswahili. Nafasi ya mwanamume na mwanamke katika ndoa inabainishwa na Kurani pamoja na hadithi za Mtume (A.M.I.N.) katika utamaduni wa Waswahili. Sengo anaeleza zaidi kwamba anayepinga maelekezo hayo au kuyageuza anarejelewa kama muasi, msaliti na mshirikina. Mtoto wa kiume na mtoto wa kike ambaye amefikisha umri wa kuoa au kuolewa, anapaswa kutafutiwa mchumba na wazazi. Harakati zote zinazofanywa na barobaro au mwanamwari zinawaelekeza kupata jiko ili kuwa mume au mke ambaye anatarajiwa kutekeleza majukumu yake ya kindoa. Ndoa ni miongoni mwa asasi za kijamii ambazo zina mchango mkubwa katika kuendeleza na kugandisha itikadi za kiuana kwa wanaume na wanawake na kuchukulia itikadi hizi kama za kimaumbile na za kawaida (Murithi, 2017). Kwa hivyo, mwanamume anaoa kwa matarajio ya kupata mke ambaye ataweza kuendeleza majukumu yake ya kindoa kama inavyobainika katika methali hizi za Kiswahili:

**Jedwali 13: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi za Ndoa**

| Na. | Methali ya Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Asiye na mke yu uchi. |
| 2. | Talaka ni kuvuliwa nguo. |
| 3. | Ndoa ni kutia mkono kizani. |
| 4. | Mke hulia kabla ya kuolewa na mume hulia baada ya kuoa. |
| 5. | Atabaki mtoto wa kiume mwanao mpaka umwozeshe, wa kike atabaki mwanao mpaka kufa kwake. |
| 6. | Ndoa ni nguo inayochanika. |

Mke ni utambulisho na ufahari kwa mume kiutamaduni katika jamii nyingi. Mhojiwa MSA 3 tarehe 11/05/2018 akifafanua kuhusu itikadi hii alidai kwamba, mwanamume bila mke humuwia vigumu kushughulikia na kufanikisha masuala ya nyumbani mwake. Mhojiwa alitoa maoni zaidi kwamba mke ndani ya nyumba humfanya mume na nyumba kwa ujumla kuwa na utaratibu na heshima. Itikadi hii inaelezwa katika methali ya (1) ambayo inamaanisha kwamba mwanamume ambaye hana mke analinganishwa na binadamu aliye uchi. Mke anarejelewa kama nguo ambazo zinaficha viungo vya mwanamume ili asiaibike. Yeye mhojiwa MSA 4 tarehe 12/05/2018 alisema kwamba hakika hakuna binadamu anayependa kuonwa akiwa uchi. Kulingana na maoni hayo, mambo ya nyumbani yakiharibika na kwenda kombo, ili kulinda heshima na staha ya mume na nyumba yake; hivyo, mke anajaribu kuyasitiri. Itikadi hii inamaanisha kwamba mume hawezi kuishi bila mke kutokana na thamani yake kwake. Sifa anazopewa mwanamke ni kulingana na mtazamo wa Nadharia ya Itikadi. Kwa mujibu wa Gramsci (1985) mwanamke anashawishika na kukubali nafasi ya kumtumikia mwanamume. Sannaudin (2015) anaunga mkono hoja hii kwamba, wanawake wanafidiwa kwa kupewa sifa chanya ilhali wanabainishwa kwa mapana kuwa jukumu lao la msingi ni kushughulikia kazi zao za nyumbani. Itikadi

inayobainika ni ya haja ya mwanamume kuoa kwa ajili ya kusaidiwa na mke kuratibu masuala ya nyumbani. Itikadi hii inaonesha kuwa mwanamume anapaswa kuoa na kuishi na mke nyumbani kwa ajili ya kusaidiwa. Mwanamume anadhihirika kama asiyeweza kupanga mambo ya nyumbani bila mke; hivyo, mke ndiye anastahili kufanya kazi hizo.

Aidha, itikadi inashadidia kuwa hata kama kuna matatizo ya kindoa, mwanamke anashawishika kuvumilia kwa ajili ya heshima anayotarajia kutoka kwa jamii. Mwanamke huendelea kulinda umaarufu na kudai heshima hiyo, hata kunapotokea jambo la kusababisha talaka. Methali ya (2) 'Talaka ni kuvuliwa nguo' inafafanua zaidi itikadi ya haja mwanamke kuishi na mume na kuvumiliana kwenye ndoa kwa ajili ya kulinda heshima. Kulingana na methali hii, tunawasilishiwa itikadi ya kuvumiliana katika ndoa na kuzuia mambo yanayoweza kusababisha talaka. Mhojiwa ZNB 2 tarehe 24/05/2018 alisema kuwa katika mila ya Waswahili mume ndiye humpa talaka mke na mke huomba talaka. Maoni ya mhojiwa yanadokeza kwamba mume ndiye mwenye mamlaka na uamuzi wa 'kumvua nguo' mwanamke. Mke huomba talaka kutoka kwa mume wake na mume akiwa hajaridhia, mke huyo hatakuwa huru kufanya uchaguzi anaotaka. Kulingana na Nadharia ya Itikadi, wenye mamlaka wanatumia nafasi zao wanazoshikilia katika kuamulia wale walio chini ya utawala wao. Nguvu na mamlaka hayo yanawaelekeza kufanya uamuzi unaolenga kutekeleza na kutimiza malengo yao dhidi ya wanyonge. Kwa hivyo, wanaume kama kundi lenye mamlaka wanatekeleza maamuzi kuhusu ndoa kati yao na wake zao ambao wako chini yao. Maamuzi haya yanafanywa dhidi ya

uhuru wa wanawake. Hali hii ina mizizi yake katika dini ya Kiislamu ambayo iliathiri utamaduni wa Waswahili.

Kwa mujibu wa mitazamo inayoshikiliwa na jamii kiutamaduni, itikadi hii inavyoelezwa katika methali ya (2) ‘Talaka ni kuvuliwa nguo’ inamwelekeza mwanamke kuonekana mtumwa wa ndoa kwa kunyenyekea na kutii ili asije kuvuliwa nguo. Itikadi hii inashawishi mwanamke kukubali kufungiwa kwa asasi ya ndoa akiogopa kuaibika na kulaumiwa kuwa chanzo cha kuharibika kwa ndoa yake. Mwanamume kwa upande mwingine anaonekana kuwa na mamlaka ya kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu ndoa kati yake na mke wake. Itikadi hii haiungwi mkono na mhimili wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambao unatarajia wanaume na wanawake washughulikie ndoa kwa kushirikiana bila kuathiriwa na majukumu ya kimaumbile. Hali hii haimpatii mwanamke uhuru wa kuamua kuhusu suala hili la talaka. Suala la ndoa linahitaji nguvu na mikakati ya pamoja ili kuweza kudumu na kulitafutia suluhisho mwafaka.

Asasi ya ndoa haifai kuchukulia kiurahisi kwa sababu ya uchangamano wake. Ndoa inahitaji subira, umakini na uamuzi sahihi. Mawazo haya yanaungwa mkono na Abdulla (2016) ambaye anatambua umuhimu wa kuwa na uvumilivu katika ndoa. Methali ya (3) katika Jedwali Na. 15, inalinganisha ndoa na kutia mkono mahali fulani katika giza. Kutia mkono gizani ni kutia mkono mahali ambapo huna uhakika na utakaposhika; yaani, unabahatisha. Unaweza kutia mkono mahali unapolenga na kutarajia unachokitaka au unatumbukiza mkono kwa kitu hatari. Mhojiwa MSA 2, tarehe 10/05/2018 alitoa maoni kwamba, kufanya uamuzi wa kufunga ndoa kwa kuona umbo la mtu,

tabasamu, sauti yake na kudhani ndiye anafaa kama mume au mke si sahihi. Baada ya kuoana mambo ambayo hayakutarajiwa yanapatikana kutoka kwake. Hii ndiyo ilikuwa sababu kuu kwa wazazi miongoni mwa Waswahili kuwachagulia watoto wao wenza. Itikadi ndani ya methali hii kuhusu ndoa kati ya mume na mke ni kuvumiliana kwa sababu hakuna jambo timilifu. Kwa hivyo, kila mmoja anakuwa na mapungufu yake. Kulingana na maana hii, ni muhimu kwa wanandoa kuvumiliana ili kuendeleza amani. Maoni haya yanaungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo inasisitiza kushirikiana kwa wanaume na wanawake kuendeleza ndoa kama mojawapo ya majukumu yao ya kijamii kwa kuwa binadamu si mkamilifu na kuna haja ya kuvumiliana.

Pamoja na hayo, methali ya (4) inawasilisha itikadi ya kiuana kwa miktadha tofauti kama ifuatavyo: kwanza, binti akishakuwa mwanamwari hulilia kuolewa, yaani anakuwa na tamaa ya kuolewa. Tamaa ya kuolewa si uchaguzi anaoufanya kwa hiari na uhuru wake, bali ni ukubalifu na ushawishi wa kiitikadi uliopo katika jamii kwamba msichana akifikisha umri wa kuolewa, aolewe kwa haraka. Mawazo haya yanajikita katika Nadharia ya Itikadi kwa mhimili unaosema kwamba ukubalifu unatokana na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala. Utawala unalenga kujitolea na kutumika kwa tabaka tawaliwa Mtoto wa kike anashawishika na kuamini kuwa kuolewa ni jambo zuri analotamani lakini ni itikadi inayoendelezwa wanaume ya kuendelea kuwadhibiti wanawake kwenye ndoa. Kwa hivyo, mwanamwari hata kama hasukumwi moja kwa moja atakuwa anaitikia msukumo wa kijamii wa haja ya kuolewa na kuishi na mume.

Itikadi kama inavyobainisha msichana kutamani kuolewa katika methali (4), ni hali anayoikuta ya kijamii na kuikubali kwa kushawishika nayo kama jamii inavyotarajia. Hata kama hawako tayari, uamuzi umeshafanywa na jamii anamoishi. Kwa hivyo, hana budi kutekeleza yanayotarajiwa kutoka kwake bila msukumo wake binafsi. Kwake mwanamume, itikadi hii inashadidia utekelezaji wa majukumu yake kama wajibu unaomsubiri kama mume katika kumudu familia yake. Msichana anatamani kuolewa ili aweze kuwa na nyumba yake kuliko kuendelea kuishi kwa wazazi wake. Pamoja na hayo, mtoto wa kike akishakua anaanza kutamani kiumbe cha kiume kwa sababu ya miundo ya kijamii. Millet (1970) anatambua kuwa kuna uwezo wa wanaume unatokana na miundo ya kijamii ambayo inawashawishi wanawake kukubali hadhi na uwezo walio nao wanaume. Kulingana na mawazo ya Millet, mtoto wa kike ambaye ametimiza umri wa kuolewa anatamani kupata mume. Mtoto wa kike anaona nyumbani kwao hakumfai tena.  Anatamani kuwa na mwanamume mwenye uwezo na hatimaye aweze kusaidiwa.

Muktadha wa pili, siku ya ndoa, bibi harusi mara nyingi hulia akiwa anaozwa. Machozi yake yanaashiria ama furaha au majonzi akifikiria asasi anayoiingia jinsi atakavyopambana nayo. Bibi arusi amekuwa nyumbani kwao anatunzwa na kupewa kila kitu na wazazi wake sasa majukumu yanatarajia kuwa juu yake. Hata kuwaacha wazazi wake ni jambo linalomhuzunisha. Aidha, kwa upande wa mume kulia kwake baada ya kuoa, kunaashiria majukumu mazito yaliyo mbele yake ya kuhangaikia familia. Kulingana na mhojiwa MSA 4 tarehe 12/05/2018 mume ndiye anatarajiwa kuwajibikia familia yake. Mume anatakiwa kutunza mke wake vizuri kwa kununua chakula, nguo, vipodozi na mahitaji mengine yote

ya mke na watoto. Itikadi hii inayodhihirisha kuwa wanaume wanashughulikia majukumu mengi kiasi cha kuwalemea kuliko wanawake inaendelezwa kwa kupotosha hali halisi. Wanawake kutokana na majukumu ya kijamii wanayoshughulikia ni mengi kiasi cha kutowapatia uhuru. Madai haya yanaendelezwa na tafiti kadhaa zikiwa ni pamoja na Ndungo (1998), Momanyi (1998), Sanauddin (2015) na Dipio (2019) ingawa katika tafiti hizo hawabainishi majukumu hayo vile yanaendelezwa kwa ukubalifu unaotokana na ushawishikaji wa kiitikadi. Mawazo haya yanaegemezwa kwenye mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaodai kwamba uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi na ukweli katika jamii. Itikadi hii inaathiriwa na ung'amuzi potoshi kwa njia ya kiushawishi. Majukumu haya miongoni mwa mengine, yanamfanya mume kuonekana kuzidiwa na kazi nyingi na 'kulia' akishaoa lakini mke anabainika kuwajibikia majukumu zaidi.

Isitoshe, katika jamii ya Waswahili, mtoto wa kiume akioa anakabiliana na majukumu ya kiume anayotarajiwa kuyafanya. Itikadi hii inaendelezwa na mawazo ya Muniu (2013) kwamba wanaume wana majukumu mazito wanayotengewa na jamii. Mhojiwa ZNB 1 tarehe 23/05/2018 alisema kwamba majukumu anayokuwa nayo mume ni pamoja na kutafuta chakula, kutunza mke na watoto pamoja na kuwapatia mahitaji yao yote ya msingi. Kiutamaduni, majukumu kwa mtoto wa kiume akishakua yanamuwajibisha kwenda kutafuta ili akimu maisha ya familia yake. Kulingana na itikadi inavyoelezwa katika methali (5), muda wa matembezi ya mwanamume utakuwa unalenga kuhangaikia na kutafutia familia yake. Kwake mtoto wa kike hata akiwa ameolewa, ana uwezo wa kurudi na kuangalia wazazi wake kwa sababu yeye anatunzwa na mume wake

kwa kuletewa kila anachohitaji nyumbani. Naye mhojiwa wa kiume ZNB 3 tarehe 25/05/2018 alitoa maoni yake kwamba mtoto wa kike anapoolewa, anakuwa na majukumu machache ikilinganishwa na mtoto wa kiume. Mhojiwa alieleza kwamba mtoto wa kike anapata muda wa kuwasaidia wazazi wake kwa sababu akili yake imetulia tofauti na ilivyo kwa mtoto wa kiume. Kwake mtoto wa kiume, akili zake zinatawaliwa na fikira kuhusu mzigo ulio mbele yake wa kutunza na kuwajibikia familia yake ambayo iko karibu naye. Vilevile, itikadi hii inadhihirisha kuwa wanaume wanashughulikia majukumu mengi kuliko wanawake hadi wanasahau kuwatunza wazazi wao. Itikadi hii ina ushawishi ambao unaficha ukweli kuhusu mahusiano kati ya wanaume na wanawake kulingana na mawazo ya Nadharia ya Itikadi.

Methali hii ya (5) inahakikiwa kwa muktadha mwingine. Jamii inaamini kuwa mtoto wa kiume ana uwezo wa kumudu na kuhangaikia familia kwa sababu ya ujasiri, ugumu pamoja na sifa ya kuthubutu kuhusu masuala mbalimbali. Mtoto wa kike kwa upande mwingine, kutokana na sifa zake za kuwa mwororo kimwili na kutokuwa mkakamavu, anahurumiwa na kutetewa daima na wazazi wake kwa kipindi chote cha maisha yake na kuendelea kuwa mwana wao. Maoni haya ni kulingana na maoni ya mhojiwa LMU 3 tarehe 16/05/2018. Mtoto wa kike na mtoto wa kiume wanalelewa na kukua kwa njia tofauti kwa kuwatengea majukumu yao kulingana na uwezo wao kijinsi. Itikadi inayobainishwa na methali hii ni kwamba, mtoto wa kiume anachukuliwa kuwa mpambanaji, yaani aliye na uwezo wa kujikimu kimaisha na kushughulikia maslahi ya familia yake akishaoa. Mtoto wa kike kwa upande mwingine anachukuliwa kuwa dhaifu, laini na ambaye ni wa kutetewa kila mara. Itikadi hii inadhihirisha mahusiano ya

utegemezi wa mwanamke. Utegemezi huu unatokana na unyonge ambao jamii inauendeleza kwa kiumbe wa kike anaobandikwa pamoja na kuchukuliwa kama asiye na uwezo. Hali hii inathibitishwa na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaosema kwamba utamaduni wa tabaka tawala unaendeleza ubaguzi kati yao na watawaliwa au watu wa kawaida; Huwachukulia kama wasio na uwezo na ni watu wa hadhi ya chini.

Ndoa ni asasi nyeti ambayo inahitaji maandalizi mwafaka na kila upande uwe umedhamiria kuingia katika asasi hii bila kushurutishwa na hali fulani. Pamoja na hayo, ili ndoa idumu kunatakikana kusaidiana katika majukumu ya kifamilia ili isionekane ni wajibu wa mtu mmoja kiasi cha kulemewa kama inavyopendekezwa katika methali hiyo hapo juu. Itikadi hii inabainishwa na methali ya (6). Nguo inapokuwa mpya inapendeza na kuvutia. Inapoanza kuchakaa inaendelea kuchanika. Kulingana na muktadha wa utafiti huu, mhojiwa MSA 3 tarehe 11/05/2018 alitoa maoni yake kuhusu methali hii kwamba mke na mume wanapoishi pamoja katika ndoa, kadri muda unavyoendelea, mapenzi yanafifia na kupungua na kunabaki mazoea tu. Kutokana na maoni haya, tunatambua kuwa ndoa ni asasi ambayo inahitaji uvumilivu. Hali hii inasababishwa na majukumu ya kiuana ambayo yanarundikana ndani ya familia kwa mume na mke kama vile kutafuta chakula, kupika chakula, malezi ya watoto na mahitaji mbalimbali. Katika hali hii, kuna mambo mengine ambayo hayapewi kipaumbele na hatimaye kuachana nayo tofauti na ilivyokuwa kwenye ndoa changa.

Methali hii ya (6) inabainisha zaidi itikadi ya uvumilivu kwenye ndoa. Kulingana na itikadi hii, mume na mke wanapaswa kuvumiliana katika ndoa kwa kuweka msisitizo katika mambo ambayo ni ya msingi katika familia kwa njia ya ushirikiano na kuachana na mambo mengine kama yalivyokuwa yanatokea kwenye ndoa changa. Itikadi hii inatokana na ukweli kwamba mapenzi ya ndoa yanachakaa. Wanandoa kwenye suala hili la ndoa wanapaswa kuliendeleza kwenye misingi ya amali za kibinadamu kwa kuzingatia upendo, ushirikiano na kuvumiliana kama inavyoungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba wanaume na wanawake washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana bila kuathiriwa na majukumu ya kimaumbile.

**4.2.1.1 Itikadi za Kiuana kuhusu Suala la ndoa za Mitala**

Ndoa za mitala katika jamii za Kiafrika zinadhihirisha kutamalaki kwa maisha magumu kwa wanandoa na watoto. Ndoa za aina hii zinaishia kuvunjika au wahusika kuishi kwa migogoro. Zaidi ya hayo, watoto wanaathirika kutokana na ndoa za aina hii. Mwakila (2017) anathibitisha mawazo haya. Anamwonesha mhusika, Bi. Mkubwa anayetoroka baada ya kushindwa kuishi maisha ya ndoa za mitala. Katika jamii ya Waswahili kuna methali ambazo zinazungumzia suala hili la kuoa wanawake zaidi ya mmoja au ndoa za mitala. Kuoa wake zaidi ya mmoja katika jamii ya Waswahili ni suala ambalo linaungwa mkono kutokana na mila ambazo ziliingiliana na dini ya Kiislamu ingawa sio suala la lazima. Mawazo haya yanaungwa mkono na Hamad (2018) ambaye anaeleza kwamba dini inaruhusu kuoa mke zaidi ya mmoja lakini hailazimishi. Kuoa mke zaidi ya

mmoja kunawanufaisha wanaume kuliko wanawake. Methali zifuatazo katika Jedwali Na. 14 zinadhihirisha hilo:

**Jedwali 14: Methali kuhusu Ndoa za Mitala**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Ukewenza una karaha. |
| 2. | Aliye na wake wawili kabeba mzegamzega. |
| 3. | Akataye kula humwongezea mke mwenziwe. |

Methali ya (1) inabainisha itikadi ya matatizo yanayotokea katika ndoa za mitala. Familia ya mke zaidi ya mmoja aghalabu haitakuwa na amani. Wakewenza hawakosi mifarakano inayosababishwa na kuoneana wivu pamoja na kushindania mume. Chanzo cha wivu ni wakewenza kutaka kuwa maarufu kwa mume wao. Khatib (2014) anatambua kwamba, ndoa za wakewenza katika jamii ya Waswahili zinazua changamoto na matatizo hasa kwa wanawake. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa mhimili wake wa uendelezaji wa umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa inaunga mkono suala la kuungana kwa wanawake kuliko kuendeleza uadui kati yao. Wanawake wanapaswa kupeana nguvu za kujitolea badala ya kutazamwa kama kundi linaloendeleza utawala wao kwa kupigana wao kwa wao.

Methali ya (2), inadhihirisha namna ndoa za mitala zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kati ya mwanamume na mwanamke. Mzegamzega ni kitu mbacho ni kizito kubeba. Methali hii inamzungumzia mwanamume aliyeoa wake wawili au zaidi kulinganishwa na mtu aliyebeba mzigo mzito ambao unampa taabu. Asilimia kubwa ya Waswahili kiitikadi huwa na mke zaidi ya mmoja (Mmenuka, 2012). Jambo hili linatokana na itikadi ya kiutamaduni iliyo na mizizi yake katika

dini ya Kiislamu inayoruhusu ndoa za mitala. Kwa mujibu wa mhojiwa LMU 1 tarehe 15/05/2018 utamaduni wa Waswahili, unaruhusu mwanamume kuoa mke zaidi ya mmoja. Mhojiwa alieleza kwamba, mwanamume akiamua kuoa mke zaidi ya mmoja lazima awahudumie kisawasawa. Mume anayo majukumu ya kuwatimizia mahitaji yao wake zake; hulazimika kutoa usawa hata katika mapenzi. Majukumu haya yanaonekana kuwa mengi na yanayompa wasiwasi mwanamume. Inadhihirika kwamba ni vigumu kuwatunza na kuwatimizia haja zao wake hao kwa njia ya usawa kama inavyowasilishwa na mwanamume kubeba mzegamzega.

Mhojiwa MSA 4 tarehe 12/05/2018 alisema kwamba mwanamke Mswahili akitamani kitu lazima apewe na mume wake. Mahitaji hayo ya mwanamke, ni wajibu wa mume kuyatimiza kwa wake aliowaoa kwa njia iliyo sawa. Methali hii inaeleza hali ambayo ni ngumu kwa mwanamume kuitekeleza hivyo, kuwa mzigo kwa mume. Nadharia ya Ufeministi inapendelea itikadi za uana za aina hii zinazoonekana kutobadilika zitathiminiwe kila mara kwa muktadha wa kijamii bali si kama suala la kimaumbile. Ni wajibu kwa mwanamume kutimiza haya yote na hana budi kuhimili na kuvumilia changamoto alizohiari kuchagua mwenyewe. Binadamu, ni kiumbe ambaye anakuwa na mapendeleo yake. Hata hivyo, ni jambo gumu kwa mume kuweza kugawanya mahitaji ya wanawake kwa njia iliyo sawa. Itikadi katika methali hii inaonesha kuwa mwanamume kuoa wake wawili au zaidi ni mzigo mkubwa hasa katika kutimiza mahitaji yao.

Methali ya (3) inamzungumzia mke ambaye ananunuliwa mahitaji na mume wake lakini anayakataa. Mke huyo atakuwa amempatia fursa mke mwenzake ya

kuongezewa ilhali yeye akikosa. Mahitaji hayo ni kama nguo, zawadi na ardhi. Kwa kawaida, hali kama hizi hutokea wakati kuna hali ngumu kama vile uhaba wa chakula na ulitima. Haya ni maoni kulingana na mhojiwa MSA 4 yaliyofanyika tarehe 12/05/2018. Mhojiwa aliendelea kudai kwamba mume atakuwa amepitia hali ngumu kutafuta mahitaji kwa ajili ya wake zake. Mwanamke kukataa kile ambacho mume wake amekitafuta kwa jasho, kutamfanya kukosa kabisa. Itikadi inayobainika katika methali hii ni kwamba wakewenza wanaoneana wivu unaosababishwa na kutoaminiana kutokana na huduma zipatikanazo kutoka kwa mume wao. Katika utafiti huu tumebaini kwamba uamuzi wa mwanamume kumpa mgao wa mke wake mmoja kwa mke mwingine unadhihirisha uwezo na mamlaka yake kwa wake zake. Hali hii inamweka katika nafasi ya mbele huku wake zake wakiwa kwenye daraja la chini la kugawiwa na kunyimwa. Pia, inathibitishwa na mhimili wa Nadharia ya Itikadi wa kuwatenga watawaliwa ili kuweza kutawaliwa vizuri. Mwanamume ambaye anawakilisha kundi tawala anatumia itikadi ya kutenganisha wake zake ambao wanawakilisha kundi tawaliwa kwa kuweka hali ya kutoafikiana kati yao ili waweze kutawaliwa vizuri na hatimaye kuweza kuwatumia atakavyo. Kitendo cha mke wake pia kukataa mgao wake kinadhihirisha kutokuwepo kwa amani kati ya wanandoa hao.

#### 4.2.1.2 Itikadi kuhusu Ushirikiano wa Kindoa

**Jedwali 15: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Ushirikiano**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Ndoa huandikwa mbinguni. |
| 2. | Mzaa mume hakufa wala mzaa mke. |

Mwanamke au mwanamume anaweza kuwa amedhamiria na kutamani kuolewa au kumuoa mtu fulani lakini huenda hilo lisitimie kwa sababu ya imani kuwa Mungu alipenda iwe hivyo. Waswahili kutokana na utamaduni wao ulio na misingi katika dini, wanaamini kwamba ndoa inapangwa na Mungu. Mume na mke wanapaswa kuridhika na uchaguzi aliowafanyia Mungu. Methali ya (1) inaeleza itikadi hii. Kulingana na maoni ya mhojiwa ZNB 2 tarehe 24/05/2018, mapungufu yanayojitokeza baada ya kufunga ndoa yakubalike kwa kuwa ni uamuzi unaotoka kwa Mungu. Itikadi inayodhihirika ni kuvumiliana kwa mume na mke kwenye ndoa kutokana na uchaguzi wanaoufanya kwa kukubaliana kuishi pamoja. Itikadi hii inamfunga mwanamke kwenye ndoa bila hiari ya kujinusuru katika ndoa ambayo inaweza kuishia kuwa mbaya. Itikadi hii inaendelezwa kwa mujibu wa mhimili wa Nadharia ya Itikadi ya ushawishi na ukubalifu kwa wanawake kuendelea kunyenyekea ndoa. Katika utafiti huu inaoneshwa kuwa mwanamke ndiye anaathirika na kulazimika kunyenyekaea ndoa. Mwanamke anatarajiwa kuzikubali changamoto zinazoibuka katika ndoa na kuendeleza majukumu anayotengewa kwa vile ni kudra kutoka kwa Mungu. Ukubalifu huu unachukuliwa kama jambo la kawaida ilhali si sahihi kwa sababu unalenga kumdhulumu mwanamke.

Methali hii ya (2), inamaanisha kwamba wazazi wa mume na mke bado wapo na wanaishi kwa ajili ya majukumu yao. Mume wa mke fulani alizaliwa na wazazi wake. Vilevile, mke wa mume fulani alizaliwa na wazazi wake.Wazazi katika jamii ya Waswahili wanakuwa na nafasi muhimu katika ndoa za wana wao kwa kuwashauri daima, hata kama wameoa au wameolewa. Kwa mujibu wa mhojiwa ZNB 4 tarehe 26/05/2018, mume na mke wanapaswa kuishi pamoja, vizuri na

kwa amani bila kusumbuana. Mmoja kati yao akizua sintofahamu, wazazi wa mwingine wanaingilia kati. Wazazi wanaweza hata kumshauri kuachana naye ili waweze kumtafutia mwingine (mume/mke) akaoe au akaolewe. Kwa hivyo, mume na mke wanapaswa kuishi vizuri bila kuzuliana matatizo ambayo yanaweza kusababisha ndoa yao kutodumu kutokana na maelekezo na ushauri utakaotolewa na wazazi. Methali hii inabainisha itikadi ya mchango na nafasi kubwa ya wazazi katika kudumusha au kuvunjika kwa ndoa za watoto wao. Mahusiano ya kiuana yanayoendelezwa na itikadi hii ni mchango wa wazazi katika kuamua na kuzipatia ndoa za watoto wao dira kwa kuchangia mashauri kama ilivyokuwa hata kabla ya kuoana.

### 4.2.2 Itikadi za Kiuana na Suala la Uzazi

**Jedwali 16: Methali za Kiswahili kuhusu itikadi ya Uzazi**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Kuku akiacha wana ana mayai tumboni. |
| 2. | Nyumba ya mgumba haina matanga. |
| 3. | Furaha ya nyumba ni watoto. |

Methali ya (1) katika Jedwali Na. 16 inamaanisha kwamba kuku anayeacha vifaranga wake huwa yuko karibu kuanza kutaga mayai. Methali hii inatudhihirishia kwamba kuku huyo ana majukumu muhimu mawili, kwanza, kutunza vifaranga na pili, kubeba mayai tumboni na kutaga. Kwa kuongozwa na mhimili wa Nadharia ya Udenguzi unaosema kwamba matini huwa na mielekeo mingi ya maana ambayo huibua fasili nyingi; itikadi ya mwanamke kuwa kama chombo cha kuzaa inabainika. Methali hii imehusisha maana yake na mwanamke. Majukumu mfululizo ya kuku yanafananishwa na majukumu muhimu ya mwanamke ya kuzaa na kulea watoto.

Itikadi ya haja ya mwanamume kuzaa na kumiliki watoto inadhihirika katika methali ya (2) na ya (3). Katika methali ya (2), mgumba - mwanamume ambaye hana uwezo wa kuzaa au hana mbegu za uzazi hatapata watoto wa kumzika baada ya kifo chake. Itikadi katika methali ya (3) vilevile inafafanua zaidi kuhusu haja ya kuwa na watoto nyumbani ambapo ukosefu wa watoto nyumbani huleta huzuni. Kwa hivyo, kuna umuhimu wa mwanamume kuzaa watoto watakaomfaa. Mwanamume kuzaa na kumiliki watoto ni jambo la fahari katika jamii ya Waswahili. Kila mwanamume anasifiwa kuwa na watoto hasa wa kiume ili aheshimike na kutambulika katika jamii. Watoto hao wanatarajiwa kuendeleza majukumu ya baba yao ya kifamilia baada ya kuzeeka au hata kufariki Majukumu hayo ni pamoja na kumzika baba yao na hatimaye kumfanyia matanga. Kulingana na mhojiwa LMU 1 tarehe 15/05/2018, katika mila na desturi za Waswahili, matanga huwekwa na watoto nyumbani baada ya kifo cha baba yao.

### 4.2.3 Itikadi za Kiuana na Malezi ya Watoto

Katika jamii za Waswahili, zipo methali za kiuana kuhusu malezi na kutunza watoto. Itikadi hii ya malezi inajitokeza na kudhihirika zaidi kwa kuegemeza malezi ya watoto kwa wanawake huku wanaume wakibainika kutowajibikia malezi ya watoto. Wanaume hawahusishwi na malezi ya watoto kwa kuwa imezoeleka kuwa ni kazi ya wanawake. Wanawake nao wanashawishika na kukubali jukumu hili kama kazi yao. Mifano ya methali zifuatazo inabainisha itikadi hii:

**Jedwali 17: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Malezi**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Kuku mwenye watoto halengwi jiwe. |
| 2. | Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. |
| 3. | Akosaye la mama hata la mbwa yuamwa. |
| 4. | Pepo i chini ya nyayo za mama. |

Katika methali hii ya (1), Jedwali Na. 17 matumizi ya maneno haya ‘kuku mwenye watoto’ inaashiria kuku jike. Kuku jike ndiye daima huwa na vifaranga wake akiwatunza. Methali hii inawasilisha itikadi ya nafasi muhimu ya mama katika malezi na utunzaji wa watoto. Mama mwenye watoto hapaswi kuwekwa katika hali hatarishi, yaani ‘kulengwa jiwe’. Kwa maelezo ya mhojiwa MSA 1 yaliyofanyika Mombasa tarehe 9/05/2018 katika maeneo ya Kiembeni, alisema kwamba, mama ndiye mama wa jamii. Mama huyo akidhurika, watoto ambao ndio kizazi cha kesho na jamii nzima kwa jumla itaathirika. Itikadi ya methali hii inamkinga mama kwa sababu ya majukumu anayofanya la kulea watoto ambao ni dhaifu. Mama akilengwa jiwe, atalemazwa au atakufa na watoto watakuwa wameachwa yatima au wanaweza hata kuumizwa. Kwa vile anayewajibika katika malezi amedhurika, watoto ‘vifaranga’ wataishi kwa taabu kwa kukosa mama wa kuwatunza. Kwa hivyo, mama wa watoto akiathirika, wanaoathirika zaidi ni watoto ambao hawana hatia – kupiga kuku mwenye watoto ni uhasama na unawasababishia watoto kupata shida zaidi. Itikadi ya kukinga, kulinda na kutomweka mwanamke aliye na sifa ya mama katika maisha ya hatari inabainika katika methali hii. Katika Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mwanamume anapaswa kuhusika katika jukumu la malezi na utunzaji wa watoto. Mwanamume anapaswa kwanza kutambua nafasi muhimu ya mwanamke kama mama katika malezi na utunzaji wa watoto na pili, kumkinga mwanamke mwenye watoto.

Itikadi ya kumwajibisha mwanamke kwa malezi ya watoto inaendelezwa zaidi katika methali ya (2). Methali hii inabainisha mwanamke kama chanzo cha maarifa kwa watoto. Mtoto asiyepata malezi na mafunzo mazuri ya mama yake, anaishia kupata matatizo. Katika mazungumzo na mhojiwa LMU 2 kutoka Lamu, tarehe 16/05/2018, alinukuu mafundisho ya dini kwa kumrejelea Nabii Ibrahim. Mhojiwa alitoa maoni kwamba mama ni *madrasat*, yaani shule ambayo ukiiandaa vizuri utaandaa taifa imara. Mhojiwa aliendelea kusema kwamba, akipatikana mama ambaye ameelimika vizuri ataweza kulea watoto vizuri ambao wataweza kuwa nguzo muhimu katika taifa lao. Itikadi hii inayoelezwa na methali (2) inaafikiana na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi kwa mawazo ya Steady (1981) unaobainisha wanawake kama wenye uwezo na maarifa ya malezi ya watoto kwa misingi ya maadili. Ni dhahiri kwamba, jukumu hili la mwanamke kama mama analobeba anapaswa kuheshimiwa na kusaidiana na wanaume. Kutokana na ufafanuzi huo, mama anaachiwa wajibu wa kuwaadabisha watoto kama mwalimu muhimu na wa kwanza katika kukuza watoto kitamaduni. Mwanamume ambaye ni baba anadhihirika kutokuwa na nafasi hiyo ya kuadabisha watoto. Itikadi katika methali hii inamtambua mama katika nafasi hii muhimu ya kuwa mwalimu kwa watoto.

Aidha, methali za Kiswahili zinaonesha itikadi ya mwanamke kuwa na wajibu wa kunyonyesha watoto wake. Methali hii ya (3) inaendeleza itikadi hii na inamaanisha kwamba mtoto anapaswa kuamwa (kunyonya) titi la mama. Mtoto atanyonya titi la mtu mwingine kama ameshindwa kabisa kupata maziwa ya mama yake mzazi. Maziwa ya mama ndiyo yanategemewa kunyonywa na

kumkuza mtoto. Methali hii inadhihirisha itikadi ya malezi ya mtoto kuwa ni jukumu la msingi la mama. Mhojiwa MSA 2 tarehe 11/05/2018 alisema kwamba mtoto amkosaye mama anakosa maziwa yake yaliyo matamu na atakubali kwa mfano kunywa maziwa ya ng'ombe au ya kununuliwa. Itampasa mtoto huyo aridhike na chochote anachokipata ili apate kuishi. Mtoto huyo inabidi akubali apewacho, kwani si kupenda kwake na hana namna nyingine. Inabainika kupitia kwa maoni ya mhojiwa kwamba mwanamke anawajibishwa kwa malezi ya watoto wake. Kulingana na itikadi hii, mama asipowatunza watoto wake, watakua kwa taabu, kama inavyodhihirishwa na matumizi ya maneno 'hata la mbwa yuamwa'. Katika muktadha wa utafiti huu, methali hii inabainisha itikadi ya thamani ya mama kwa malezi ya watoto.

Maana ya methali ya (4) ni kwamba heshima iko kwenye miguu ya mama. Ukitaka kupata heshima hiyo huna budi kuinama. Ukishainama tayari unaonesha heshima. Kwa hivyo, methali hii inabainisha itikadi kuwa radhi za mama ni muhimu. Katika utamaduni wa Waswahili wenye misingi ya dini ya Kiislamu (Abdulaziz, 1979; Derek, 1985), mama ana nafasi kubwa ya kuelekeza watoto kwa njia iliyonyooka kimaadili. Mama ana usemi mkubwa kwa watoto wake hata siku ya akhera. Ili mtoto aweze kuingia peponi anapaswa kumheshimu mama. Itikadi hii inashadidiwa na kauli ya kidini kwamba mama mshikie mara tatu na mara ya nne ndiyo ya baba. Imani hii inatokana na nafasi kubwa anayoshikilia mama kimajukumu. Kwa hivyo, itikadi hii inamfanya mama kuendelea kuthaminiwa kuwa yeye ndiye anayechangia katika uamuzi wa maisha ya mtu (mwanawe) siku ya ahera ama kwenda peponi au jahanamu. Itikadi ya kiuana inaonesha kwamba, katika familia za Waswahili mapenzi na heshima ya

mwanamke hutokana na majukumu maalumu ambayo anatekeleza. Kwa mujibu wa mhojiwa ZNB 4 tarehe 26/05/2018, wazazi wa kiume na wa kike wanatekeleza majukumu yao ya nyumbani kama jamii inavyowatarajia lakini mama ana majukumu mengi zaidi. Katika methali hii, itikadi inamtukuza zaidi mama na kumpa heshima kutokana na wajibu alio nao. Mama ni kinara wa kuwajali, kuwaonyesha upendo, kuwatunza na kuwahurumia watoto. Kwa ujumla, methali zimewasilisha itikadi zinazobainisha mchango mkubwa wa mwanamke. Mwanamke ameoneshwa kuwa na uwezo wa kuamua kizazi cha jamii, na kutawala katika kutekeleza majukumu yake. Pamoja na hayo, amedhihirika kuwa na uwezo wa kuiathiri jamii kwa kuchukua mkondo wa umama, tofauti na itikadi zinazojulikana za mwanamume kuwa anatawala na kuiathiri jamii ya Waswahili kwa kuelekea mkondo wa ubabedume.

### 4.2.4 Itikadi na Urembo

Itikadi za kiuana kuhusu suala la uzuri katika methali za Kiswahili, mwanamke anafaa atunzwe vizuri ili adumishe uzuri na aweze kuvutia. Methali kuhusu itikadi hii zinawasilishwa na kuhakikiwa hapa chini.

**Jedwali 18: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Urembo**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Mke ni nguo mgomba kupalilia |
| 2. | Adhabu ya juu ya mwanamke ni kumfungia katika kasri lisilokuwa na kioo |

Methali ya (1) katika Jedwali la 18 inalinganisha hali ya kupendeza na kuvutia kwa mke na mgomba ambao unapaliliwa ili uweze kustawi vizuri. Mgomba kuweza kustawi vizuri unatakiwa kupaliliwa na kutoa masago. Mwanamke anaweza kuvutia na kumchagiza atende anayotarajiwa inafaa atunzwe vizuri. Mhojiwa LMU 3 tarehe 17/05/2018 alisema kuwa, ili mwanamke aweze kuvutia

na kuonekana mzuri anapaswa kupewa vipodozi na nguo nzuri na kwa mume wake. Mhojiwa alieleza zaidi kwamba ni wajibu wa mume kuzingatia maslahi ya mke wake kama anatarajia mambo mazuri kutoka kwake. Kwa kurejelea maoni ya mhojiwa pamoja na uhakiki wa methali, mwanamke anashawishika kuwa anapaswa kutunzwa na mwanamume ili aweze kuonekana vizuri. Mwanamume asipoweza kufanya hivyo mwanamke hataweza kuonekana maridadi. Itikadi inayodhihirika ni mwanamke kujiremba kwa ajili ya kuvutia wanaume. Hivyo, kushawishika kujiona kama chombo cha anasa kwa mwanamume. Hata hivyo, hii ni itikadi inayomshushia hadhi. Aidha, mwanamke kuonekana vizuri na kuvutia kunategemea mume wake kama mgomba unavyomtegemea mpaliliaji. Itikadi ya utegemezi inadhihirika kwa kuwaelekeza mume na mke kuendeleza hadhi zao kwa misingi ya uana kulingana na majarajio ya jamii kiutamaduni. Hadhi ya mwanamke ya kuabudu uzuri wake wa sura kama zana ya kupendwa zaidi inaimarishwa na ukubalifu wa nafasi hii kwa kujitambua kuwa kwenye nafasi hiyo ya kutunzwa kwa ajili ya kumvutia mwanamume.

Mfano wa (2) ni methali inayobainisha mwanamke kwenye nafasi ya kujiremba. Mwanamke anakubali na kushawishika kujiremba kwa ajili ya kumvutia mwanamume. Wajibu wa mwanamke wa kufanya hivyo unaelezwa pia na Momanyi (2007). Methali hii inamaanisha kwamba mwanamke kutopewa nafasi ya kujiremba ni adhabu kubwa kwake. Mwanamke akiishi katika nyumba ya kifahari bila kioo atajihisi hana raha na hiyo inakuwa adhabu ya hali ya juu. Kasri katika methali hii, linarejelewa kama jumba la kifahari ambamo mna kila kitu kinachohitajika na kumfanya mwanamke atulie na kuwa na raha. Ndani ya kasri hamkosekani vitu kama vile vyakula vya kila aina tena vingi, maji

moto/baridi/safi, wafanyakazi na taa za rangi tofautitofauti. Kutokana na hayo yote, mke angetulia na kupata amani. Mbali na mambo hayo yote mazuri, mali nyingi na kupewa kila kitu, mke haridhiki na kutulia kwa sababu ya ukosefu wa kioo. Itikadi inayobainishwa na methali hii ni haja ya mke kujirembea ili aonekane mzuri. Kwa mujibu wa Nadharia ya Itikadi mwanamke anashawishika kukubali jukumu la kujiremba na kushawishika nalo ili aweze kumvutia mume. Mwanamke kuonekana kama chombo cha anasa kwa mwanamume ni itikadi ambayo haiungwi mkono na mhimili wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambao unapendelea usawa wa binadamu katika masuala ya utamaduni na Uana.

### 4.2.5 Itikadi kuhusu Wakwe

Itikadi kuhusu wakwe inahitaji uangalifu sana. Wakwe wana nafasi kubwa katika kuelekeza itikadi ya kiuana kati ya mume na mke. Itikadi hii inahusisha sifa za utiifu na heshima ya hali ya juu kiasi cha kuonekana kwamba wakati wowote kuna hatari inayoweza kutokea. Mama mkwe yupo kwa ajili ya kuratibu suala la ndoa kati ya mkwe wake au mkaza mwana. Mama mkwe katika jamii ya Waswahili ndiye anayeheshimika zaidi. Aidha heshima fulani inafaa kuwepo kati ya mume na mama mkwe. Mume anapokosana na mama mkwe wake, anakuwa ameamua kukata mahusiano yote.

**Jedwali 19: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi na Wakwe**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Kijicho cha mkwe hakiachishi mume. |
| 2. | Mtu msi mke sahibuye shemeji. |
| 3. | Kupendwa na mke ni kuchukiwa na wazazi. |

Methali ya (1) inamaanisha kwamba ubaya wa mkwe haupaswi kuwa chanzo cha ndoa ya mume au mke kuvunjika. Pengine kunaweza kutokea hali ya mkwe

kufarakana na mke/mume wake lakini haimaanishi kuibuka kwa vurugu kati ya wapendanao. Mhojiwa LMU 2 tarehe 16/05/2018 alitambua kwamba mkwe anaweza kuona labda mume hana mali na utajiri ili kuweza kukimu maisha ya binti yao lakini binti yao hayuko tayari kuachana na mume wake, yaani mapenzi yanatokea kati ya wawili. Jambo la msingi ni mapenzi, maridhiano na ushirikiano kati ya mume na mke. Suala la ndoa na maamuzi linafaa kuachiwa mume na mke. Utaratibu wa kuhusisha wazazi katika kuamua ndoa za watoto wao ndio unaosababisha kuendeleza imani kwamba hata baada ya kuoana wazazi wanakuwa na maamuzi katika ndoa ya wana wao.

Methali ya (1) inabainisha itikadi ya mapenzi kama msingi wa ndoa kati ya mume na mke. Jambo hili linaungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa mhimili unaopendekeza kuendeleza amali za kibinadamu kwa upendo. Kwa hivyo, upendo kati ya mume na mke ni nguzo muhimu katika kuimarisha ndoa kuliko mahusiano ya kindoa kuathiriwa na watu wengine ambao hawapaswi kuwa na uhusiano wa moja kwa moja katika ndoa. Kijicho cha mkwe ni miongoni mwa mambo yasiyo ya kweli na hayana mashiko. Hivi ni visingizio tu ambavyo haviwezi kumfanya mume kuachana na mke wake. Ingawa mkwe ni kwa pande zote mbili lakini sanasana inaangaliwa kwa upande wa mke. Kuna vigezo ambavyo wakwe wanataka kuviona. Hivi ni pamoja na utajiri. Ukosefu wa vigezo hivi unaweza kuchagiza mume kutothaminiwa na hata kuchukiwa. Mapenzi yakiwepo kati ya mume na mke ndilo jambo la muhimu.

Aidha, methali ya (2) inafafanua kuhusu mahusiano na wakwe. Methali hii inamaanisha kwamba, mwanamume ambaye hana mke kwa sababu fulani kama

vile kutengana au kufariki, uhusiano mwema uliokuwa umejengeka kati yake na ndugu za aliyekuwa mke wake haufutiki. Shemeji ndiye anakuwa rafiki yake wa kuzungumza naye na kupata ushauri. Ingawa methali inamzungumzia shemeji lakini kuna nafasi ya kuwarejelea wengine katika familia ya mke wake. Kwa hivyo, uhusiano wa mume na mke haufutiki. Hata mke akiachana na mume wake bado uhusiano na shemeji utaendelea kuwepo. Kwa mfano, kama mume ana mambo fulani ya kushughulikia ataendelea kushauriana na shemeji zake pamoja na kuwa aliachana na ndugu yao. Itikadi hii inaendeleza kuwa uwepo wa shemeji ni ushahidi kuwa mke au mwanamume aliwahi kuolewa/kuoa. Ndoa ni kiungo muhimu katika jamii ya Waswahili. Inaweka daraja kati ya familia zilizohusika katika ndoa wakati fulani. Kutokana na masikilizano na heshima inayotamalaki miongoni mwa ndugu kutoka kwa familia hizo kama inavyostahili kiutamaduni, kunabainika kuwepo kwa amani, udugu na urafiki kati ya familia hizo na hatimaye utulivu wa jamii kwa ujumla.

### 4.2.6 Itikadi ya Udhalilishaji

Kiutamaduni, mwanamke mswahili anapaswa kuwa na sifa fulani maalumu ili akubalike na kuheshimika katika jamii; na jamii inatarajia na kuamini hivyo. Sifa hizo zina mchango mkubwa katika kuendeleza staha na maadili katika jamii kulingana na utamaduni. Mwanamke akifanya kinyume na matarajio ya jamii kuhusu mienendo yake atakuwa ameasi mila na desturi kwa kujiaibisha mwenyewe na jamii nzima. Kwa upande wa Kiswahili, itikadi dhalilishi zinabainishwa katika methali zifuatazo:

**Jedwali 20: Methali kuhusu Itikadi ya Udhalilishaji.**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Mwanamke ni bidhaa mbovu |

Methali hii ya 1 katika Jedwali la 20 inaeleza itikadi kwamba, makosa ya mwanamke ni rahisi kujulikana. Kulingana na sifa na tabia zake katika jamii, mwanamke anafaa kujihadhari kwa makosa ambayo yanaweza kumharibia sifa. Makosa kama vile kuzini kwa mwanamke kunaweza kumsababishia kupata mimba ambayo itakuwa inaonekana kwa kila mmoja. Kupata mimba si dhambi bali dhambi ni kupata mimba kwa mtu asiye halali. Kama mwanamke alipata mimba kwa njia zisizo za halali na haki, anaaibika na kukashifiwa na jamii. Wanawake wana maumbile tofauti na wanaume kwa sababu waliumbwa kuwa na uwezo wa kushika na kubeba mimba pamoja na kujifungua watoto, tofauti na wanaume. Wanawake wakiwa wajawazito kwa mfano, watajulikana kutokana na hali wanazopitia kulingana na maumbile yao. Mhojiwa MSA 1 tarehe 9/05/2018 alieleza kwamba ujauzito huo kama umepatikana kwa njia isiyo halali kulingana na matarajio ya jamii, atatambulika na kulaumiwa kwa makosa hayo kama vile kuavya mimba. Kama kuna hali iliyotokea bila utaratibu unaokubalika kimila, kama vile kupata mimba nje ya ndoa au kuitoa mimba, ni wazi itajulikana. Katika hali hii mwanamke anapaswa kuwa mwangalifu wakati wote asije kufanya mambo yatakayomwaibisha.

Makosa ya mwanamume si rahisi kujulikana kwa sababu ya maumbile yake na mtazamo wa jamii.  Mwanamume kwa mfano, hashiki na kubeba mimba ndipo ionekane kama alama dhahiri. Pia, suala la ubikira kwa mwanamume

halidhihiriki. Kwa msichana ambaye anatarajiwa kuolewa, yaani mwanamwari, inafaa awe bikira mpaka apate mumewe. Pindi anapokosea kutimiza mila hii, atajulikana na atapatikana na hatia. Itikadi hii ya kwamba mapungufu ya mwanamke hayafichiki kutokana na maumbile yake, kwa kuegemea vigezo vya kushika ujauzito na kubeba mimba pamoja na suala la ubikira, inawafanya wanawake na wanaume kuendeleza itikadi kwamba mwanamke ana mapungufu na jamii kwa ujumla inamchukulia hivyo. Nadharia ya Itikadi inabainisha hali hii kwa mhimili unaosema kwamba utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi. Binadamu huchukulia fikira ambazo siyo za kweli na kuzifanya zionekane kuwa za kweli. Udhalilishaji wa wanawake unaendeleza kuwashawishi na kuwafanya wakubali kutambua kwamba jinsia ya kiume ni bora kuliko ya kike. Kwa njia hiyo utawala wa wanaume unaendelezwa kwa kuwafanya wanawake kutawaliwa. Ubovu wa ubidhaishaji wa mwanamke unagubika ubovu wa ubidhaaishaji wa mwanamume na kuhalalisha matendo ya mwanamume. Kiitikadi mwanamke anashawishika kutojiamini na kutokuwa jasiri katika kukabiliana na changamoto anazokumbana nazo kimaisha na jamii, kutochangamkia masuala yanayoleta usawa wa kiuana kwa kuwa na mtazamo wa upande mmoja.

### 4.2.7 Itikadi za Kiuana na Suala la Heshima

Katika jamii ya Waswahili, mwanamume anapaswa kumsikiliza na kumheshimu mke wake. Jedwali la 21 ni methali zinazoonesha heshima:

**Jedwali 21: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Heshima**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Mume si mbabe kwa mkewe. |
| 2. | Mke ni dada mdogo. |
| 3. | Mwanamke hupewa nyama ya ulimi na mwanamume hupewa nyama ya paja. |

Methali hii ya (1) inamaanisha kwamba, mume hapaswi kuwa mkatili na mkali kwa mke wake. Maana katika methali hii inawiana na maana ya methali 'Mke ni dada mdogo'. Itikadi inayobainika katika methali hizi ni kwamba mahusiano ya mume kwa mke wake yanapaswa kuwa ya upendo na kuheshimiana. Kwa mujibu wa mhojiwa, mume hapaswi kuwa mkali na kuonesha udhalimu kwa mke wake. Hii ni kulingana na utamaduni wa Waswahili. Mume hata akiwa shujaa, ana vyeo kadhaa na majukumu ya kifahari, akifika kwa mke wake inambidi kuwa mpole. Mume akiwa mkali kwa familia yake, kutaibuka uhasama na hatimaye kuharibika na hata kuvunjika kwa ndoa. Mwanamume anapaswa kuwa mvumilivu na mpole kwa mke wake. Hali hii itasababisha amani na kudumu kwa familia. Itikadi iliyomo katika methali hii inapingana na imani inayoshikiliwa katika mila za Kiafrika kwamba, mume anafaa kuonyesha mke wake nguvu na ukali ili amtii na kumheshimu.

Mwanamke anapaswa kuambiwa maneno ya kumshawishi, kumbembeleza na asikaripiwe. Kulingana na mhojiwa ZNB 1 tarehe 23/05/2018, mwanamke daima aambiwe maneno mazuri hata kama mengine ni ya uongo ili mwanamume apate mwitiko mzuri. Mwitiko huu mzuri unatarajiwa katika vitendo kama kupika chakula kitamu, kupiga nguo pasi na kusinga. Methali ya (3) inafafanua zaidi itikadi hii. Ulimi ni kiungo laini cha mwili wa binadamu ambacho kinatumiwa

katika kuongea. Kwa hivyo, nyama ya ulimi inaashiria maneno mazuri, yenye upendo kutoka kinywani mwa mwanamume kwa mke wake. Mwanamume hupewa nyama ya paja. Nyama ya paja ni nyama ya mnofu bila mfupa. Itikadi hii inabainisha ushawishi wa mwanamke, kiumbe wa kudanganywa na chombo cha mapenzi.

### 4.3 Hitimisho

Katika sura hii ilidhamiriwa kubainisha itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na za Kiswahili. Methali za jamii hizi zinabainisha itikadi za kiuana ambazo zinadhihirisha wanaume kuwa na majukumu, hadhi na haki tofauti na wanawake. Imebainishwa kwamba majukumu, hadhi na haki za wanaume na wanawake hujikita katika mila za utamaduni wa kijamii ambapo wanaume wanakuwa na hadhi ya juu na mamlaka huku wanawake wakichukuliwa kama raia wa daraja la pili, nafasi ambayo wanaikubali kwa kushawishika nayo. Pia, imebainika kuwa itikadi za kiuana zinaimarishwa na ukubalifu na ushawishikaji kama anavyodai Gramsci (1985) kuhusu utekelezaji wa majukumu, haki za mwanamke na mwanamume na hadhi wanazoshikilia katika jamii. Wanawake wameoneshwa wakijitolea kuwatumikia wanaume kwa hiari. Itikadi za kiuana ambazo zimebainika katika methali zinawasilisha mwanamume kuwa na uwezo na nafasi ya juu zaidi ya mwanamke. Itikadi hizi zimebainika kutokana na uhakiki wa data kwa kuongozwa na Nadharia teule.

# SURA YA TANO

# ITIKADI NA MAHUSIANO YA KIUANA KATIKA METHALI ZA KINYANKOLE NA KISWAHILI

## 5.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia mtafiti amebainisha itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Katika sura hii methali zinachanganuliwa na kuonesha namna itikadi za kiuana zinadhihirisha mahusiano ya kiuana kwa ukubalifu. Baadhi ya methali, kwa mfano, zinabainisha mahusiano ya mke kuwa anapaswa kunyenyekea mume wake vile vile ni mtu wa kukaa nyumbani, kupika na kutunza watoto, hali anayoshawishika nayo na kuikubali. Methali zimechanganuliwa katika muktadha wa utamaduni wa Wanyankole na Waswahili kulingana na amali zao za kijamii. Aidha, methali hizo zimefafanuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia za Itikadi na Ufeministi wa Kiafrika ili kuweza kudhihirisha jinsi mahusiano ya kiuna yanavyoendelezwa na itikadi za kiuana kwa ukubalifu na ushawishi.

## 5.1 Itikadi na Mahusiano ya Ndoa katika methali za Kinyankole

Ndoa ni mojawapo ya asasi za kijamii zinazoshadidia wanaume kuwatawala wanawake (Ogutu na wenzake, 2020). Ogutu na wenzake waanaendelea kusema kwamba, ndoa inatumiwa na wanaume kuwatawala wanawake kwa vishawishi vinavyowafanya wakubali nafasi zao katika jamii. Mwanamke anakuwa kwenye nafasi ya kumtii mume wake ili adumishe ndoa na amani kati yake na mume wake. Maoni haya yanasisitizwa katika utenzi wa Mwanakupona (King’ei, 2000:

99) ambapo Mwanakupona anamhusia binti yake kumheshimu na kumtii mume wake na aepuke kubishana naye:

> Fuata yake idhini,
> Awe radhi kwa yakini,
> Wala sikae ndiani,
> Saa yane kasia.

Naye Angella (2018: 85) anasema kwamba heshima na utiifu wa mwanamke unamfanya aishi na mume wake bila ugomvi:

> mwanamke anafanya uamuzi wake bila kushurutishwa kumheshimu mumewe kumtendea mema.

Kuna amali ambazo mwanamke anastahili kutekeleza na sifa anazostahili kuonesha ili kuweza kudumisha amani na ndoa. Hizi ni pamoja na utiifu, heshima pamoja na kumhudumia mume wake. Itikadi hii inamshawishi mwanamke kukubali nafasi yake ya utiifu kwa mume ndani ya asasi ya ndoa huku mwanamume naye akiabainika kuendeleza itikadi za mfumodume zinazohalalisha mamlaka yake ya ukubalifu na mila za kitamaduni za kunyenyekewa na wanawake (Momanyi, 2001). Katika jamii ya Wanyankole, methali zinazodhihirisha itikadi hizi zipo na zinabainishwa katika Jedwali la 22:

**Jedwali 22: Methali kuhusu Itikadi na Mahusiano ya Ndoa**

| **Na.** | **Methali ya Kinyankole** | **Tafsiri yake kwa Kiswahili** |
|---|---|---|
| 1. | *Otamanya ekimutungire eyeiba agikwatisa omukono gumwe.* | Asiyejua kinachommudu, hushika zubu la mumewe kwa mkono mmoja. |
| 2. | *Oshwerwa ayoroba* | Aolewaye huwa mnyenyekevu. |
| 3. | *Omukazi kyemirire tamanya gabo yeiba.* | Mwanamke mroho hajali mlo wa mume wake. |
| 4. | *Akari ahamahega, karinda nyineeka.* | Chakula kitamu mekoni, kinasubiri mwenye boma. |

Itikadi ya kiuana kuhusu ndoa katika methali ya (1) inabainisha mahusiano ya kiuana kwamba mke anapaswa kuwajibikia ndoa yake ili iweze kudumu. Methali hii inamaanisha kuwa mke asiyemakinikia ndoa yake atapata hasara. Uzembe wa mke kuhusu ndoa yake unaelezwa na ‘kushika zubu la mume wake kwa mkono mmoja’, ishara ya kuzembea majukumu muhimu yaliyomtoa kwao. Neno ‘zubu’ linasimamia kiini cha ndoa. Mawazo haya yanaungwa mkono na Mwamzandi (2016) anayesema kwamba zubu ni mdokezo wa maisha ya ndoa na mahusiano yanayotarajiwa na wanajamii baina ya mke na mume. Mwamzandi anaendelea kusema kwamba, kuwa na zubu kwa mwanamume na vilevile kutokuwa nalo ni njia ya kufafanua mahusiano ya yule mwenye mamlaka, vilevile, asiyekuwa nalo katika jamii. Kulingana na mawazo hayo, mwanamume anashawishika kuwa na mahusiano ya kimamlaka dhidi ya mwanamke kwa sababu yeye ana zubu na mwanamke hana. Itikadi hii inamfanya mwanamume kubainika kutumia taswira ya zubu kumtawala mwanamke. Kwa kutokuwa na zubu, mwanamke anashawishika kukubali kumtambua mume wake kama mwenye mamlaka na anayepaswa kuhudumiwa; na mke wake ndiye anakuwa na jukumu hilo. Maoni haya yanathibitishwa na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaodhihirisha kuwa ukubalifu unapatikana kutokana na ushawishi wa tabaka tawala, ambapo utawala huo unalenga tabaka linalotawaliwa kujitolea kulitumikia tabaka tawala.

Wanaume wanaendeleza utawala na mamlaka yao juu ya wanawake kupitia asasi ya ndoa kwa kuwafanya washawishike na itikadi ambayo wanakubali kuwa asasi ya ndoa ni sehemu muhimu ya maisha yao na wanapaswa kuishughulikia kwa makini. Kwa hivyo, mahusiano yanayobainika ni wajibu wa mke kudumisha ndoa kwa kutimiza mahitaji kama kumheshimu, kumtii, kumfurahisha na

kutomkasirikia mume. Kulingana na mhojiwa SHM 4 tarehe 21/04/2018, maisha ya mwanamke na mwanamume katika jamii ya Wanyankole yanatawaliwa na itikadi na mahusiano yanayokubalika na kutekelezwa katika jamii hiyo, yaani ya mke kumtii na kumheshimu mume.

Pamoja na mwanamke kumakinikia ndoa yake, anatarajiwa kumnyenyekea na kumtii mume wake. Itikadi hii inaelezwa katika methali mbalimbali za Kinyankole. Wingi wa methali hizi ni uthibitisho kuwa mahusiano ya mwanamume na mwanamke katika ndoa ni ya utawala na utawaliwa mtawalia. Methali (2) katika Jedwali la 24 inaeleza kwamba mwanamke ambaye anaolewa na kudumisha ndoa ni yule anayepaswa kumtii mume wake. Itikadi hii inadhihirika katika methali za Kinyankole ambapo mwananamke anaikubali. Itikadi hii inaendeleza mahusiano ya kuwa ndoa ni dhamana ambayo mwanamke hastahili kuichezea. Wafula na Njogu (2007) wanatambua kwamba unyamavu wa mwanamke ni kitengo cha utamaduni ambacho kinamkandamiza katika jamii. Mawazo ya Wafula na Njogu yanakubaliana na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba tabia za uana ambazo zinaonekana kutobadilika zitathminiwe muda wote kwa muktadha wa kijamii, na si kama suala la kimaumbile. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa unyamavu wa mwanamke unaoendelezwa kwa ushawishi na ukubalifu kwenye ndoa unamnyima uhuru wake na kubainika kama raia wa daraja la pili katika jamii.

Momanyi (2002) anaeleza kwamba ndoa, unyamavu na ukosefu wa uhuru wa kufanya maamuzi ni mambo ambayo yanachangia mwanamke wa Kiafrika kubanwa na mila zinazomdunisha chini ya mfumo dume. Mwanamume kwa

upande mwingine anabainika kuwa huru na itikadi za kuumeni. Itikadi ya unyenyekevu wa mwanamke katika asasi ya ndoa inadhihirika kwa kutojibizana na mume wake, kutokaidi maelekezo na maagizo ya mume wake bali aoneshe utiifu na unyenyekevu. Katika mila na desturi za Wanyankole, mwanamke anatarajiwa kutumia njia zozote mwafaka kudhibiti ndoa yake. Asipozingatia sifa za unyenyekevu nautiifu, ataharibu ndoa yake na jamii itamlaumu kwa kuvunjika kwa ndoa hiyo. Kwa kutumia neno ‘oshwerwa’ (aolewaye), ni ishara ya ukubalifu wa kutekeleza mahitaji na sheria za ndoa kulingana na utamaduni wa Wanyankole kama vile kumheshimu na kumtii mume wake. Mwanamke huikubali hali hiyo huku mwanamume akibainika kuwa na uwezo wa kusema. Kulingana na Nadharia ya Itikadi, upande wenye nguvu unakandamiza upande ulio dhaifu kwa kuonesha upande wao kuwa unafaa kusikilizwa. Itikadi hizi zinazoendeleza mahusiano ya kiuana ya upande wa mwanamume kunyamazisha upande wa kike kwa sababu mwanamke anachukuliwa kuwa dhaifu na sauti ya kiume ndiyo inafaa kusikika.

Katika utamaduni wa Wanyankole kama ilivyoelezwa awali, mke anatarajiwa kuwa chini ya mamlaka ya mume wake, kumtii na kupokea maelekezo kutoka kwake (Samwiri, 2007; Kirindi, 2008; Rutaraaka, 2008). Katika methali ya (2), itikadi ya utawala wa mfumo dume inadhihirika bayana kwamba mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke ni ya mtawala na mtawaliwa, mwanamume akiwa mtawala na mwanamke akiwa mtawaliwa. Itikadi hii inaungwa mkono na Nadharia ya Itikadi kwa kurajelea mhimili unaosema kwamba watawala wanaendeleza imani ya utawala kwa ukubalifu kwa kutumia itikadi kuliko nguvu za kulazimisha. Mhimili huu umeweza kubainisha kuwa itikadi katika methali hii

inamshawishi mwanamke kuwa anapaswa kunyenyekea mwanamume huku mwanamume akiwa kwenye nafasi ya mamlaka na akitarajia kunyenyekewa. Mahusiano yanayoendelezwa na itikadi hii ni ya ukubwa wa mwanamume na kuheshimika pamoja na kuwa na cheo cha juu. Kwa upande wake, mwanamke anabainika kuwa chini ya mwanamume kama raia wa daraja la pili. Mwanamke anabainishwa na methali za Kinyankole kama chanzo cha heshima kwa mwanamume.

Kuhusu itikadi ya mwanamke kuwa mtiifu kwa mwanamume inasisitizwa pia na Mavisi (2016:70). Mavis anasema kwamba;

> Tamaduni nyingi humtaka mwanamke awe mnyenyekevu, mnyamavu, mpole na mtiifu wala asiwe na hiari katika maisha yake yote ya kujichagulia au kujiamulia lolote lile.

Unyamavu wa kushawishika na kuukubali ni itikadi inayomnyima haki mwanamke wa Kinyankole. Utamaduni unaendeleza ukubalifu huu wa kutosema na kujibizana na mume wake. Kulingana na Nadharia ya Itikadi hususani mhimili wa ung’amuzi potoshi, mwanamke anapaswa atambue kuwa itikadi hizi zinalenga kuendeleza utawala wa wanaume kwa kupotosha hali halisi katika jamii na hawapaswi kuathiriwa na ung’amuzi potoshi na kuikubali hali ya kudhulumiwa. Mhojiwa KRH 2 tarehe 18/04/2018, alieleza kuwa kwa mujibu wa mafundisho ya kiutamaduni, mwanamke anapobaini kuwa mume wake ana ghadhabu atie maji mdomoni; maji hayo asiyameze wala kuyatema. Kitendo hiki kilimsaidia kutojibizana na mume wake. Hivyo, mke anafanywa kuamini na kukubali kuwa ili aweze kudumisha ndoa yake na kuishi kwa amani, anapaswa

kumheshimu mume wake. Mume akiwa ameudhika, mke awe mwangalifu kwa sababu atapata matatizo, hata kama hajamkosea.

Mwanamke anastahili kutunza na kutoa huduma stahiki kwa mume wake. Mwanamke anatarajiwa kujali na kumwajibikia mume wake kwa kupika mlo aupendao. Hata kabla ya kujifikiria mwenyewe, mke anapaswa kuweka kando chakula cha mume wake kwanza. Jukumu hili ni kati ya majukumu muhimu ya mwanamke katika jamii ya Wanyankole anayotazamiwa kuyashughulikia. Methali ya (3), kinyume na matarajio hayo, inadhihirisha mke ambaye ni mroho, asiyejali kumhudumia mume wake kwa kuandaa na kumtengea chakula. Itikadi katika methali hii inafanya kiumbe cha kike kuwa na wajibu wa kujali masurufu ya kiumbe cha kiume. Itikadi hii inamshawishi mwanamke kukubali jukumu la kushughulikia maslahi ya mume kama analopaswa kulitekeleza na mwanamume anashawishika kukubali kuwa, kuhudumiwa na mwanamke ni haki yake. Itikadi hii inawafanya mwanamke na mwanamume kuamini kwamba nafasi ya mwanamke ni kumpa kipaumbele mume wake hata kabla ya kujifikiria. Mume naye anatarajia kupokea huduma hizo kutoka kwa mke wake. Wote, wanaume na wanawake wanaathiriwa na itikadi hii katika kuendeleza mahusiano yao, mmoja akitarajia kuhudumiwa na mwingine akitarajia kutoa huduma kwa mwingine. Kwa mujibu wa Nadharia ya Itikadi hususani mhimili wa ukubalifu, mwanamume anatawaliwa kiitikadi kwa kutimiziwa anayotarajia kuwa ndiyo maslahi anayopaswa kupata kutoka kwa mke wake. Mwanamke akitekeleza haya, ataishi vizuri kwa amani na mume wake kwa sababu ataepuka makosa ya kumuudhi mume wake, hatimaye kusababisha mfarakano.

Methali ya (4), mwanamke anatarajiwa kushughulikia maslahi ya mume wake. Mke anapotayarisha chakula lakini hastahili kula kabla ya mume wake kufika nyumbani. Mume anaweza kuwa ameenda kujumuika na wenzake kama vile mikutanoni au kunywa pombe; mke hapaswi kupakua chakula hicho kabla ya mume wake kurejea nyumbani. Hata kama kuna watoto ambao wanataka kula inabidi wasubiri baba yao arudi ili chakula kipakuliwe. Katika hali ambapo kitoweo kizuri kimeletwa nyumbani kama vile nyama, baada ya mke kushughulikia mapishi, mume wake ndiye alitakiwa kugawa nyama. Itikadi hii inadhihirisha heshima mume anayostahiki kutoka kwa mke wake. Kwa upande wa mwanamke anabainika kukubali hali na hadhi yake ya kuheshimu mume wake na kuchukulia kuwa ni wajibu wa mke wake kushughulikia maslahi yake. Itikadi hii inajikita katika mfumo dume wa mwanamke kutumikia mwanamume.

Itikadi namna inavyodhihirika katika methali ya (4), inaendeleza kukweza mwanamume, anayepaswa kuhudumiwa na mwanamke. Mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unatuelekeza kuwa jamii inafaa kuendelezwa kwenye misingi ya amali za kibinadamu kwa kuzingatia uwepo wa usawa wa binadamu katika masuala ya utamaduni. Itikadi hii vile inadhihirisha mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke kwa mujibu wa mhimili huu si sahihi kwa kuwa inabainisha mwanamke kuwa mtumishi wa mwanamume. Kuhusu itikadi ya ndoa, imedhihirika kuwa mahusiano ya kiuana kati ya mwanamke na mwanamume katika jamii ya Wanyankole yana misingi yake katika ukubalifu na ushawishikaji wa kiitikadi ulio na mizizi yake katika utamaduni unaotawaliwa na mfumo dume. Ndoa zinazoathiriwa na itikadi za kiuana zinadhihirisha kuwa mume na mke huwa wamekubali kuwepo kwa hali hii katika ndoa kama Ogutu

na wenzake (2020) wananvyoshadidia. Aidha, imebainika kuwa itikadi ya mke kuwa mhudumu wa mume wake inaendelezwa kwa ukubalifu kutekeleza jukumu hili ambapo limeoneshwa kuwa kuna tofauti kuhusu usawa kati ya mwanamume na mwanamke.

### 5.1.1 Itikadi za Kiuana kuhusu Mahusiano ya Ukewenza

Ukewenza ni itikadi inayobainishwa na methali kadhaa za Kinyankole. Methali hizo zinawaonesha wakewenza wakioneana wivu miongoni mwao. Itikadi inayobainishwa katika methali kuhusu ukewenza inadhihirisha ukosefu wa utulivu na amani miongoni mwao, watoto na mume wao (Dipio, 2019). Methali zifuatazo inatufafanulia moja kwa moja athari hizi za ukewenza.

**Jedwali 23: Methali kuhusu Mahusiano ya Ukewenza**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1.<br>2. | *Enkoni etaire mukabaro kwogireeba ogirenzya irembo.*<br>*Mukasho akuha omubazi obu mureire kwo.* | Fimbo itumiwayo kupiga mkemwenza uipatapo unaitupa mbali.<br>Mamako wa kambo hukupatia dawa kama mmelala njaa. |

Mamlaka ya wanaume yanayotokana na utawala wa mfumo dume katika jamii. Wanaume waliweza kuwachapa wake zao viboko walipokuwa wanakosea. Wlikuwa wanahifadhi bakora vizuri kwa ajili ya kuwapiga wake zao walipokosea. Kitendo hiki si cha kibinadamu na kinaingilia haki za binadamu. Methali ya (1) inaonesha mkemwenza ambaye anachukua bakora ya mume wao na kuitupa mbali. Mke huyo kwanza anatambua dhuluma za mume wao kwa mke mwenzake. Aidha, mkemwenza anatambua kuwa adui yao anayewatesa kama wanawake ni mwanamume. Hii ndiyo sababu ana hiari kutupa fimbo

inayotumiwa na mume kuwanyanyasa. Mkemwenza anapopata bakora hiyo inayotumiwa na mume kupiga mke mwenzake anaitupa mbali ili isije ikatumiwa tena kuwapiga. Kitendo hiki cha kutupa bakora ni kitendo cha kupinga dhuluma na unyanyasaji wa mume anaowafanyia. Mhimili wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba wanawake wanapaswa kukuza na kuendeleza umoja wao kama kundi linalodhulumiwa unaafikiana na kitendo cha mke kutupa bakora ya mume wao kuonyesha kutoridhika kwao. Jambo hili ni dalili ya wanawake kupeana nguvu kwa kujitolea badala ya kuchukuliwa kama kundi linaloendeleza utawala wao kwa kuchukiana. Mke huyo anatambua kuwa ni wao ndio waathirika kama wanawake.  Pamoja na hayo, kitendo hiki kinaashiria juhudi za pamoja na kuungana kwa wanawake ili kuweza kujitetea mbali na tofauti kati yao. Mke aliyeolewa pamoja na mwenzake anatambua haja ya kuungana na kusaidia mke mwenzake na kujisaidia mwenyewe. Isitoshe, kitendo hiki kinaonyesha huruma na kujaliana kati ya wake wenza hawa tofauti na vile wanabainishwa kama viumbe ambao hawapatani abadani ndani ya ndoa.

Pamoja na hayo, methali (2) inamrejelea mama wa kambo ambaye anatafutia ‘dawa’ mtoto wa kambo baada ya “kulala njaa”. Itikadi hii inamaanisha kwamba mama wa kambo pamoja na taswira anayochorewa kuwa katili, mwenye chuki (Ssetuba, 2002), anaweza kutafuta suluhisho kwa mtoto wa kambo baada ya kukumbwa na tatizo. Itikadi hii ya mama wa kambo kuokoa mtoto wa kambo, ni udhihirisho kwamba anajali na ana upendo kwa mtoto huyo. Itikadi hii inaungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa mhimili ambao unapendelea kukuza na kuendeleza umoja wao kwa kupeana nguvu za kujitolea badala ya kupigana wao kwa wao.

### 5.1.2 Itikadi na Mahusiano ya Utawa wa Mwanamke

Majukumu na nafasi ya mwanamke kulingana na desturi za kitamaduni katika jamii za Kiafrika yanajikita kwa mazingira ya nyumbani. Opunde na wenzake (2018) wanaeleza kwamba wanawake wanatengewa majukumu ya kulinda boma huku wanaume wakiwa na uhuru wa kutembea pamoja na kutoka nyumbani kwenda kutafuta mahitaji ya familia. Mwanamke alitarajiwa kubaki na kufanya kazi za nyumbani. Kazi za wanawake wa Kinyankole kuitamaduni zilikuwa ni za nyumbani kama vile kupokea wageni, kuwahudumia na kuwapikia waume zao (Kirindi, 2008). Itikadi hii inaelezwa katika methali za Kinyankole zifuatazo:

**Jedwali 24: Methali kuhusu utawa wa mwanamke.**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri yake kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omukazi atarikumanya iba ku ariremu arara omumaarwa.* | Mwanamke asiyejua kwamba mumewe yumo hulala katika baa akinywa pombe. |
| 2. | *Omukazi ozenga ashombera abaana ekihinzi* | Mwanamke mzururaji huambukiza watoto mafua. |

Methali ya (1) inamhusu mwanamke ambaye anakunywa pombe na kusahau kwamba mume wake yuko nyumbani. Mwanamke wa aina hiyo anaishia kulala kilabuni akiendelea kunywa pombe na kusahau kurudi nyumbani. Katika utamaduni wa Wanyankole kwa mujibu wa mhojiwa SHM 1 tarehe 19/04/2018, wanaume na wake zao katika hali nyingine waliandamana pamoja kwenda kunywa pombe nyakati za jioni baada ya kazi. Mwanamke alikuwa anaruhusiwa kunywa pombe na kurudi mapema ili aendeleze majukumu yake ya nyumbani pamoja na kumuandalia mume wake chakula cha jioni. Mahusiano yanayoendelezwa na Itikadi katika methali hii ni kwamba mwanamke anapaswa kutekeleza shughuli zake chini ya sheria zinazowekwa na mwanaume kulingana

na matarajio ya utamaduni. Hii inamaanisha kwamba mwanamke hana uhuru wa kufanya uamizi kuhusu maisha yake. Pia, mwanamke anapaswa kuwa mwangalifu na kupanga muda wake vizuri ili asije akasigana na mume wake.

Fauka ya hayo, methali ya (2) inabainisha itikadi inayoendeleza mahusiano ya haja ya mwanamke kukaa nyumbani ili aweze kuepuka matatizo ambayo yanaweza kuhatarisha usalama na afya ya watoto na familia kwa ujumla. Maana ya nje ya methali hii ni kwamba, mwanamke ambaye hatulii nyumbani analeta na kuambukiza watoto mafua. Mafua katika methali hii yanarejelea matatizo. Kwa hivyo, mwanamke ambaye hakai na kutulia nyumbani anaisababishia familia madhara. Itikadi hii ina ushawishi wa juu wa kutaka mwanamke afungiwe nyumbani kwa sababu majukumu yake kiutamaduni ni ya nyumbani. Kwa madai ya mhojiwa KRH 2 tarehe 18/04/2018, mwanamke alikuwa hastahili kutoka nyumbani bila sababu ya msingi. Alipaswa kutoka kwa lengo maalumu na baada ya kuomba ruhusa na kuidhinishwa na mume wake. Mwanamke alitarajiwa kuwa nyumbani akishughulikia majukumu yake ya upishi, usafi wa nyumba na malezi. Alipolazimika kutoka, alipaswa kuwa na sababu maalumu kama vile kuwatafutia watoto chakula. Hivyo, kutembea kwa mwanamke kunawekewa mipaka. Itikadi hii inachangia pakubwa katika kufafanua na kuwaweka mwanamume na mwanamke katika nafasi zao maalumu kulingana na hadhi zao za kiuana. Kutawishwa kwa mwanamke kunamnyima uhuru na haki zake za msingi. Mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unabainisha kuwa jamii iendelezwe kwenye misingi ya amali za kibinadamu kama njia ya kuimarisha usawa kati ya wanaume na wanawake. Vilevile, mhojiwa KRH 3 tarehe 17/04/2018, alitoa maoni yake kwamba katika jamii ya Wanyankole, mwanamke

na mwanamume wako huru kwenda kutafutia mahitaji ya familia na kumudu familia zao bila vikwazo vya kuathiriwa na hisia za kiuana na kuwatenganisha kwa misingi hiyo. Itikadi inayobainishwa katika methali hii inapingana na mawazo ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika pamoja na maoni ya mhojiwa wa KRH 3 tarehe 17/04/2018. Kupitia mawazo haya ya kinadharia tunabaini kuwa hakuna usawa wa binadamu kati ya wanaume na wanawake. Mwanamke anaelekea kukubali kanuni hizi za kiutamaduni zinazowekwa na jamii kwa azma ya kutekeleza majukumu yake.

### 5.1.3 Itikadi na Mahusiano ya Uzazi katika Methali za Kinyankole

Katika sura iliyotangulia itikadi ya haja ya wanawake kuwazalia waume zao watoto wengi imebainishwa. Itikadi hii wanawake wanashawishika nayo lakini haiakisi uhalisia wa mambo. Suala la uzazi pia limeonyeshwa kuwa linaweka maisha ya wanawake kwenye hatari hadi kusababisha vifo vyao. Watoto hao wengi wanaozaliwa kipaumbele kinapewa watoto wa kiume (Sanauddin, 2015). Itikadi ya uzazi na hasa upendeleo wa kuzaa watoto wa kiume inabainika katika jamii zinazotawaliwa na mfumodume na mtoto wa kike kuchukuliwa kama mali (Dzahene-Quarshie na Omari, 2021; Sanaudini, 2015). Upendeleo wa watoto wa kiume ni itikadi ambayo inakubalika na wanaume pamoja na wanawake. Mtoto wa kiume kupendelewa na wanaume ni imani kuwa ataweza kuendeleza ukoo, kusaidia katika kazi kama za ufugaji wa ng’ombe na kuwatunza wazazi wakiwa wazee Itikadi hii inabainika kutokana na mila za tamaduni nyingi katika jamii za Kiafrika na ulimwengu kwa ujumla (Kiyimba, 2005) kama inavyotokea katika methali zifuatazo:

**Jedwali 25: Methali kuhusu Itikadi na Mahusiano ya Uzazi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omukazi owoyesiga takuzarira mwojo.* | Mke umwaminiye hakuzalii mtoto wa kiume. |
| 2. | *Abaana nibahwa omumukazi tibahwa mu mushaija.* | Watoto huisha tumboni mwa mke siyo kwa mume. |

Methali ya (1) inadhihirisha itikadi inayowasilisha mahusiano ya haja ya wanawake kuwazalia waume zao watoto wa kiume. Methali hii inazungumzia mke anayepatwa kupendwa na kuaminiwa na mume lakini anasaliti kwa kutomzalia mtoto mvulana. Mwanamume anaoa mke kwa mujibu wa methali hii akitarajia kupata watoto wa kiume. Kauli 'Takuzalira mwojo'/'hakuzalii mvulana' inathibitisha hoja hii kwamba mwanamke anapaswa kuzaa watoto wa kiume kwa ajili ya kumridhisha mume wake. Itikadi hii ya kiutamaduni inawashawishi wanawake kukubali kuwa kuwazalia wanaume watoto wa kiume ni wajibu usioepukika. Miongoni mwa Wanyankole, mwanamke kutozaa mtoto wa kiume ni itikadi inayomwelekeza mwanamume kuoa mke mwingine au na hata kumtaliki mke alieshindwa kuzaa mtoto wa kiume. Kirindi (2008) anathibitisha itikadi hii kwamba katika hali nyingine mtoto wa kiume wa ndugu yake mume (kaka yake), alitunzwa ili amsaidie katika ufugaji wa ng'ombe. Mtoto huyu aliweza kurithi mali ya baba yake mdogo hata kama alikuwa na watoto lakini wa kike.

Upendeleo wa kuzaa mtoto wa kiume unadhihirishwa katika mila ya Kinyankole ambapo mtoto wa kiume alipoanza kumea meno, alikalishwa juu kwenye mgongo wa ngo'mbe jike mmoja hadi mwingine. Mila hii iliashiria kwamba hiyo

ni mali na urithi wake. Mtoto wa kiume aliambiwa kuwa baraka zake ziko nyumbani kwa baba yake. Kwa mtoto wa kike alipomea meno, alikalishwa chini mbele ya nyumba akitazama mbele. Kitendo hiki kiliashiria kwamba maisha ya baadaye ya mtoto huyo yako mbele anakoangalia. Msichana alipewa kibuyu na kuambiwa kwamba bahati yake na mali yake vipo kwa atakayekuwa mume wake. Mhimili wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kulingana na Njogu na Chimerah (1999) wanatambua kwamba wanadamu wote wanapaswa kuwa sawa kwa upande wa utamaduni na kimenke pamoja na kupigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu bila kujali maumbile. Kwa hivyo, kupitia kwa mhimili huu wa nadharia ya Ufeministi mahusiano vile yanaendelezwa na itikadi hii yanapingana na matarajio ya nadaria kwa kuendeleza ubaguzi wa kiuana. Watoto wamedhihirika kuwa wanatenda na kuchangia maendeleo ya jamii bila kuzingatia kuwa mmoja ni mtoto wa kiume au ni wa kike.

Watoto wa kike wamekuwa wakimudu kufanya kazi zinazochukuliwa kuwa ni za kiume kulingana na misingi ya utamaduni wa Wanyankole, kama vile kupeleka ng’ombe malishoni na kukama ng’ombe, miongoni mwa kazi zingine. Utekelezaji wa majukumu na michango yao haiakisi itikadi za kiutamaduni kuhusu thamani ya kuzaa watoto wa jinsi fulani. Mahusiano haya yanaafikiana na matarajio ya mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba tabia za kiuana ambazo zinaonekana kutobadilika zitathminiwe kila mara kwa muktadha wa kijamii, na si kama suala la kimaumbile. Aidha, ushawishikaji wa mwanamke kuwajibishwa kuzaa watoto wa kiume haumtendei haki kwa sababu maendeleo ya jamii hayategemei kuwepo kwa jinsi moja bali yanatokana na mchango na thamani ya kila mtoto, tofauti na matarajio ya itikadi hii ya

kiutamaduni. Utafiti unaonesha kwamba, mtoto wa kiume na wa kike, kila mmoja ana mchango wake bila kuzingatia maumbile yao. Itikadi za kiutamaduni kuhusu suala la uana bado zinaathiri ukuaji, utendaji kazi wa watoto kwa kupatia kipaumbele na kuwathamini watoto wa kiume. Imebainika kuwa, itikadi ya kuzaa na upatikanaji wa watoto wa kiume inachangia pakubwa katika kufanya maamuzi yanayohusu mahusiano baina ya mwanamke na mwanamume, suala ambalo linaendelezwa kwa ukubalifu. Methali hizi zina athari ya kushawishika kwa wanawake kukubali kuwa kuzaa watoto wa kiume ni suala muhimu zaidi. Mulokozi (2017) anaunga mkono wazo hili kwa kutambua kuwa methali kama chombo cha itikadi, zinawasilisha Imani za jamii kwa ushawishi mkubwa na kupatia kipaumbele suala la kuzaa watoto.  Methali hii inaendeleza imani ya kunasibisha kuoa mke kwa ajili ya kuzaa na kupendelea watoto wa kiume.

Pamoja na wanaume kutarajia wanawake kuzaa watoto wa kiume, wanaume wanadhihirika kuwa na uwezo mkubwa wa kuendelea kuzaa watoto hata kwenye umri wa uzee kuliko wanawake. Katika jamii ya Wanyankole watoto wengi walihitajika kwa ajili ya kupigana vitani, kuzalisha mali kwa kufanya kazi kama vile kulima ili familia ipate chakula cha kutosha. Familia ilijulikana kwa sababu ya kuzaa na kuwa na watoto. Kuwa na watoto wengi kulichukuliwa kama utajiri mkubwa. Kwa hivyo, itikadi ya methali hii inaendeleza mahusiano ya wanaume kushawishika kuoa wake wengi kwa ajili ya kupata idadi kubwa ya watoto. Methali ya (2) inadhihirisha namna mwanamume anavyochukua nafasi ya mbele katika uwezo wa kuzaa watoto kuliko mwanamke. Methali hii inamaanisha kwamba, mwanamke anafikia muda fulani na anakatika hedhi. Mwanamke anapokatika hedhi hawezi kuendelea kuzaa. Kwa upande wa mwanamume

anabainika kuwa na uwezo wa kuendelea kuzaa hata katika umri wa uzee. Uwezo huu wa mwanamume wa kuendelea kuzaa, unampa fursa ya kuoa na kuzaa kadri ya uwezo wake. Itikadi hii inampa mwanamume fursa na uwezo wa kuoa mke mwingine ili aweze kuendelea kuzaa kwa kupanua familia. Kupitia methali hii tunabaini hali halisi ambayo mwanamke anakumbana nayo kama mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inavyodai kuwa fasihi ni jukwaa la kuelezea hali halisi ya mwanamke anayokumbana nayo ili iweze kueleweka bayana. Hivyo, ni dhahiri kwamba mwanamke yupo kama chombo cha kuzaa watoto kwa mwanamume.

Kuhusu itikadi ya uzazi, tumebaini kuwa mwanamume anaendeleza kutawaliwa kwa mwanamke na kumfanya kushawishika na haja ya kuzaa watoto wa kiume kwa madai kwamba wana mchango mkubwa. Imedhihirika pia kuwa mwanamke hahusiki katika kufanya maamuzi ya kupanga uzazi ilhali mwanamume ana uhuru wa kuzaa watoto zaidi, hali inayompatia nafasi ya kuoa kadri anavyotaka. Itikadi hii inamfanya mwanamke kudhihirika kutokuwa na haki juu ya suala la uzazi. Mahusiano yanayoendelezwa na itikadi hii hayafai kwa sababu yana upendeleo kwa wanaume.

### 5.1.4 Itikadi na Mahusiano ya Malezi

Wanaume kama kundi lenye mamlaka wanawatengea wanawake jukumu la malezi ya watoto kwa kutumia njia ya ushawishi wa kiitikadi. Itikadi ya kiuana kuhusu mahusiano ya malezi ya watoto inawafanya wanawake kushawishika kuwa jukumu la malezi ni wajibu wao kwa sababu ya jinsia yao. Mwanamke ametengewa majukumu ya malezi, na kutoa maelekezo na mafunzo kwa watoto.

Itikadi hii inasisitizwa na Ogutu na wenzake (2020) wanaodai kwamba watu wenye mamlaka na uwezo wanatumia madaraka yao kuwatawala wengine kwa kutumia ushawishi. Wanaendelea kusema kwamba malezi kama mojawapo ya asasi za kijamii, yanaendeleza utawala wa wenye uwezo juu ya wasio na uwezo. Pamoja na wanaume kutarajia wanawake kuzaa watoto wengi, kupendelea kuzaa watoto wa kiume kama iilivyobainika hapo juu, ni itikadi inayoonesha kuwa malezi ya watoto kwa ukubalifu ni jukumu la wanawake; methali hizo inawasilishwa katika Jedwali la 26:

**Jedwali 26: Methali kuhusu Itikadi na Mahusiano ya Malezi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omuzaire arangwa engozi* | Mzazi hutambuka kwa mbeleko. |
| 2. | *Akaana keiba kajumisa nyinako* | Mtoto mwizi husababisha kutukanwa kwa mama yake. |
| 3. | *Omwana mubi ajumisa nyina* | Mtoto mbaya husababisha kutukanwa kwa mama yake. |

Mwanamume anapendelea kuoa mke mwenye uwezo wa kuzaa na kulea watoto. Itikadi hii ya kiutamaduni inawafanya wanawake na wanaume kuendeleza mahusiano hayo kwa ukubalifu kuwa mwanamke anastahili kuwajibikia jukumu la malezi ya watoto. Maoni kulingana na mhojiwa KRH 4 tarehe 18/04/2018, yanabainisha kuwa mzazi anayetambulishwa kwa mbeleko ni mwanamke kwa sababu ndiye anazaa na kutarajia kulea wana. Maoni haya yanaungwa mkono na Craig (2006) ambaye anasema kwamba jukumu la malezi ya watoto ni la akinamama hata hivyo haonyeshi kuwa jukumu hilo linashughulikiwa na wanawake kwa kushawishika na kulikubali. Katika jamii ya Wanyankole,

mwanamke anakubali kuwajibikia kulea watoto kama jukumu lake muhimu. Opunde na wenzake (2018: 321) wanaeleza kwamba:

> ndoa hujengwa na mwanamke katika jamii ya Kiafrika. Mama anatarajiwa kuwa mlezi mkuu katika jamii.

Methali ya (1) katika Jedwali la 23 inaeleza kuhusu mzazi kutambulika kwa mbeleko. Mbeleko ni nguo au kitambaa ambacho kinatumiwa kumfungia mtoto mgongoni. Nguo hii kwa kawaida inatambulishwa na sifa kama kununuka mkojo wa mtoto, ukuukuu kwa sababu ya kuifua kila mara, na wakati mwingine ni chafu. Mbeleko kiutamaduni inahusishwa na mzazi wa kike ambaye anaitumia kubeba mtoto mgongoni kama sehemu ya malezi. Mhojiwa KRH 1 tarehe 17/04/2018 alieleza kwamba kimila, mwanamke akionekana kila mara yuko maridadi, anashukiwa kutokuwa na watoto nyumbani wa kuwahudumia. Yeye mwanamume kulingana na utamaduni anatarajiwa kisimamia malezi na utunzaji wa Watoto hao. Hivyo, kwa misingi ya itikadi hii, mwanamke hutengewa jukumu la malezi, ilhali mwanamume akihusishwa na majukumu yaliyo tofauti na malezi ya watoto.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inapingana na mahusiano haya yanyoaendelezwa na itikadi hii kwa ushawishi na ukubalifu wa jukumu la malezi ya watoto kuwa juu ya wanawake. Wanawake na wanaume washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana bila kuathiriwa na majukumu ya kimaumbile kama mhimili huu unavyotarajia. Itikadi hii ya kiuana ya malezi ya watoto kama jukumu maalumu la mwanamke, inaendeleza mahusiano ya

kutenganisha malezi kwa mwanamke. Mawazo haya yanaungwa mkono na Samuel (2018: 43) ambaye anasema kwamba:

> Mtoto hulelewa na wazazi wote wawili. Inapotokea udhaifu kwa mtoto, sharti wazazi wote wawili wakubali ni tatizo lao wote, na wawajibike kama wazazi kupata suluhu.

Mhimili wa Nadharia ya Itikadi unashadidia kwamba itikadi zinazalishwa kwa sababu ya vigezo vinavyounda jamii. Ukubalifu wa kutenga jukumu la malezi ya watoto kwa wanawake ni matokeo ya itikadi za kiutamaduni.

Methali ya (2) na ya (3) zinaendelea kumwajibisha mwanamke kwa malezi ya watoto. Mama anapaswa kulea watoto kwenye misingi ya maadili mema. Methali hizi mbili zinaonesha kuwa mtoto mwenye utovu wa nidhamu anamfanya mama yake kulaumiwa na jamii. Usimamizi wa tabia na mienendo ya watoto katika utamaduni wa Wanyankole ni wajibu wa mama. Kulingana na mhojiwa SHM 2 tarehe 20/04/2018, jukumu hili lina chanzo chake katika amali za kiutamaduni ambapo mke alistahili kubaki nyumbani kwa ajili ya malezi ya watoto na kutekeleza majukumu mengine ya nyumbani huku mume akitarajiwa kushughulikia majukumu mengine ya nje kama kuwinda na kulisha wanyama. Kwa hivyo, mama kuwa karibu na mtoto wake kwa muda mrefu kulimwajibisha na kumfanya akubali jukumu la malezi kama lake. Kirindi (2008) anathibitisha kwa kueleza kwamba mtoto akiwa na tabia mbaya katika jamii, mama analaumiwa kwa kutotekeleza majukumu yake ipasavyo kiasi hata cha kupewa talaka.

Itikadi hii ya malezi kama inavyoelezwa katika methali hizi mbili, yaani methali ya (2) na ya (3), inaafikiana na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaodai kwamba

itikadi zinazalishwa kwa sababu ya vigezo vinavyounda jamii. Inadhihirika wazi katika methali hizi kwamba itikadi ya utenganishaji wa majukumu ya malezi kwa mwanamke haitokei kwa kulazimishwa bali ni kwa ukubalifu na ushawishi wenye misingi yake katika utamaduni unaodumishwa kwa msingi wa mfumodume. Itikadi hii inabainisha mahusiano ya mwanamke (mama) kutengewa majukumu ya malezi ya watoto nyumbani na mwanamume (baba) kuendeleza majukumu mengine tofauti na malezi. Mahusiano haya yanayoendelezwa na itikadi hii hayaafikiani na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi unaosema kwamba, jamii iendelezwe kwenye misingi ya amali za kibinadamu. Amali zinazorejelewa ni kama upendo na ushirikiano. Kwa hivyo, kuna haja ya wanaume na wanawake kushirikiana kulea watoto kuliko kuwasusia wanawake wajibu huo.

Kuhusu itikadi ya malezi na utunzaji wa watoto, imebainika kwamba mahusiano yanayodhihirika kati ya wanaume na wanawake, wajibu wa wanawake kukubali kutekeleza majukumu ya malezi na kutunza watoto, kuwalea kwa maadili mema kulingana na misingi inayokubalika ya jamii ya Kinyankole, hayatoi haki sawa. Wanawake wanabebeshwa mzigo mkubwa wa malezi hata kama wanayatekeleza kwa ukubalifu huku wanaume wakibwaga majukumu hayo kwawanawake.

### 5.1.5 Itikadi za Kiuana kuhusu Mahusiano ya Uongozi

Mwanamume katika jamii zinazotawaliwa na mfumodume anaonekana kuwa kiongozi mwenye msimamo na mwanamke anawekwa katika nafasi ya kutawaliwa na kupokea maagizo (Mwamzandi, 2016). Mwamzandi anabainisha kwamba, mwanamume ana umaarufu na anapewa mamlaka katika jamii.

Mwanamume anapaswa kuwa kiongozi wa familia, hakimu, mwenye msimamo na anayetarajiwa kuheshimiwa kwa sababu ya uwezo mkubwa alio nao. Mawazo haya yanaungwa mkonona Malenya na wenzake (2020: 57):

> Mwanamume anadai kwamba amepewa uwezo mkubwa
> na Mungu wa kumtawala mwanamke.

Methali zimedhihirisha kuwapo kwa majukumu ambayo yanampa mwanaume nafasi ya kusimamia shughuli za familia tofauti na mwanamke. Jamii huyachukulia majukumu hayo kuwa ni ya mwanamume (Mosha, 2016). Mwanamume na mwanamke kwa pamoja wanayakubali majukumu hayo kuwa ni ya wanaume. Itikadi inayobainisha mahusiano ya mwanamume katika nafasi hii ya uongozi na mamlaka inaendelezwa na desturi ya kiutamaduni ambapo mwanamume ana uwezo na mamlaka zaidi ya mwanamke. Itikadi hii ipo na inathibitishwa katika methali za Kinyankole zifuatazo kuhusu majukumu, haki na hadhi katika jamii hiyo:

**Jedwali 27: Methali kuhusu Mahusiano ya Uongozi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri yake kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omushaija ahatari omukazi acwa orubanza.* | Pasipo na mwanamume, mwanamke huamua kesi. |
| 2. | *Omukazi tatiiza ngundu ya iba.* | Mwanamke hapeani fahali wa mumewe. |
| 3. | *Omushaija tahinduka aharurimi, ahinduka ahakitanda.* | Mwanamume hageuki kwa ulimi wake hugeuka kitandani. |

Methali ya (1) katika Jedwali Na. 22 inamaanisha kwamba, mwanamke anapata fursa ya kuamua kesi kama mwanamume hayupo. Methali hii inawasilisha itikadi inayoibua mgongano wa majukumu ya kiuana kitamaduni. Katika jamii ya Wanyankole mwanamume ndiye anapaswa kuwa jaji wa kutatua migogoro au kuamua kesi. Mawazo haya yanaungwa mkono na Maitaria pamoja na Momanyi (2016). Hapa mwanamke anapata nafasi ya kuamua kesi ikiwa tu mwanamume

hayupo. Kwa hivyo, mwanamke, hatarajiwi kutekeleza jukumu hili kama mwanamume yupo. Kwa mujibu wa mhojiwa SHM 4 tarehe 21/04/2018, si lazima mwanamume awe hayupo kabisa ndipo mwanamke aamue kesi. Kulingana na maoni hayo, mwanamume anaweza kuwepo lakini akawa hana uwezo, yaani ‘gumegume’ (omushaja aremirwe). Itikadi hii inaathiri utekelezaji wa majukumu ya kiuana kwa kuwafanya wanawake kukubali kuwa uwezo wa kuamua kesi katika jamii ni wa wanaume.

Pia, itikadi inayodhihirika katika methali ya (1) inaonyesha kwamba mwanamke ananyimwa haki ya kuaminiwa na mamlaka ya kuamua kesi kwa kujitegemea. Mwanamume anatengewa jukumu la kuwa jaji kama jukumu lake maalumu tofauti na mwanamke. Mahusiano ya kiuana kama yanavyoendelezwa na itikadi hii yanafafanuliwa zaidi na mawazo ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Mhimili unaosema kwamba wanawake wazinduke na kubadili mielekeo ya jinsi wanavyojiona katika uhusiano na wanaume, unatubainishia haja ya wanawake kujiamini katika kutekeleza majukumu ambayo kiutamaduni yanachukuliwa kuwa ya kiume. Wanawake wana uwezo sawa na wanaume kwenye nafasi hii ya kuwa waamuzi. Itikadi hii haifai kwa sababu inaendeleza ung’amuzi potoshi. Wanawake wana uwezo wa kushiriki katika kutatua migogoro ya kijamii hata inayowahusu wanaume. Kulingana na mhimili wa Nadharia ya Itikadi kwa mujibu wa Gramsci (1971), wenye nguvu na mamlaka wanaendeleza itikadi ya kutojiamini na kutojiweza kwa watawaliwa ili wenye mamlaka waendelee kuonekana kuwa ndio wenye uwezo na maamuzi sahihi. Kwa hivyo, kulingana na mhimili huu wa Nadharia ya Itikadi, wanaume wanaendeleza itikadi ya kuwachukulia wanawake kuwa ni viumbe wenye uwezo mdogo mbele yao.

Wanawake wanaweza tu kujaribu kutenda iwapo wanaume hawapo au wameshindwa.

Mamlaka ya mwanamume dhidi ya mwanamke ni mahusiano ya kiuana yanayoendelea kubainishwa na itikadi katika methali ya (2). Mwanamke hana fursa ya kutekeleza maamuzi. Mavisi (2016) anasema kwamba mwanamke ni kiumbe asiye na uwezo wa kujiamulia. Mahusiano ya kiuana yanaathiriwa na itikadi hii ya mfumodume ambapo mwanamke anachukuliwa kuwa hana mamlaka ya kupeana kitu kutoka nyumbani. Kuna vitu vingine nyumbani kama ng'ombe ambavyo mwanamke hana mamlaka kupeana kama inavyodhihirika katika methali hii ya (2). Kulingana na maelezo katika methali hii, mwanamke hana ruhusa na mamlaka ya kumpa jirani fahali wa mume wake. Wanyankole kiutamaduni huwa wanapeana fahali kwa ajili ya kuzalisha kutokana na utamaduni wao wa ufugaji wa ng'ombe. Mwanamke yuko huru kupeana vitu vidogovidogo ambavyo ana mamlaka juu yake, kama mtandio. Itikadi inayowasilishwa katika methali hii inabainisha mahusiano kwamba wanawake wana mipaka ya mamlaka yao kiuana kuhusu utekelezaji wa maamuzi, itikadi ambayo hata wao wanaikubali kutokana na kushawishika na itikadi.

Pia, wanawake hawawezi kutekeleza maamuzi wenyewe bila kuidhinishwa na wanaume. Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika inawataka wanawake kubadili mielekeo ambayo inawanyima nafasi za kuwa na mamlaka ya kutekeleza maamuzi fulani. Mielekeo kama hii inaendelea kuwaweka kwenye ngazi ya kutawaliwa na wanaume. Kulingana na mazungumzo na mhojiwa KRH 1 tarehe 17/04/2018 katika Wilaya ya Kiruhura, mume kama hayuko nyumbani, mke

wake hapaswi kumwazimisha huyo fahali. Kama atamwazimisha fahali huyo kwa jirani atakuwa amepewa ruhusa na mume wake. Naye mhojiwa SHM 2 tarehe 20/04/2018 alibainisha kuwa jamii ya Wanyankole inaendelezwa kwa misingi ya uana. Mifano iliyotolewa ilikuwa inashadidia uendelezaji wa majukumu na nyadhifa kwa misingi ya uana. Mhojiwa aliendelea kusema kuwa ng'ombe ni mali ya mume katika jamii ya Wanyankole. Mwanamume ana mamlaka ya kuazimisha atakavyo. Iwapo mwanamke itambidi kuazima kitu, yuko huru kuazima mtandio kwa sababu ndio anaomiliki na kuwa na mamlaka juu yake. Miliki ya mke na mume ambayo kila mmoja ana mamlaka juu yake pamoja na thamani yake inabainishwa. Miliki ya mke ikiwa ni mtandio na miliki ya mume ikiwa ni ng'ombe. Uwezeshwaji kiuchumi kati ya mke na mume ni tofauti, jambo ambalo linazua tofauti za kiuana katika suala la kumiliki mali. Mawazo haya yanaungwa mkono na March na Mukhopadhyay (1999). March na Mukhopadhyay wanadhihirisha kuwa mwanamke hana fursa ya kuwa na mamlaka juu ya rasilimali. Mamlaka ya mwanamke yanatambulika kwa vitu vidogovidogo anavyomiliki na thamani yake ni ya chini ikilinganishwa na thamani ya ng'ombe ambao wanamilikiwa na mwanamume. Hali hii inaendeleza tofauti kati ya mwanamume na mwanamke kiuchumi.

Methali ya (3), 'mwanamume hageuki kwa ulimi wake' inamaanisha kwamba akitoa kauli yake haibadiliki. Mahali pekee anapobadilika ni kitandani akiwa na mke wake kwa tendo la ndoa. Itikadi inabainisha mwanamume kuwa na msimamo na kutobadilikabadilika mbele ya mwanamke. Mwanamume anapaswa kuwa na msimamo kwa mambo yanayojenga familia yake. Kwa mujibu wa mhojiwa KRH 1 tarehe 17/04/2018, sifa za kutokuwa na msimamo thabiti

zinahusishwa na mwanamke. Mke anaposema jambo fulani, na kama mume ana kauli na mtazamo tofauti, la mume hafai shurti litekelezwe. Jamii ya Wanyankole inamtarajia mume kutobadilika katika tabia, mienendo na maamuzi anayofanya. Methali hii inampa mwanamume haki ya kujieleza na kutoa maoni na kutompa mke nafasi ya kujieleza au kutoa maoni yake. Ingawa mume anakuwa na msimamo kwa kauli yake haimaanishi kwamba analosisitiza ni sahihi na mke hana mawazo yanayoweza kuwa bora na sahihi hata kuliko ya mume. Itikadi hii inamfanya mwanamke kuihusisha na jinsi yake na kuikubali, jambo ambalo si sahihi.

Kitendo cha kugeuka kitandani kwa upande mwingine kinadhihirisha kuwa mume hubadilika kwa matendo fulani maalumu tu kama vile akiwa kitandani na mke wake. Kuna kauli zinazotolewa na mkuu wa familia 'nyineeka' ambazo hazipaswi kubadilika. Mhojiwa SHM 2 tarehe 20/04/2018 kwenye maelezo yake alitoa mfano kwa kumrejelea mtoto wa kike kwamba malezi yake ni mojawapo wa masuala ambayo yanaangaliwa kwa umakini. Kiutamaduni, kuna mila na desturi za Wanyankole ambazo hazistahili kubadilika kulingana na maoni ya mhojiwa KRH 4 tarehe 18/04/2018. Mke hastahili kushawishi mume wake kutekeleza jambo fulani na akakubali bila kuchunguza zaidi. Itikadi hii inaendeleza mahusiano ya mwanamume kutobadilikabadilika kimsimamo tofauti na mwanamke. Itikadi hii inaendeleza kutawaliwa kwa wanawake kwa kuwafanya wakubali mahusiano hayo kwa kushawishika kuwa wanapaswa kuwa katika nafasi hiyo ya kufuata maamuzi ya wanaume. Katika utafiti huu, kwa kuongozwa na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imedhihirika kuwa itikadi hii inanyima wanawake uhuru wa kuwasilisha mawazo yao.

Wanaishia kufuata maagizo ya wanaume, hali inayowashushia hadhi. Methali hii inampa mwanamume haki na uhuru wa kutoa maoni na kunyima mwanamke nafasi ya kutoa maoni yake. Ingawa mume anakuwa na msimamo kwa kauli yake, haimaanishi kwamba jambo analoshikilia ni sahihi na kwamba mwanamke hana mawazo yanayoweza kuwa bora na sahihi hata kuliko ya mwanamume.

### 5.1.6 Itikadi za Kiuana kuhusu Kazi

Kazi hutekelezwa katika jamii kulingana na jinsi ya mtu. Mawazo haya yanaungwa mkono na Owu-Ewie (2019). Katika jamii ya Wanyankole, wanawake walikuwa wanalima mashambani mwao, kupanda, kupalilia na kuvuna, kuchanja kuni msituni na kuchota maji. Wanaume walikuwa wanashughulikia kazi za ufugaji na ujenzi. Mwanamke hakujali sana mwonekano wake kwa wengine bali alizingatia majukumu yake aliyostahili kuyatekeleza. Majukumu hayo ndiyo yalimfanya apate sifa stahiki. Maana yake, mwanamke mvivu hakuwa na nafasi na hakupendelewa na methali nyingi zinamhujumu.

**Jedwali 28: Methali kuhusu Mahusiano ya Kazi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri yake kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Kankore nsiimwe akasa ahekire iba amaguru gayata esaano.* | 'Nifanye kazi nipate sifa' kasaga na mume mgongoni miguu ya mume ikamwaga unga. |
| 2. | *Omukazi tayeihira nyama ahabugamba.* | Mwanamke hajitolei nyama kwenye uchaga. |
| 3. | *Omushaija ku ashoberwa aretsa, omukazi ku ashoberwa arira.* | Mwanamume akizidiwa na changamoto huvuta sigara, mwanamke yeye hulia. |

Methali ya (1) inamhusu mwanamke ambaye anasaga wimbi akiwa amebeba mume wake mgongoni. Mwanamke anafanya kitendo hicho akiwa na imani ya kupata umarufu na ukubalifu wa mume wake kuwa ni mfanyakazi hodari. Wakati

anaendelea kusaga, miguu ya mume ambaye amembeba mgongoni inamwaga unga. Itikadi hii vile inaendeleza mahusiano ya kiuana inaafikiana na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaosema kwamba, huu ni ukubalifu wa hali inayowekwa na kundi tawala ili kuendelea kutumikiwa na kundi tawaliwa bila kutambua na kutathmini hali zao za unyanyasaji. Mwanamke anaoneshwa kuwa anashawishika na kukubali kufanya kazi kwa ajili ya kupata umaarufu kutoka kwa mume wake kama thamani ya jasho lake, mradi mume anamtambua kama mfanya kazi kwa bidii.

Mwanamke anayetafuta sifa kutoka kwa mume wake, anaishia kupata hasara ikiwemo miguu ya mume wake inavyomwaga unga. Hasara hii inatokea kwa sababu ya mwanamke kufanya kazi kwa kutarajia sifa kama thamani ya juhudi zake. Boserup (1970) anaunga mkono mawazo haya. Anaeleza kuwa wanawake hufanya kazi ambayo mapato yake hayakadiriwi. Kwa kurejelea mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mahusiano ya kumpa thamani mwanamke kwa kulinganisha na kiwango chake cha ufanyaji wa kazi ni unyanyasaji na unyonyaji ambao wanawake hawapaswi kuunga mkono. Itikadi hii ya kiuana inaendeleza mahusiano ya ubwana wa mwanamume na utumwa wa mwanamke.

Kwa mujibu wa mhojiwa wa SHM 3 tarehe 21/04/2018 alieleza kwamba misingi ya kibinadamu kuna mambo ambayo yanafaa na yasiyofaa kutekelezwa kwa sababu ya kutaka kupendwa na kusifiwa. Jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika methali hii haikubaliki na haifai. Chanzo cha itikadi hii ni mila na desturi za jamii ya Wanyankole ambayo inamuumba mwanamke kama kiumbe anayetarajiwa kuhukumiwa na mwanamume kwa kuangazia utekelezaji wake wa majukumu.

Katika muktadha mwingine, mwanamke anatazamiwa kufanya kazi ili amfurahishe mume wake. Samwiri (2007) anadhibitisha itikadi hii ya kwamba sifa kuu ya mwanamke mzuri ni yule mkakamavu na mfanyakazi hodari.

Pia, kuna methali za Kinyankole katika muktadha wa kazi zinazomdhihirisha mwanamke asiyeweza kufanya kazi kwa kujitegemea. Mwanamke anachukuliwa kuwa dhaifu tena mvivu. Udhaifu huu unachukuliwa kuwa wa kimaumbile. Ili mwanamke aweze kufanya kazi na kufanikiwa, anapaswa kusaidiwa na mume wake, hali anayoshawishika kuikubali. Methali ya (2) inazungumzia mahusiano hayo. 'Mwanamke hajitolei nyama kwenye uchaga', inafafanua zaidi kuhusu itikadi ya kumchukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu. Katika mila na desturi za Wanyankole, baada ya kuwinda, nyama ingewekwa kwenye uchaga ambao ulitengenezwa jikoni. Mhojiwa wa KRH 1 tarehe 17/04/2018 anadai kuwa mwanamume alikuwa na jukumu la kutoa nyama uchagani kwa sababu mwanamke hakuwa na uwezo wa kutoa nyama hiyo kwenye uchaga. Itikadi hii inabainisha mahusiano ya uwezo wa mwanamume kwa upande mmoja na udhaifu wa mwanamke kwa upande mwingine katika utekelezaji wa majukumu yao. Tukiongozwa na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, unaosema kwamba wanawake na wanaume washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana tunagundua kwamba udhaifu wa mwanamke ni wa kusingiziwa.

Methali ya (3) katika muktadha wa kufanya kazi, inabainisha mwanamume kama mvumilivu, mdadisi, jasiri na mwenye kutafakari anapokumbana na changamoto fulani. Itikadi hii inaashiriwa na kuvuta sigara ilhali mwanamke ana hiari ya kulia pindi apitiapo changamoto. Itikadi inayobainishwa kwa upande wa mwanamke ni

ya woga, udhaifu na kuongozwa na mihemko. Mwanamke akitingwa na jambo gumu ana hiari kulia kuliko kujaribu kutafuta suluhisho. Mhojiwa SHM 2 tarehe 20/04/2018 anasema kwamba mwanamume si rahisi kusalimu amri kuhusu mambo yanayomsibu lakini hata hivyo imebainika kwamba unyonge wa mwanamke ni wa kusingiziwa na unashadidiwa na kudumishwa na methali hizi zinazoeneleza itikadi zenye mfumodume. Maoni haya yanaendelezwa na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambapo ujasiri, udadisi na uvumilivu wa mwanamume na uoga, udhaifu, mihemko ya wanawake ni mahusiano yanayodhihirisha uwezo wa mwanamume kuliko mwanamke. Itikadi hii inaathiri utambuzi wa uwezo wa mwanamke kwa kuendeleza ‘udhaifu’ wake huku mwanamume akichukuliwa kuwa mwenye uwezo. Katika jamii ya Wanyankole, kutokana na mhojiwa wa 14, tunagundua kwamba kuna mseto wa mawazo kuhusu itikadi hii. Kuna kundi la wale wanaoathiriwa na itikadi za kiutamaduni na kuna wale ambao wameathiriwa na mabadiliko ya kijamii kutokana na elimu. Wanawake wanashiriki katika kutekeleza shughuli ambazo kiutamaduni ni za kiume. Wanafuatilia na kutimiza ndoto zao za maisha wanayotarajiwa kuishi bila kuyatelekeza. Wanawake wanaozingatia itikadi za kiutamaduni wanashikilia na kuamini kwamba mwanamke ni kiumbe dhaifu akilinganishwa na mwanamume.

### 5.1.7 Itikadi za Kiuana kuhusu Mahusiano na Wakwe

Wakwe wanabainika kuwa na mamlaka katika ndoa za watoto wao. Wakwe hutaka kudhibiti, kuingilia kati na kuzivuruga ndoa za watoto wao. Owu (2019) anabainisha kwamba wanandoa wanapaswa kulinda ndoa zao dhidi ya kuvurugika. Wanastahili kuishi kwa amani na wakwe zao ili ndoa zao

zisivunjike. Itikadi hii ipo katika methali za jamii ya Wanyankole. Mkwe anatarajiwa kuheshimiwa na ndugu za mume au mke. Mume na mke wanapaswa kuwa waangalifu katika uhusiano na wakwe wao hasa mamamkwe kwa sababu anaweza ama kuhimili ndoa na kuiendeleza au kuivunja. Mamamkwe anaweza kuifanya ndoa iwe na matatizo chungu nzima. Wakwe walikuwa na nafasi kubwa katika ustawi wa ndoa (Kirindi, 2008). Kwa hivyo, ndoa ya furaha na amani ilichangia pakubwa na ushirikiano mwema na wakwe. Methali kuhusu suala hili zinawasilisha itikadi tofauti kuhusu mahusiano na wakwe kama ifuatavyo:

**Jedwali 29 : Methali kuhusu Mahusiano na Wakwe**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri yake kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Otakareebaga kabi ka nyinazaara ati "ninza owa maawe".* | Asiyejua ubaya wa mama mkwe eti "naenda kwa mama". |
| 2. | *Tocwa gwa muhara wawe mukwe wawe atakaizire.* | Usikate kesi ya binti yako kabla mkwe wako kufika. |

Methali hii ya (1) inamuasa mwanamume au mwanamke kuwa mwangalifu na mama mkwe. Inamuonya mke au mume kuhusu ubaya wa mama mkwe; inasisitiza kuwa hafai kuchukuliwa kama mama yako. Kulingana na mhojiwa SHM 4 tarehe 21/04/2018 mama mkwe anakuwa chanzo cha kuvunjika kwa familia. Owu (2019) anaunga mkono maoni hayo kwamba, kufanikiwa ama kuvunjika kwa ndoa kunategemea mahusiano yaliyopo kati ya wanandoa na wakwe zao. Wakwe huwa wanahusika moja kwa moja katika masuala ya familia za watoto wao. Wakwe hushiriki katika masuala ya ndoa ya watoto wao, kwa madai ya kuwapa nasaha na mwongozo katika ndoa. Hata hivyo, uingiliaji huu unasababisha msuguano ambao hatimaye unaibua chuki kati yao. Itikadi ya wakwe kuhusika moja kwa moja kwenye ndoa ya watoto wao halifai kwa sababu

inakwaza uhuru na upendo kati ya mume na mke. Mahusiano yanayoendelezwa na itikadi hii ya kiutamaduni, kwa mujibu wa mhimili wa Nadharia ya Ufeministi, ni mila ambayo haiendelezi muamana kati ya wanandoa sanasana inaathiri uhuru wa mwanamke. Upendo wa wanandoa ni jambo ambalo la msingi katika kuendeleza ndoa kuliko kutegemea nguvu kutoka nje. Hivyo, wakwe wanapaswa kuwaheshimu watoto wao waliooana. Aidha, ni wajibu wa mume na mke kuwarudishia heshima wakwe zao lakini kwa kuzingatia misingi ya haki na uhuru wa kila mmoja.

Methali ya (2) inamaanisha kwamba, wazazi wa msichana hawapaswi kukata kesi ya mtoto wao kama mume wake hayupo. Kunapotokea mzozo kati ya mume na mke wake, mke akaamua karudi nyumbani kwao, wazazi huwa na shauku ya kujua sababu ya kurejea nyumbani. Kulingana na mila za Kinyankole, mzozo unapotokea, mke anaweza kukimbilia kwa wazazi wake. Jambo hili halikupendelewa na wazazi na ndugu za mke. Kiutamaduni, mume alitakiwa amfuate mke wake ili aweze kumrudisha nyumbani. Kabla ya uamuzi kutolewa na wazazi wa msichana kuhusu mzozo uliopelekea binti yao kurudi nyumbani, ilibidi wazazi wa msichana wasubiri mkwe wao aweze kusikilizwa kwanza. Baba au ndugu za mke kumuamini binti yao na hatimaye kukata kesi kabla ya kusikiliza upande wa mkwe wao haikuruhusiwa. Ilikuwa vigumu kumuamini binti yao. Methali hii inawasilisha itikadi ya kwamba binti haaminiwi kuwa anaweza kusema ukweli. Aidha, inatarajiwa kuwa binti yao ndiye chanzo cha mgogoro wowote baina yake na mumewe. Hii ndiyo sababu ya wazazi wa upande wa msichana kumsubiri mkwe wao kuliko kutegemea tu taarifa za binti. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, inadai kuwa kiumbe wa kike awe kwa wazazi wake

kama msichana au kwa mume wake kama mke, hana haki ya kusikilizwa. Kipaumbele anapewa mwanamume hata kama ndiye mkosaji. Itikadi hii inaendeleza mahusiano ya ukandamizaji wa mwanamke chini ya utamaduni ambao unaendelezwa kwa misingi ya mfumodume.

Aghalabu huaminika kuwa ugomvi hutokea kwa sababu ya mke kushindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na matarajio ya jamii. Mawazo hayo ni kwa mujibu wa mhojiwa KRH 1 tarehe 17/04/2018. Katika utafiti huu, tunadhihirisha kuwa mahusiano haya yanaathiriwa na itikadi ambayo inadhihirisha wanaume kuwa ndio wanaopaswa kuwa mbele na wana haki ya kusikilizwa kwanza. Mahusiano haya ya kiitikadi yanafanya wanawake kushawishika kukubali nafasi ya kutawaliwa kama raia wa daraja la pili. Mhimili wa nadharia ya Itikadi unaosema kuwa imani zinazoendeleza utawala wa tabaka tawala zinapotosha watu wa tabaka la chini katika jamii kwa kuficha masuala ya msingi kuhusu unyanyasaji katika mahusiano ya kijamii kati ya matabaka, unaunga mkono mawazo haya. Vilevile, kwa sababu ya wanaume kuweka mfumo unaowabainisha kuwa watawala kwenye familia zao, wao ndio wanakuwa chanzo cha mzozo katika familia kwa kutaka kulazimisha utawala wao kwa wanawake. Kwa hivyo, itikadi hii ambayo inaendeleza mahusiano ya mwanamume kupewa kipaumbele, mamlaka na haki na kwa upande mwingine mwanamke kubainika kuwa chanzo cha ugomvi katika kifamilia kiasi cha kutoaminiwa kwa utetezi anaoutoa mbele ya wazazi wake si sahihi. Kutokana na haki anayopewa mkwe kulingana na methali hii, tunaweza kubainisha mahusiano yasiyodhihirisha usawa wa kiuana kati ya mwanamke na mwanamume.

### 5.1.8 Itikadi za Kiuana kuhusu Mahusiano ya Mjane

**Jedwali 30: Methali kuhusu Mahusiano ya Wajane**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omufakazi taijuka kitara.* | Mjane hakumbuki ghala. |
| 2. | *Omukazi iba ku afa arya enkoko* | Mke anakula kuku mume wake anapofariki. |
| 3. | *Omufakazi tagaya nfuni.* | Mjane hadharau dhakari fupi. |

Methali ya (1) inamaanisha kwamba ni vigumu mjane kukumbuka ghala. Mwanamke 'kukumbuka ghala' ni wakati anaenda kwenye ghala kupata chakula kwa ajili ya kumpikia mume wake. Mume wake akishafariki, mwanamke haoni tena haja ya kwenda kwenye ghala. Katika jamii ya Wanyankole, ghala hutumiwa kuhifadhia aina mbalimbali za vyakula. Ghala halikuishiwa na chakula na mwanamke alikuwa anatoa chakula kwa ajili ya mapishi hasa kwa ajili ya mume wake. Mwanamke alitarajiwa kumhudumia mume wake; kumpikia ilikuwa ni mojawapo ya majukumu yake ya msingi. Itikadi katika methali hii inabainisha kuwa mwanamke hasumbuki tena kutafuta chakula kwenye ghala kwa sababu mume wake aliyemshughulisha hayupo, kiasi cha kusahau ghala. Itikadi hii inaonesha kwamba mwanamke anapaswa kumpatia kipaumbele mume wake kwa kumhudumia na kujali masilahi yake hata kuliko kujijali mwenyewe. Kauli 'taijuka kitara' (hakumbuki ghala) inadhihirisha namna mwanamume anavyokwezwa. Anakuwa na thamani ambayo inapewa kipaumbele kiasi cha mjane kutojijali. Mwanamke wa aina hii anaathirika na kushawishika na itikadi inayomfanya kukubali hali na nafasi yake kama mhudumu wa mwanamume bila kulazimishwa. Itikadi inambainisha mwanamke mbele ya mwanamume kuwa yupo kwa ajili ya kumtumikia. Nadharia ya Itikadi inabainisha kuwa uendelezaji wa utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali halisi katika jamii.

Hivyo, mahusiano haya yanamfanya mwanamke kuamini fikira ambazo si za kweli na kuzifanya kuonekana za kweli. Wanaume wanaendeleza itikadi hii kwa kuwapotosha wanawake katika jamii kuficha masuala ya msingi kuhusu unyanyasaji katika mahusiano ya kijamii kati yao na wanawake.

Vilevile, itikadi katika methali ya (2) inadhihirisha mahusiano ya unyanyasaji wa mwanamke. Maana ya methali ni kwamba mke anapata fursa ya kula nyama ya kuku kama mume wake amefariki. Katika mila na desturi za Wanyankole, mwanamke alikuwa haruhusiwi kula nyama ya kuku. Alipodiriki kula nyama hiyo alirejelewa kama mlafi. Ulikuwa ni mwiko kwa mwanamke kula kuku na vyakula vingine ambavyo vilitengewa wanaume. Methali hiiinatuwasilishia mwanamke ambaye anakula kuku baada ya mume wake kufariki. Kitendo hiki kinadhihirisha kuwa mwanamke anatimiza aliyokuwa amenyimwa na mume wake kwa misingi ya mila na desturi za Wanyankole. Kwanza, mwanamke kula nyama ya kuku baada ya kifo cha mume wake inadhihirisha kwamba alikuwa anatimiza masharti ya jamii dhidi ya hiari na uhuru wake. Ndiyo maana baada ya kifo cha mume wake anapata uhuru wa kula nyama ya kuku. Huu ni uamuzi anaoufanya kwa hiari yake aliyokuwa amenyimwa na mume wake.

Pili, nyama ya kuku katika jamii ya Wanyankole inawakilisha mlo mzuri wa kusaidia kujenga mwili ambao mwanamke anaukosa. Hali hii inamfanya kuwa na udhaifu wa mwili na afya, hatimaye kuwa katika nafasi ya unyonge. Kutokana na mjadala huu inabainika kwamba mwanamke anaasi itikadi ya mfumodume ambayo inamnyima haki yake ya kula anachotaka. Hali hii inaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba wanawake

wazinduke na kubadili mielekeo ya jinsi wanavyojiona katika uhusiano na wanaume. Mwanamke anatambua kuwa kukatazwa kula nyama ya kuku ni itikadi ambayo inaumbwa na jamii kwa lengo la kuendeleza utawala wa wanaume. Itikadi hii inapotosha hali halisi katika jamii. Mwanamke kula kuku baada ya kifo cha mume wake, ina maana kwamba anaweza hata kula nyama ya kuku wakati mume wake yuko hai. Itikadi hii inabainisha wazi upendeleo kwa mwanamume na kudhulumiwa kwa mwanake kwa upande mwingine. Mahusiano ya kumzuia mwanamke kuwa na uhuru wa uchaguzi wake ni ya kimamlaka kati ya mwanamume na mwanamke yanavyodhihirika katika jamii ya Wanyankole kupitia methali zao.

Itikadi katika methali ya (3) inabainisha mahusiano ya mwanamke kama mtegemezi na mhitaji ambapo maisha yake yanamtegemea mwanamume. Methali hii inamaanisha kwamba mke ambaye amepoteza mume wake hawezi kudharau dhakari fupi ambayo amebahatika kuipata. Mwanamke anadhihirika kufarijika na zubu la mume wake kabla ya kifo chake. Maana ya ndani ya methali hii ni kwamba, kabla ya kifo cha mume wake anapata kila kitu kwa sababu anatosheleza mahitaji yake. Baada ya kifo cha mume wake, anaambiwa hana budi kupokea na kuridhika na chochote anachopata kwa sababu aliyekuwa anampa huduma stahiki hayuko. Kwa kuongozwa na nadharia ya Itikadi, mwanamke anashawishika kukubali ya kwamba maisha yake yanahimiliwa na mwanamume. Itikadi hii vile inaendeleza mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke katika methali hii haiakisi hali halisi. Mawazo haya yanadhihirika kupitia kwa mhimili unaosema kwamba utawala wa tabaka tawala unatimizwa kwa kupotosha hali

halisi. Wanaodhulumiwa wanakubali hali na hadhi zao kwa kuathiriwa na ung'amuzi potoshi.

Itikadi inayoendelezwa kwa mwanamke mjane katika methali ya (3) ni upokezi na utegemezi ambao umejikita kwenye matumizi ya sitiari ya uume. Mwamzandi (2016) katika utafiti wake anadhihirisha suala hili. Mwamzandi anafafanua kwamba wanaume wanapewa mamlaka zaidi kuliko wanawake; mamlaka yanayotokana na uamilifu wa dhakari ambao unafafanua mahusiano ya wanawake na wanaume. Mahusiano ya kiuana kwamba mjane hawezi kuhimili maisha yake bila kutegemea mwanamume yanamweka mwanamke katika nafasi ya utegemezi na mwanamume kama anayewajibikia kukimu maisha ya mwanamke. Hali halisi ya utegemezi wa mwanamke inadhihirika kupitia mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba fasihi hutumiwa kama jukwaa la kuelezea hali ambayo mwanamke anakumbana nayo ili ieleweke kwa wengine. Hivyo, nafasi ya mwanamke kama mtegemezi kupitia mahusiano yake na mwanamume katika jamii imebainika kupitia methali za Kinyankole.

### 5.1.9 Itikadi za Kiuana kuhusu Mahusiano ya Udhalilishaji

Methali zimetumiwa kudhalilisha wanawake na kubainika kuwa ni viumbe wanaopaswa kuwa kwenye daraja la pili katika jamii ambazo zinaendelezwa kwa misingi ya mfumodume. Methali za aina hii haziakisi uamilifu wa methali kama semi zenye maarifa, kama inavyodhihirika katika methali zifuatazo:

**Jedwali 31: Methali kuhusu Mahusiano ya Udhalilishaji**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Eyi abakazi bashagire abandi babahindura abazaana.* | Pale ambapo wanawake ni wengi, wengine hugeuzwa kuwa watumwa. |
| 2. | *Abakazi ne'ndeere tizihwa murutookye.* | Wanawake ni majani ya migomba hayamaliziki shambani. |

Maana ya nje ya methali ya (1) ni kwamba, wanawake wakiwa wengi, wengine wanageuzwa kuwa watumwa. Methali hii inamaanisha kwamba, kwa sababu ya idadi kubwa ya wanawake wengine wanapoteza thamani yao kama wake na kuishia kufanya kazi za kitumwa. Katika jamii ya Wanyankole kulikuwa na kitengo cha watumwa waliotumikia nasaba ya ufalme kama vile ukoo wa Bahinda. Familia nyingine zenye hadhi kama vile matajiri, pia walikuwa na watu wa kuwafanyia kazi. Hivyo, familia kama hizo ungekuta mume mmoja ana wake zaidi ya wanne. Wanawake wengine waligeuzwa wafanya kazi shambani kwa ajili ya kuzalisha mali. Itikadi inayowasilishwa katika methali hii inabainisha ukubalifu wa hadhi ya wanawake kuwa ni wenye thamani duni na ni viumbe wa kiwango cha chini. Mwanamke anaweza kuolewa akawa mke baadaye akageuzwa mtumwa ili kumtumikia bwana mwenye nyumba. Itikadi inayobainika katika methali hii inaendeleza mahusiano ya ubwana na utwana kati ya mwanamume na mwanamke kwa utaratibu huo. Mahusiano haya yanamvunjia heshima, kama mke nyumbani na haki zake kama binadamu. Itikadi hii haina nafasi kwa sababu kwanza kabisa, aghalabu wanawake hawaungi mkono kuwa wanawake wa ziada kwa mwanamume. Pili, kwa sababu ya wanawake kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali na kujiendeleza. Hali hii inawafanya

kujiimarisha na kujitegemea kiuchumi. Itikadi hii kama inavyowasilishwa katika methali hii inamvunjia heshima na kumdhalilisha mwanamke huku ikimtanguliza mbele mwanamume.

Aidha, methali ya (2) inamaanisha kwamba, wanawake ni wengi sana na wanapatikana popote. Wanawake wanalinganishwa na majani ya migomba kiistiari kwa sababu ya wingi wao. Majani ya migomba huwa ni mengi na ya kila aina. Huwa yanatumiwa kufunika chakula wakati wa maandalizi ya mapishi katika jamii ya Wanyankole. Mpishi hutumia majani mazuri ambayo hayajachanika ili kufunika chakula. Mpishi anachukua muda wake kuchagua na kukata majani mazuri. Ina maana kwamba yuko huru kuyatupa akiona kwamba hayafai, na kukata mengine mazuri yatakayofanya kazi hiyo vizuri. Itikadi ya thamani duni ya wanawake katika methali hii inaendeleza mahusiano ya udhalilishaji wao. Kwa kawaida, kitu kikiwa kingi, thamani na bei yake inashuka lakini si kwa binadamu. Binadamu wote wana haki sawa na hakuna anayepaswa kudhalilishwa na mwenzake. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inathibitisha suala hili kwa mhimili wake kwamba, jamii iendelezwe kwenye misingi ya upendo, kushirikiana na kuheshimiana. Hata vivyo, wanawake ndio wanachangia Zaidi maendeleo ya familia zao; wanashiriki katika kazi ndogondogo zinazosaidia kuhimili uchumi wa nchi.

Katika methali za Kinyankole imebainishwa namna itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kati ya mwanamume na mwanamke. Imedhihirishwa kwamaba mahusiano ya kiuana kati ya mwanamume na mwanamke yanaathiriwa na itikadi za mfumodume. Mahusiano hayo kuhusu

utekelezaji wa majukumu na haki kati ya wanawake na wanaume ni ya kimamlaka ambapo mwanamume anakuwa mbele na mwanamke amewekwa kwenye nafasi yake kama kiumbe wa daraja la pili. Mahusiano haya yanaendelezwa kwa misingi ya ukubalifu na ushawishi wa wanaume na wanawake katika nafasi zao kama jamii inavyozitenga na kuzikubali. Uchunguzi huu unathibitisha kwamba itikadi hizi za ubaguzi wa binadamu kwa msingi wa uana na itikadi za mfumodume zinazomtanguliza mwanamume zinaendelezwa na kuimarishwa kwa kushawishika na kukubalika kwa nafasi hizi kwa njia ya ung’amuzi potoshi kupitia kauli za kimethali na miktadha yake mbalimbali.

## 5.2 Itikadi na Mahusiano ya Kiuana katika Methali za Kiswahili

Sehemu hii inawasilisha methali za Kiswahili na itikadi mbalimbali za kiuana zinazoendeleza mahusiano ya kiuana. Wanawake na wanaume wanawajibishwa kutekeleza majukumu yao maalumu ya kimaumbile na kijamii kama yanavyotengwa kwa misingi ya utamaduni. Utamaduni wa Waswahili uliathiriwa na dini ya Kiislamu (Mbaabu, 1985; Sengo, 1992). Kulingana na dini ya Kiislamu kwa mfano, mwanamke hapendekezwi na hapendelewi kuwa jaji. Kipaumbele anapewa mwanamume kwa sababu hutumia urazini zaidi, na mwanamke huongozwa na hisia (Maawy, 2009). Inakubalika mwanamke kuwa jaji lakini hawezi kuwa kadhi. Katika kazi sifika za Waswahili kama vile Utenzi wa Mwanakupona, mwanamke anawasilishwa kama mke wa nyumbani kulingana na utamaduni wa Waswahili wenye asili ya Kiislamu wa Karne ya 19 (King’ei, 2000). Hivyo, katika muktadha huu, utafiti huu umechanganua itikadi hizi za kiuana katika methali za Kiswahili na kubainisha namna zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana.

### 5.2.1 Itikadi na Mahusiano ya Ndoa

**Jedwali 32: Methali za Kiswahili kuhusu Mahusiano ya Ndoa**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Mwanamke kipofu huangaza nyumba. |
| 2. | Mke bila mume ni kama shamba lisilolimwa. |
| 3. | Uganga haumweki mume. |
| 4. | Cheko la mke kwa mume ni kheri ya nyumbani. |
| 5. | Jicho la mume ni mkewe. |

Mwanamume anaoa na kuishi na mke nyumbani kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya nyumbani. Itikadi hii inaendelezwa zaidi na methali ya (1) ambayo inamaanisha kwamba mwanamke hata kama ni kipofu, ana uwezo wa kuleta nuru nyumbani. Nuru inayoletwa na mwanamke hata kama ni kipofu ina ushawishi mkubwa wa kumfanya kukubali jukumu la kuratibu nyumba kama lake. Inadhihirika kuwa nafasi muhimu ya mwanamke katika familia ni kuleta furaha nyumbani. Itikadi hii inabainisha ukubalifu wa mwanamke kwamba nafasi yake ni ya kutekeleza majukumu ya nyumbani. Itikadi hii haiafikiani na mtazamo wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa sababu inaendeleza mahusiano kwamba mwanamume huoa mke kwa kigezo cha uwezo wake wa kutengeneza nyumbani. Nafasi hii ya mwanamke inaibua imani ambayo ipo na inashikiliwa katika jamii ya Waswahili kwamba mke anaolewa kwa ajili ya kutumikia na kuhudumia mwanamume.

Methali hii ya (2) ina ujumbe kuwa mwanamke anapaswa kuolewa ili aishi na mume ambaye ana uwezo wa kutimiza mahitaji yake. Kulingana na itikadi inayodhihirika katika methali hii, maisha ya mwanamke yanakuwa kamili kama ana mume. Inawasilisha itikadi ya haja ya mwanamke kuolewa ili apate mume

atakayekidhi mahitaji yake na kumfanya akubalike katika jamii. Mwanamke ambaye hana mume analinganishwa na shamba lisilolimwa ambalo linaonekana baya pamoja na kuvutia wanyama na wadudu hatari. Mwanamke huyo hatavutia, atabadilika kitabia na kuwa chanzo cha maovu kama vile ukahaba huku akijaribu kujikimu kimaisha. Itikadi inayobainika katika methali hii inaendeleza mahusiano kwamba mke anaolewa kwa ajili ya kutoshelezewa mahitaji. Ina maana kuwa mwanamke hawezi kujitegemea na kutosheleza mahitaji yake bila mume. Hata kama anatengana na mume itikadi hiyo ya kijamii inamshawishi kupata mume mwingine ili aolewe. Kulingana na mhojiwa ZNB 1 tarehe 23/05/2018 mwanamume ni nguzo kuu katika maisha ya mke. Mume anapaswa kutoa huduma kwa mke wake kama vile kununua chakula, kununua nguo kwa ajili ya mke na kumtunza kwa ujumla ili aonekane vizuri na kuvutia. Itikadi hii kwa upande wa mwanamume inamtambulisha kama mwenye uwezo mkubwa na nafasi muhimu katika maisha ya mwanamke. Haja ya mwanamke kuolewa kwa ajili ya kutoshelezewa mahitaji ni mahusiano yanamfanya kuwa mtumwa wa ndoa. Itikadi hii inathibitishwa na mhimili wa Nadharia ya Itikadi ambayo inamshawishi mwanamke kukubali hadhi yake ya unyonge na kumbainisha mwanamume kama mwenye uwezo. Wajibu huu wa mwanamume kwa mwanamke unamfanya mwanamke kushawishika kuolewa kwa lengo la kutunzwa na mume wake. Asipoolewa ‘ataonekana kama shamba lisilolimwa’. Kuna haja ya wanawake kubaini ukweli kwamba wao pia ni binadamu ambao wanaweza kujikimu kimaisha bila kuwategemea wanaume na kama kuna haja ya kushirikiana na wanaume katika ndoa mahusiano hayo yawe ya kimlishano na si ya kiutegemezi. Mawazo haya yanaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya

Ufeministi wa Kiafrika kwamba, wanawake wanapaswa kuzinduka na kubadili itikadi ya namna wanavyojiona katika uhusiano na wanaume.

Aidha, mwanamke anashauriwa kushughulikia majukumu yake kikamilifu ili aweze kuendelea kudhibiti ndoa yake. Itikadi katika methali hii inamfanya mwanamke kushughulikia majukumu yake ya kudhibiti ndoa ipasavyo. Itikadi hii inadhihirika katika methali ya (3). Mwanamke anashawishika kukubali kuwa anapaswa kumhudumia mume kwa umakinifu. Hii ni njia ambayo itamwezesha mwanamke kumudu ndoa yake badala ya kutumia njia za ushirikina. Jukumu hili kwa mwanamke linaendelezwa kama la kawaida na sehemu ya kazi zake za kike. Mhojiwa ZNB 4 tarehe 26/05/2018 anasema kwamba, mambo muhimu yanayofaa kuzingatiwa na mke ili kudumisha upendo kati yake na mume wake ni yale yanayomtuliza mume kama vile kumvua koti lake akiwa anatoka safarini au kazini, kumletea maji ya kunywa, kumuuliza habari za huko atokako, kumletea chakula, wakati wa kulala mke amsingesinge mumewe na ampapasepapase kuliko kuhadaiwa na kuliwa pesa na waganga. Mulokozi (1999) anathibitisha maoni haya kuhusu sifa za mwanamke katika Utenzi wa Mwanakupona. Timammy na Swaleh (2013) wanathibitisha zaidi hoja hii kwamba mwanamke atumie mbinu zijulikanazo kama vile kumlea mume wake kama anavyomlea mtoto kulingana na mila za Waswahili. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika mahusiano ya mwanamke kubainika kwenye nafasi ya kumhudumia mwanamume yanamnyima uhuru wa kujitegemea na kuendelea kuonekana kuwa mtumwa mbele ya mwanamume.

Mwanamke katika jamii ya Waswahili anatarajiwa kudhihirisha tabia ambazo zinaleta amani na utulivu nyumbani. Mhojiwa MSA 1 tarehe 9/05/2018, anatoa maoni kwamba mwanamke hafai kuonesha sura ya huzuni kwa mume wake. Daima anapaswa na kutarajiwa kuwa na uso wa furaha na bashasha hata kama kuna jambo ambalo limemkasirisha na ameudhika. Mtoa hoja aliendelea kueleza kwamba siku zote, kwa Waswahili, mapenzi hutoka kwa mwanamke. Kwa hivyo, mwanamke mwenye busara humfurahisha mume wake kwa mujibu wa matarajio ya utamaduni kama inavyothibitishwa na methali ya (4). Vitendo vya mke huleta raha na amani nyumbani**.** Cheko linaashiria mambo yote ya kufurahisha ambayo mke atamfanyia mume wake. Wandera (1996) anatambua mambo muhimu yanayomfurahisha mwanamume kama vile maandalizi ya chakula kizuri, shughuli nzuri za chumbani, maneno matamu kwa mume, ampe maji moto ya kuoga, avae nguo zenye mapambo, awe na lugha nzuri chumbani, asuke nywele zake vizuri na ajipodoe. Mambo haya yakitekelezwa yanasaidia kudumisha amani nyumbani.

Mwanamke kuwa kwenye nafasi ya kuleta amani na utulivu nyumbani, ni mahusiano ya kiitikadi yanayoendelezwa na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaodai kwamba ukubalifu unapatikana kutokana na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala. Mwanamke anakubali nafasi yake kuwa jukumu la kumpembejea mume wake ni kazi anayopaswa kuwajibikia. Ukubalifu huu unasababishwa na wanaume kupotosha uhalisia kwa ajili ya kutaka kuhudumiwa na wanawake daima. Wanawake nao wanashawishika na kuikubali hali hii. Mahusiano ya kiuana yanayoendelezwa katika methali hii ni kwamba mke ana wajibu wa kumfurahisha mume wake. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika haiafikiani na

mahusiano haya ya kiuana kwa sababu hakuna muamana kati ya mwanamume na mwanamke. Itikadi hii inamshushia thamani mwanamke na kumfanya kuwa chombo cha kumpembejea mwanamume.

Katika methali ya (5) thamani ya mke inabainishwa kwa kuwa na mume wake. Jicho ni kiungo cha mwili ambacho ni muhimu sana kwa binadamu kwa kazi yake muhimu ya kuona na kumuelekeza binadamu katika kufanya mambo yake. Jicho pia ni kiungo ambacho ni chepesi kudhuriwa na linahitaji umakini sana kulitunza dhidi ya hatari yoyote kwa ajili ya utendaji kazi wake. Katika methali hii ya (5) mke amelinganishwa na jicho kwa thamani. Huu ni ushawishi wa aina nyingine kutoka kwa wanaume kama Nadharia ya Itikadi inavyobainisha. Ukubalifu wa wanawake kujiona wenye thamani kwa wanaume wanaporejelewa kama 'jicho la mume' unajikita kwenye ushawishi wa itikadi za tabaka tawala (wanaume). Wanawake wanashawishika na kukubali kuwa bila wao katika maisha ya wanaume, inakuwa vigumu wanaume kujitegemea. Jicho kwa binadamu ni kiungo muhimu kinachopaswa kutunzwa kwa umakini kwa sababu ya umuhimu wake kwa. Vilevile, kwa sababu ya manufaa ya mke kwa mume wake, mke anapaswa kutunzwa na kulindwa kwa manufaa ya mume. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa haja ya kutunza mke ni kwa ajili ya kutimizia mume mahitaji yake. Methali hii inaelekeza mwanamume asiwe anaangalia mambo mengine zaidi ya mke wake kama mhojiwa LMU 3 tarehe 16/05/2018 anavyotambua. Inadhihirishwa kuwa jukumu la mume kuhakikisha mke wake analindwa na yuko nyumbani ametunzwa salama na ametulia, ni kwa ajili ya kumtumia kutekeleza maslahi yake.

### 5.2.2 Itikadi kuhusu Ushirikiano wa Mume na Mke katika Ndoa

Binadamu aliumbwa akiwa na mapungufu yake. Mume na mke ni binadamu wanaoishi pamoja baada ya maridhiano halali. Kila mmoja anakuwa amepitia malezi tofauti toka utotoni hadi wanapoamua kuoana. Kwa hivyo, mazingira ya malezi, elimu na hali ya kiuchumi yanachangia kuhusu kuandaa aina ya mume au mke jinsi atakavyokuwa. Mume na mke wanakutana baada ya kila mmoja kulelewa na kukuzwa kwa njia na mazingira tofauti. Kwa upande wa jamii ya Waswahili, zipo methali zinazozungumzia itikadi za kiuana kuhusu ushirikiano wa mume na mke kwenye ndoa. Ushirikiano baina ya mke na mume hauepukiki. Itikadi ya ushirikiano kwenye ndoa katika methali zifuatazo inaungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa mhimili unaosema kwamba wanaume na wanawake washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana bila kuathiriwa na majukumu ya kimaumbile.

**Jedwali 33: Methali za Kiswahili kuhusu Mahusiano ya Ushirikiano wa kindoa**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Kuishi wawili ni kuvumiliana. |
| 2. | Ndoa ya furaha ni muungano. |
| 3. | Mke ni nguo ya mume na mume ni nguo ya mke. |
| 4. | Nyege ni kunyegezana, mapenzi ya upande mmoja hayanogi. |

Methali ya (1) ya Kiswahili ilirejelewa na kuchanganuliwa katika muktadha wa uana kwa kuzingatia mume na mke. Kiutamaduni, mwanamume anatarajiwa kuwa na mienendo fulani na kutekeleza majukumu fulani maalumu kama vile kutafuta chakula na kununua nguo. Mwanamke anatarajiwa kuwa awe mkarimu, mcheshi na mtekelezaji wa majukumu yake kama kupika, kulea watoto, kufua na kudumisha usafi wa nyumbani. Kwa kuwa jamii inaweka vigezo hivi na

inatarajia vitekelezwe, na kwa sababu mume na mke ni zao la jamii kitabia, wao wanajaribu kuhakikisha kuwa vigezo hivyo vinatekelezwa. Katika kujaribu kutekeleza wajibu huu upande mmoja unajikuta umekwaza upande mwingine. Kulingana na mhojiwa MSA 4 tarehe 12/05/2018 kuvumiliana na kusameheana ni suluhisho la kutatua matatizo na changamoto zinazoibuka kati ya mume na mke kama watu wanaoishi pamoja.

Methali ya (2) inalenga wanandoa kuungana katika kutekeleza shughuli za kindoa. Muungano kati ya mume na mke unadhihirika katika kuvumiliana, kupendana na maridhiano kati yao. Ndoa inafaa kuendelezwa kwa furaha ili kuwe na amani ndani ya familia. Nguzo muhimu ya furaha hiyo ni muungano. Itikadi inayobainika katika methali ni haja ya mume na mke kuungana katika ndoa. Itikadi hii inaendeleza mahusiano ya ushirikiano na kuvumiliana ambako kunasababisha furaha katika ndoa kwa sababu hakuna binadamu aliye kamili. Viashiria hivi vikiwepo na kuzingatiwa yaani ushirikiano, uvumilivu na maridhiano amani inakuwepo na hatimaye ndoa inaendelezwa kwa furaha. Mawazo haya yanaungwa mkono na mhimili wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaodai kwamba wanaume na wanawake washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana bila kuathiriwa na majukumu yao ya kimaumbile. Mahusiano ya wanaume na wanawake kuwajibika kwa kushirikiana pamoja kama inavyoungwa mkono na mhimili huu yanadhihirika katika methali nyingine ya (3).

Nguo ina kazi ya kusitiri uchi wa binadamu. Mavazi ni ishara kwamba binadamu hapendelei kuonysha uchi wake. Kuvaa nguo kunaonesha hali bora ya kuishi.

Katika methali hii ya (3), mke anafananishwa na nguo ya mume wake na mume anafananishwa na nguo ya mke wake. Mume ana wajibu wa kusitiri udhaifu wa mke wake na mke pia anapaswa kusitiri udhaifu wa mume wake. Binadamu si mkamilifu kwa hivyo kuna haja ya kuvumiliana na kushirikiana. Mume na mke wakiwa hadharani, nyuso zao ziwe na tabasamu na wanatakiwa kutotangaza matatizo ya nyumba yao. Kwa hakika ni jambo la ushenzi mke na mume kutoleana maneno makali na kuharibiana sifa hadharani. Haya ni maoni ya mhojiwa LMU 1 tarehe 15/05/2018. Methali hii inaendeleza mahusiano ya kuheshimiana kati ya mke na mume. Kama inavyodhihirika kwamba kuvaa nguo kunaonysha hali bora ya kuishi, mke na mume waishi pamoja kwa hali nzuri. Mume na mke wakifaana, kutakuwa na hali bora ya kuishi kati yao katika familia.

Kimsingi, mapenzi ni kiini cha ndoa kwa mume na mke. Methali ya (4) inamaanisha kwamba, nyege ni hamu ambayo mtu anakuwa nayo ya kutaka mapenzi. Ili mapenzi yakolee kila mmoja, yaani mume na mke wana nafasi na mchango wa kuyanogesha. Kulingana na mhojiwa MSA 3 tarehe 11/05/2018, mke ana wajibu wa kuridhisha mume wake kimapenzi. Mke anapaswa kutumia mbinu zote kama alivyofunzwa na makungwi kuhakikisha kwamba mume wake halalamiki. Maoni ya mhojiwa yanatofautiana na jinsi itikadi inaelezwa katika methali hii.  Methali hii inaeleza dhana ya 'nikune nikukune'. Ili mahaba yanoge kila mmoja awajibikie nafasi yake ipasavyo. Itikadi inayobainishwa inaendeleza mahusiano ya kushirikiana kati ya mume na mke katika kufanikisha ndoa kama Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inavyodai. Aidha, kwa mujibu wa mhojiwa wa 34, methali hii inaeleza zaidi kuhusu haja ya mume kuwajibika kwa kutimiza

mahitaji ya mke kama vile kumnunulia nguo, na kumfanyia mambo mazuri yanayotarajiwa na wanawake wa Kiswahili.

### 5.2.3 Itikadi za Kiuana kuhusu Mahusiano ya Ndoa za Mitala

Jamii nyingi za Kiafrika zinashadidia ndoa za mitala. Ndoa hizi zinasababishwa na utamaduni wa mfumodume ambao ndio unatawala katika familia na jamii kwa ujumla. Mwanamume kuoa wake wengi kunampa sifa katika jamii. Wanaume wanaoa mke zaidi ya mmoja kwa kutarajia kufaidika kutokana na mpango huu wa ndoa. Faida mwanamume anazotarajia kufaidika nazo ni kama vile kuangaliliwa maslahi yake kama kuandaliwa chakula, usafi na kupewa mahaba matamu (Mnenuka, 2012). Katika jamii za Waswahili pamoja na utamaduni wao, wanaume na wanawake wanaendeleza ndoa za aina hii wakichochewa pia na dini ya Kiislamu ambayo inaruhusu mume kuoa zaidi ya mke mmoja.

**Jedwali 34: Methali kuhusu Mahusiano ya Ndoa za Mitala**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Mke wa kwanza ni kama mama |
| 2. | Aliyeoa wake wawili kabeba mzegamzega |

Methali ya (1) inamaanisha kwamba mke wa kwanza atunzwe vizuri na mume wake kama mama anavyostahili kutunzwa. Methali hii inabainisha haja ya kumtunza mke wa kwanza vizuri. Wanaume wanapopata mke zaidi ya mmoja wanasahau majukumu yao ya kuwatunza waze zao wa kwanza na wanaishia kuwatelekeza (Wamitila, 2001). Methali hii inabainisha ushawishi na ukubalifu wa wanawake kuolewa pamoja. Hata kama wameolewa pamoja, mke wa kwanza anapaswa kupewa huduma maalumu. Itikadi hii inamfanya mke wa kwanza kushawishika kuwa maarufu zaidi mbele ya mume kuliko mke wa pili. Hali hii ya

upendeleo inaibua chuki na wivu kati ya wake hao, jambo ambalo linatimiza lengo la mwanamume kuwa kwenye nafasi ya kutawala na kutumikiwa. Mahusiano haya yanaafikiana na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaosema kwamba utawala unalenga kujitolea na kutumika kwa tabaka tawaliwa wakitumikia kundi dogo la watawaliwa. Itikadi hii inatimizwa kwa kutenganisha wake hawa kwa kutunza vizuri mke wa kwanza. Mke wa kwanza anajiona kuwa ndiye muhimu zaidi kwa mume. Aidha, katika muktadha wa kiudenguzi, methali hii inaibua maana kwamba, 'mama' ana wajibu wa kutunza watoto wake. Kwa hivyo, mwanamume anapooa anatarajia kutunzwa na mke wake kama mama anavyotunza mtoto wake. Itikadi hii inaendeleza upendeleo wa mwanamume kushughulikiwa maslahi yake na kubainika kama kiumbe aliye bora kuliko mwanamke.

Methali ya (2) inamaanisha kwamba mume mwenye mke zaidi ya mmoja ana mzigo mkubwa na kwamba wanawake hao hawana uwezo wa kufanya lolote pasipo kubebwa/kusaidiwa na mwanamume. Kwamba mwanamume ana uwezo na anawasaidia wanawake hao kwa kuwaweka pamoja na kumudu kuwahudumia anavyotaka. Mahusiano hayo kama yanavyoendelezwa na Itikadi ya kiuana tumeyafikia kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia ya Udenguzi kwa mujibu wa Derrida (1960). Mhimili huu unadai kuwa matini yoyote haina maana moja anayoweza kuitegemea msomaji bali ni maana nyingi za maandishi katika lugha kulingana na kiashiria na kiashiriwa. Neno 'mzegamzega' katika methali hii ni mkururo wa vitu au ubebaji wa vitu vingi kwa pamoja ilhali mbebaji akionekana kama vile kulemewa. Kwa hivyo, ingawa mwanamume anaonekana kuwa na

uwezo wa kubeba wake zake, mwenyewe anachorwa kuwa analemewa na ‘mzigo wake.

### 5.2.4 Itikadi za Kiuana na Mahusiano ya Kiuana kuhusu Uzazi

Methali katika sehemu hii zinahusu furaha ya mwanaume aipatayo kwa kupata watoto, na jinsi uzazi unavyoimarisha mahusiano kati ya mwanamke na mwaname. Methali hizo zinabainishwa katika Jedwali Na 36:

**Jedwali 35: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Uzazi**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Nyumba ya mgumba haina matanga. |
| 2. | Furaha ya nyumba ni watoto. |

Haja ya kuwa na watoto ambao wanatarajia kuleta furaha kwa upande wa mwanamume ni itikadi ambayo inadhihirika katika methali ya (1). Mwanamume anategemea watoto hao kumfaa katika umri wa uzee. Watoto wa kiume hasa ndio wanatarajiwa kuendeleza familia ya baba yao (Ba, 1981). Mwanamke hatarajiwi kuhusika katika kuendeleza majukumu ya nyumbani baada ya kifo cha mume wake ikiwemo kuweka matanga ya mume wake. Itikadi hii inaendeleza mahusiano kuwa mwanamke haaminiwi na kupewa dhamana ya kuendeleza familia baada ya kifo cha mume wake. Mwanamke pia anabainika kama asiye na mamlaka juu ya maamuzi fulani baada ya kifo cha mume wake. Mhojiwa MSA 2 tarehe 11/05/2018 anaeleza kwamba baada ya kifo cha mume, mwanamke anakaa eda na baada ya eda anaweza kuolewa tena kwingine. Imani ya mwanamume inabaki kwa watoto ambao anawategemea kuendeleza familia, wala si mke ambaye anaweza kuondoka wakati wowote baada ya eda. Watoto, hasa wa kiume ndio wanachukuliwa kuwa wa muhimu ili kuweza kuendeleza familia ya baba yao kuliko mwanamke. Kwa kurejelea mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa

Kiafrika itikadi hii inamdhulumu mwanamke kwa mila na desturi hizi ambazo zinampendelea kiumbe wa kiume. Imebainika kuwa mwanamke anatumiwa tu kama chombo cha kuzaa watoto kwa mwanamume. Hadhi hii ya mwanamke kama chombo cha kuzaa inamchukulia kuwa wa daraja la chini na wa kudhulumiwa haki zake.

Fauka ya hayo, katika methali ya (2), jukumu la msingi kuhusu mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume ni upatikanaji wa watoto. Mwanamke ambaye hawezi kuzaa watoto hapendelewi kwa sababu atakuwa ameshindwa kutekeleza wajibu wake. Mwanamke anashawishika na kukubali jukumu hili. Tunadhihirisha kuwa upatikanaji wa watoto ni juhudi za mume na mke kwa kushirikiana. Hivyo, watoto ni furaha kwa wazazi wote, na si kwa mzazi wa kiume pekee kama inavyodhihirika katika methali ya (1). Mawazo haya yanaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambao unasisitiza kushirikiana kwa mwanamume na mwanamke kwenye misingi ya amali za kibinadamu ili kuendeleza jamii kwa njia ya usawa.

### 5.2.5 Itikadi za Kiuana kuhusu Mahusiano ya Malezi ya Watoto

Itikadi ya wanawake kutengewa jukumu la malezi na kutunza watoto ipo katika jamii nyingi za Kiafrika. Methali za Kiswahili zinadhihirisha uchangamano katika suala la malezi. Kuna methali ambazo zinatenga jukumu la malezi kwa wanawake. Pia, zipo methali ambazo zinaonesha ushirikiano wa wazazi wote kuhusu malezi ya watoto wao. Mifano ya methali zifuatazo inabainisha itikadi hizi:

**Jedwali 36: Methali za Kiswahili kuhusu Mahusiano ya Malezi**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Jogoo halei mwana. |
| 2. | Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha mamaye. |
| 3. | Mkono mmoja haulei mwana. |
| 4. | Kuzaa ni shani ya Mungu, malezi ni wajibu wetu. |

Methali (1) imerejelewa kitaashira. Ndege na wanyama wana sifa ambazo zinaweza kutumiwa kufafanua tabia za binadamu. Jogoo ni kuku dume ambaye anabainika kutokuwa na jukumu la kulea wana. Kazi ya kulea wana ni ya koo (Wamitila, 2001). Jogoo amerejelewa kuwakilisha mwanamume kwa kuwa anatumia vishawishi kwa mwanamke kwa ajili ya kujiridhisha kimapenzi. Kitendo hiki ni kama jogoo anavyoonekana akidonoadonoa chakula huku akitoa sauti inayoashira kumwitia kuku chakula. Katika utamaduni wa Waswahili, jukumu la kulea watoto ni la wanawake. Kulingana na mhojiwa LMU 2 tarehe 16/05/2018, mume anatengewa majukumu mengine maalumu tofauti na ya malezi ya watoto. Kazi na majukumu maalumu ya mwanamume na mwanamke yanapata ukubalifu kulingana na matarajio ya jamii ya Waswahili. Ukubalifu huu unatokana na hadhi ya kiuana katika jamii ambapo mwanamume anatengewa majukumu yake ya kiume tofauti na majukumu ya malezi.

Kazi ya malezi inaamriwa na jinsi ya mtu kiutamaduni. Itikadi ya malezi katika methali (1) inabainisha kuwa kazi ya ulezi wa watoto ni ya mwanamke. Itikadi katika methali hii inaendeleza mahusiano ya utenganishaji wa jukumu hili kwa misingi ya kiuana. Itikadi hii ni kinyume na matarajio ya mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosisitiza wanawake na wanaume kushughulikia majukumu ya kijamii kwa kushirikiana. Kwa hivyo, mahusiano kati ya

mwanamume na mwanamke kama yanavyoendelezwa na itikadi hii kwa ukubalifu yanampatia mwanamke mzigo mkubwa wa kulea watoto. Kazi hii kubwa inawekwa katika mikono ya mwanamke pekee yake. Hatimaye, nguvu za mwanamke zinaendelea kunyonywa kwa sababu thamani ya juhudi zake haihesabiki. Mwanamume kubainika kama kiumbe ambaye hana uwezo wa kulea watoto, ni itikadi ya uendelezaji wa ubabedume. Kulingana na mhimili wa Nadharia ya Itikadi ambapo wanaume kama kundi linalowekwa mbele, linaendeleza uwajibishwaji wa wanawake kwa ulezi wa watoto kuwa ni jukumu lao kwa njia ya ushawishi. Wanawake nao wanajikuta wanakubali jukumu la malezi kuwa ni lao.

Pia, itikadi ya ulezi inaendelezwa katika methali ya (2). Methali hii inadai kwamba mtoto anapobebwa mgongoni huwa anaangalia kisogo cha mama yake. Methali hii inamaanisha kuwa mama ni mfano wa kuigwa na watoto kwa sababu watoto huwa wanafuata mienendo ya mama zao. Kulingana na methali hii mama ana jukumu la kuwaelekeza watoto kwa maadili mema na kuwaadabisha. Maisha na tabia za mama na mienendo yake inaathiri watoto kwa asilimia kubwa kwa maisha yao ya utu uzima. Itikadi ya ulezi inaendeleza mahusiano ya mwanamke kuwa ndiye anayepaswa kulea watoto kwa maadili mema na inaelekea kuweka masharti kuhusu mwanamke kuwajibika na kuwa makini katika malezi. Mwanamke anadhihirika kushawishika na kukubali jukumu hili la malezi kwa mujibu wa Nadharia ya Itikadi. Mwanamume huoneshwa kwa upande mwingine kujitenga na malezi. Mwanamke kama mama anatarajiwa kulea watoto kwa misingi ya jamii kiutamaduni. Kwa hivyo, methali inamhadharisha mama kwanza kuwa makini katika malezi ya watoto kwa kuwa mtoto huiga na kuelekezwa na

mienendo ya mama. Mwanamke aliye na sifa maalumu ya mama anatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa watoto kama jamii inavyomchukulia.

Malezi ya watoto yana mchango mkubwa katika kujenga familia na jamii kwa ujumla na yanahitaji juhudi za pamoja za wazazi wawili. Methali ya (3) ina maana ya kwamba malezi ya mtoto yanahitaji kutumia mikono yote miwili. Methali hii inawasilisha itikadi ya malezi ya mwana kuwa ni jukumu la wazazi wawili. Itikadi inayodhihirika katika methali hii inaendeleza mahusiano ya wazazi kushirikiana kwa malezi ya watoto. Maoni haya yanaendelezwa na Plaskow (2007) kwamba, wanaume wanaweza kutekeleza majukumu ambayo yanadhaniwa kuwa ya wanawake kiutamaduni. Katika utamaduni wa Waswahili, jukumu la kulea watoto linatengewa mama. Jukumu hili lina chanzo chake katika matarajio ya jamii kwa kuyahusisha na maumbile ya mwanamke katika kubeba mimba, kujifungua na kunyonyesha. Mhojiwa LMU 4 tarehe 17/05/2018 anaunga mkono madai hayo kwamba jukumu la malezi ya watoto ni la mama. Mhojiwa anaeleza zaidi kwamba, hata katika matembezi, kufanya kazi kama za kulima, mke anaonekana amebeba mtoto mgongoni pamoja na kuni kichwani ilhali baba hana chochote.

Ingawa methali (3) inabainisha haja ya kushirikiana kwa mwanamume na mwanamke kuhusu malezi, mwanamke anashawishika kwamba ndiye anayepaswa kushughulikia malezi ya watoto kama jamii inavyotarajia kiutamaduni. Methali hii inaonesha itikadi ya kiuana kwa mujibu wa Bressler (2007) kwamba ukubalifu wa watawaliwa bila kupinga ni mitazamo inayoonekana kuwa ya kawaida ilhali ilitengenezwa kwa lengo la kulinufaisha

kundi mahususi katika jamii. Itikadi kama inavyodhihirika katika methali hii inapingana na matarajio ya kiutamaduni kwa muktadha wa jamii ya Waswahili. Itikadi inabainisha haja ya wazazi wote kushirikiana katika malezi ya watoto. Mahusiano yanayoendelezwa ni kwamba mtoto ni wa mwanamke kwa malezi yake, tofauti na itikadi ya methali hii ambayo inaendeleza mahusiano ya wanaume na wanawake ya kushirikiana kwa pamoja katika malezi ya watoto. Kwa hakika ni vigumu kumlea mtoto kwa mkono mmoja, ndivyo ilivyo kwa malezi ya watoto. Methali hii inawasilisha itikadi ya ushirikiano katika kulea watoto na ni jukumu la wazazi wawili. Methali hii inapingana na imani kama inavyobainika katika jamii ya Waswahili kiutamaduni. Inaelezea uhusiano kimajukumu na ushirikiano wa wazazi wawili katika malezi ya watoto.

Methali ya (3) na ya (4) zinaendeleza itikadi ya kushirikiana kwa wazazi kuhusu malezi ya watoto. Methali hizi hazitenganishi jukumu la malezi kwa jinsi mahususi kati ya mwanamume na mwanamke. Ingawa, kiutamaduni majukumu ya mwanamume yapo na yanajulikana tofauti na malezi ya watoto. Majukumu ya kiume kulingana na utamaduni wa Waswahili ni pamoja na kuvua samaki, kufuga na kujenga. Kwa upande wa mwanamke, yapo majukumu yanayojulikana kama vile kushona na malezi ya watoto (Al Mwaawy, 2009). Mwaawy anasisitiza kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya mwanamke kulingana na utamaduni wa Waswahili ni malezi ya watoto. Aidha, methali inafafanua kwamba baada ya kubarikiwa kupata watoto, ni wajibu wa wazazi wote kulea watoto hao. Mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaafikiana na maoni yetu. Mhimili huu unasema kwamba wanawake na wanaume washughulikie majukumu ya kijamii kwa kushirikiana bila kuathiriwa na

majukumu ya kimaumbile. Itikadi kama zinavyobainika, zinaonesha haja ya mahusiano ya utegemeanaji kati ya mwanamume na mwanamke katika kuendeleza malezi ya watoto.

### 5.2.6 Itikadi kuhusu Mahusiano ya Nguvu, Mamlaka na Uongozi

Itikadi za kiuana na mifumo ya kiutamaduni katika jamii za Kiafrika zinaendelea kubainisha kuwa wanaume wanapaswa kuwa na mamlaka na uwezo wa kuongoza wanawake (Dzahene-Quarshie na Omari, 2021). Itikadi hii ya kiuana inapata ukubalifu na ushawishikaji wa wanawake wa kuendelea kutumikia nafasi zao kama kundi linalotawaliwa na kuwa viumbe wa daraja la pili katika jamii huku wanaume wakiwekwa kwenye nafasi ya mbele. Itikadi hii ya mamlaka na uongozi wa wanaume inadhihirishwa na methali za Kiswahili zifuatazo:

**Jedwali 37: Methali kuhusu Mamlaka ya Mwanamume**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Kichwa cha nyumba ni mume na shingo yake ni mkewe. |
| 2. | Kuku jike hawiki penye jogoo. |
| 3. | Mwanamke hukunjwa na mwanamume huvunjwa. |
| 4. | Udhaifu wa mume humpa mke kiburi. |

Kulingana na methali ya (1), kichwa ni sehemu ya juu ya mwili wa binadamu inayohimiliwa na shingo. Shingo ni kiungo cha mwili kilichopo kati ya mabega na kichwa kilicho na kazi ya kuhimili kichwa. Kwa maana nyingine, kichwa ni mtu anayepewa jukumu la kuongoza wengine katika familia (BAKITA, 2015). Katika methali hii mume anarejelewa kama kichwa cha nyumba na mke ni shingo. Kwa muktadha huo, mume ndiye anachukua nafasi ya uongozi katika familia tukirejelea maana ya pili ya kichwa kulingana na Kamusi Kuu ya Kiswahili. Mke kuwa shingo anachukua jukumu la kuhimili kichwa (mume) au

kusaidia kichwa katika kutekeleza majukumu yake. Kichwa hakiwezi kutekeleza kazi zake bila shingo na shingo haitatekeleza kazi yake bila kichwa. Mahusiano yanayooneshwa katika methali hii ni ya utekelezaji wa majukumu maalumu kwa njia ya ushirikiano. Maoni haya yanaungwa mkono na mhimili wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaodai utekelezaji wa majukumu ya kijamii wanaume wakishirikiana na wanawake bila kuathiriwa na majukumu ya kimaumbile. Katika kutekeleza majukumu haya, kunabainika utegemezi wa mume na mke katika kufanikisha majukumu hayo. Muhimu kuzingatia ni kwamba, mume hawezi kufanikiwa bila mke. Mwanamume kupendekezwa na jamii inayotawaliwa kwa mfumedume kuwa kichwa cha nyumba unaendeleza utawala, kujiashiria kwa mwanamume kuwa ni muhimu kuliko mwanamke.

Aidha, methali ya (2) inabainisha itikadi ya mwanamke kuwa hastahili kutoa sauti mbele ya mwanamume. Hata katika jumuia pana, mwanamke hapaswi na hawezi kuinua sauti yake; hawezi kuongea kwa sauti ya juu na hawezi kuongoza. Katika methali hii **k**uku jike analinganishwa na mke na jogoo analinganishwa na mume. Tunaporejelea kuku jike anakuwa na sifa za upole na unyamavu. Jogoo anakuwa na sifa ya kuwika. Mke akiwa na mume wake nyumbani au hadharani, hapaswi kutoa sauti mbele ya mume wake. Kulingana na mhojiwa LMU 4 tarehe 18/05/2018, mke hatarajiwi kujigamba mbele ya mume wake na kujifanya mbabe. Jamii inamtarajia mwanamke kuwa mtiifu, mnyamavu, mpole na msikivu kwa mume wake na wanaume wengine nje ya familia. Mume ndiye anapaswa kuwa na sauti ya juu mithili ya jogoo. Katika utamaduni wa Waswahili, mke anatarajiwa kuwa chini ya mume.

Mhojiwa ZNB 3 tarehe 25/05/2018 alidai kuwa, mwanamke akiwa na wanawake wenzake anaweza kutoa sauti, anaweza kuwa shujaa, anaweza kuongoza wanawake wenzake lakini akiwa na mume wake anapaswa kuwa chini yake kwa kumnyenyekea na kumtii. Maoni ya mhojiwa tunayakanusha katika mjadala huu. Kwa mujibu wa mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika binadamu wote wana haki sawa. Hakuna kiumbe ambaye anapaswa kuwa na nafasi ya kusema na kunyamazisha kiumbe mwingine. Vilevile, mwanamume kujipendekeza kuwa na uhuru wa kusema ni kujitakia makuu, kutaka kuendelea kutawala na kujiashiria kuwa ni muhimu kuliko wanawake.

Katika methali ya (3) mwanamke anastahili kulainishwa na kurekebishwa na mume wake. Mwanamke kiitikadi anapaswa kusimamiwa na mwanamume ili aweze kufanya mambo mazuri kama inavyotarajiwa na jamii. Mwanamke asiporekebishwa anaweza hata kuchangia uharibifu wa mwanamume. Mawazo haya yanaoneshwa katika kauli ya ‘kuvunjwa kwa mwanamume’. Mume anaweza kuwa na sifa nzuri lakini tabia mbaya za mke wake zinabadilisha tabia za mume.

Mhojiwa MSA 3 tarehe 11/05/2018 alisema kwamba kama mwanamke hawezi kuwajibikia majukumu yake kulingana na mila ya Waswahili, mume wake huwajibika kumtengeneza kulingana na jinsi anavyotaka na kutarajiwa awe. Mhojiwa aliendelea kusema kwamba kukunjwa kwa mwanamke ni kurekebishwa kwake kama tabia zake ni hazifai na hatekelezi majukumu yake ipasavyo. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika haikubaliani na itikadi hii ya kiutamaduni pamoja na maoni ya mhojiwa. Mhimili unaosema kwamba binadamu wote wana

hadhi sawa na haki sawa katika jamii unathibitisha hoja hii. Hakuna binadamu ambaye anapaswa kuwa na mamlaka juu ya binadamu mwengine kwa misingi ya kiuana. Itikadi katika methali hii inabainisha mahusiano ya mwanamume kuwa mwenye uwezo na mamlaka kuhusu mwanamke. Pia, tabia na mienendo ya mwanamke kuwa inamuathiri mume wake ama kwa kuchangia maendeleo yake au kutoendelea kwake ni itikadi ambayo inaendeleza utukufu wa mwanamume kwa upande mmoja na kulaumiwa kwa mwanamke kwa upande mwingine, mahusiano ambayo hayafai.

Kulingana na methali ya (4), udhaifu wa mume nyumbani unampa mke wake nafasi ya kuwa na kiburi. Itikadi inayodhihirika katika methali hii na vile inavyobainika katika utamaduni wa Waswahili, mume hatarajiwi kuwa dhaifu katika hali zote ndani na hata nje ya familia. Mwanamume anapaswa kuonyesha mamlaka yake kwa mke wake. Utamaduni wa Waswahili unaweka vigezo ambavyo vinamtambulisha mume. Vigezo hivyo ni pamoja na uwezo wake wa kuwajibikia majukumu yake, kuwa mwangalifu, kuridhisha mke wake kimapenzi, namna anavyozungumza na tabia zake. Maoni haya ni kwa mujibu wa mhojiwa LMU 1 tarehe 15/05/2018. Mume anapotekeleza mambo hayo atakuwa ameonyesha uwezo, hatimaye kuheshimiwa. Mume anapofanya kinyume na mambo hayo hatakuwa ametimiza wajibu wake na kutodhihirisha sifa za mume. Atachukuliwa kuwa dhaifu na kudharauliwa na mke wake na jamii. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, Itikadi za uana ambazo zinaonekana kutobadilika inafaa zitathminiwe kwa muktadha wa kijamii (Lomotey na Chachu, 2020). Itikadi kwamba wanaume wana mamlaka juu ya wanawake na ndio wanaopaswa kuwa kwenye nafasi ya uongozi ni mfumo wa kiutamaduni ulio na

misingi katika ubabedume. Itikadi hii ya kiubabedume haimpatii mwanamke fursa ya kuwa huru na kujitegemea. Anaoneshwa kuwa kiumbe anayepaswa kuwa chini ya mamlaka ya mwanamume. Plascow (2007) anadai kwamba mwanamume kuwa mwenye mamlaka na kuendeleza mahusiano ya kimabavu kwa mwanamke si jambo linalokubalika.

### 5.2.7 Itikadi kuhusu Mahusiano na Wakwe

Mahusiano na wakwe yanahitaji uangalifu sana. Mkwe katika mila za Waswahili huheshimiwa sana pengine kuliko wazazi wa upande wa mume. Methali zifuatazo zinaonesha mahusiano hayo:

**Jedwali 38: Methali kuhusu Mahusiano na Wakwe**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Chui naye ana mkwe. |
| 2. | Asemaye mengi hajui amemtukana mkwe. |

Katika methali ya (1), chui ni mnyama anayejulikana kuwa mkali na mwenye vitendo vya kikatili kwa wanyama wengine porini. Kuna binadamu ambao wana sifa kama za chui. Mtu wa aina hiyo, huwa ni mkali na anaogopwa. Katika uhusiano wa kindoa kuna wanaume ambao uhusiano wao na wake zao ni kama wa chui na wanyama wengine porini. Wanaume wa aina hii huwa wanaathiriwa na mielekeo ya kiubabedume. Mwanamume wa aina hiyo hata kama ni mkali namna gani, pia huwa na mke, hivyo atakuwa na wakwe. Mkwe katika mila za Waswahili huheshimiwa sana hata kuliko wazazi wa mume. Mke ndiye kiungo muhimu kati ya familia ya mume na ya kwao. Mhojiwa MSA 3 tarehe 11/05/2018 alisema kwamba, mume akimkosea mkwe wake na kumuudhi, huenda ndoa isidumu. Kwamba, anaweza kuzungumzia tabia mbaya za huyu mkwe wake kwa binti yake. Jambo hili linaweza kumuathiri binti yake na

kuyeyusha mapenzi yakena hatimaye kusababisha kuvunjika kwa ndoa. Pili, wazazi wa binti wanaweza kumshauri binti yao kuachana na mume mwenye tabia mbaya. Heshima hiyo inamfanya mume anayelinganishwa na chui kuwa mtiifu kwa wakwe zake. Mume akiendeleza ujabari wake atamkosa mke wake. Katika methali hii kiutamaduni, itikadi inayobainika inaendeleza haja ya kuwepo kwa heshima kati ya mume na wakwe zake. Heshima ni jambo la msingi katika kuleta na kuendeleza mahusiano ya amani na utulivu kati ya mume na mke pamoja na aila zao.

Pamoja na hayo, methali ya (2) inaendeleza itikadi ya heshima kwa wakwe. Methali hii inamaanisha kwamba, mume asemaye maneno mengi kwa kuropokwa, atajikuta amemtukana mama mzaa mke, yaani mkwe. Mume wa aina hiyo hatatambua kuwa amemtukana mama mkwe kwa sababu ya kupayukwa na maneno. Itikadi iliyomo katika methali hii ni kwamba, mtu anatakikana amheshimu sana mama mkwe. Anapaswa kuwa mwangalifu na achague ni maneno gani ya kusema na yepi yasiyostahili. Kulingana na maoni ya mhojiwa, kimila mume wa mke fulani hatakikani kuongea maneno mengi na mkwe wake kwa sababu anakuwa na heshima kubwa sana kwa aliweza kukupatia mke. Mahusiano yaliyopo ya mume na mama mkwe, yanadhihirisha ukinzani. Anaweza kufanya maisha yako ya kindoa kuwa mazuri au anaweza kukuharibia ndoa yako.

### 5.2.8 Itikadi za Kiuana kuhusu Mgawanyo wa Majukumu

Katika jamii ya Waswahili kitamaduni, wanawake wana shughuli zao maalumu za kike ambazo wanaziendeleza bila kuhusisha wanaume. Shughuli hizi

zinaendelezwa katika vikao vya wanawake peke yao (Gower, 1996). Hii ni ishara ya kuendeleza umoja wao kama kundi linalodhulumiwa na hatimaye kujiimarisha na kujiendeleza kama wanawake wenye lengo moja.

**Jedwali 39: Methali za Kiswahili na Mahusiano ya Utenganishaji wa Majukumu**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1 | Buibui ni mke. |
| 2 | Eda ya mke hakuna eda ya mume. |

Methali ya (1) katika utamaduni wa Waswahili, inaeleza kuwa buibui ni vazi la wanawake. Vazi hili linagubika mwili mzima na kuacha sura tu ili kusitiri viungo vya mwanamke. Kwa mujibu wa mhojiwa LMU 3 tarehe 16/05/2018, wanaume hawastahili kuingilia masuala ya kike kwa sababu wao si wanawake. Kwa upande mwingine, aliendelea kusema kwamba, nao wanawake hawaruhusiwi kushiriki kwenye mabaraza ya wanaume ambapo kunazungumziwa mambo ya kiume na wanaume. Katika mabaraza ya wanawake, kunazungumziwa mambo ya kike na ya wanawake hasa namna ya kuimarisha ndoa. Wanaume hawapaswi kujiingiza katika mambo hayo kwani hawana haja nayo. Itikadi hii inaendeleza mahusiano ya kutenganisha majukumu kati ya wanawake na wanaume. Mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake ni kwamba wanawake kama kundi, kuna mambo yao yajulikanayo kama ya kike. Mwanamke akiwa amevaa 'buibui' lake mmefichama mambo mengi ambayo yanajulikana kwake mwenyewe. Mwanamume kwa vile havai buibui hakuna namna atakavyojua mambo hayo ya ndani ya buibui hilo. Maelezo ya methali hii yanabainisha hali maalumu ya wanawake wanayokuwa nayo ambayo inafahamika kwao tu. Itikadi hii inaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi unaosema kwamba

wanawake wanapaswa kukuza na kuendeleza umoja wao kama kundi linalodhulumiwa. Umoja huu unaendelezwa kwa kupeana nguvu za kujitetea badala ya kutazamwa kama kundi linaloendeleza utawala wao kwa kupigana wao kwa wao. Mahusiano yanayoendelezwa ni kwamba wanawake wanapaswa kuendeleza umoja wao kama kundi lenye changamoto ambazo zinazotokana na kutawaliwa kwao kwa msingi wa ubabedume.

Vilevile, itikadi hii inaendelezwa zaidi katika methali (2). Maana ya methali hii ni kwamba, eda ni kipindi cha miezi mitatu au minne na siku kumi ambacho mwanamke anachopangiwa kukaa, ama akitalikiwa au akifiliwa mume wake katika utaratibu huo kabla ya kuolewa tena. Kwa hivyo, eda ni suala la wanawake peke yao na ndio wanaopangiwa kipindi hiki wala si wanaume. Kulingana na mhojiwa ZNB 2 tarehe 24/05/2018, kipindi hiki kinadhamiria kuangalia ikiwa mke huyo ana mimba ya aliyekuwa mume wake. Katika mahojiano na msailiwa wa kike, alisema kuwa methali hii inadhihirisha masuala maalumu ya wanawake ambayo hayawahusu wanaume. ‘Eda ya mke hakuna eda ya mume’ tunaonysha itikadi kwamba wanawake kama kundi linalodhulumiwa wana matatizo maalumu ambayo wanapaswa kukabiliana nayo kama wanawake. Mawazo haya yanaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaotarajia wanawake kujitambua katika uhusiano na wanaume. Utambuzi huu unawafanya kuendeleza umoja wao na hatimaye kujitetea.

**5.3 Hitimisho**

Mjadala kuhusu itikadi za kiuana umeweza kutoa hali halisi inayoelezwa katika methali kuhusu mahusiano ya kiuana kati ya wanawake na wanaume. Methali

zinadhihirisha kwamba itikadi shawishi inaendelezwa kwa mwanamke kuendelea kubainika kuwa chini ya mwanamume. Wanawake kuwasilishwa kama viumbe wasio na mamlaka na wategemezi ni itikadi inayotokana na amali za kifamilia na kijamii kwa njia ya ukubalifu. Shah na wenzake (2018) wanathibitisha hoja hii kwamba utawala wa kundi lenye mamlaka dhidi ya kundi tawaliwa unaendeleza mamlaka yake kwa kuwashawishi watawaliwa kuamini kwamba mahusiano yanayoendelezwa kati yao ni kwa manufaa yao, jambo ambalo si la ukweli.

Itikadi hii inabainisha namna wanaume wanavyotekeleza na kuhalalisha mamlaka yao juu ya wanawake na jinsi wanavyoendeleza nafasi yao katika jamii kupitia kwa ukubalifu wa wanawake katika methali za Kinyankole. Itikadi kama jambo la msingi katika utafiti huu, limekuwa kigezo cha kupima na kutathmini misimamo ya Wanyankole na Waswahili. Tumeweza kubainisha jinsi itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano kwa kushawishika na ukubalifu wa majukumu na hadhi ya wanawake. Utafiti unaona kuwa, ukubalifu wa utekelezaji wa majukumu, uendelezaji wa hadhi ya mwanamke na haki yake kati yake na mwanamume katika methali za Kinyankole na Kiswahili unasababishwa na namna wanavyoelewa na kuendeleza maisha kwa njia inayoonekana kuwa ya kawaida. Uelewa na uendelezaji wa maisha unaathiriwa na mfumodume ambao unajikita katika mila za kitamaduni.

# SURA YA SITA

# UKINZANI WA ITIKADI ZA KIUANA NA ATHARI ZAKE KATIKA METHALI ZA KINYANKOLE NA KISWAHILI

## 6.0 Utangulizi

Katika Sura ya Tano mtafiti amechunguza itikadi za kiuana zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Sura hii ya sita, mtafiti anajadili namna itikadi hizo za kiuana zinavyoibua ukinzani katika methali za Kinyankole na Kiswahili pamoja na kubainisha athari zake kuhusu usawa wa kiuana. Ukinzani katika sura hii umerejelewa kama ukweli mwingine unaoibuka kupinga ukweli uliopo au ukweli unaosemwa katika methali. Uhakiki wa methali katika sura hii unaongozwa na Nadharia ya Itikadi, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na Nadharia ya Udenguzi ili kuweza kudhihirisha ukinzani wa itikadi na athari zake katika methali za jamii tajwa, yaani za Kinyankole na Kiswahili.

## 6.1 Ukinzani wa Itikadi za Kiuana na Athari zake katika Methali za Kinyankole

Itikadi kinzani zinazojadiliwa katika methali ni zile zinazohusu masuala ya uzazi, malezi na utunzaji wa watoto, ndoa, wazazi wa kambo, uongozi, uzalishaji wa mali, uhuru, ukuzaji na maendeleo ya jamii. Methali hizi zinazopatikana kwenye kategoria moja na kuibua ukinzani ndizo zimejadiliwa. Ukinzani ni ukweli au kauli ambayo ni kinyume na jambo linalosemwa, au ni ukweli mwingine unaoibuka kupinga ukweli uliopo (Miller na Brown, 2013). Wanaendelea

kusema kwamba kauli mojawapo kati ya hizo zinazokinzana si sahihi. Nao Mbusya na wenzake (2018) wanauelezea ukinzani wa methali kama unyume wa kimaana unaoibuliwa na methali. Katika utafiti huu tumerejelea methali za Kinyankole na Kiswahili zenye maana inayokaribiana kuhusu itikadi za kiuana lakini kwa njia ya unyume. Tunazingatia jinsi maana na maelezo ya kiitikadi katika methali inavyopingana na kuwasilisha maana tofauti kuhusu mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake. Tumefanya hivi kwa kuzingatia ukweli kwamba methali ni utanzu wa fasihi simulizi ambao unawasilisha maana zaidi ya moja.

Hussein (2009) anasema kwamba methali kama ilivyo kwa matini nyingine zozote zenye maana pana, zinawasilisha maana tofautitofauti. Maana hizi hueleweka kulingana na muktadha wa jamii husika (Finnegan, 1970). Methali ni kivuli cha utamaduni ambao unaobadilika (Webster, 1982). Kwa hivyo, methali za Kinyankole na Kiswahili zimerejelewa kama kivuli cha utamaduni unaobadilika kwa kubainisha maana katika methali jinsi zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana. Aidha, itikadi ni dhana badilifu kulingana na maendeleo ya kijamii (Murithi, 2018). Kwa hivyo, maana inayowasilishwa katika methali si ile moja bali ni tofauti kulingana na muktadha wa matumizi. Kauli hii inaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Udenguzi unaosema kuwa, matini huwa na mielekeo mingi ya maana ambayo huibua fasili nyingi kutokana na jinsi maana za lugha zinavyopingana zenyewe. Pamoja na hayo, kulingana na Mieder (1989), mtu anatumia methali kulingana na mahitaji ya hali, na siyo kulingana na maana iliyozoeleka kwa wengi.

### 6.1.1 Suala la Ndoa

Ndoa ni mojawapo ya hatua kuu katika maisha ya watu wazima, awe mwanamume au mwanamke. Hii ni asasi muhimu ya utamaduni inayounganisha familia na koo pamoja na kuendeleza mila na jamii. Asasi hii inahitaji subira pamoja na kufanya uamuzi sahihi kwa sababu taasisi ya ndoa huwa na changamoto hasa katika Karne ya 21 kama Angela (2018) anavyoeleza. Aidha, Mutua na wenzake (2017) wanadai kuwa asasi ya ndoa inatumiwa kiitikadi kudhulumu wanawake. Kwa hivyo, uamuzi unaofanywa ni wa milele katika maisha ya mtu bali si kimbilio. Watoto wa kike waolewe kama wamekua ili waweze kuwa na mchango mkubwa wa kuhimili familia. Asasi ya ndoa kama asasi ya kiutamaduni ingawa inabainika kuwa muhimu katika jamii, ni mojawapo ya asasi ambazo zinaendeleza ubaguzi wa kiuana. Asasi hii inawapatia wanaume kipaumbele na kuwakandamiza wanawake. Wamitila (2002) anashadidia mawazo haya kwa kueleza kuwa ndoa ni asasi ambayo imeathiriwa na itikadi ya kwamba, wanaume wana uwezo zaidi kuliko wanawake. Hatimaye, itikadi hii inawafanya wanaume kukandamiza wanawake kuwachukulia kama chombo cha kuzaa, kuwatunza wanaume na kuwaridhisha kimapenzi **(**Mavisi, 2016).

Katika jamii ya Wanyankole, mtoto wa kike alilelewa na kuandaliwa kwa majukumu yake ya kuolewa. Mila hii inaendelezwa na itikadi za kiuana ambazo zinajikita kwenye mfumo wa kuumeni ambapo watoto wa kike lengo lao la msingi ni kuolewa. Mtoto wa kike alipoanza kumea meno, alikalishwa chini uani, mbele ya nyumba akitazama mbele. Mila hii iliashiria kwamba mtoto huyo ni msafiri wala si wa kukaa nyumbani kwa wazazi wake milele. Alipewa kitoma na kuambiwa kwamba bahati yake na mali yake ipo kwa mume wake mtarajiwa.

Kwa upande wa mtoto wa kiume, yeye alikalishwa kwa mgongo wa ng'ombe jike (mtamba) mmoja hadi mwingine kuashiria kwamba huo ni utajiri wake na baraka zake ziko hapo nyumbani kwa wazazi wake (Kirindi, 2008). Methali katika Jedwali Na. 40 zinazungumzia suala hili la ukinzani kuhusu ndoa:

**Jedwali 40: Methali Kinzani kuhusu Ndoa**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Enyamwonyo ku ekura eribwa omwishiki ku akura ashweerwa.* | Ndizi inapokuwa tayari huliwa msichana anapokua huliwa. |
| 2. | *Entorobo etari yaawe otoroboza not'omukanwa.* | Msichana mdogo asiye wako unamharibu bila huruma. |

Methali ya (1) inahusu itikadi kuwa msichana anapoolewa anatarajiwa kuwa amekua na kukomaa na kwamba yuko tayari kwa ndoa. Itikadi hii inabainika kwa kutumia analojia ya mkungu wa ndizi ambao unaliwa kama umekuwa tayari. Methali haipendekezi kula mkungu wa ndizi ambao ni mchanga. Ufananishaji wa msichana na mkungu wa ndizi iliyokomaa unaibua itikadi inayokinzana na maana ya itikadi katika methali ya (2). Itikadi katika methali ya (2) kwanza inadhihirisha mwanamume kuhusisha msichana mdogo kwa mapenzi; Pili, kudhihirisha kuwa kitendo hiki cha kinyama, mwanamke yupo kama chombo cha kuridhisha uchu wa mwanamume kimapenzi. Mwanamume anayeshirikisha msichana mdogo kwenye mahusiano ya kimapenzi anaonyesha kitendo cha ukatili, haonyeshi huruma kwake. Methali ya (1) inabainisha haja ya msichana kuolewa kama amefikisha muda ambao unafaa na yuko tayari. Methali hii inaendelea kudhihirisha haja ya mwanamume kuoa msichana ambaye amekua na yuko tayari.

Methali ya (2) inaeleza unyama wa mwanamume anaofanyia mtoto mdogo wa kike kwa sababu ya itikadi kwamba kiumbe cha kike kuwepo kwake ni kuishia mikononi mwa mwanaume kama mke. Wasichana kulingana na utamaduni wa Wanyankole, walipobaleghe walianza kufikiria ndoa kwa sababu itikadi ya ubabedume inawafanya waamini hivyo kwamba walipaswa kuolewa haraka. Methali hii inabainisha mwanamume anayeishia kuharibu 'toroboza' msichana mdogo kwa sababu ya athiri ya itikadi kuwa, kiumbe cha kike hitama yake ni kufanya ngono naye bila hata kuzingatia umri na madhara yanayoambatana na kitendo hicho kwa madai ya kutokuwa mtoto wake mradi si maharamu. Methali inabainisha itikadi ya unyama wa mwanamume, kutokuwa na huruma kwa msichana mdogo ambaye si mtoto wake wa damu. Hajali kuhusu madhara yanayompata msichana mdogo wala kumhurumia kwa sababu si mtoto wake.

Mwanamume anaendelea kuwa na mahusiano ya kimapenzi na msichana mdogo kwa madai kuwa hana uhusiano naye. Chanzo cha ukatili huu ni taasubi za kiume ambazo zinachukulia kiumbe cha kike kama chombo cha mapenzi kwa mwanamume bila kujali madhara ya mtoto mdogo wa kike. Mtoto mdogo ambaye hajakuwa tayari na hajafikisha umri wa kuolewa hata kama mwanamume hana uhusiano wa damu naye hafai kuharibiwa maisha. Methali hii inawasilisha itikadi ambayo inapingana na itikadi nyingine katika methali ya Kinyankole (1).

Methali tofautitofauti za Kinyankole kuhusu suala la ndoa zinamtarajia msichana kuharakisha kuolewa ili aishi na mume. Katika methali ya (1), itikadi inayowasilishwa inabainisha haja ya msichana kuolewa akiwa ameshafikisha umri wa kuolewa. Methali ya (1) inakinzana na methali ya (2) ambayo

inaonyesha mwanamume ambaye anashirikisha msichina mdogo katika mapenzi ambaye hajatimia. Ukinzani wa itikadi katika methali hizi unaonyesha kuwa mwanamke ni kifaa cha kuridhisha uchu wa mwanamume. Vitendo hivi vya kiunyama havina nafasi katika mahusiano ya kiuana kati ya mwanamume na mwanamke. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inashadidia mawazo haya kwenye mhimili wake unaosema kwamba tabia za uana ambazo zinadhalilisha wanawake kwa misingi ya maumbile yao hazifai. Mwanamke katika methali (2) anadhulumiwa na kudunishwa katika jamii.

### 6.1.2 Suala la Ndoa za mitala

Hardy (1994) anabainisha kuwa ndoa za mitala ni amali ya kiutamaduni inayoendelezwa wanaume ili kuweza kuwatawala wanawake nyumbani. Ndoa hizo zinawafanya wanaume kuwa na mamlaka dhidi ya wanawake kwa kuwatawala na kuwadhibiti. Mawazo haya yanaafikiana na maoni ya Nadharia ya Itikadi ambayo inawafanya wanawake kuchangia utawala wao bila kupinga. Methali zifuatazo za Kinyankole zinawasilisha ukinzani wa itikadi za kiuana ambao unaathiri usawa wa kiuana kama ifuatavyo:

**Jedwali 41: Methali Kinzani kuhusu Ndoa za Mitala**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Abakazi abashweire hamwe nigo mahari.* | Wanawake waolewao pamoja ndio wivu. |
| 2. | *Enkoni etaire mukabaro kwogireeba ogirenzya irembo.* | Bakora itumiwayo kupiga mkemwenza ukiipata unaitupa mbali. |
| 3. | *Ekibaaju okitega nyoko kizarwa mukasho.* | Unayotarajia kutoka kwa mama yako unayapata kutoka kwa mama wa kambo. |
| 4. | *Ku ogaya obukono bukye bwa nyoko ebikono ebihango bya mukasho bikweshumba ohendeka* | Unapodharau mikono midogo ya mama yako, mikono mikubwa ya mama wa kambo inakuepa na kuanguka chini. |

Methali ya (1) inawasilisha itikadi ya wivu ambao unaendelezwa na wanawake ambao wameolewa pamoja. Wanawake hao huendeleza chuki na uhasama kati yao na hivyo kutoishi kwa amani.  Hawatakiani mazuri; wanaoneana wivu. Itikadi inayoelezwa katika methali hii inasababishwa na mila ya Kinyankole ya wanaume kuoa mke zaidi ya mmoja kwa ajili ya kuhudumiwa. Katika methali ya (1) tunadhihirishiwa itikadi ya kutopatana kwa wakewenza. Ukinzani wa itikadi ya kiuana kuhusu wakewenza unaibuliwa na methali ya (2). Methali (1) inabainisha na kusisitiza mzozano wa wakewenza ambapo wanaendeleza uhasama kati yao kwa ajili ya kutaka umaarufu kwa mume wao. Methali ya (2) inabainisha umoja wa wakewenza na kuibua ukinzani wa itikadi maafuru ya chuki na uhasama wa wakewenza. Dipio (2019) anatambua kwamba wakati mwingine wakewenza wanatambulika kuwa wanaunganishwa pamoja na hali ya kuolewa na mume mmoja.

Wakewenza wanajulikana kwa kushindania mume, kuoneana wivu na kuchukiana. Itikadi inayoelezwa katika methali (1) ni ya chuki kati ya wakewenza. Methali (2) inaonesha mkemwenza ambaye anachukua bakora ya mume wao na kuitupa mbali. Kitendo hiki kinatokana na itikadi ya ubabedume kuwa wanawake wanapaswa kuwa chini ya wanaume kama watawaliwa, kiasi hata cha kuwachapa viboko. Mke mmoja anatambua dhuluma za mume wao kwa mke mwenzake. Pia, anatambua kuwa mtesi wao ni mwanamume.  Hivyo, mkemwenza anapopata bakora hiyo inayotumiwa na mume kupiga mke mwenzake anaitupa mbali ili isije ikatumiwa tena kuwapiga. Kutupa bakora ni kitendo cha kupinga dhuluma na unyanyasaji wa mume anaowafanyia. Mke huyo anatambua kuwa naye atapigwa baada ya mwenzake.  Pamoja na hayo, kitendo

hiki kinaashiria juhudi za pamoja na kuungana kwa wanawake ili kuweza kujitetea mbali na tofauti kati yao ndani ya familia. Mawazo haya yanaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambao unasema kwamba, wanawake wanapaswa kukuza na kuendeleza umoja wao kama kundi linalodhurumiwa kwa kuchangiana nguvu za kujitetea badala ya kutazamwa kama kundi linaloendeleza utawala wa wanaume ilhali wao wakipingana. Mkemwenza anatambua haja ya kuungana na kusaidia mwenzake na kujisaidia mwenyewe. Aidha, kitendo hiki kinaonesha huruma na kujaliana kati ya wakewenza hawa, tofauti na jinsi wanabainishwa na methali ya (1) kuwa wao ni viumbe ambao hawapatani abadani ndani ya ndoa. Itikadi katika methali ya (2) inapingana na itikadi katika methali ya (1).

Methali ya (3) inazungumzia ukinzani katika ndoa za mitala kwa kumrejelea mama wa kambo. Suala la mama wa kambo linaibuka katika itikadi ya mfumodume, ambao unachagiza wanaume kuoa mke zaidi ya mmoja (Baruah, 2008). Mama wa kambo katika jamii nyingi ulimwenguni husifika kwa maovu na kuwanatesa watoto wa kambo (Bahn na Hong, 2019). Itikadi za kumsawiri mama wa kambo zimeendeleza chuki bila sababu za msingi. Methali ya (3) inaibua ukinzani wa itikadi za kiuana kuhusu mama wa kambo. Inaeleza kwamba, mambo mazuri ambayo unayataka au kuyatarajia kwa mama yako mzazi badala yake yanapatikana kwa mama wa kambo. Maelezo ya methali hii yanabainisha itikadi ya mchango na nafasi chanya ya mama wa kambo. Itikadi hii inampa sifa chanya mama wa kambo na kuonesha umuhimu wake katika kuendeleza familia. Nadharia ya Mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosisitiza usawa wa binadamu katika masuala ya utamaduni na uana ambapo jamii inapaswa

kuendelezwa kwenye misingi ya amali za kibinadamu unaunga mkono itikadi hii. Hii ni kudhihirisha ubinadamu wa mama wa kambo kinyume na inavyochukuliwa na jamii nyingi.

Athari ya ukinzani huu kuhusu usawa wa kiuana ni kwamba kuna haja ya kushirikiana kwa wakewenza kwa ajili ya haki zao za msingi. Mhimili wa nadharia ya Usawa wa kiuana unaounga mkono mawazo haya ni ule unaosema kwamba, wanawake wanapaswa kukuza na kuendeleza umoja wao kama kundi linalodhurumiwa. Jambo hili linaendelezwa kwa kupeana nguvu za kujitolea badala ya kutazamwa kama kundi linaloendeleza kutawaliwa kwao kwa kupigana wao kwa wao. Aidha ushirikiano huu wa wakewenza unahitajika kwa ajili ya maslahi ya watoto wa kambo.

Itikadi ya uadui wa mama wa kambo unaendelezwa kwa mfano wa methali ya (4) Methali inamwonesha mama huyu kama mtu mwenye hila, mwovu, mwenye chuki, anayeendekeza vitendo vya kutesa watoto asiowazaa. Uhusiano huu unaendeleza kudhalilika kwao na hatimaye kuendelea kukaliwa na wanaume. Methali hii inamsihi mtoto kutegemea uwezo mdogo lakini wa dhati kutoka kwa mama yake kuliko kutegemea uwezo mkubwa wa mama wa kambo ambaye hawezi kumfaa. Kulingana na itikadi hii, mama wa kambo anarejelewa kama katili ambaye hafai kuaminika kwa malezi na utunzaji wa watoto wa mkemweza. Itikadi hii ya kutoamini mama wa kambo katika methali hii inakinzana na itikadi inayoibuliwa katika methali ya (3).

### 6.1.3 Suala la Mke kumtii Mume

Wanawake wanabainishwa katika methali kuwa viumbe ambao wanapaswa kuwatii, kuwanyenyekea, na kuwafurahisha wanaume katika ndoa. Itikadi hii inadhihirika katika jamii nyingi za Kiafrika. Mawazo haya yanaendelezwa na Mwamzandi (2016) akirejelea Utenzi wa Mwana Kupona (1858). Anasema kwamba Mwana Kupona anamwelekeza mtoto wake wa kike namna ya kumtunza mume wake kwenye asasi ya ndoa. Itikadi hizi zinashinikizwa na mila za jamii zinazoathiriwa na mfumo dume. Momanyi (2007) anabainisha kuwa itikadi hii inaendeleza dhuluma kwa wanawake ilhali wanaume wanapaswa kuendeleza muamana mzuri kati yao na wanawake. Muamana huu ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha utangamano wa kijamii kuliko wanawake kuendelea kutambuliwa kama raia wa daraja la pili na kudhulumiwa. Wanawake nao wanachangia kwa kiasi kikubwa kuleta amani katika jamii; kwa hiyo, kuna haja ya kuheshimiana baina ya pande hizi mbili. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, wanawake kwa wanaume wanapaswa kuwa na haki sawa kwenye ndoa. Hivyo, yawapasa kuwasilisha mawazo yao kwa njia huru, kuwajibikia majukumu bila kutegemea hali za kike au kiume pamoja na kuchangia mawazo bila ya kuwa na vizuizi vinavyosababishwa ukandamizaji wa kiuana. Itikadi katika methali zifuatazo katika jedwali Na. 44 inaonyesha ukinzani kuhusu mahusiano ya wanaume na wanawake.

**Jedwali 42: Methali Kinzani kuhusu Mke Kutii Mume**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omukazi omira ekiniga amira engundu yeiba.* | Mwanamke amezaye ghadhabu humeza pandikizi la mume wake. |
| 2. | *Omukazi otaine bwengye asheka iba aine ekiniga.* | Mwanamke mjinga hucheka mumewe akiwa amekasirika. |

Methali ya (1), inadhihirisha kuwa mke hatarajiwi kukasirika au kuonesha gadhabu kwa mume wake. Itikadi hii inamshawishi mke kukubali nafasi yake ya unyamavu kuwa kama njia ya kumdhibiti mume wake hata kama ni mkali kiasi gani. Methali ya (2) inabainisha itikadi ya mke ambaye anamdhihaki mume wake wakati ana hasira. Mke wa aina hiyo anarejelewa kama mjinga. Itikadi katika methali hii inadhihirisha ushawishi kuwa mwanamke anapomdhihaki mume wake wakati amekasirika atarajie kuadhibiwa. Ushawishi wa itikadi katika methali hii kwa mujibu wa mhimili wa Nadharia ya Itikadi unadhihirisha kwamba mwanamke anaikubali hali hii kuwa ya kawaida na kuendeleza unyamazishaji na utiifu kwa mume wake. Aidha, methali hii inambainisha mwananamke akipinga itikadi ya unyamazishwaji. Wanaume wanajua kwamba wanawake kama kundi linalodhulumiwa wanaweza kupinga unyanyasaji huo. Ili kuendeleza utiifu wa wanawake, wanaimarisha itikadi hii kama juhudi za kimakusudi za kuwafanya wanawake kushawishika kukubali nafasi hii bila juhudi za kutumia nguvu. Licha ya mke wa aina hii kuonesha uwezekano wa mwingiliano huru na mume wake, hapendelewi na anachukuliwa kama mjinga. Mwanamke kuitwa mjinga ni njia ya kumdhalilisha ili ashawishike kukubali nafasi yake ya usikivu na utiifu kwa mwanamume. Methali ya (1) inadhihirisha itikadi inayopendelewa na wanaume kwa mujibu wa mfumodume na inamsifia

mwanamke kwa kuwa na unyamavu kama njia ya kumdhibiti mume wake. Methali ya (2) inadhihirisha itikadi inayokinzana na matarajio yanayolenga kuendeleza utawala wa wanaume. Mwanamke anapobainika kupinga matarajio ya mila ya kiutamaduni ya kuwa mnyamavu mbele ya mume wake anarejelewa kuwa mjinga. Huu ni ukinzani unaoibuliwa na umeweza kubainisha upendeleo kwa wanaume ili waonekane kuwa juu ya wanawake.

### 6.1.4 Suala la Uzazi

Itikadi ya uzazi hasa upatikanaji wa watoto wengi ni jambo ambalo jamii inayoongozwa kwa amali za ubabedume inawatarajia wanawake kuwajibikia. Watoto ni shani ya Mungu. Mahenge (2008) anasema kwamba watoto ni baraka anayopewa mtu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Methali katika jamii nyingi za Kiafrika zinabainisha kuwa wanawake wanapaswa kuwa na uwezo wa kuzaa watoto wengi. Aidha, itikadi za kiuana za kiutamaduni zinabainisha upendeleo wa kuzaa watoto wa kiume kuliko watoto wa kike (Kiyimba, 2005; Sanaudin, 2015). Watoto wa kiume wanapendelewa kwa sababu ya kuimarisha, kupanua na kuendeleza ukoo wa upande wa mume. Watoto wa kiume wanabaki na wazazi wao na kuwatunza wakiwa wazee. Katika jamii ya Wanyankole itikadi hii ipo ambapo mke ndani ya ndoa anatarajiwa na kushawishika kuzaa watoto wengi. Hata hivyo, kuna itikadi inayowasilisha unyume na kuangalia kitendo chenyewe cha kuzaa kuwa ni hatari kwa mwanamke. .Methali za Kinyankole zinabainisha itikadi kinzani kuhusu suala hili la uzazi. Ukinzani unajadiliwa katika Jedwali la 43:

**Jedwali 43: Methali Kinzani kuhusu Itikadi ya Uzazi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omwana omwe tamara nyina obugumba.* | Mtoto mmoja haondolei mamake utasa. |
| 2. | *Okuzaara kwita abakazi.* | Kuzaa huua wanawake. |
| 3. | *Omukazi owoyesiga takuzarira mwojo.* | Mwanamke unayemwamini hakuzalii mtoto wa kiume. |
| 4. | *Boona baana.* | Wote ni watoto. |

Methali ya (1), inazungumzia mwanamke anayezaa mtoto mmoja. Inaeleza kwamba mtoto mmoja hamuondolei mwanamke utasa. Mwanamke mwenye mtoto mmoja analinganishwa na tasa. Neno tasa linawasilisha maana ya kiumbe wa jinsi ya kike ambaye hana uwezo wa kutunga mimba na kuzaa (BAKITA, 2015). Hata hivyo, kiuhalisia, mwanamke mwenye uwezo wa kuzaa mtoto mmoja hawezi kulinganishwa na mwanamke tasa. Kulingana na maana ya msingi, jinsi neno tasa linavyotumiwa katika methali, linaibua ukinzani dhidi ya maana ya msingi iliyozoeleka. Mhimili wa Nadharia ya Udenguzi unaosema kwamba, matini huwa na mielekeo mingi ya maana ambayo huibua fasili nyingi kwa sababu ya maana za lugha kupingana zenyewe. Tumefikia maana hii kwa kuhakiki ukinzani wa matumizi ya 'mama wa mtoto mmoja' na 'mwanamke tasa' katika methali moja. Itikadi inayobainika katika methali hii inaibua ukinzani kuhusu haja ya wanawake kuzaa watoto wengi kuwa ni itikadi shawishi ya wanaume. Kwa mujibu wa mhojiwa KRH 4 tarehe 18/04/2018, katika utamaduni wa Wanyankole, mwanamke tasa anapofariki anapitishwa kwenye mlango wa nyuma ya nyumba akipelekwa kuzikwa. Kwa upande mwingine, mwanamke aliyewahi kuzaa mtoto hata kama ni mmoja anapitishwa kwenye mlango wa mbele wa nyumba. Kitendo hiki kinaashiria heshima kwa mama aliyewahi kuzaa.

Kwa hivyo, itikadi hii kulingana na mila ya Wanyankole inaibua ukinzani wa itikadi inayowasilishwa katika methali hiyo ya (1).

Aidha, methali hii ya (1) inaendeleza ukinzani wa itikadi katika methali (2) kuhusu suala la uzazi. Mwanamke anaposhawishika na itikadi ya kupaswa kuzaa watoto wengi, methali (2) inaeleza itikadi kwamba, tendo la kuzaa na upatikanaji wa watoto ni hatari kwa mwanamke. Wanawake kuzaa watoto kunahatarisha maisha yao, na pengine hata kusababisha vifo vyao. Itikadi hii inakinzana na itikadi ya haja ya kuzaa watoto wengi kama inavyodhihirika katika methali ya (1).

Isitoshe, itikadi katika methali (1) pamoja na kuonysha haja ya mwanamke kuzaa watoto wengi, haibainishi jinsia ya watoto ambao mwanamke anapaswa kuzaa. Itikadi hii ni tofauti na jinsi imejadiliwa katika methali ya (3). Methali katika jamii nyingi zinabainisha upendeleo wa wanawake kuzaa watoto wa kiume kuliko  wa kike. Lugano (1989) anasema kuwa wanawake ambao wanazaa watoto wa kiume wanapendelewa katika tamaduni za Kiafrika kuliko watoto wa kike. Anaendelea kudai kuwa wanawake wanapozaa watoto wa kike pekee wanalaumiwa. Aidha, mwanamke asipopata mtoto kabisa pia analaumiwa. Itikadi hii inaendelezwa kwa ukubalifu na kuchukuliwa kuwa jambo la kawaida. Itikadi ya kuwachukulia watoto wa kike kuwa hasara inaendelezwa na Kiyimba (2006) na Sanauddin (2015) ambao wanakubaliana na madai kuwa watoto wa kike wakiolewa wanachangia maendeleo kwa upande wa mume na wanakuwa sehemu ya familia za wanaume wanakoolewa.

Methali ya (3) inamtarajia mwanamke kuzaa watoto wa kiume. Wanawake ambao walishindwa kuzaa watoto wa kiume kwa waume zao katika jamii ya Wanyankole, walichukuliwa kuwa wasaliti kama itikadi inavyoelezwa katika methali hii ya (3). Mwanamke kutozaa watoto wa kiume kwa mume wake, kulisababisha mwanamume kuoa mke mwingine ambaye alitarajiwa kuzaa watoto wa kiume. Methali hii inawasilisha maana ya kinyume na methali ya (4) ambayo haizingatii kuzaa jinsi fulani mahususi. Methali ya (4) inabainisha itikadi kwamba, haidhuru kuzaa watoto wowote bila kuzingatia jinsi zao. Jambo muhimu linalodhihirishwa katika methali hizi ni upatikanaji wa watoto. Itikadi hii inabainisha kuthamini kila mtoto anayezaliwa bila upendeleo wa jinsia fulani. Kulingana na itikadi inayowasilishwa katika methali hii, watoto wote ni sawa isipokuwa tofauti zao za kimaumbile.

Ukinzani unaodhihirika katika methali ya (2) unaonesha kwamba suala la uzazi kwa wanawake ni shughuli ambayo inahatarisha maisha yao. Itikadi ya kuwatarajia wanawake kuzaa watoto wengi jinsi inavyobainishwa katika methali ya (1) haizingatii madhara yanayoambatana na uzazi kwa wanawake. Ukinzani wa itikadi unapendekeza kujihadhari na kuzaa hasa upatikanaji wa watoto wengi kama itikadi inavyomtaka mwanamke katika methali ya (1). Uzazi na upatikanaji wa watoto una madhara yake. Mwanamke hapaswi kuchukuliwa kama karakana ya kuzaa watoto dhidi ya maisha yake. Katika Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mhimili unasema kwamba wanawake wazinduke na kubadili mielekeo hususani jinsi wanavyojiona katika uhusiano na wanaume. Mhimili huu unaungwa mkono na itikadi kinzani katika methali ya (2). Ukubalifu wa itikadi ya kuzaa watoto wengi kama inavyopendelewa na wanaume ni mojawapo ya

mielekeo ambayo inapaswa kubadilishwa na wanawake wenyewe kwa sababu inaendeleza ukandamizaji wao.

Aidha, itikadi ya kuwataka wanawake kuzaa watoto wa kiume katika methali ya (3) inapingwa na itikadi katika methali ya (4). Jamii inayotawaliwa kwa misingi ya ubabedume, inapendelea kuzaa watoto wa kiume kuliko watoto wa kike (Sanaudin, 2015). Watoto wa kike wanachukuliwa kuwa wasio na thamani na hawachangii maendeleo kwa wazazi wao bali wanachangia maendeleo kwa waume zao. Methali ya (4) inakanusha madai haya ambapo inadhihirisha itikadi ya kwamba watoto wa kike na wa kiume wana hadhi sawa. Maoni haya yanaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba jamii iendelezwe kwenye misingi ya amali za kibinadamu bila kuzingatia maumbile. Ukinzani huu vile unadhihirisha itikadi ya kuthamini watoto wote wanaozaliwa bila upendeleo inapatia mtoto wa kike haki sawa na mtoto wa kiume, tofauti na itikadi shawishi ya ubabedume inayoendeleza kuthamini watoto wa kiume. Itikadi ya kupendelea watoto wa kiume ina uelekeo wa mantiki ya chini. Kulingana na mhojiwa wa 12, watoto wa kike wanahimili familia za wazazi wao kuliko watoto wa kiume katika hali fulani kwa sababu watoto wa kiume wakishaoa wanakabiliana na majukumu ya familia zao na kutelekeza wazazi wao.

Kuhusu kipengele hiki cha uzazi, tumeweza kuhakiki methali za Kinyankole na kuibua ukinzani wa itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya wanawake na wanaume ya kuzaa watoto. Kutokana na methali hizi, imebainika wazi kuwa jukumu la wanawake la kuzaa watoto wengi ni ushawishi wa itikadi za kiuana

ulio na msingi katika mfumodume. Methali ambazo zinakinzana na itikadi hii zimebainishwa. Methali hizi kinzani zimeonesha kuwa licha ya itikadi nyingine kuwataka wanawake kuzaa idadi kubwa ya watoto, suala hili linahatarisha maisha yao. Pia, itikadi ya wanawake kutarajiwa kuzaa watoto wa kiume inaibua ukinzani kama ilivyochanganuliwa hapo juu. Methali hizi zimeweza kuwasilisha unyume wa itikadi ambapo hazibainishi upendeleo wa kuzaa watoto wa jinsi moja dhidi ya nyingine. Methali ambazo zinaeleza itikadi za kuzaa watoto wa kiume zinaathiriwa na mfumodume katika jamii ya Wanyankole. Wanawake kwa wanaume wanalikubali suala hili la kuzaa watoto kuwa la wanawake na wanalichukulia kama jambo la kawaida kwao lakini si sahihi. Aidha, tumeweza kuonesha kuwa ukinzani wa itikadi unaoibuliwa unaathiri usawa wa kiuana.

### 6.1.5 Suala la Malezi

Ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole kuhusu uzazi unaonesha changamoto zinazoambatana na uzazi kwa wanawake. Pia, watoto wote wanaoletwa duniani na wazazi wao ni sawa na wana haki sawa licha ya wanaume wa Kinyankole kutarajia wanawake kuzaa watoto wengi na kupendelea uzazi wa watoto wa kiume. Suala la uzazi linambatana na malezi ya watoto wanaozaliwa. Salem (2013) anaeleza kwamba malezi ya watoto na kuwatunza ni jukumu la wanawake. Methali za Kinyankole zinazobainisha itikadi ya malezi ya watoto kwa wanawake zipo. Hata hivyo, kuna methali za Kinyankole ambazo zinaibua ukinzani wa itikadi hii. Ukinzani huu wa itikadi za kiuana unabainisha jukumu la malezi ya watoto kwa wazazi wa kiume na wa kike kwa kushirikiana. Itikadi hii inaelezwa katika Jedwali Na. 44 kama ifuatavyo:

**Jedwali 44: Methali kinzani kuhusu itikadi ya malezi ya watoto**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1.<br>2. | *Omuzaire arangwa engozi*<br>*Akaana keiba kajumisa nyinako* | Mzazi hutambuka kwa mbeleko.<br>Mtoto mwizi hutukanisha mama yake. |

Methali ya (1) inaeleza itikadi ya mzazi kutambulishwa na mbeleko. Mbeleko inabainisha wajibu wa mzazi katika malezi. Mhojiwa SHM 4 tarehe 21/04/2018 alidai kwamba mzazi anayetambulishwa na mbeleko ni mzazi wa kike. Kwamba, mbeleko inahusishwa na jukumu la malezi ambalo ni la mwanamke. BAKITA (2015) wanafasiri neno mzazi kuwa ni baba au mama wa mtu yeyote. Pia, neno mbeleko linafafanuliwa kiishara kulingana na nadharia ya udenguzi kwamba lugha ina utelezi na inajidengua. Kwa mujibu wa nadharia hii kwa hivyo, neno mbeleko linajidengua na kuwa na dhima ya ishara ya kurejelea wazazi wote. Kwa hivyo, kuna mzazi wa kike na mzazi wa kiume ambao wanarejelewa katika methali hii. Kwa hivyo, Itikadi inayobainika katika methali hii inahusisha suala la malezi ya mtoto na wazazi wa pande zote tukirejelea dhima ya viashiria mzazi na mbeleko. Matumizi ya neno mbeleko yanasimamia suala la malezi na malezi hayo ni wajibu wa wazazi pande zote yaani mzazi wa kiume na mzazi wa kike. Methali ya (2), inawajibisha mwanamke kwa malezi watoto. Kulingana na muktadha huu, methali ya (1) jinsi inavyowasilisha itikadi ya kuwajibisha wazazi wote wawili kwa malezi ya watoto inaibua ukinzani na methali ya (2) ambayo inawajibisha na kutenga jukumu la malezi ya watoto kwa mzazi wa kike.

Maana kinzani inayoibuliwa katika methali ya (1) kwa kujidengua inaonyesha kuwa nafasi ya malezi ya watoto ni kwa wazazi wote wawili. Itikadi kinzani

katika methali (1) inaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaodai kuwa wanaume na wanawake washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana bila kuathiriwa na majukumu ya kimaumbile. Itikadi inayoibuliwa katika methali ya (1) inadhihirisha haja ya usawa wa kiuana kuhusu ushirikiano katika jukumu la malezi kwa mzazi wa kiume na mzazi wa kike. Ushirikiano kuhusu jukumu la malezi vile linabainika katika methali hii linaimarisha usawa wa kiuana ilio na msingi kwenye haki za binadamu, tofauti na itikadi katika methali ya (2) inayomtengea mwanamke malezi ya watoto. Kuhusu kipengele hiki cha malezi na kutunza watoto, methali zinazowawajibisha wanawake kwa malezi ya watoto zinaibua maana mpya ambayo inabainisha malezi ya watoto kuwa jukumu la wazazi wote wawili kinyume na itikadi zinazotenga malezi ya watoto kwa mama mzazi.

### 6.1.6 Suala la Uongozi na Mamlaka

Mwanamke hakutarajiwa kuwa kwenye nafasi za uongozi katika tamaduni mbalimbali za kiasili barani Afrika (Maitaria na Momanyi, 2016). Alipaswa kuwa kwenye nafasi ya kuelekezwa na kuongozwa na mwanamume. Mwanamke aliweza kupata fursa ya kuongoza tu kama mwanaume hakuwepo. Itikadi hii imedhihirika katika methali za Kinyankole ambazo zimejadiliwa katika sura za awali. Methali zinaendeleza itikadi zinazowabainisha wanaume kama wenye uwezo, wenye mamlaka na wenye nguvu dhidi ya wanawake. Shah na wenzake (2018) wanasema kwamba wanaume wanahalalisha mamlaka na uwezo wao kupitia semi zinazoakisi mfumodume. Tofauti na itikadi hizo, uhakiki wa mifano ya methali za Kinyankole umeweza kuibua ukinzani wa itikadi kuhusu uongozi pamoja na methali zinazobainisha itikadi kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye

hana mamlaka na anayepaswa kuongozwa. Methali hizo za Kinyankole katika Jedwali Na. 45 ni hizi zifuatazo:

**Jedwali 45: Methali Kinzani kuhusu Uongozi na Mamlaka**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omushaija ahatari omukazi acwa orubanza.* | Pasipo na mwanamume, mwanamke huamua kesi. |
| 2. | *Omukazi tatiiza ngundu ya iba.* | Mwanamke hatoi fahali wa mumewe. |
| 3. | *Omushaija tahinduka aharurimi, ahinduka ahakitanda.* | Mwanamume hageuki kwa ulimi, hugeuka kitandani. |
| 4. | *Abashaija tibagaywa.* | Wanaume hawadharauliwi. |
| 5. | *Akashaija kakye okayira nseeri.* | Mwannamume mdogo hudharauliwa mbali. |

Methali ya (1) inamaanisha kwamba mwanamke anakuwa na mamlaka ya kutekeleza maamuzi kama hakuna mwanamume. Kwanza, methali hii inaibua ukinzani kati ya sehemu zake mbili. Upande wa kwanza wa methali unaonesha kutokuwepo kwa mwanamume kunampa fursa mwanamke kuamua kesi. Nafasi hii ya mwanamke kuamua kesi inabainishwa na sehemu ya pili ya methali. Kulingana na methali hii, mwanamke ana uwezo wa kuamua kesi. Itikadi katika methali hii kuhusu uwezo wa mwanamke kuamua kesi wakati mwanamume hayupo, ina maana pia anaweza kuamua kesi hata mwanamume anapokuwepo. Uwezo huu wa mwanamke kuwa na nafasi sawa na mwanamume unasisitizwa na Maitaria na Momanyi (2016:25) ambao wanasema:

> Katika jamii ya leo na kulingana na katiba ya nchi, mwanamke na mwanamume wana nafasi sawa katika harakati mbalimbali za kijamii. Hali hii na juhudi za wanawake katika kuufikia usawa wa kijinsia.

Mawazo haya yanaendelezwa na mhimili wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaosema kwamba, wanaume na wanawake washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana, bila kuathiriwa na majukumu ya kimaumbile.

Aidha, methali ya (2) inamaanisha kwamba mwanamke hana mamlaka ya kumpa yeyote fahari wa mume wake. Itikadi inayoelezwa ni kuwa mwanamke nyumbani hana mamlaka na hawezi kutekeleza maamuzi mwenyewe bila kuidhinishwa na mume wake ilhali methali ya (1) inampa uwezo wa kutekeleza maamuzi. Pia, methali inamfanya kuwa kaimu katika utekelezaji wa maamuzi kama mwanamume hayupo. Huu ni ukinzani unaobainika katika methali hii ya (2).

Ukinzani wa itikadi za kiuana unaoibuliwa kuhusu uongozi katika methali, unamweka mwanamke katika nafasi ya kuwa na mamlaka na kutekeleza maamuzi katika jamii ya Wanyankole. Hivyo, itikadi zinazombainisha mwanamke kama asiyeweza kutekeleza maamuzi inaendelezwa kwa misingi ya kiubabedume kwa kuwanufaisha wanaume na kuwadhulumu wanawake. Mawazo haya yanaungwa mkono na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaosema kwamba, utamaduni wa tabaka tawala hautambui hisia na haja za watu wa kawaida (Watawaliwa). Wanaendeleza ubaguzi kati yao na watawaliwa na kuwachukulia kama wasio na uwezo na ni watu wa hadhi ya chini. Itikadi hii ya ubaguzi inalifanya kundi la tabaka tawala kutojali watawaliwa.

Methali ya (3) inaeleza maana ambayo inaibua ukinzani wa itikadi. Sehemu ya kwanza ya methali inayoeleza kuwa ‘mwanamume hapaswi kugeuka kwa ulimi wake’ inamaanisha kuwa kauli anayotoa haibadilishi. Sehemu ya pili ya methali

inaeleza kuwa mwanamume anageuka kitandani akiwa na mke wake. Kulingana na maana ya methali inayoibuliwa na sehemu mbili za methali kunaibuka ukinzani. Mawazo haya yanaungwa mkono na Milner (1969) akinukuliwa na Sanaudin (2015) kwamba kila sehemu ya methali inaweza kupewa thamani ya uchanya na uhasi kutegemea kama methali hiyo inawasilisha itikadi chanya au hasi, inawasilisha maana au la na inajenga au inabomoa. Katika utafiti huu, uchanya na uhasi katika methali umerejelewa kama ukinzani. Matumizi ya neno ‘kugeuka’ kwenye pande mbili za methali inamaanisha kwamba kuna hali fulani ambazo zinamfanya ageuke, yaani kubadilisha msimamo. Mwanamume anaonekana akibadilishwa na hali fulani ingawa hababadilishi msimamo wake. Kugeuka kitandani kunadhihirisha kwamba uwezekano wa kubadilisha msimamo upo. Ukinzani huu unatubainishia kwamba wanaume wanajiwekea hali ya kujiashiria kwa ajili ya kuendelea kuwatawala wanawake. Hali hii inathibitishwa na Malenya na wenzake (2020: 56) wananaosema kwamba:

> Mwanamume amejisawiri kama mtu maalum.Amejipa uwezo na nguvu nyingi ambapo anasema wale watu wengine ni ovyo. Mwanamume…anapewa huduma zote anazohitaji zikiwemo za kimapenzi na kutimiziwa haja zake jumla. Kwa hivyo mwanamke anasalia kuishi katika kivuli cha mwanamume kwa kumtumikia.

Mwanamume kubadilishwa na mambo fulani katika hali fulani ni ukinzani unaodhihirika katika methali hii. ‘Kugeuka kitandani’ kunamaanisha mwanamume hapaswi kubadilisha msimamo kulingana na utamaduni wa Wanyankole. Anabadilishwa na mambo maalumu. Maana yake kuna uwezekano wa mume kubadilika kwa matendo fulani. Mhojiwa wa KRH 4 tarehe 18/04/2018 alisema kuwa, kuna kauli zinazostahili kutolewa na mkuu wa familia; akizisisitiza na haziwezi kubadilika. Aliendelea kueleza kuwa kitamaduni, kuna

mila na desturi za Wanyankole ambazo hazistahili kubadilika. Ingawa mhojiwa anaeleza maoni hayo, inadhihirika kuwa kuna uwezekano wa mwanamume wa kubadilisha msimamo wake. Mke huwa hastahili kumshawishi mume wake kutekeleza jambo fulani na akakubali bila kuchunguza zaidi ni itikadi ambayo inajikita kwenye mfumodume lakini katika methali hii, mwanamume anabadilishwa na mambo fulani. Itikadi shawishi ya mfumodume inafunika ukweli huu kwa kutaka kuendeleza ubainifu wa uwezo na mamlaka ya wanaume kwa kuonesha kuwa ana msimamo kulingana na matarajio ya jamii.

### 6.1.7 Suala la Kazi

Mwanamke huchukuliwa kama asiyeweza kufanya kazi kwa kujitegemea na ni dhaifu. Udhaifu huu ni wa kiutegemezi, anategemea mwanamume katika kufanikisha shughuli zake. Methali kinzani zinakanusha madai haya kama zinavyojadiliwa katika Jedwali la 46:

**Jedwali 46: Methali Kinzani za Kinyankole kuhusu Kazi**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Omukazi ku ayikarira taimuka.* | Mwanamke atupapo mweleka hainuki/hanyanyuki. |
| 2. | *Omukazi omuhingi atega eiguru entabire.* | Mwanamke mkulima hugema shamba mbingu. |
| 3. | *Omukazi taba mugyenyi.* | Mwanamke hawi mgeni. |
| 4. | *Engaro ibiri nokunabisana, omukazi yaba nayara ekitanda omushaija nahanika enkindi* | Mikono miwili ni kuoshana, mke anapokuwa anatandika kitanda, mume anaangika juu nguo za ndani. |

Kwa mujibu wa methali ya (1) mwanamke anaelezewa na methali hii kwamba, anapofanikiwa kutekeleza shughuli fulani hathubutu kuendelea hatua zaidi kuikamilisha kwa sababu ya kuchukuliwa kuwa dhaifu. Itikadi hii inaeleza maana zaidi kwamba, uwezo wa kutupa mweleka ni wa mwanamume kwa kuwa

kunahitaji nguvu nyingi ambazo mwanamke hana. Methali ya (2) inawasilisha itikadi inayomtarajia mwanamke kujishughulisha na kazi kwa bidii na hapaswi kuwa mvivu. Mwanamke anayejibidiisha na kazi, mfano kutayarisha shamba lake kwa ajili ya kupanda pindi mvua inaponyesha hawezi kuwa mvivu kama itikadi ya methali ya (1) inavyomsawiri. Huu ni ukinzani wa kiitikadi unaoibuliwa na methali hizi. Aidha, methali ya (3) inasisitiza jinsi mwanamke anavyojibidiisha na kazi hata kwenye mazingira anapopaswa kuwa mgeni. Kwenye mazingira haya ya ugeni, mwanamke anapotarajiwa kulakiwa na kuhudumiwa, hasubiri kutunzwa kama mgeni kwa sababu ya sifa yake ya kuwajibikia kazi. Hii ni itikadi inayodhihirisha kuwa mwanamke ni mchapakazi, kinyume na methali hizo zinazoelezea udhaifu na kutojiweza kwa mwanamke.

Utamaduni wa Wanyankole unasisitiza utenganishaji wa majukumu ya kiuana ambapo mwanamume anapaswa kutekeleza majukumu yake tofauti na ya mwanamke. Maoni haya ni kwa mujibu wa mhojiwa wa 4 ambaye anaeleza kwamba ugawaji wa majukumu kiutamaduni kwa misingi ya uana kunaendeleza amani, utulivu na kusababisha maendeleo kwa njia ya kutekeleza majukumu maalumu ambayo jamii inatenga kwa kila upande kulingana na jinsi.

Methali ya (4) inawasilisha itikadi iliyo kinyume na maoni ya mhojiwa wa 4. Mwanamume na mwanamke wanadhihirika kuwajibikia kazi kwa ushirikiano. Methali ya (4) ni udhihirisho kuwa wanaume wanapaswa kushirikiana na wanawake katika uendelezaji wa kazi. Ushirikiano huo hautegemei uwezo wa wanaume na udhaifu wa wanawake bali ni utekelezaji wa majukumu kwa pamoja kwa msingi wa haki sawa kati yao. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mhimili

unaodai kuwa wanaume washughulikie majukumu yao ya kijamii kwa kushirikiana bila kuathiriwa na hali za kimaumbile unasisitiza hoja hii.

Ukinzani unaobainika katika methali hizi unaonesha kuwa itikadi ya wanawake kutengewa kazi zao za kike na wanaume kazi za kiume ni kuendeleza ubaguzi kwa misingi ya kiuana kwenye uga wa kazi. Itikadi hii ya kiuana katika methali ya (4) pamoja na maoni ya mhojiwa wa 4 haviafikiani. Wanawake wanapaswa kushirikiana na wanaume katika kuchuma na kutafuta mahitaji ya familia. Matarajio ya itikadi hii ni utegemezi wa mwanamke kwa mwanamume, yaani mfumodume kwa misingi ya kiutamaduni.

### 6.1.8 Suala la mahusiano na Wakwe

Wanandoa wanapaswa kuishi kwa amani na wakwe zao ili ndoa zao zisivunjike. Mawazo haya yanaungwa mkono na (Owu, 2019). Itikadi hii ipo katika methali za jamii nyingi za Kiafrika ikiwemo jamii ya Wanyankole. Mkwe huheshimiwa sana na ndugu za mume na mke. Wakwe huweza kuchangia ndoa kudumu na hata kinyume chake, yaani kuvunjika. Kwa mujibu wa Kirindi (2008) wakwe walikuwa na nafasi kubwa katika ustawi wa ndoa. Kwa hivyo, ndoa ya furaha na amani ilichangia pakubwa na ushirikiano mwema na wakwe. Hata hivyo, pamoja na mwelekeo huo wa pamoja kuhusu itikadi za uana kumekuwapo na ukinzani katika methali za jamii za Kiafrika kuhusu nafasi ya wake, kama methali zifuatazo za Kinyankole zinavyokinzana.

**Jedwali 47: Methali Kinzani za Kinyankole kuhusu Mahusiano na Wakwe**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | *Otakareebaga kabi ka nyinazaara ati "ninza owa maawe"* | Asiyejua ubaya wa mama mkwe eti "naenda kwa mama". |
| 2. | *Tocwa gwa muhara wawe mukwe wawe atakaizire.* | Usiamue kesi ya binti yako kabla mkwe wako kufika. |

Kulingana na ufafanuzi wa awali, mama mkwe anachukuliwa kuwa hawapendelewi na kuaminiwa kusimamia mahusiano ya ndoa ya wana wao. Inaaminiwa kuwa tabia za mama mkwe zinaweza kusababisha kuvunjika kwa ndoa za watoto wao. Kwa hivyo, mume na mke wanashauriwa kuwa waangalifu na mama wakwe kama wanataka ndoa zao zidumu. Itikadi hii inabainika katika methali ya (1) kwenye Jedwali Na. 47 ambapo mama mkwe anaoneshwa kama asiyepaswa kuaminiwa au kuwa huru naye. Methali ya (2) kwa upande mwingine inabainisha uaminifu wa mkwe kwa wakwe zake. Methali hii inamaanisha kuwa mkwe hapaswi kutoa uamuzi kuhusu kesi ya binti yake kama mume wa binti yake (mkwe) hayupo. Itikadi katika methali ya (2) inakinzana na itikadi katika methali ya (1). Methali ya (2) inaweka imani na hadhi kwa mkwe kwa kutochukua hatua yoyote kama mkwe huyo hajafika ilhali methali ya (1) inaasa kutomwamini mama wakwe. Ukinzani huu unadhihirisha mchango wa mkwe katika kuimarisha ndoa ya watoto wao, tofauti na mama mkwe anavyobainishwa kama mtu mbaya. Ukinzani huu wa kiuana unaobainika katika methali hizi unaonesha kuwa, mama mkwe anakuwa chanzo cha kuvuruga ndoa za watoto wao na hatakiwi kuhusika katika ustawi wa ndoa hiyo.

Katika utamaduni wa Wanyankole wakwe walikuwa na mchango katika kuhimili familia. Ushirikishaji wa wakwe ilikuwa njia mojawapo muhimu katika usuluhishaji wa matatizo kwa wanandoa katika jamii ya Kinyankole kama isemavyo kwamba 'Penye wazee hapaharibiki neno'. Wazee ndio wanaotengeza pale ambapo wanajenzi au vijana wanaposhindwa kwa sababu ya kuzingatia pupa katika utoaji wa suluhu au uamuzi wa busara. Hata hivyo, katika methali ya (2) mwanamke anabainika kutokuwa na haki ya kusikilizwa; mwanamume ndiye anapewa kipaumbele. Kusubiri hadi mume wake asikilizwe ni kitendo kinachomdhulumu. Kwa sababu ya jamii inayotawaliwa na wanaume, uwezekano wa mwanamke kuwa upande sahihi nao unakuwa mdogo. Itikadi hizi jinsi zinavyoendelezwa, zinamchukua mwanamke kama binadamu wa daraja la pili, ambaye hapewi kipaumbele. Mhimili wa Nadharia ya Itikadi unasema kwamba utamaduni wa tabaka tawala unaendeleza ubaguzi kati yao na watawaliwa kuchukulia kama wasio na uwezo na ni watu wa hadhi ya chini. Mwanamke kama anayewakilisha kundi la tabaka la chini, anabainika kuwa anabaguliwa pamoja na kuchukuliwa kutokuwa na haki yake kama mwanamke.

### 6.1.9 Suala la Ujane

**Jedwali 48: Methali Kinzani za Kinyankole kuhusu Ujane**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1.<br>2. | *Omufakazi taijuka kitara.*<br>*Egabo yabaana eigutsya ba nyinabo.* | Mjane hakumbuki ghala.<br>Mlo wa watoto hushibisha mama yao. |

Methali ya (1) inamrejelea mjane ambaye hana jukumu la kumshughulisha kwa sababu mume wake ambaye alipaswa kuhudumiwa alifariki. Mwanamke

kiutamaduni alikuwa anaenda kwenye ghala kutoa chakula ili aweze kumuandalia mume wake. Kwa vile mume wake hayupo, mke hana haja tena ya kukumbuka ghala. Itikadi ya methali hii inamaanisha kwamba jukumu muhimu la mwanamke ni kumhudumia mume wake kwa kumpikia chakula. Methali ya (2) inawasilisha maana kinzani kwamba, mwanamke aliye na sifa ya mama anakuwa na dhamana kwa watoto wake kwa kuwahudumia. Itikadi hii inadhihirishwa kupitia maana ya methali inayowasilishwa kwamba chakula ambacho mwanamke (mama) anawatayarishia watoto wake kinampa shibe. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika mwanamke mwenye sifa ya mama amekuwa na dhamana ya malezi na kutunza watoto na ni vigumu kuwatelekeza watoto aliowazaa. Dipio (2019) anatambua kuwa mama ana upendo wa karibu sana na watoto wake. Huduma kwa watoto inawakilishwa na chakula ambapo mama yao anafarijika watoto hao wanapokuwa katika hali nzuri.

Itikadi katika methali ya (1) inayombainisha mwanamke kuwa yupo kwa ajili ya kumhudumia mume wake si sahihi. Methali (2) inaibua ukweli mwingine kwamba mama anafarijika watoto wake wakiwa wameshiba. Watoto wake hawawezi kushiba kama hajawaandalia chakula. Hii ni tofauti na itikadi inavyobainika katika methali (1) ambayo imawasilisha mjane kutokuwa na uwezo wa kukumbuka ghala baada ya kifo cha mume wake. Itikadi katika methali ya (2) inakinzana na itikadi katika methali ya (1) inayodhihirisha kuwa mwanamke anashughulikia maslahi ya mume wake tu kiasi kwamba mume wake anapofariki mke huyo hawajibishwi na majukumu mengine kama ya kuwahudumia watoto wake. Itikadi hii inaendelea kuimarishwa na mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaodai kuwa tabaka tawala linaendeleza ukubalifu

unaopatikana kutokana na ushawishi wa itikadi zao zinazolenga kujitolea na kutumika kwa tabaka tawaliwa wakitumikia kundi dogo la watawala. Mama kuwapatia watoto wake chakula ni jukumu analofanya kwa hiari na ndio maana anafarijika baada ya watoto wake kushiba kwa mlo anaowaandalia. Pia, huduma za mama kwa watoto wake zinaendelea hata baada ya mume wake kufariki. Itikadi hii ni kinyume na itikadi inavyobainika katika methali ya kwanza inayoeleza kwamba mwanamke anapopoteza mume wake, hana haja tena na ghala.

### 6.1.10 Suala la Udhalilishaji

Mwanamke anawekwa katika hali duni na utamaduni wa jamii yake. Utamaduni huo unambainisha kama mwenye thamani duni na kinyume chake mwanamume kubainika kama kielelezo cha jamii (Mavisi, 2016). Methali za Kinyankole ambazo hazikithamini kiumbe cha kike zipo. Hata hivyo, kunabainika itikadi katika methali ambayo inapingana na itikadi dhalilishi kama inavyojadiliwa hapa. Mwanamke anachukua nafasi maalumu katika ndoa. Katika baadhi ya methali za Kinyankole mwanamke anatukuzwa kwa sababu ya nafasi yake katika kuendeleza familia. Ndiyo maana husemwa, hata mwanamume ni mwana wa mama wa kipindi fulani.

**Jedwali 49: Methali Kinzani za Kinyankole kuhusu Udhalilishaji wa Wanawake**

| Na. | Methali ya Kinyankole | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| 1.<br>2. | Abakazi baba amasha ganibw’ente.<br>Omukazi mubi ahita “boojo ni mwaare”. | Wanawake ni samadi ya ng’ombe.<br>Bora mwanamke asiyevutia kuliko “Wavulana tandikeni tulale”. |

Methali hii ya (1) inalinganisha thamani ya mwanamke kisitiari na samadi ya ng'ombe. Mhojiwa KRH 3 tarehe 17/04/2018 alitoa maoni kwamba, ng'ombe anapokuwa malishoni hatambui thamani ya samadi yake; anaitupa ovyo bila kujali. Inamaanisha kwamba samadi hiyo kwa ng'ombe haina thamani hata kama ina mchango kwa kuongeza mbolea na kurutubisha mimea. Itikadi hii ndivyo inadhihirisha mwanamke kuonekana kama kiumbe asiye na thamani katika mahusiano na mwanamume. Methali ya (2) ambayo inaeleza kuhusu mke ambaye si mzuri wa sura anakuwa muhimu kuliko wavulana nyumbani kwa sababu ya mchango wake maalumu unaotokana na majukumu yake ya nyumbani. Kimsingi, mwanamke anapaswa kuwa mrembo kwa vigezo vya kiutamaduni (Kirindi, 2008). Hata kama hajatimiza vigezo hivi kulingana na itikadi katika methali ya (2), thamani yake hailinganishwi na kitu kingine chochote kile. Mwanamke anachukua nafasi muhimu ndani ya nyumba.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwenye mhimili unaoeleza kuwa tabia za uana ambazo zinaonekana kuvunjia heshima mwanamke zitathminiwe kila mara kwa sababu mwanamke ana haki yake ya msingi. Nafasi ya mwanamke haiwezi kubadilishana na wavulana nyumbani kwa sababu ya majukumu yake maalumu. Ukinzani unaoibuliwa na methali ya (2) unabainisha thamani ya mwanamke katika maendeleo ya familia tofauti na itikadi dhalilishi katika methali (1) kwa kuwafananisha na samadi ya ng'ombe huku wanaume wanabainika kama kielelezo. Methali za aina hii zinahitaji ufafanuzi wa kimuktadha ili ziweze kuendelea kutambulika kama kauli za hekima; la sivyo, hazifai katika kubainisha mahusiano ya kiuana.

### 6.2 Ukinzani wa Itikadi za Kiuana na Athari zake katika Methali za Kiswahili

Zipo methali anuwai za Kiswahili zinazobainisha ukinzani wa itikadi za kiuana. Wanawake wamedhihirishwa kama wenye uwezo wa kutekeleza majukumu ambayo kiutamaduni yanachukuliwa kuwa ya kiume. Aidha, wanawake wanadhihirika kushikilia nafasi maalumu zenye mchango mkubwa katika jamii. Aidha, wanawake wamebainika katika nafasi za mamlaka na uongozi, nafasi ambazo zimechukuliwa kuwa za wanaume katika tafiti mbalimbali. Wanawake hawatumii mamlaka yenye nguvu; mamlaka yao yanabainika kupitia uongozi wao wa busara (Dipio, 2019). Methali za Kiswahili zinazobainisha mahusiano ya kiuana zinaangazia masuala ya ndoa, wazazi wa kambo, uzazi, malezi na utunzaji wa watoto, uongozi, uzalishaji wa mali, uhuru na maendeleo ya jamii zipo.

#### 6.2.1 Suala la Ndoa

Asasi ya ndoa katika jamii ya Waswahili ni muhimu zaidi kwa maisha ya mwanamume na mwanamke (Sengo, 1992). Asasi hii inabainisha majukumu ya mke na mume katika jamii ya Waswahili ambapo mke anadhihirika kuwa mwenye majukumu maalumu anayotengewa na anayopaswa kuyatekeleza katika familia. Majukumu hayo ni tofauti na anayotengewa wanaume. Hatimaye, wanawake wanakuwa kwenye nafasi zao kimajukumu na kihadhi kwa mujibu wa desturi za jamii ya Kiswahili. Ndoa katika jamii ya Waswahili ni jukumu la mume kuiendesha na kukidhi mahitaji ya familia (Momanyi, 1998). Vilevile, mwanamke katika utamaduni wa Waswahili anapaswa kuolewa ili aishi na mume ambaye ataweza kumpa mahitaji ya msingi na kumtunza. Aidha, ana nafasi ya

kuendeleza familia yao iwapo mume amelemewa na majukumu (Maitaria, 2018). Data ya methali zinazoibua ukinzani kuhusu suala la ndoa katika jamii ya Waswahili inawasilishwa katika jedwali la 50:

**Jedwali 50: Methali Kinzani kuhusu Suala la Ndoa**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Asiye na mke yu uchi. |
| 2. | Mke bila mume ni kama shamba lisilolimwa. |
| 3. | Eda ya mke hakuna eda ya mume. |
| 4. | Buibui ni mke. |
| 5. | Talaka ni kuvuliwa nguo. |
| 6. | Mkeo akikwambia ‘niwache’ nawe ridhia na mwingine kimbilia. |
| 7 | Kosa moja haliachishi mke. |

Methali hii ya (1) inamzungumzia mwanamume ambaye hana mke. Huyu analinganishwa na mja aliye uchi. Mwanamume aliye uchi anaaibika kwa sababu hakuna binadamu anayetaka kuonekana uchi wake. Methali inabainisha haja wa mwanamume kuoa na kuishi na mke ambaye ataweza kusitiri uchi wake. Kulingana na itikadi katika methali hii, mwanamume anachukuliwa kuwa kiumbe ambaye hawezi kutimiza mambo fulani peke yake bila mwanamke. Anatarajiwa kuishi na mwanamke kama mume na mke ili mke aweze kusitiri mapungufu yake. Nadharia ya Itikadi, kupitia mhimili unaosema kwamba ukubalifu unapatikana kutokana na ushawishi wa itikadi za tabaka tawala ambapo utawala unalenga kujitolea na kutumika kwa tabaka tawaliwa kulitumikia kundi dogo la watawala. Itikadi hii inaendeleza ushawishi wa mwanamke kukubali kuolewa kwa imani kuwa anapaswa kuishi na mume kwa sababu ana mchango mkubwa katika maisha yake. Hatimaye, itikadi hii inamfanya mwanamke kuishia kuyatumikia maslahi ya mwanamume. Ukubalifu huu wa kiitikadi unatawala mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume kwenye ndoa.

Methali ya (2) ‘Mke bila mume ni kama shamba lisilolimwa’ inamrejelea mwanamke ambaye hana mume. Itikadi ya methali hii inamtaka mwanamke kuolewa ili aweze kuishi na mume wa kumtunza. Mwanamke ana imani kuwa kuolewa ni kwa ajili ya heshima na utambulisho wake katika jamii, kama Ezeifeka (2017) anavyotambua. Ezeifeka anasema kwamba mwanamke anajiona kuwa mwenye bahati anapoposwa akiwa bado mwari na urembo wake haujafifia. Itikadi zinazoelezwa katika methali hizi zinaibua ukinzani, yaani methali ya (1) inabainisha haja ya mwanamume kuishi na mke kwa ajili ya kumsaidia na methali ya (2) inabainisha haja ya mwanamke kuishi na mume atakayemtunza. Ukinzani unaoibuliwa katika methali hizi unadhihirisha haja ya mwanamume na mwanamke kila mmoja kumhitaji mwingine kutokana na nafasi ya kila mmoja kwenye familia. Maana hii inayoibuliwa inakinzana na tafiti za awali, ukiwemo wa Ezeifeka (2017) ambao unadai kuwa mwanamke ndiye ana haja ya kuolewa ili aweze kuishi na mume kwa ajili ya kupata mahitaji ya msingi na kutunzwa.

Aidha, methali ya (3) na methali ya (4), zinakinzana na methali ya (2), Methali ya (2) na ya (4) zinaibua maana ya wanawake kushirikiana na kujitegemea kama kundi linalodhulumiwa kwa kushughulikia maslahi yao kwa pamoja bila kutegemea wanaume. Wanawake wanabainika kuwa katika makundi yao kwa ajili ya kushughulikia maslahi yao kama njia ya kujikimu (Caplan, 1982). Vilevile, kunaibuka itikadi ya wanawake kutaka kuwa huru na kushughulikia mambo yao bila vikwazo vya wanaume. Itikadi hii inasisitizwa na methali ya (3), na methali ya (4), ‘Buibui ni mke’. Kwa upande mwingine, methali ya (2) inabainisha itikadi ya haja ya mwanamke kuolewa ili aweze kuwa na mume

atakayemsaidia. Itikadi hii inaonesha kwamba mwanamke hawezi kukamilika na kujitegemea bila mume, yaani mwanamke anabainika kama mtegemezi katika methali hii. Maana inayowasilishwa katika methali hii inakinzana na maana katika methali ya (3) na (4).

Aidha, kuhusu suala la talaka kati ya mume na mke, kuna methali ambazo zinazungumzia jambo hili kwa njia inayoibua ukinzani. Methali ya (5), inamaanisha kwamba talaka si jambo zuri kutokea kati ya mume na mke. Methali hii inadai kwamba talaka inapotokea inaathiri wanandoa, yaani mke na mume. Kwa hivyo, kulingana na itikadi inayoelezwa katika methali hii, talaka si jambo zuri kutokea kati ya wanandoa. Methali ya (6) 'Mkeo akikwambia niwache nawe ridhia na mwingine kimbilia' inaeleza kwamba mke wako anapokwambia uachane naye, kubali matarajio yake kisha uharakishe kuoa mke mwingine. Kulingana na itikadi inayobainishwa na methali hii, kwanza, mwanamume anaonekana kuwa mwenye mamlaka kuamua juu ya talaka kati yake na mke wake. Pili, mwanamume anabainika kutoathirika na talaka itakayotokea kati yake na mke wake bali anapata fursa ya kuoa mke mwingine. Methali hizi mbili zinabainisha itikadi kinzani. Methali ya (1) inaonesha hasara kwa mwanamume na mwanamke talaka inapotokea. Methali ya (2) inabainisha mwanamume kama mwenye mamlaka ya kutoa talaka, na kwamba hapati hasara yoyote talaka inapotokea. Itikadi hii inadhihirishwa na kutokuwepo kwa ugumu wowote wa kuacha au kutaliki mke; hata hivyo atapata mke mwingine haraka.

Pamoja na hayo itikadi ya methali (6) inaibua ukinzani wa kiitikadi na methali ya (7). Methali ya (6) inamaanisha kwamba kama mke anahitaji talaka, mume wake

asikawie kumpa hiyo talaka. Methali hii inaendelea kumpa fursa mwanamume ya kuharakisha kuoa mke mwingine akishatoa talaka kwa mke wa kwanza. Itikadi hii inambainisha mwanamume kama kiumbe asiye na subira katika kusuluhisha mambo madogo yanayowakumba katika ndoa na ana ruhusa ya kutoa talaka kwa mke wake wakati wowote na kuoa mke mwingine. Maana inayoibuliwa na methali hii ni kwamba hakuna haja ya kuvumiliana kati ya mke na mume ikiwa kumetokea kutoelewana kati yao na talaka ndiyo suluhisho la haraka. Kwa upande mwingine, methali ya (7) inahusu itikadi ya haja ya mwanamume na mwanamke kuvumiliana kwenye ndoa. Mwanamke kama amekosea hakuna haja ya kukimbilia talaka kama njia ya kusuluhisha changamoto za ndoa kama inavyobainishwa na methali ya (6).

### 6.2.2 Suala la Ukewenza na Wazazi wa Kambo

**Jedwali 51: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Ndoa za Mitala**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1.<br>2 | Mama wa kambo si mama.<br>Baba wa kambo si baba kunichukuza mikoba na ufunguo wa shaba. |

Methali ya (1) inamaanisha kwamba mama wa kambo ni mama asiyekuwa na uhusiano wa damu kwa mtoto au asiyemzaa mtoto lakini ni mke wa baba yake. Methali ya (2), baba wa kambo ni baba asiyekuwa na uhusiano wa damu kwa mtoto au asiyemzaa mtoto lakini ni mume wa mama yake. Maelezo katika methali hii yanakana baba wa kambo kuwa kwenye nafasi ya baba mzazi wa mtoto. Itikadi ya baba wa kambo na mwana ni kumchukua kama mtumishi wake, kama inavyodhihirika katika methali kwa kumbebesha mikoba na funguo. Methali ya (1) na ya (2) zinakinzana kimaana. Tafiti za awali zimebainisha mama

wa kambo kuwa ndiye huchukiwa kwa tabia zake za kutowapenda watoto wa kambo. Ulashevna (2019) anasisitiza hoja hii kwamba, thamani ya mama kwa kila mtu haiwezi kulinganishwa na chochote. Mama huwa tayari kwa lolote kwa ajili ya watoto wake. Mhimili wa Nadharia ya Udenguzi unadhihirisha kuwa na unyume. Kwa hivyo, mama anasifiwa kwa kuwajibikia watoto wake, kwa upande mwingine inaonesha kuwa mama wa kambo anachukuliwa kinyume chake. Katika methali ya (2) tunabainisha itikadi ambayo inakinzana na itikadi ya awali. Baba wa kambo pia hapendelewi kwa dhamana ya malezi ya mtoto asiyemzaa. Ataishia kumtumia kufanya kazi za sulubu badala ya kumjenga. Ukinzani katika methali hizi unabainisha haja ya watoto kutunzwa na wazazi waliowazaa, na sio kulelewa ama na baba au mama wa kambo. Ukinzani huu hatimaye unawataka wazazi wa kibiolojia kuwalea wenyewe watoto wao.

### 6.2.3 Suala la Uzazi

Methali zifuatazo zinaonesha ukinzani kuhusu itikadi ya kuzaa na haja ya kuwa na watoto kwa wanawake na wanaume.

**Jedwali 52: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Kuzaa**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1.<br>2. | Nyumba ya mgumba haina matanga.<br>Mtoto ni wa mama kwa baba huenda nasaba. |

Methali ya (1) inamaanisha kwamba mwanamume ambaye hana mtoto, anapofariki hana kumbukumbu yote. Methali hii inabainisha itikadi ya haja ya mwanamume kuzaa na kuwa na watoto. Watoto hawa ndio wanatarajiwa kuendeleza familia ya baba yao anapofariki na kuweza kumzika. Arnold na wenzake (1998) wanasema kuwa, haja ya wanaume kuzaa watoto wa kiume ni

kwa sababu ya kutaka kusaidiwa wakati wa uzee. Kwa upande mwingine, methali ya (2) inaeleza itikadi ya kuhusishwa watoto na mama yao na kwa upande wa mwanamume kunaenda sifa ya kutambulika kuwa baba fulani. Methali hizi zinaibua ukinzani wa itikadi za kiuana ambapo methali ya (1) inamtaka mwanamume kuzaa na kuwa na watoto watakaomfaa baada ya kifo chake na methali ya (2) inabainisha itikadi inayohusisha watoto na mama yao. Mama anahusishwa na watoto kwa sababu ya dhamana anayokuwa nayo kwa watoto. Dhamana hii inatokana na majukumu ya kubeba mimba, kuzaa, malezi na wajibu mkubwa kwa ujumla anaokuwa nao kwa hao watoto. Diabah na Appiah (2015: 11) wanasema kwamba, wanawake ndio wanaozaa binadamu, awe mwanamume au mwanamke; wanawajibika pia kuwatunza viumbe hao wanaozaa na kuwaelimisha. Wanaendelea kusema kwamba tofauti na mwanamke kuchukuliwa kuwa dhaifu na asiye na nguvu, mwanamke huyo anazaa wanaume wanaodhaniwa kuwa wenye nguvu na mamlaka. Kwa namna hii inaweza kufasiliwa kuwa mwanamke anawasilishwa kuwa mwenye nguvu mamlaka pia. Methali hii, ‘Mtoto ni wa mama kwa baba huenda nasaba’ inadhihirisha itikadi ya kimamlaka ya wanawake kwa watoto. Hali hii inatokana na nafasi muhimu wanayoshikilia katika jamii ya kuzaa, kulea, kutunza na kuelimisha watoto.

### 6.2.4 Suala la Malezi

Wanaume wanabainika kuwa hawapaswi kuwajibikia malezi ya watoto. Malezi ya watoto na kuwatunza ni jukumu la wanawake. Methali ambazo zinabainisha itikadi inayowajibisha wazazi wa kiume (wanaume) kuhusika na malezi ya watoto pamoja na kushirikiana na wazazi wa kike katika kutekeleza malezi pia zipo. Mifano ifuatayo inatudhihirishia itikadi kinzani kuhusu malezi ya watoto:

**Jedwali 53: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Malezi**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Jogoo halei mwana. |
| 2. | Baba n’kanye mwanawe. |
| 3. | Mkono mmoja haulei mwana. |
| 4. | Kuzaa ni shani ya Mungu malezi ni wajibu wetu. |

Katika methali ya (1) kunabainika itikadi inayotenganisha jukumu la malezi ya watoto na wanaume. Kutenganisha majukumu ya malezi na wanaume, inamaana kwamba wanawake kwa upande mwingine ni wao wanaowajibishwa na malezi. Itikadi hii inabainishwa na matumizi ya taashira ya ‘jogoo’ anayewakilisha wanaume. Kazi ya malezi ya watoto inaachiwa wanawake. Karata na wenzake (2021) wanaeleza kwamba mwanamke anajengwa na kuaminishwa na mfumo wa jamii kuwa kazi yake kubwa ni kulea familia. Itikadi hii inathibitishwa kupitia mhimili wa Nadharia ya Itikadi unaotambua kwamba watawala wanaendeleza imani ya utawala kwa ukubalifu ambao unatokana na ushawishi wa tabaka tawala. Kwa hivyo, wanaume kama kundi lenye mamlaka wanatumia njia shawishi ili kuwafanya wanawake kukubali jukumu la malezi ya watoto kuwa ni lao.

Karata na wenzake (2021) wanaendelea kujuza kwamba malezi ya watoto katika tamaduni za Kiafrika ni jukumu la kila mmoja. Kulingana na maoni ya Karata na wenzake, mwanamume pia ana wajibu wa kushughulikia malezi ya watoto. Itikadi hii inadhihirika katika methali ya (2) na inamtaka baba ambaye ni mzazi wa kiume kuwajibikia malezi ya watoto kwa maadili mema. Uwajibikaji wa baba kwa malezi unawasilishwa kwa matumizi ya neno ‘n’kanye’. Neno hili lina maana  ya kuonya au kuwahadharisha watoto kutorudia vitendo fulani. Kwa

mujibu wa mhimili wa Nadharia ya Udenguzi wa uainishaji wa dhana zote kiulimwengu kwa kuzingatia uwili, mwanamke na mwanamume, dhana hizi zinakaribiana kimaana. Kwa hivyo, kunaibuka ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali hizi mbili kuhusu suala la majukumu ya malezi ya watoto. Methali ya (1) inamtenga mwanamume na majukumu ya malezi ilhali methali ya (2) inadhihirisha kuwa mwanaume huyohuyo anapaswa kuwajibika kwa malezi ya watoto.

Aidha, methali ya (3) ‘Mkono mmoja haulei mwana’ na methali ya (4) ‘Kuzaa ni shani ya Mungu malezi ni wajibu wetu’ zinabainisha itikadi ambazo zinaibua ukinzani wa itikadi za kiuana kuhusu malezi ya watoto dhidi ya methali ya (1) ‘Jogoo halei mwana’. Methali ya (3) na ya (4) zinasisitiza haja ya kushirikiana kwa wazazi wote wawili kwenye malezi ya watoto. Methali ya (3) ‘Mkono mmoja haulei mwana’ inaashiria kuwa ni vigumu mkono huo mmoja kulea mwana, kwa hivyo kuna haja ya kutumia mikono miwili ambayo ni ushirikiano wa mwanamke na mwanamume. Vilevile, methali ya (4) sehemu yake ya pili inaeleza kwamba malezi ya watoto ni ‘wajibu wetu’. Matumizi ya kimilikishi hiki nafsi ya kwanza wingi inatusisitizia itikadi hii ya kushirikiana katika jukumu la malezi. Maelezo haya ya kiitikadi katika methali hayabainishi wala kutenganisha ni nani kati ya akinamama au akinababa wanapaswa kushughulikia malezi ya watoto na ni nani hawapaswi kushughulika na malezi. Itikadi katika methali hizi inaakisi matarajio ya jamii yenye mfumo dume ya Waswahili kiutamaduni kuhusu malezi. Kulingana na maoni ya mhojiwa MSA 3 tarehe 11/05/2018 katika eneo la Mombasa na mhojiwa LMU 3 tarehe 16/05/2018, katika eneo la Lamu walidai kwamba mwanamke aliye katika nafasi ya mama, ni

jukumu lake kuwalea, kuwatunza na kuwaelekeza watoto kwa sababu mtoto ni kioo cha wazazi wake, hasa mama yake. Katika uhakiki wetu wa methali hizi hatuafikiani na mawazo ya wahojiwa. Uchambuzi wa methali kiudenguzi unaonesha kuwa mwanamke na mwanamume katika methali hizi za Kiswahili wanapaswa kuwajibikia malezi ya watoto kwa pamoja. Itikadi hii inatofautiana na itikadi katika methali ya (1) inayombainisha mwanamume kutowajibikia malezi ya watoto pamoja na maoni ya wahojiwa.

### 6.2.5 Suala la Uongozi na Mamlaka

Wanawake wanachangia pakubwa katika maendeleo ya jamii. Licha ya mchango wao wa kimaendeleo katika nyanja mbalimbali za kijamii, itikadi za kiuana zinaendeleza ubaguzi wao katika uwanja wa uongozi na utekelezaji wa mamlaka kama inavyobainishwa na tafiti mbalimbali (Ndungo,1998; Kiyimba, 2001; Dipio 2019; Gyan, 2020). Itikadi hii ya kutawaliwa kwa mwanamke katika methali za Kiswahili imejadiliwa katika sura za awali. Hata hivyo, zipo methali za Kiswahili zenye ukinzani wa itikadi zinazoangazia suala la uongozi na mamlaka.  Baadhi ya methali hizo zinabainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 54: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Uongozi na Mamlaka**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Amemfanya mumewe ng'ombe ya shemere. |
| 2. | Udhaifu wa mume humpa mke kiburi. |
| 3. | Kuku jike hawiki penye jogoo. |

Methali ya (1) inahusu mwanamke ambaye anamfunga shemere mume wake mithili ya ng'ombe. Shemere ni chuma kinachowekwa kwenye pua ya ng'ombe ili kumwongoza na kumdhibiti. Katika muktadha wa utafiti huu, methali hii

inambainisha mwanamke ambaye anamuongoza na kumdhibiti mume wake kwa nguvu. Mwanamume hatarajiwi kudhibitiwa kwa njia hiyo na kuonekana kuwa dhaifu. Mwanamume kulingana na mila ya Waswahili anapaswa kuonesha nguvu na mamlaka kwa mke wake. Sifa hizi zinamfanya mwanamume kuonesha uwezo wake, na siyo kubururwa kama ng'ombe aliyefungwa shemere. Hii ni itikadi inayodhihirika kwenye mfumo wa kuumeni. Murithi (2017) anasema kwamba mfumo wa kuumeni ni mfumo wa kijamii ambao unaamini kuwa wanaume ni wenye nguvu, wenye mamlaka na ni a bora katika nyanja mbalimbali, kama vile uongozi, siasa na hata katika familia kuliko wanawake. Itikadi hii inabainika katika methali ya (2) ambapo inaelezwa kuwa mwanamume hapaswi kuwa dhaifu kwa sababu anapoonyesha udhaifu huo mke wake humdharau na kumuonesha kiburi.

Miongoni mwa sifa zinazomfanya mwanamume kuwa dhaifu ni kutokuwa na sauti katika familia yake, kutokuwa na msimamo na kutofanya maamuzi. Atadhihirika kutokuwa na uhuru wa kutekeleza maamuzi kama kiongozi katika familia na hatimaye kuchukuliwa kuwa dhaifu na kudharauliwa na mke wake, jambo linalofanya mke kuwa na ujeuri. Kuhusu methali hizi mbili, kunaibuka ukinzani wa kiitikadi. Methali ya (1) inabainisha mwanamke ambaye anaongoza na kudhibiti mume wake na methali ya (2) ambayo inaonyesha mwanamume hapaswi kuwa dhaifu mbele ya mke wake, Anafaa kuwa na mamlaka ili aweze kudhibiti mke wake. Pamoja na hayo, methali (3) inaeleza itikadi ya mwanamke kuwa hapaswi kutoa sauti yake mbele ya mwanamume. Mwanamume uamuzi anaofanya ni wa mwisho. Kwa upande mwingine itikadi inayoibuliwa katika methali ya (1) inasawiri mwanamke ambaye ana mamlaka na uwezo wa kudhibiti

mwanamume kwa 'shemere'. Huu ni ukinzani wa kiitikadi unaoibuliwa kati ya methali hizi mbili.

### 6.2.6 Suala la Maslahi

Mwanamke anawasilishwa katika tafiti kadhaa kama anayepaswa kushughulikia maslahi ya mwanamume (Kaole, 2018). Itikadi hii inawachukulia wanawake kama chombo cha kuhudumia wanaume, kuwabagua na kuwatengea nafasi ya chini kuliko wanaume (Lee, 2015). Maoni haya yanaendelezwa na Kaole 2018: kwamba:

> Mwari hufunzwa jinsi ya kutunza ndoa yake
> kwa kumpa mume mahitaji yake yote kama
> kumpa chakula cha ndoa na kumridhisha

Katika jamii ya Waswahili, itikadi hii ipo lakini pia kuna itikadi ambayo inakinzana nayo katika methali za jamii ya Waswahili. Itikadi kinzani inadhihirisha kuwa ni wajibu wa mume kutunza mke wake vizuri na kumuangalilia maslahi yake.

**Jedwali 55: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Maslahi ya Mume na Mke**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Ametoa nguo jogoo mkewe hakuzipata. |
| 2. | Mke wa kwanza ni kama mama. |
| 3. | Anayenyimwa ugali na mkewe huvunja nyumba. |

Methali ya (1) inarejelea jogoo ambaye anawapa nguo wanawake wengine badala ya kumjali mke wake. Jogoo ni kuku dume ambaye anawakilisha wanaume wanaotelekeza majukumu ya kutunza wake zao kwa kuwajali wanawake wa nje ya ndoa. Methali hii inamrejelea mume ambaye anashindwa kumhudumia mke wake. Mume huyo anaishia kupeleka huduma ambazo zinapaswa kuwa za mke

wake kwa mahawala. Kulingana na itikadi katika methali hii, mwanamume anapaswa kutoa huduma na kuzingatia maslahi ya mke wake. Methali ya (2) inabainisha umuhimu wa kumtunza mke wa kwanza vizuri. Itikadi inayoibuliwa katika methali hii ni kinyume na itikadi ya methali ya (1) ambayo inamhusu mume anayemtelekeza mke wake kwa kutunza wanawake wengine ilhali methali ya (2) inamtaka mwanamume kumtunza mke wake wa kwanza kama mama yake mzazi. Wanaume wanapopata wake wengine wanasahau majukumu yao ya kuwatunza waze zao wa kwanza na wanaishia kuwatelekeza (Wamitila, 2009).

Methali ya (3) inayohusu mke kumnyima mumewe ugali kunaweza kusababisha kuvunjika kwa familia. Itikadi katika methali hii ni kwamba, mwanamke ana jukumu la kujali mahitaji ya mume wake iwapo anataka ndoa yake idumu. Aidha, kwa kufanya hivyo ataishi kwa amani na mume wake kwa sababu atakuwa ameshughulikia mambo muhimu ipasavyo. Tatizo litatokea pindi mke anapofanya kinyume chake, yaani kushindwa kutekeleza wajibu wake kwa mumewe.

Methali hizi mbili kwa kuzichunguza, mume anabainika kutomwajibikia mke wake (katika methali (1). Itikadi inadhihirisha kutohukumiwa kwa mwanamume kuhusu kumhudumia mke wake ilhali methali ya (3), mke asipowajibika kwa kuzingatia masilahi ya mume wake, athari yake inabainika. Kitendo hicho kinasababisha kuvunja ndoa yake. Hivyo, itikadi katika methali ya (1) na ya (3) zinakinzana. Ukinzani huo unadhihirisha kuwa mwanamume halaumiwi kwa kutelekeza na kutomhudumia mke wake lakini kwa upande wa mwanamke analaumiwa kwa kushindwa majukumu yake kwa mume wake. Mwanamume

anachukulia kuwa huduma za mke kwake ni haki. Ukinzani huu unaonesha mamlaka ya mwanamume na ubabedume alio nao katika jamii. Mawazo haya yanaungwa mkono na Malenya na wenzake (2020). Malenya na wenzake wanasema kwamba wanawake wanashughulikia kazi muhimu katika jamii lakini wanasawiriwa kwa mtazamo hasi na mwanamume anajipatia uwezo mkubwa wa kumtawala mwanamke.

### 6.2.7 Suala la Wakwe

Wakwe wanachukua nafasi ya kuwaelekeza watoto wao namna ya kuishi katika ndoa. Katika jamii ya Waswahili, wazazi wanakuwa washauri muhimu wa ndoa za watoto wao (Sengo, 1992). Ingawa wakwe kwa upande mwingine, wanachukuliwa kuwa wenye kusababisha matatizo kwenye ndoa za watoto wao (Chapman, 2015). Chapmana anasisitiza zaidi kwamba, wanandoa wanapaswa kuwa makini kwa kuweka mikakati ya kuishi na wakwe zao kwa amani kwa ajili ya ufanisi wa ndoa zao. Ufanisi wa ndoa kwa upande mmoja na kusambaratika kwake kunategemea mahusiano na wakwe (Owu, 2019). Methali zifuatazo za Kiswahili zinaibua itikadi ambazo zinakinzana kuhusu suala la wakwe:

**Jedwali 56: Methali kuhusu Itikadi Kinzani kuhusu Wakwe**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Kijicho cha mkwe hakiachishi mume. |
| 2. | Chui naye ana mkwe. |
| 3. | Mama mkwe hafungui mdomo. |

Methali ya (1) inamrejelea mkwe ambaye anaonesha wivu na kutotaka mafanikio ya mkazamwana wake. Methali inaeleza kwamba, tabia ya aina hii ya mkwe haifai kuharibu mapenzi ya mke na mume kiasi cha kuwatenganisha. Itikadi

inayobainika ni kwamba wakwe huwa na tabia ambazo zinaweza kuchangia kuvunjika kwa ndoa; kwa hivyo, wakwe sio watu wa kutegemewa. Methali ya (2) inamaanisha kwamba chui anayechukuliwa kuwa ni mnyama mkali na yeye ana mkwe. Kulingana na itikadi inayobainika katika methali hii, mume wa fulani anayewakilishwa na chui anapaswa kuwa na uhusiano mwema na wazazi wa mke wake. Uhusiano huu unaendeleza ushirikiano na amani na wakwe, tofauti na methali ya (1) ambayo inabainisha uhasama wa wakwe. Aidha, methali ya (3) inabainisha itikadi ya mama mke kuwa hapaswi kuingilia mambo ya kindoa ya watoto wake kwa kusema maneno ovyoovyo. Itikadi hii inamaanisha kwamba mama mkwe ajihadhari na maneno ambayo yanaweza kuvunja ndoa ya mwanawe. Aidha, mama mkwe asijiingize kwenye masuala ya ndoa ya watoto wake. Maamuzi kwenye ndoa ni kati ya wanandoa. Itikadi katika methali hizi, yaani ya (1) na ya (3) zinaibua ukinzani ambapo kwamba mkwe anaonesha kijicho kwa kujihusisha katika ndoa ya mwanawe; na kwamba mkwe anatarajiwa kunyamaza, kuwa mwangalifu na kutojihusisha katika ndoa ya watoto wake, mtawalia.

### 6.2.8 Suala la Uwajibikiaji wa Majukumu

Mwanamke anachukuliwa kama kiumbe dhaifu sana sana katika jamii za Kiafrika. Itikadi hii inaelezwa na wasomi mbalimbali (Kerschen, 1998 Hussein, 2009; Lee, 2015 Gyan, 2020). Mwanamke anatambuliwa kama anayepaswa kuhimiliwa na mume ili kuweza kutekeleza majukumu yake na mwanamume anaelezewa kama mwenye nguvu za kimwili na hatimaye kubainika kama kama kiumbe anayechukua nafasi ya mbele. Katika methali za Kiswahili zifuatazo,

kunaibuka ukinzani wa itikadi hii tofauti na uwezo na majukumu kati ya wanaume na wanawake vile yanabainishwa na tafiti za awali:

**Jedwali 57: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Uwajibikiaji wa Majukumu**

| Na. | Methali za Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Mama msaji baba msonobari |
| 2. | Mke hulia kabla ya kuolewa na mume hulia baada ya kuoa. |

Methali ya (1) inamlinganisha mwanamke na msaji ambao ni aina ya mti unaotoa mbao mgumu. Mwanamume analinganishwa na mti wa msonobari ambao ni laini na unaotoa mbao ambazo zinatumiwa kutengeneza samani za thamani. Kulingana na matumizi ya istiari hizi za msaji na msonobari, mwanamke anabainishwa kama mwenye uwezo wa kuhimili majukumu mengi ya kifamilia anayotengewa. Majukumu hayo anayoshughulikia yanadhihirika kuwa mazito na yanayohitaji mtu mwenye nguvu. Kulingana na ufafanuzi huu, mwanamke anabainika kuwa na uwezo wa kipekee wa kumudu majukumu ya nyumbani. Hivyo, itikadi inayochukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu si sahihi kama Sagheer na Zubair (2020) wanavyoonyesha kwamba maendeleo ya jamii hayazingatii ujinsia. Wanathibitisha madai yao kwa kunukuu methali ya Kimarekani kwa kumrejelea (Kerschen, 1998) kwamba:

‘Mama yako huvaa buti za kivita’

Itikadi inayodhihirisha kwamba ujenzi wa jamii ambayo ni kazi nzito, wanawake wanapaswa kushiriki. Itikadi hii inakinzana na jinsi mwanamke anavyosawiriwa

kama kiumbe dhaifu. Udhaifu huu ambao mwanamke kama unavyoendelezwa na jamii ni wa kusingiziwa.

Methali ya (2) inaibua ukinzani yenyewe katika sehemu zake mbili. Sehemu ya kwanza inamhusu mwanamke anayelia kabla ya kuolewa. Mhojiwa LMU 2 tarehe 16/05/2018 alisema kwamba mwanamke kulia kabla ya ndoa kunaashiria kutamani ndoa ili aishi na mume wake. Upande wa pili wa methali unamweleza mwanamume ambaye analia baada ya kuoa. Mume kulia baada ya kuoa kunaashiria majukumu mengi anayopaswa kuyawajibikia. Itikadi hii inamaanisha kwamba mume anawajibika kutunza familia na kuangalia maslahi ya mke wake. Kwa hivyo, anakuwa na kibarua kigumu; na mke kwa upande wake anapata afueni kwa kutohangaika. Methali hii ina ushawishi wa kuwafanya wanawake wakubali kuwa wanaume wana majukumu mengi. Hali hii inawafanya wasihoji kuhusu majukumu wanayobeba kwa upande wao.

**6.3 Hitimisho**

Kupitia Nadharia ya Udenguzi, methali za Kinyankole na Kiswahili zimechunguzwa. Katika methali hizi kumeibuka ukinzani wa itikadi za kiuana. Uhakiki wa kiudenguzi umesaidia kuibua itikadi za kiuana ambazo zinakinzana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Itikadi hizo ambazo zimeibuliwa na kudhihirisha ukinzani katika methali zinaathiri mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake kwa njia chanya ingawa itikadi hizi chanya zimekuwa zinafunikwa na itikadi za mfumo wa utawala wa wanaume. Imebainika pia kwamba maana zinazoibuliwa na itikadi za kiuana kulingana na nadharia ya udenguzi, zinaathiri usawa wa kiuana kwa njia tofauti; si kwa udunishaji tu wa

wanawake na kuwakweza wanaume kama inavyodaiwa na tafiti za awali. Ukinzani huu wa itikadi za kiuana kama unavyoibuka katika methali za Kinyankole na Kiswahili umechangia kuelewa zaidi mahusiano ya wanaume na wanawake. Mahusiano hayo yanajikita kwenye utekelezaji wa majukumu kati ya wanawake na wanaume na haki stahiki ya wanaume na wanawake. Ukinzani unabainisha mseto wa itikadi, yaani ubadilikaji wa itikadi za kiuana kuhusu haki za wanaume na wanawake, hadhi zao katika jamii pamoja na utekelezaji wa majukumu yao. Kuna ukinzani wa itikadi za kiuana unaobainisha upendeleo wa wanaume dhidi ya wanawake. Ukinzani huu unaakisi uhasi katika utekelezaji wa majukumu kwa wanawake, kulaumiwa kwa wanawake, kuathirika kwa wanawake ilhali wanaume wanaendeleza uimarishaji wa ubabe. Kuna methali ambazo zinaibua ukinzani unaobainisha haja ya kushirikiana kwa wanaume na wanawake, asasi ya ndoa kuwa na changamoto zake licha ya ndoa kuchukuliwa kuwa ni jambo zuri na linalotamaniwa, mamlaka ya wanaume na wanawake kuwa na uwezo wa kuongoza, malezi ya watoto kama jukumu la wazazi wa pande zote, tofauti na inavyobainika katika tafiti nyingi za awali kwamba malezi ni jukumu linalotengewa wananwake.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.0 Utangulizi

Katika sura ya sita ukinzani wa itikadi za kiuana umebainishwa na athari zake kwa usawa kati ya wanaume na wanawake. Mtafiti amefanya hivi kwa kuhakiki methali za Kinyankole na Kiswahili. Katika sura hii, muhtasari wa utafiti unaelezwa kwa kurejelea kila sura, matokeo ya utafiti na mchango wake pamoja na changamoto na mapendekezo kuhusu maeneo mengine ya kufanyia utafiti kuhusu itikadi za kiuana.

## 7.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura saba. Sura ya Kwanza inazungumzia misingi ya utafiti kwa kurejelea mawazo ya kiulimwengu, Kiafriaka, Afrika Mashariki na jamii mahususi za Wanyankole na Waswahili kuhusu itikadi za kiuana na mchango wa methali katika utafiti wa kitaaluma hasa katika suala la uana. Pia, suala la utafiti limedhihirishwa. Utafiti umelenga kuchunguza itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Malengo mahususi yamekuwa ni: Kubainisha itikadi za kiuana zinazojitokeza katika methali za Kinyankole na Kiswahili; Kuchunguza namna itikadi za kiuana zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana pamoja na kuhakiki namna methali za Kinyankole na Kiswahili zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana. Isitoshe, upeo wa utafiti umejadiliwa na kuonesha kuwa methali za Kinyankole na Kiswahili zinazohusu uana ndizo zimetafitiwa.

Sura ya Pili imelenga yale yaliyokwishaandikwa yenye uhusiano na itikadi za kiuana. Maandishi haya yametengwa katika mafungu kulingana na dhana muhimu za utafiti. Dhana hizo ni itikadi, uana na methali. Imebainika kupitia tahakiki kuhusu itikadi za kiuana na methali kwamba utafiti kuhusu itikadi za kiuana hususani jinsi zinavyoendeleza mahusiano ya kiuana kwa kuchagiza ukubalifu na ushawishi pamoja na ukinzani wa itikadi za kiuana ulikuwa haujafanywa kabla. Katika sura hii pia tumewasilisha na kujadili nadharia ambazo zimetumiwa katika utafiti huu. Hizi ni; Nadharia ya Itikadi, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika Steady na Nadharia ya Udenguzi. Mihimili ya nadharia hizi imeweza kutuongoza katika uhakiki wa yaliyoandikwa kuhusu mada, kukusanya data, uchanganuzi wa data, kuwasilisha matokeo ya utafiti na hatimaye kuhitimisha.

Sura ya Tatu, inaangazia utaratibu na mbinu ambazo zimetumiwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data na hatimaye kuiwasilisha na kuhitimisha. Mbinu za maktabani na nyanjani zimetumiwa. Pia sampuli lengwa imebainishwa kuwa ni vitabu vya methali. Njia ya kimakusudi ya sampuli mkufu imetumika kama mbinu ya usampulishaji. Pia, taratibu umetumiwa katika ukusanyaji wa data na uteuzi wa vifaa vilivyotumika umefafanuliwa. Pamoja na hayo, njia ya kimaelezo ambayo imetumika kuchanganua data imefafanuliwa. Aidha, namna suala la maadili ya utafiti lilivyozingatiwa limefafanuliwa.

Katika Sura ya Nne, itikadi za kiuana zinazojitokeza katika methali za Kinyankole na Kiswahili zimebaininishwa. Imebainika kuwa itikadi za kiuana zinadhihirisha wanaume kuwa na majukumu, hadhi na haki tofauti na wanawake.

Nafasi hii ya wanawake na wanaume katika jamii hujikita katika mila za utamaduni wa jamii ambapo wanaume wanakuwa na hadhi na mamlaka ya juu huku wanawake wakichukuliwa kama raia wa daraja la pili. Imebainika kuwa itikadi za kiuana zinaimarishwa na ukubalifu na ushawishikaji kuhusu utekelezaji wa majukumu, haki na hadhi wanazoshikilia wanawake na wanaume katika jamii. Wanawake wanakubali kuwatumikia wanaume kwa 'hiari'. Imedhihirika kuwa itikadi za kiuana zinazojadiliwa zinajikita kwenye itikadi kuu ya utawala wa ubabe-dume.

Uchunguzi katika Sura ya Tano, unalenga namna itikadi za kiuana zinavyodhihirisha mahusiano ya kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Methali ambazo zimechanganuliwa katika Sura ya Nne zimerejelewa ili kutimiza lengo letu katika sura hii. Vilevile, uchanganuzi wa data, umewekwa katika mada kuu za: itikadi za kiuana kuhusu ndoa; itikadi za kiuana kuhusu kuzaa; itikadi za kiuana kuhusu malezi ya watoto; itikadi za kiuana kuhusu uzalishaji wa mali; itikadi za kiuana kuhusu uongozi na mamlaka pamoja na itikadi za kiuana kuhusu ukuzaji wa jamii kwa mujibu wa malengo wa utafiti. Imedhihirika kuwa methali zinaendeleza itikadi za kiuana za ubaguzi wa kiuana kati ya mwanamume na mwanamke kwa ukubalifu na ushawishi unaowaweka wanawake kwenye nafasi ya kuwatumikia wanaume kwa utiifu. Majukumu ya wanawake wanayotekeleza pia ni kutokana na ukubalifu ambao ni ung'amuzi-potofu.

Sura ya Sita inahusu uhakiki wa methali za Kinyankole na Kiswahili na kuibua ukinzani wa itikadi za kiuana na athari zake kwa usawa wa kiuana. Ukinzani katika sura ya sita umerejelewa kama ukweli mwingine unaoibuka kupinga ukweli uliopo au ukweli unaosemwa katika methali. Imebainika kwamba methali za Kinyankole na Kiswahili zinaibua ukinzani wa itikadi za kiuana. Ukinzani huu umedhihirika kwa kuongozwa na Nadharia ya Udenguzi ya Derrida (1960). Kuna itikadi zinazolenga usawa wa kiuana kati ya wanaume na wanawake katika vipengele vya uzazi, malezi, ndoa, uongozi, kazi na ukuzaji wa jamii kijamii. Tumeonesha jinsi itikadi hizo zinavyopotoshwa na itikadi zenye nguvu za ubabedume kwa njia ya kimakusudi. Tumeongozwa na Nadharia ya Itikadi kufikia matokeo haya. Aidha, katika sura hii imedhihirika namna ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili unavyoathiri usawa wa kiuana. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ya Steady (1981), imedhihirika kuwa ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili unaathiri usawa wa kiuana kwa njia tofauti. Athari hizi mbalimbali zinajikita kwenye nyanja za kijamii, kiuchumi na utawala kupitia vipengele kama vile; uzazi, malezi, utunzaji wa watoto na ndoa; uzalishaji wa mali; uongozi na mamlaka pamoja na ukuzaji wa jamii. Methali zinaeleza itikadi hizi kinzani na kuonesha kuwa wanawake na wanaume wanapaswa kushirikiana katika kutekeleza majukumu yao bila upendeleo, kwa mfano kuzaa watoto wengi kwa wanawake kunahatarisha maisha yao.

### 7.2 Matokeo na Mchango wa Utafiti

Katika lengo la kwanza, itikadi za kiuana zimedhihirishwa katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Imebainika kwamba itikadi za kiuana zilizo na msingi

wa ubabedume zinaendeleza kutawaliwa kwa wanawake kimakusudi kwa njia ya ukubalifu na ushawishi kuhusu masuala ya uzazi; malezi na utunzaji wa watoto; ndoa; kazi; uongozi na mamlaka pamoja na ujasiriamali. Itikadi za kiuana zinaendeleza kutenga na kugawa majukumu kwa misingi ya kiuana, kutengwa kwa mwanamke, kudhulumiwa haki za mwanamke na kudhalilishwa kwake kupitia ukubalifu na ushawishi wake. Wanawake wamedhihirika kama binadamu wa daraja la pili katika jamii na wanachukulia itikadi hizi kuwa za kawaida ilhali ni ung'amuzi potoshi.

Lengo la pili limeangazia ni namna gani itikadi za kiuana zinadhihirisha mahusiano ya kiuana kati ya mwanamke na mwanamume katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Mahusiano yanayoendelezwa na itikadi za kiuana ni ya kumtaka mwanamke kuendeleza majukumu yake akiwa chini ya mamlaka ya mwanamume, haki zake kudhulumiwa na kuchukuliwa kama binadamu wa kiwango cha chini. Mahusiano ya aina hiyo yanaendelezwa kupitia uzazi, malezi, ndoa, uongozi na mamlaka, kazi pamoja na ukuzaji na maendeleo ya jamii kwa misingi ya kijamii. Mahusiano haya yanaendelezwa na imani ambazo zinajikita kwenye utawala wa mfumodume. Mwanamke anakubali na kushawishika kuwa jukumu na nafasi yake ni kumtumikia na kumtii mwanamume.

Katika jamii ya Waswahili, itikadi ya haja ya upatikanaji wa watoto wengi pia imebainika kuwemo katika methali zao. Katika methali hizo imedhihirika kuwa kupata watoto huleta faraja katika familia. Pia, ni faraja kwa kuwa watoto, hususani wa kiume wanakusudiwa kuendeleza majukumu ya familia wakati baba

yao amefariki. Mwanamke haaminiwi na kupewa dhamana ya kuendeleza familia baada ya kifo cha mume wake. Pia, mwanamke anabainika kama asiye na mamlaka juu ya maamuzi fulani baada ya kifo cha mume wake; badala yake watoto wa kiume ndio wanatarajiwa kubeba 'mikoba hiyo'. Kwa ujumla, mahusiano ya kiuana kuhusu suala la uzazi katika methali za Kinyankole na Kiswahili yanaendelezwa na itikadi ya ukubalifu na ushawishi wa mwanamke kuzaa watoto wengi na kuwathamini watoto wa kiume. Itikadi hizi zinaendelea kushadidia kuwa mwanamke yuko chini ya mwanamume. Wanawake kubainishwa kama viumbe wasio na mamlaka kuhusu uzazi ni itikadi inayotokana na amali za kijamii kwa njia ya ukubalifu.

Aidha, katika lengo la tatu, uhakiki wa methali za Kinyankole na Kiswahili umefanywa kuhusu namna methali zinavyoibua ukinzani wa itikadi za kiuana pamoja na kujadili athari zake kwa usawa wa kiuana. Imebainika kuwa kuna methali za Kinyankole na Kiswahili zinazoibua ukinzani. Ukinzani unaobainishwa na methali hizo unaonesha nafasi chanya ya mwanamke, mahusiano ya ushirikiano wa mwanamke na mwanamume katika utekelezaji wa majukumu, umama wa mwanamke pamoja na mwanamke anayepaswa kuwa na haki stahiki na nafasi yenye hadhi katika jamii. Methali zinadhihirisha haja ya kurekebisha itikadi zinazowabagua wanawake, na itikadi zinazodhihirisha wanawake kunyimwa uhuru wa kujichagulia. Itikadi za kiuana ambazo zimeibuliwa zimejadiliwa kwa kuzingatia mada zifuatazo: Itikadi za kiuana kuhusu kuzaa na malezi ya watoto, Itikadi za kiuana kuhusu ndoa, Itikadi za kiuana kuhusu uzalishaji wa mali, Itikadi za kiuana kuhusu uongozi na mamlaka pamoja na itikadi za kiuana kuhusu ukuzaji wa jamii kwa misingi ya kijamii.

Maana ambazo zinaibuliwa zimefikiwa kwa kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya Itikadi, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika pamoja na mhimili ya Nadharia ya Udenguzi unaosema kuwa matini ya kifasihi inaibua maana anuwai. Ukinzani wa itikadi za kiuana katika methali umeibuliwa kulingana na Nadharia ya Udenguzi ambapo maana anuwai za methali zimeibuliwa kulingana na muktadha wa uana. Itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili zimebainika kuwa zinabadilika kulingana na mahitaji na hali ya kijamii na kiuchumi.

Imebainika kuwa  ukinzani wa itikadi za kiuana unaathiri usawa wa kiuana kwa njia tofauti.  Athari hizi mbalimbali zinajikita kwenye nyanja za kijamii, kiuchumi na kiutawala kupitia vipengele vya uzazi, malezi, utunzaji wa watoto na ndoa; uzalishaji wa mali; uongozi na mamlaka pamoja na ukuzaji wa jamii. Itikadi zinazokinzana katika methali zinaonesha kuwa wanawake na wanaume wanapaswa kushirikiana katika kutekeleza majukumu yao bila upendeleo, kwa mfano kuzaa watoto wengi kwa wanawake kunahatarisha maisha yao. Aidha, watoto wanaozaliwa wana thamani inayolingana bali si kupendelea jinsi moja dhidi ya nyingine. Imedhihirika pia malezi ya watoto yanahitaji ushirikiano wa mwanamume na mwanamke na kuvumiliana kwenye ndoa.

Pia, utafiti huu umechunguza kama kuna usawa wa kiuna unaobainishwa na itikadi tofauti zinazoibuliwa na methali kinzani kwa kuzingatia suala la uzazi, malezi, utunzaji wa watoto na ndoa; Uzalishaji wa mali; uongozi na mamlaka pamoja na ukuzaji wa jamii. Imebainika  kuwa ukinzani unaoibuliwa katika methali za Kinyankole na Kiswahili unawaweka wanawake kwenye nafasi za kimamlaka, uhuru na hadhi sawa na wanaume katika nyanja mbalimbali. Hata

hivyo, imebainishwa kuwa itikadi za kiuana zenye mfumodume zina ushawishi mkubwa wa kuhalalisha mamlaka, hadhi na uhuru wa wanaume kama jambo la kawaida na kugubika itikadi zinazoendeleza usawa wa kiuana. Wanawake kama kundi tawaliwa wanakubali kutawaliwa na kuonekana kama raia wa daraja la pili katika jamii. Kwa kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya Udenguzi, tumebaini kuwa ukinzani wa itikadi za kiuana unampatia mwanamke nafasi ya kutekeleza majukumu yake kwa uhuru. Aidha, mwanamke anabainika kuwa na haki na hadhi sawa na mwanamume kuhusu utekelezaji wa majukumu ya malezi na utunzaji wa watoto katika jamii. Itikadi zenye mfumodume zinamshawishi na kumfanya akubali majukumu anayotengewa kama mwanamke kupitia vipengele kama vile kuzaa watoto, malezi na utunzaji wa watoto, ndoa, wazazi wa kambo, uongozi na mamlaka, utekelezaji wa majukumu na kazi.

Kupitia uhakiki wa methali za Kinyankole na Kiswahili imegunduliwa kwamba itikadi za kiuana zenye msingi wa mfumodume ni kikwazo kuhusu usawa wa kiuana kati ya wanaume na wanawake. Kusawazisha mahusiano ya kiuana kati ya wanaume na wanawake ni njia ya kutafuta usawa wa kiuana kama anavyoeleza Ssetuba (2005).

### 7.3 Changamoto za Utafiti

Kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo zimeibuka katika mchakato wa utafiti huu, hususani wakati wa kukusanya data. Imemuwia vigumu mtafiti kuwapata wasailiwa wenye maarifa asilia wa Kiswahili kwa sababu wengi wameathiriwa na usasa.

Ufafanuzi wa methali umeathiriwa na mabadiliko ya kisasa. Wahojiwa wamekuwa hawajikiti katika mila asilia za Waswahili hasa kwa upande wa wasailiwa wa kike ambao wamepata mwamko wa usawa. Ufafanuzi wa kimuktadha kiutamaduni unafifia kwa sababu ya mitazamo ya kiuana ya kisasa iliyo na athari za Kimagharibi, hasa kwa wanawake wasomi.

Katika maeneo ya Lamu, kuwahoji wasailiwa wa kike ilikuwa vigumu kwa mtafiti kwa sababu mila na utamaduni hauruhusu kutangamana na wanaume. Katika jamii ya Waswahili wenye msingi wa dini ya Kiislamu ni nadra wanawake kuruhusiwa kuwa katika maeneo ya umma au kutangamana na jinsi ya kiume.

Aidha, ratiba ya mtafiti na wasailiwa ilitatizwa kiasi kwa sababu ulikuwa ni mwezi mtukufu wa Ramadhani ambapo mikutano ya baada ya Adhuhuri haikuwezekana kuendelea jinsi ilivyokuwa imepangwa.

Hata hivyo, njia anuwai zilitumika kutatua changamoto hizo kwa kuzingatia muktadha wa kila tatizo lililoibuka. Miongoni mwake, Mtafiti alitumia watafiti ndugu zao kama watafiti wasaidizi kuwafikia na kupata data kwa njia ya kurikodi maoni yao. Pia, mtafiti aliendesha mahojiano kwa njia ya simu. Kwa mfano, mtafiti aliweza kumhoji msailiwa, mwandishi wa Dafina Hazina ya Kiswahili, kitabu cha methali kwa njia ya simu. Mwandishi huyo kwa sasa anaishi Omani. Kitabu chake kimetusaidia sana kuchambua methali hizo.

## 7.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu inapendekezwa kwamba, methali za Kinyankole na Kiswahili zinazodhihirisha itikadi dhalilishi kwa wanawake zitafitiwe na kuchanganuliwa zaidi kwa kuzihusisha na hali ya kisasa ya jamii ya Wanyankole na Waswahili. Uchanganuzi huo uibue uamilifu wa methali kwa njia chanya kimakusudi ili kuweza kusuluhisha changamoto za kiuana katika jamii za Wanyankole na Waswahili zinazobadilika, kwa sababu methali ni hazina ya jamii na ni kauli zenye hekima katika jamii. Vilevile, methali zinabeba mafundisho na falsafa ya Wanyankole na Waswahili, utamaduni na mila zao. Kwa hivyo, zinapaswa kuendeleza thamani hiyo, yaani 'kauli zenye hekima'. Hekima kupitia methali haiwezi kuendelezwa kwa njia hasi na kudhalilisha binadamu kwa njia yoyote ilhali ikaendelea kurejelewa kama hekima.

Kwa vile methali hazifai kubadilishiwa miundo yake kutokana na umuhimu wake wa kuhifadhi utamaduni wa jamii, kuna haja ya kuzitathmini kwa mtazamo mpya ili ziafikiane na matarajio ya jamii.

Pia, kuna haja ya kuendeleza tafiti za uana kwa kuhusisha mafundisho ya dini na amali za kitamaduni kulingana na muktadha wa kisasa wa jamii za Wanyankole na Waswahili. Hii ni kwa sababu jamii zinabadilika kulingana na mahitaji na wakati. Analojia ya kitunguu inabainisha hoja hii kama Lovenduski na Norris (1996) wanavyosisitiza. Wanasema kwamba, ganda la kitunguu linapoambuka jingine bichi linajitokezea. Kwa njia hiyo, jinsi ambavyo kitunguu kina magamba yake, ndivyo mahusiano ya kiuana yana magamba yake kati ya mwanamke na mwanamume katika jamii za kisasa. Hii itasaidia kuendeleza mitazamo na itikadi

za kiuana zenye malengo jumuishi yaliyo na misingi katika usawa wa kiuana bila kuzingatia maumbile ya mtu na upendeleo wa kijinsi. Mwanamke kuwa wa jinsi ya kike au mwanamume kuwa wa jinsi ya kiume si hatia inayostahili adhabu ya aina yoyote kutoka kwa binadamu mwenzake.

Katika utafiti huu imedhihirika nyanjani kuwa vurugu za kiuana na kuvunjika kwa familia katika jamii ya Waswahili na Wanyankole zimekithiri na kuna ukuruba na itikadi za kiuana. Huvyo, ni muhimu kutafitia zaidi itikadi za kiuana, hususani namna zinavyoathiri saikolojia ya wanaume na wanawake katika kuzusha vurugu za kiuana na kusambaratisha familia.

Aidha, jamii ielimishwe kuhusu juhudi za pamoja za wanawake na wanaume katika kuchangia maendeleo ya jamii, malezi ya watoto nyumbani kukweza jinsi moja na kupuuza jinsi nyingine inawakuza watoto kwenye misingi ya kutofautisha majukumu na nafasi zao katika jamii. Kuna haja ya kubadilisha mtazamo huu katika ufafanuzi wa methali kulingana na mahitaji na muktadha wa jamii ya Wanyankole na Waswahili. Kulingana na mwingiliano huu wa majukumu, kuna haja ya kuongeza juhudi za kushirikiana kati ya mwanamke na mwanamume.

Kwa kuwa mila na desturi za Wanyankole na Waswahili zinafundishwa kwa watoto na kuimarisha itikadi zao kuhusu mahusiano yao katika kuwaandaa kwa majukumu yao ya baadaye, ni muhimu kuingiza mitazamo mipya iliyo na malengo ya kutanzua kiumbe binadamu na mwenziwe kwa misingi ya amali na

baadhi ya itikadi za kitamaduni ambazo zinachagiza ubaguzi wa kiuana na kudhulumiwa kwa jinsi moja kwa kutwishwa na kulemazwa na majukumu.

Inapendekezwa kuwa watafiti waendelee kuchunguza methali za kiuana katika muktadha husika bila kutupilia mbali baadhi ya methali ambazo zinaelekea kudhalilisha jinsi moja kisintaksia. Methali hizi zinaweza kupewa maana chanya katika kufafanua masuala ya uana. Hii ni kwa sababu methali ni kiwakilishi cha utamaduni wa jamii. Kuzitupilia mbali ni njia mojawapo ya kudidimiza utamaduni wa jamii.

Ndoa ni asasi iliyo na changamoto nyingi za aina yake kama ilivyobainika katika utafiti huu, hasa kwa kuzirejelea methali za Kiswahili ambazo zimeliwasilisha suala la ndoa kwa njia hiyo. Kwa hivyo, kunahitajika uamuzi na mipango ya kimakusudi baada ya kudhamiria kuoa au kuolewa ili kunufaika nalo kuliko kubahatisha. Kwa mfano, ni jambo la msingi sana watoto wa kiume na wa kike ambao wamefikia umri wa kuoana, waruhusiwe kuchumbiana wao wenyewe. Uamuzi unaofanywa na wao wa kufunga ndoa ni muhimu katika kudumisha upendo na amani ndani ya ndoa yao. Katika mila ya Waswahili, hii ndiyo ilikuwa itikadi muhimu kwa sababu ya kuchaguliwa na kuozesha/kuozeshwa. Kuwe na asasi maalumu za kuelekeza ndoa, kutoa nasaha na mawaidha kuhusu ndoa, kama ilivyo kwa makungwi wa Uswahilini. Huduma hii katika jamii ya Wanyankole haizingatiwi na huenda ndiyo sababu ya kukithiri kwa vurugu za kiuana .

Makungwi watambuliwe na wapate mafunzo zaidi kitaalamu kuhusu mahusiano ya kiuana ili waweze kuwafunda wanaohusika. Pia, kuwe na mafunzo ya aina

hiyo kwa wanaume/wavulana wanaotaka kuoa. Ndoa ni uchaguzi wa mtu kuhusu maisha yake ya baadaye. Uchaguzi usipofanywa kwa urazini kutakuwa na athari hasi za kudumu kuhusu maisha yako.

Amali na itikadi za kiuana ambazo zina sura ya ushirikiano na maridhiano zitambuliwe na kukubaliwa kwa sababu ni sehemu ya maisha ya wanajamii. Itikadi za kiuna zilizo chanya zinapoimarishwa, inakuwa rahisi kwa jamii kuendelea. Itikadi za kiuana ambazo zinachochea uhasama na chuki zibadilishwe au zitupiliwe mbali kwa sababu ni kikwazo na ziko dhidi ya haki za msingi za binadamu na hatimaye kutoendeleza jamii husika. Kwa mantiki hii, itikadi hizi ambazo zinaweza kuendeleza ubinadamu kwa kuzingatia haki za msingi bila upendeleo na ubaguzi wa kiuana zisisitizwe kwa lengo la kuimarisha usawa wa kiuana.

Mabadiliko ya mienendo na tabia za kitamaduni yatoke ndani kwa ndani. Yawe na uasilia wa Kiafrika. Mabadiliko hayo yakipuuza amali ambazo zinadhaniwa kuwa haziendani na wakati, matokeo yake ni kuingizwa kwa athari za ugeni ambazo zinachukuliwa kuwa za kisasa; kwa mfano, katika ndoa za Waswahili bibi arusi kuvaa gauni na kubadilisha taratibu za kitamaduni za kuendesha shughuli za kindoa. Athari inayobainika ya kuiga tabia kutoka nje na kuzichukulia kuwa za kisasa zinakithiri kuliko usasa ulio na misingi ya Kiafrika.

Mwanamke akiajiriwa atapungukiwa na muda, tofauti na kama alivyokuwa nyumbani kabla ya kupata kazi. Kwa hivyo muda wa kufua, kupika na majukumu mengine utapungua. Jambo hili linamuathiri mwanamume

kisaikolojia. Anafikiri mke anafaa zaidi kuwepo ili amhudumie. Kisaikolojia, anaambiwa na akili yake kwamba kazi hii imembadilishia utaratibu wa maisha. Jambo hili litapingana na matarajio ya mumewe na jamii kwa ujumla. Hivyo, ni muhimu kutambua kuwa maisha hubadilika. Nafasi ya baadhi ya itikadi hizi za kiuana katika jamii inafaa kubadilishwa ili kuendana na wakati. Mahitaji ya jamii za kisasa yanabadilika hasa katika nyanja za kiteknolojia, kiuchumi, na kielimu.

### 7.5 Hitimisho

Utafiti huu umedhihirisha uwepo wa itikadi za kiubabedume katika methali za Kinyankole na Kiswahili. Itikadi hizo zinaendeleza mahusiano ya kimamlaka ya wanaume dhidi ya wanawake, mamlaka ambayo yanatokana na ushawishi wa wanaume na mila za kiutamaduni zenye mfumodume ambazo zinaendelezwa katika jamii za Wanyankole na Waswahili. Wanawake kama kundi tawaliwa wanakubali majukumu wanayotengewa kama majukumu ya msingi wanayopaswa kuyafanya. Aidha, wanawake wanashawishika kukubali nafasi yao ya kuwatumikia wanaume pamoja na hadhi yao kama raia wa daraja la pili katika jamii. Itikadi za kiuana kama zinavyobainika katika methali za Kinyankole na Kiswahili zinadhihirisha nguvu zinazoegemea upande wa wanaume. Itikadi hizi zinakandamiza ukosoaji wake. Zinachukuliwa na wanajamii kama za kimaumbile na kuendeleza tofauti katika mahusiano ya kiuana kati ya mwanamume na mwanamke pamoja na utekelezaji wa majukumu yao ya kiuana. Aidha, imebainika kwamba kuna itikadi za kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili zinazoibua ukinzani dhidi ya mahusiano ya kiuana. Wanawake wamebainishiwa nafasi zao muhimu katika kuendeleza nyumba na jamii, kushirikiana na mwanamume katika kutekeleza majukumu ya kijamii, mwenye

heshima na hadhi, wenye mamlaka na waanaopigania haki na uhuru wao, tofauti na tafiti za awali ambazo kwa mapana zimesawiri mahusiano dhalilishi ya mwanamke. Utafiti huu pia unawasilisha ukinzani wa itikadi za kiuana kuhusu mahusiano ya kiuana kati ya mwanamume na mwanamke, itikadi zinazobainisha haja ya ushirikiano kati ya mwanamke na mwanamume katika kutekeleza majukumu yao. Mwanamke amebainika akiwa na mchango mkubwa katika kuendeleza nyumba, kusetiri aibu za nyumbani, mwenye mamlaka, mchango kama mwalimu wa kwanza katika kuadabisha watoto ambao ndio kizazi cha kesho katika jamii. Methali za jamii ya Wanyankole na Waswahili zinawaonesha wanawake kama watawaliwa ambao wako chini ya mamlaka ya wanaume hata kama wanabainika kuwa na uwezo. Wanawake wanashawishika na kuikubali nafasi hii wanayotengewa kulingana na maumbile yao ya kike.

## MAREJELEO

Abdulaziz, M. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abdulla, L. M. (2016). *Athari za Itikadi katika Nyimbo za Harusi za Kizanzibari* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Abrams, J. (2012). *Blurring the lines of Traditional Gender Roles: Beliefs of African American Women* (M.Sc Thesis, Virginia Commonwealth University).

Abrams, M. H., & Harpham, G. (2014). *A glossary of literary terms*. Cengage Learning.

Al – Maawy (2009). *Waswahili na Utamaduni wao*. Lamu: Kenya.

Al-Maawy, A. (n.d.). The reconstruction of the early struggles for independence (1807-1873). The Lamu hero: The story of Bwana Zahidi Mngumi (1760-1832). Self-pu.

Al Haj, A. (2012). *Dafina- Hazina ya Kiswahili*. Haijachapishwa.

Allagbé, A. A., & Amoussou, F. (2020). Patriarchal ideologies and female un-femininities in a contemporary feminist writing: A gender-oriented and critical discourse analysis perspective. AFRREV LALIGENS: An International Journal of Language, Literature and Gender Studies, *9*(1), 13-27.

Althusser, L. (1971). Ideology and ideological state apparatuses. Lenin and Philosophy. Trans. Ben Brewster. New York: Monthly Review Press, 127-182.

Althusser, L. (1971). Preface to Capital volume one. Lenin and philosophy and other essays.

Althusser, L. (1981). Marx's new science. *Modern Interpretations of Marx, Oxford: Blackwell Publishers*.45-70.

Angella, S. (2018). *Usawiri wa Mwanamke katika Ndoa: mifano kutoka Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu na Matini teule za kidini* (Tasnifu ya Uzamifu, Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Chuo Kikuu Cha Moi).

Ardren, T. (2008). Studies of gender in the prehispanic Americas. *Journal of Archaeological Research, 16*(1), 1-35.

Arnold, F.; Choe, M. K. & Roy, T. K. (1998). Son Preference, the Family-building Process and Child Mortality in India, Population Studies: A Journal of Demography, 52(3), 301–315.

Arora, S. (1993) “A Woman and a Guitor: Variations on a folk metaphor” proverbium 10:21.

Askew, K. M. (1999). Female circles and male lines: Gender dynamics along the Swahili coast. Africa Today, 67-102.

Ba, M. (1981). *Barua Ndefu Kama Hii.* (Maganga, C. (1994) - Mtafsiri) Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Bagheri, E. (2012). *A qualitative investigation of religion, gender role beliefs, and culture in the lives of a select group of Muslim men* (Doctoral dissertation, The University of Iowa).

Bahn, G. H., & Hong, M. (2019). Shift from Wicked Stepmother to Stepmother in Eastern and Western Fairy Tales. Psychiatry Investigation, *16*(11), 836.

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Baloyi, E. M. (2013). Critical reflections on polygamy in the African Christian context. Missionalia: Southern African Journal of Mission Studies, 41(2), 164-181.

Barbara, L., & Johanna, B. (1989). Gender and social reproduction: historical perspectives: Annual Review of Sociology, (15), 383-384.

Baruah, M. (2008). The Co-Wife and Step-Mother Motifs in Folklore: A Case Study of Some Assamese Proverbs. Indian Folklife, (31).

Bates, T. R. (1975). Gramsci and the Theory of Hegemony. Journal of the History of Ideas, 36(2), 351.

Beasley, C. (2005). *Gender and Sexuality, Critical Theories, Critical Thinkers*. London SAGE Publications.

Belenky, M. F. (1997). Althusser, Louis." Ideology and Ideological State Apparatuses." Lenin and Philosophy and Other Essays. Trans. Ben Brewster. London: New Left Books, 1971. 121-73. Atkins, G. Douglas, and Michael L. Johnson, eds. Writing and Reading Dif-ferently: Deconstruction and the Teaching of Composition and. Constructing Knowledges: The Politics of Theory-Building and Pedagogy in Composition, 167.

Boserup, E. (1970). *Woman's Role in Economic Development*. New York: St. Martin's Press

Bressler, C. (2007). *Literary Criticism; an Introduction to theory and practice*: New Jersey Upper Saddle River.

Caplan, P. (1982). Gender, ideology and modes of production on the coast of East Africa. Paideuma, 29-43.

Connell, R. (2009). Gender : in world perspective. Gender, 78–96.

Copenhaver, B. B. (2002). *The portrayal of gender and a description of gender roles in selected American modern and postmodern plays*. East Tennessee State University.

Cox, R. W. (1983). Gramsci, hegemony and international relations: an essay in method. Millennium, 12(2), 162-175.

Craig, L. (2006). Does father care mean fathers share? A comparison of how mothers and fathers in intact families spend time with children. Gender & society, 20(2), 259-281.

Crehan, K. (2011). Gramsci's concept of common sense: a useful concept for anthropologists?. Journal of Modern Italian Studies, 16 (2), 273-287.

Creswell, J. W.(2014). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches*. Sage publications.

Cuddy, A., Crotty, S., Chong, J., & Norton, M. (2010). Men as cultural ideals: How culture shapes gender stereotypes (Working Paper 10-097). Cambridge, MA: Harvard Business School.

Damon, W., Lerner, R. M., & Eisenberg, N. (Eds.). (2006). *Handbook of child psychology, social, emotional, and personality development*. John Wiley & Sons.

Davis, S. N., & Moore, S. B. (2010). Bearing children, becoming mothers: The influence of childbearing on unmarried women's gender ideology. International Journal of Sociology of the Family, 77-91.

Deka, K. (hm). The Roles, Importance and position of Female Gender in Assamese Society: analysis through the Assamese Proverbs.

Derek, N. and Thomas, S. (1985). *The Swahili: Reconstructing the History and Language of an African Society, 800-1500*. University of Pennsylvania Press, USA.

Derrida, J. (1976). Of Grammatology and Writing and Difference. (G. C. Spivak, Mtaf.). Balymore: John Hopkins.

Diabah, G., & Appiah Amfo, N. A. (2015). Caring supporters or daring usurpers? Representation of women in Akan proverbs. Discourse & Society, 26(1), 3-28.

Dipio, D. (2019). African motherhood proverbs and worldview: A matriarchal perspective. Legon Journal of the Humanities, *30*(1), 3-23.

Dwyer, D. (1978). *Images and self images. Male and Female in Morocco*. New York: Columbia University Press.

Dzahene-Quarshie, J., & Omari, S. (2021). Viewing gender through the eyes of proverbs: Reflections of gender ideology in the Akan and Swahili societies. *Journal of pragmatics*, (174) 128-142.

Eagleton, T. (1991). *An introduction to Ideology*. UK: US Library Publication.

Elam, I. (1973). *The social and sexual roles of Hima women: A study of nomadic cattle breeders in Nyabushozi county, Ankole, Uganda*. Manchester University Press.

Engles, F. (1975). The origin of the Family, Private Property and State; Moscow:Pathfinder Press. The Origin of the Family, Private Property and State; Moscow, 6, 34.

Etchezahar, E., & Ungaretti, J. (2014). Woman stereotypes and ambivalent sexism in a sample of adolescents from Buenos Aires. Journal of behavior, health & social issues, *6*(2), 87-94.

Ezeifeka, C. R. (2017). Gender stereotypes in selected Ibgo proverbs. Contemporary Journal of African Studies, *4*(2), 93-126.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. New York: Oxford University Press.

Foucault, M. (1978) Nietzsche, genealogy, history.

Garrett, S. (1987). *Gender: Society Now*. London: Tavistock Publication.

Gentile, D. A. (1993). Just what are sex and gender, anyway? A call for a new terminological standard. *Psychological science*, *4*(2), 120-122.

Gerring, J. (1997). Ideology: A definitional analysis. *Political Research Quarterly*, *50*(4), 957-994.

Ghaidan, U. (1974). Lamu: a case study of the Swahili town. *The Town Planning Review*, *45*(1), 84.

Golombok, S na Robyn F, (1994). *Gender Development*. New York: University of Cambridge.

Gower, R., Salm, S., & Falola, T. (1996). Swahili women since the nineteenth century: Theoretical and empirical considerations on gender and identity construction. *Africa Today*, *43*(3), 251-268.

Gramsci, A. (1971). Hegemony (pp. 95-123).

Greer, G. (1971). The female eunuch.

Gyan, C., Abbey, E., & Baffoe, M. (2020). Proverbs and patriarchy: Analysis of linguistic prejudice and representation of women in traditional Akan communities of Ghana. *Social sciences*, *9*(3), 22.

Haji, M. (2018). *Uchunguzi wa methali za jamii ya wamakunduchi: dhamira, fani, miktadha ya matumizi na dhima* (Tasnifu ya Uzamivu, Chuo kikuu Huria cha Tanzania) Haijachapishwa.

Hamad, K. S. (2018). *Nafasi ya Kasida za Kiswahili Katika Kumtetea Mwanamke Zanzibar* (Doctoral dissertation, The State University of Zanzibar 'SUZA').

Handayani, R. (2017). Gender Ideology in The Story of Zahra. In International Conference on Culture and Language in Southeast Asia (ICCLAS 2017) (pp. 23-26). Atlantis Press.

Hardy, B. C. (1994). Lords of creation: polygamy, the Abrahamic household, and Mormon patriarchy. *Journal of Mormon History*, *20*(1), 119-152.

Hassan, A. A. (2015). *Factors influencing the changing of gender roles among the Somali women of Garissa County* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Heywood, A. (1994). *Political ideas and concepts: An introduction*. Macmillan.

Holmes, M. (2007). What Is Gender?: Sociological Approaches, 1–209. https://doi.org/10.4135/9781446216200

Hussein, J. W. (2005). The social and ethno-cultural construction of masculinity and femininity in African proverbs. *African study monographs*, *26*(2), 59-87.

Hussein, J. W. (2009). A discursive representation of women in sample proverbs from Ethiopia, Sudan, and Kenya. Research in African Literatures, 96-108.

Ikeke, M. O. (2021). Feminist Ethics and Gender Portrayals in Urhobo (African) Traditional Music. *East African Journal of Traditions, Culture and Religion*, *3*(2), 1-10.

Jankowiak, W., Sudakov, M., & Wilreker, B. C. (2005). Co-wife conflict and co-operation. Ethnology, 81-98.

Jesee, M. J. (2017). Itikadi katika Riwaya za Awali za SA Mohamed. Kioo cha Lugha, 14(1).

Jonathan, V. (2009) Gender Ideology Construction: A life course and Intersectional Approach: Gender and society, Vol. 23, No. 3. Sage Publications, Inc.

Karata, R., Justus, M., & Mavisi, R. (2021). Vipengele Vya Ontolojia Katika Tamthiliya Za Kiswahili: Mashetani (1971) Na Kivuli Kinaishi (1990). Editon. *Consortium Journal of Kiswahili*, *3*(1), 293-306.

Kaole, U. S. (2018). *Uchanganuzi wa maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake kwa wanandoa katika jamii ya Wadigo*. (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Pwani) Haijachapishwa.

Karwemera, F. (1994). *Emicwe n'emigyenzo y'abakiga*. Kampala: Fountain Publishers.

Katrina, D. (2011). Zanzibari women's discursive and sexual agency: Violating gendered speech prohibitions through talk about supernatural sex. *Discourse & Society*, *22*(1), 3-20.

Kaveh Firouz, Z., Abbasi-Shavazi, M. J., Serajzadeh, S. H., & Ramazi, N. (2021). The Relationship between Religiosity and Family Values with Fertility Desires and Intention among Married Women in Tehran. Quarterly of Social Studies and Research in Iran, 10(2), 587-623.

Kelly, A. (1999). *Female circles & Male lines: Gender Dynamics along the Swahili Coast*. Indiana University Press.

Kennedy, E. (1973). *Destutt de Tracy and the Origins of " Ideology*". Brandeis University.

Kennedy, E. (1979). " Ideology" from Destutt De Tracy to Marx. *Journal of the History of Ideas*, *40*(3), 353-368.

Khatib, M. S. (2014). *Chanjo, Matakwa ya Mwanamume katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho wa Ushairi wa Muyaka na Shaaban Robert*. Daresalaam: TUKI

King'ei, K. G., & Ndalu, A. E. (1989). *Kamusi ya methali za Kiswahili*. East African Publishers.

King'ei, K. (2000). *Mwanakupona. Poets from Lamu*. Nairobi: Sasa sema Publications

King'ei, K. (2002). Suala la Uana katika fasihi ya Kiswahili. Uhakiki wa utafiti kutoka Kenya. *Jarida la Kiswahili*, Juzuu 65.

Kirindi, P. (2008). *History and Culture of the Kingdom of Ankole*. Kampala: Fountain Publishers.

Kishwar, M. (1996). Women and politics: Beyond quotas. Economic and Political Weekly, 2867-2874.

Kiyimba, A. (2001). *Gender Stereotypes in Folktales and Proverbs of the Baganda* (Unpublished PhD Thesis, Makerere University).

Kiyimba, A. (2005). Gendering social destiny in the proverbs of the Baganda: Reflections on boys and girls becoming men and women. *Journal of African Cultural Studies, 17*(2), 253-270.

Kobia, J. (2008). *Taswira za kiuana katika nyimbo za Tohara za Wanaume miongoni mwa Waigembe*. (Unpublished Phd Thesis, Kenyatta University).

Kochman-Haładyj, B. (2020). The vexing problem of gender stereotyping in world proverbs. *SKASE Journal of Theoretical Linguistics, 17*(1).

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Age International Publishers, New Delhi.

Kroska, A. (2007). Gender ideology and gender role ideology. The Blackwell encyclopedia of sociology.

Lee, J. F. (2015). Chinese proverbs: How are women and men represented?. *Multidisciplinary Journal of Gender Studies*, *4*(1), 559-585.

Lomotey, B. A., & Chachu, S. (2020). Gender ideologies and power relations in proverbs: A cross-cultural study. *Journal of Pragmatics*, 168, 69-80.

Lorber, J. (1994). Night to his day": The social construction of gender. Paradoxes of gender, 1, 1-8.

Lovenduski, J. na Norris, P. (Whr.) (1996). Women in Politics; New York Oxford University Press.

Lukamika, M. K., Choge, S. C., & Simiyu, F. W. (2019). Tamathali za semi zinazosawiri ubabedume katika majigambo ya miviga ya shilembe na mchezasili wa mayo ya waisukha, nchini kenya kwa mtazamo wa semantiki. East African Journal of Swahili Studies eajss.eanso.org Volume 4, Issue 1, ISSN: 1476-4687.

Mahenge, E. G. (2021). Uchambuzi wa Dhima ya Msimulizi katika Bunilizi ya Watoto ya Zindera (2008). Kioo cha Lugha, (18).

Maitaria, J. N. na Wafula, R. M. (2018). Ushairi wa Abdilatif Abdalla katika Kubainisha Utamaduni wa Waswahili. *Journal of Linguistics and Language in Education, 12*(2)

Maitaria, J. (2012). *Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali.* (Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta).

Maitaria, J., & Momanyi, C. (2016). Ushairi wa Kiswahili kama Chombo cha Ujenzi wa Utangamano wa KitaifaNchini Kenya. Kiswahili, 79(1).

Malenya, M. M., Simwa, S. P. W., & Ogola, J. O. (2020). Itikadi na Uwezo wa Kijinsia katika Nyimbo za Taarab. Editon. *Consortium Journal of Kiswahili, 2*(1), 48-60.

Malicke, J. (2013). Gender Ideology and Evaluations of a Male versus Female Target : Effects of Emphasizing versus Downplaying Gender Differences.

March, C., Smyth, I. A., & Mukhopadhyay, M. (1999). *A guide to gender-analysis frameworks*. Oxfam.

Martin, J. L. (2015). What is ideology?. Sociologia, Problemas E Práticas, (77), 9-31.

Marx, K., & Engels, F. (1975). Marx & Engels Collected Works Vol 01: Marx: 1835-1843. Lawrence & Wishart.

Mavisi, R. (2016). Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Riwaya Teule za Zainabu Burhani. *Kioo cha Lugha*, *16*(1).

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing.

Mbaabu. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar Es Salaam: Taasisi Ya Uchunguzi Wa Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam.

Mbiti, J. S. (1990). *African religions & philosophy*. Heinemann.

Mboya, L. A., Mohochi, E. S., & Kisurulia, S. (2018). Dhuluma kama kichocheo cha mzinduko wa wanawake katika riwaya ya Kiswahili.

Mbusya, C. M., & Chomba, E. N. (2018). *Mielekeo ya wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne kuhusu methali kinzani: uchunguzi katika shule za upili katika Kata ya Township, Kaunti ya Kitui; Kenya*. (Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo cha South Eastern Kenya).

McElhinny, B. (2003). Theorizing gender in sociolinguistics and linguistic anthropology. The handbook of language and gender, 21-42.

Michalos, A. C. (Ed.). (2014). Encyclopedia of quality of life and well-being research (pp. 311-1). Dordrecht: Springer Netherlands.

Mieder, W. (2004). *Proverbs: A handbook*. Greenwood Publishing Group.

Mieder, W. (1989). Proverbs of the Native Americans; A Prize Competition. Western folklore, 48(3), 256-260.

Miller, J. E., & Brown, E. K. (2013). *The Cambridge dictionary of linguistics*. Cambridge University Press.

Miller, J. H. (2009). *For Derrida*. Fordham Univ Press.

Millett, K. (1970). *Sexual Politics*. London: Virago.

Milner, G. B. (1969). Quadripartite structures. Proverbium, 14, 379-383.

Mnenuka, A. (2012). Tofauti ya dhana ya mwanamke katika jamii: mifano kutoka katika taarab (mipasho) na nyimbo za Kibena. In Swahili Forum (Vol. 19, pp. 23-44).

Momanyi, C. (1998). *Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili*. (Unpublished PhD Thesis, Kenyatta University).

Momanyi, C. (2001). Nafasi ya Mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert. *Jarida la Kiswahili, Juzuu 64*.

Momanyi, C. (2002). *Utafiti wa Kiswahili; Swala la Uana katika Utafiti wa Fasihi ya Kiswahili*. Moi University Press.

Momanyi, C. (2007). Patriarchal symbolic order: the syllables of power as accentuated in Waswahili poetry. *The Journal of Pan African Studies, 1*(8), 1-10.

Morris, H. (2007). *A History of Ankole*. Kampala: Fountain Publishers.

Mosha, D. F. (2016). Athari za Mgawanyo Tofauti wa Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto kwa Watoto. *Mulika Journal, 37*(1).

Mtajwa (2005). Historia ya Kiswahili 3, 45–49.

Mtesigwa, G. K. (2013). *Kuchunguza Matumizi ya Methali katika Jamii ya Wanyiramba* (Unpublished Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Mubarok, Y. (2017). Representation of Women in the Sundanese proverbs. *IJASOS- International E-Journal of Advances in Social Sciences*, 205–205. https://doi.org/10.18769/IJASOS.309677

Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (1999). *Research methods: Quantitative and qualitative approaches*. Nairobi. Acts press.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili; Kozi ya za Fasihi vyuoni na vyuo vikuu*. Dar es salaam.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi tatu za kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Muniu, G. G. (2013). Ujagina wa mwanamke katika pango.

Murithi, J. J. ( 2018). Uhusiano wa Itikadi na mtazamo wa mtunzi Murithi Joseph Jessee. *IOSR Journal Of Humanities And Social Science (IOSR-JHSS)* 23(9) 75-83 www.iosrjournals.org

Murithi, J. J., Wafula, R. M., & King'ei, G. K. (2019). *Itikadi katika Riwaya za Dunia Yao (2006) na Mhanga Nafsi Yangu.*

Murithi, J. (2017) Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed. (Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta).

Mutua, J., Chimerah, R., & Ngowa, N. (2017). Mitazamo ya Kusawiri Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili: Posa za Bikisiwa na Mama Ee.

Mwakila, N. U. (2017). *Kuchunguza Taswira ya Mwanamke katika Ngano za Jamii ya Wanyamwezi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Mwamzandi, I. (2016). Dhana ya Zubu katika Nyimbo za Harusi za Waswahili: Uchambuzi wa Kisaikolojia Changanuzi. *Mulika Journal*, *37*(1).

Ndungo, C. (1998). *Images of Women in African Oral Literature: A case of Gikuyu and Swahili Proverbs* (Unpublished PhD Thesis, Kenyatta University).

Ndungo, C. (2002). Social construction of gender with special reference to Gikuyu and Swahili proverbs, 64-74.

Nelson, J. A. (1993). Gender and economic ideologies. Review of Social Economy, 51(3), 287-301.

Nira, Y. (1997). *Gender and Nations*. London: SAGE Publications.

Njogu, K., na Chimerah, R. M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi,Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ogundipe, M. (1987). "The female writer and her commitment" in Eldred D Okpewho Isidore (1992) African Oral Literature Bloomington & Indianapolis: Indiana University Press.

Ogunsina, B. (1996). Gender ideology: portrayal of women in Yor [ugrave] bá ìjálá. *African languages and cultures*, *9*(1), 83-93.

Ogutu, H. O, Wandera, S., & Nabea, W. (2020). Ujitokezaji wa Hejemonia Katika Asasi Za Kijamii: Mfano wa Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi. Edition. *Consortium Journal of Kiswahili*, *2*(1), 76-88.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature Bloomington & Indianapolis*: Indiana University Press.

Opunde, Sheila Wandera, Wendo Nabea (2018). Uchunguzi wa Masuala ya Kijinsia katika Nyimbo za Daudi Kabaka. *Coretrain Journal of Humanities, Social Sciences and Education*, 1. http://www.coretrain.org

Owu-Ewie, C. (2019). Proverbs in marriage: Counselling role and implications. *Legon Journal of the Humanities, 30*(1), 24-53.

Oyaro, C. (2019). Tafsiri za methali na misemo katika mshale wa Mungu. (Tasnifu Ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu Cha Nairobi).

Parveen, K. (2012). The Relationship between Gender Ideology and Division of Labour in Sikh Households: *International Journal of Sociology of the Family, 38*(1), 105-120.

Patnaik, A. K. (1988). Gramsci's concept of common sense: Towards a theory of subaltern consciousness in hegemony processes. Economic and Political Weekly, PE2-PE10.

Plaskow, J., & Ross, T. (2007). The View From Here: Gender Theory and Gendered Realities: An Exchange between Tamar Ross and Judith Plaskow. Nashim: *A Journal of Jewish Women's Studies & Gender Issues*, *13*, 207-251.

Rasul, S. (2015). Gender and power relationships in the language of proverbs: Image of a woman. *FWU Journal of Social Sciences*, *9*(2), 53-62.

Ridgeway, C. L., & Correll, S. J. (2004). Unpacking the gender system: A theoretical perspective on gender beliefs and social relations. *Gender & society*, *18*(4), 510-531.

Sagheer, I., & Zubair, S. (2020). Women in Punjabi Proverbs: Cultural Models, Gender Ideologies and Stereotyping: Cultural Models, Gender Ideologies and Stereotyping. *Journal of Gender and Social Issues*, *19*(1), 85-98.

Salem, B. M. (2013). *Usawiri wa Jinsia Katika Lugha ya Mashairi: Mifano kutoka Mashairi ya Shaaban Robert* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Samwiri, K. (2007). *A History of the Kingdom of Ankole in Western Uganda to1896*. Kampala: Fountain Publishers.

Sanauddin, N. (2015). *Proverbs and patriarchy: analysis of linguistic sexism and gender relations among the Pashtuns of Pakistan* (Doctoral dissertation, University of Glasgow).

Sarma, P. M. (2008). The Oath on the Stone and other Musings: An editorial and a little more. Indian Folklife, (31).

Schalkwyk, J. (2000). Exercises in gender mainstreaming. Gender in development Programme, United Nations Development Programme.

Schipper, M (1991). *Source of all Evil: The Woman in African proverbs*. Nairobi; Phoenix Publishers Ltd.

Seite, A. (1989). Enfumu z'omu Runyankore Rukiga. Mbarara: Omuhanda Gw'okumanya .

Sengo, T. (1985). *The Indian Ocean Complex and the Kiswahili folklore: the case of Zanzibarian tale- performance.*

Sengo, T. S. Y. (1985). *The Indian Ocean Complex and the Kiswahili Folklore: The Case of the Zanzibarian Tale-Performance* (Unpublished PhD Thesis, University of Khartoum)

Sengo, T. S. Y. (1988). The Archives of Kiswahili Language and Folklore. *Nordic Journal of African Studies, 1*(2), 45–57.

Sengo, T. S. Y. (1992). Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini-Unguja. *Nordic Journal of African Studies, 1*(1) 53-79.

Shah, N., Sultan, R. S., & Kaker, B. (2018). Balochi oral literature and gender construction. *Pakistan Journal of Gender Studies, 16*(1), 89-102.

Simala, I (2000) Uhakiki wa Sitiara za Uana katika Ushairi wa Kiswahili. (Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapiswha, Chuo kikuu cha Moi, Eldoret)

Smith, H. (2009). Language shift, gender, and ideologies of modernity in Central Java, Indonesia. *Journal of Linguistic Anthropology, 19*(1), 57-77.

Sotiris, P. (2020). Althusser and Gramsci on Philosophy. In A Philosophy for Communism (pp. 312-335). Brill.

Ssetuba, I. (2002, Aprili). The hold of patriarchy: an appraisal of the Ganda proverb in the light of modern gender relations. In Cairo Gender Symposium organized by CODESRIA/ARC, Cairo 7th-10th.

Steady, F. C. (1981). *The Black woman cross-culturally.* Schenkman Publishing Company, Cambridge.

Stephens, M. A. (2009). Gender differences in parenting styles and effects on the parent-child relationship.

Stock-Morton, P. (1991). Experience, difference, dominance and voice in the writing of Canadian women's history. In Writing Women's History (pp. 79-106). Palgrave Macmillan, London.

Stoeltje, B. J. (2000). Gender ideologies and discursive practices in Asante. PoLAR, 23, 77.

Sultana, A. (2010). Patriarchy and women s subordination: a theoretical analysis. Arts *Faculty Journal*, 1-18.

Swaleh, K. (2012). Islamic proselytising between Lamu and Mozambique: the case of Kizingitini village. *Social Dynamics*, *38*(3), 398-418.

Sydie, R. (1987). A Feminist Perspective on Sociological Theory. Toronto: Methuen.

Theodore, G. (1996). Husbands' Participation in Domestic Labor: Interactive Effects of wives' and Husbands' Gender Ideologies. *Journal of Marriage and Family*, 58(3).

Thompson, K. D. (2011). How to be a good Muslim wife: Women's performance of Islamic authority during Swahili weddings. *Journal of Religion in Africa, 41*(4), 427-448.

Tidd, U. (2004). *Simone de Beauvoir*. Routledge.

Timammy, R., & Swaleh, A. (2013). A Thematic analysis of Utendi wa Mwana kupona: a Swahili/islamic perspective. *International Journal for Innovation Education and Research, 1*(3), 60-72.

Traci, A. (2008) Studies of Gender in the Prehispanic Americas. *Journal of Archeological Research, 16*(1).

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es salaam: Oxford University Press.

Ulashevna, T. S. (2019). The Notion of the Concept "Mother" in Proverbs (on the Proverbs in Uzbek, Russian and German). *International Journal on Integrated Education, 2*(5), 1

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2001). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi. Focus Publications.

Wandera, S. P. (1996). *Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili 1800-1900: Uhalisi au Ugandamizwaji?* (Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Egerton).

Wanyenya, W. (2020). Matumizi ya Lugha za Kiafrika Kuelekeza Wasichana Katika Masuala ya Ndoa: Mfano wa Matumizi ya Semi Katika Jamii ya Wamasaaba Nchini Uganda. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, *2*(2), 23-31.

Warren, C. A. B. (2002). ―Qualitative Interviewing, in J. F. Gubrium and J. A. Holstein (eds.). *Handbook of Interview Research*. Context and Method, Thousand Oaks, CA., Sage.

Wasike, M. W. (2020). Mwanamke wa Kisasa katika Insha za Kifasihi Magazetini: Mtazamo wa Nadharia ya Upalizi. *Mulika Journal, 38*(1).

Webster, S (1982). Women, Sex, and Marriage in Moroccan Proverbs. *International Journal of Middle East Studies, Vol.14*(2).

Woflgang. M. (1989). American Proverbs: *A Study of Text and Context*. New York.

Yitah, H. (2009). " Fighting with proverbs": Kasena Women's (re) definition of female personhood through proverbial jesting. Research in African Literatures, 74-95.

Yulianesta, Y. (2014). Representation of Gender Ideology in Indonesian Novels: The study of the Reformation Era Novel. *English and Literature Journal, 1*(2), 189-204.

Yuval-Davis, N. (1997). Gender and nation: SAGE publications. Gender and Nation, 1-168.

Zheng, X. (2018). The Analysis of Sexism in English Proverbs. *Journal of Language Teaching & Research, 9*(2).

# VIAMBATISHO

## A. Mwongozo wa maswali kwa Wahojiwa

Mpendwa mhojiwa,

Ninakusalimu.

Jina langu ni Lubuuka Yunusu, mwanafunzi wa Uzamifu katika chuo kikuu cha Kenyatta, Nairobi. Ninashughulikia utafiti kuhusu Itikadi za Kiuana katika methali za Kinyankole na Kiswahili, utafiti utakaoniwezesha kufuzu kwa shahada ya Uzamifu katika Kiswahili. Unaombwa kushiriki katika utafiti huu kwa kutoa maoni yako kwa uwazi. Taarifa utakazotoa zitatumiwa kwa madhumuni ya utafiti huu pekee na utambulisho wako hautadhihirika bila idhini yako.

Ninatanguliza shukrani zangu za dhati kwa kukubali kutoa majibu yako kuhusu maswali haya.

1. Ni mambo gani muhimu katika jamii vinayotumiwa kugawa majukumu kwa wanaume na wanawake?
2. Taja sifa muhimu zinazotambulisha hadhi ya mwanamke na mwanamume katika jamii yako.
3. Ni uwezo gani au haki mwanamke anakuwa nazo nyumbani?
4. Mwanamke analazimishwa kutekeleza majukumu yake nyumbani na kuwa katika nafasi yake?
5. Ni mambo gani yanayofanya mwanamke kutekeleza kazi zake?
6. i) Ni mambo gani yafunzwayo watoto wa kike?

ii) Ni mambo gani yafunzwayo watoto wa kiume?

7. Taja mambo ambayo yanasisitizwa wakati mwari anafundishwa? Zingatia jinsia zote mbili.

8. a) Eleza maana za methali mbili kwa mwanamke na mbili kwa mwanamume zinazomzungumzia kuhusu ndoa, tabia na kazi zao katika jamii ya Wanyankole/Waswahili.

b) Kwa nini methali hizi zinazungumzia amali hizi kwa;

i) Wanawake

ii) Wanaume

9. Taja methali ambazo zinatofautiana maana kuhusu malezi ya watoto, ndoa za mitala nafasi ya mwanamke na mwanamume katika jamii yako.

10. Taja methali zozote nne zinazompa mwanamke nafasi ya uongozi katika jamii yako.

10. a) Ni majukumu gani yanayotekelezwa mwanamke/mwanamume katika jamii yako? (kiuchumi, kijamii na kisiasa)

b) Kuna majukumu ya nyumbani ambayo yanatekelezwa na mwanamke/mwanamume kinyume na matarajio ya jamii?

11. Ni misimamo gani inayozingatiwa kwa mwanamume na mwanamke katika jamii yako?

12. Misimamo hii inaleta uhusiano gani kati ya mwanamke na mwanamume?

13. Mwanamke na mwanamume wanatambua na kuzingatia misimamo hii katika shughuli zao za kawaida katika jamii?

14. Misimamo hii inaathiri namna gani mwanamume na mwanamke katika jamii kuhusu;

i. Kuzaa na kulea watoto
ii. Ndoa
iii. Kazi
iv. Mamlaka

15. a) Kulingana na jamii yako ainisha kazi za mwanamke na za mwanamume?

b) Je, kazi hizi zinaweza kufanywa bila kuzingatia mmoja ama ni mwanamke au ni mwanamume?

16. Mwanamume au mwanamke anapoenda kinyume na tabia hizo anakuwaje?

## B. Orodha ya majedwali

Jedwali 1: Methali kuhusu Itikadi za Ndoa ........ 101
Jedwali 2: Methali kuhusu Itikadi ya Utiifu wa Mke katika Ndoa ........ 109
Jedwali 3: Methali kuhusu Ndoa za Mitala. ........ 113
Jedwali 4: Methali kuhusu Itikadi ya Ukewenza ........ 116
Jedwali 5: Methali kuhusu Itikadi za Uzazi ........ 119
Jedwali 6: Methali kuhusu Itikadi ya Malezi ........ 125
Jedwali 7: Methali kuhusu Itikadi ya Mama wa Kambo ........ 128
Jedwali 8: Methali kuhusu Itikadi ya Uongozi ........ 131
Jedwali 9: Methali kuhusu Itikadi ya Kuashiria na Uhuru wa Mwanamume.... 134
Jedwali 10: Methali za Itikadi za Kiuana na Suala la Ujasiriamali ........ 137
Jedwali 11: Methali kuhusu Uwezo wa Kufanya Kazi ........ 142
Jedwali 12: Methali kuhusu Mahusiano ya Uzuri ........ 145
Jedwali 13: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi za Ndoa ........ 149
Jedwali 14: Methali kuhusu Ndoa za Mitala ........ 158
Jedwali 15: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Ushirikiano ........ 160
Jedwali 16: Methali za Kiswahili kuhusu itikadi ya Uzazi ........ 162
Jedwali 17: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Malezi ........ 164
Jedwali 18: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Urembo ........ 167
Jedwali 19: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi na Wakwe ........ 169
Jedwali 20: Methali kuhusu Itikadi ya Udhalilishaji. ........ 172
Jedwali 21: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Heshima ........ 174
Jedwali 22: Methali kuhusu Itikadi na Mahusiano ya Ndoa ........ 177
Jedwali 23: Methali kuhusu Mahusiano ya Ukewenza ........ 184
Jedwali 24: Methali kuhusu utawa wa mwanamke. ........ 186
Jedwali 25: Methali kuhusu Itikadi na Mahusiano ya Uzazi ........ 189
Jedwali 26: Methali kuhusu Itikadi na Mahusiano ya Malezi ........ 193
Jedwali 27: Methali kuhusu Mahusiano ya Uongozi ........ 197
Jedwali 28: Methali kuhusu Mahusiano ya Kazi ........ 202
Jedwali 29 : Methali kuhusu Mahusiano na Wakwe ........ 206
Jedwali 30: Methali kuhusu Mahusiano ya Wajane ........ 209
Jedwali 31: Methali kuhusu Mahusiano ya Udhalilishaji ........ 213
Jedwali 32: Methali za Kiswahili kuhusu Mahusiano ya Ndoa ........ 216
Jedwali 33: Methali za Kiswahili kuhusu Mahusiano ya Ushirikiano wa kindoa ........ 221
Jedwali 34: Methali kuhusu Mahusiano ya Ndoa za Mitala ........ 224
Jedwali 35: Methali za Kiswahili kuhusu Itikadi ya Uzazi ........ 226
Jedwali 36: Methali za Kiswahili kuhusu Mahusiano ya Malezi ........ 228
Jedwali 37: Methali kuhusu Mamlaka ya Mwanamume ........ 232
Jedwali 38: Methali kuhusu Mahusiano na Wakwe ........ 236
Jedwali 39: Methali za Kiswahili na Mahusiano ya Utenganishaji wa Majukumu ........ 238
Jedwali 40: Methali Kinzani kuhusu Ndoa ........ 244
Jedwali 41: Methali Kinzani kuhusu Ndoa za Mitala ........ 246
Jedwali 42: Methali Kinzani kuhusu Mke Kutii Mume ........ 251
Jedwali 43: Methali Kinzani kuhusu Itikadi ya Uzazi ........ 253
Jedwali 44: Methali kinzani kuhusu itikadi ya malezi ya watoto ........ 258
Jedwali 45: Methali Kinzani kuhusu Uongozi na Mamlaka ........ 260

Jedwali 46: Methali Kinzani za Kinyankole kuhusu Kazi................................ 263
Jedwali 47: Methali Kinzani za Kinyankole kuhusu Mahusiano na Wakwe ... 266
Jedwali 48: Methali Kinzani za Kinyankole kuhusu Ujane.............................. 267
Jedwali 49: Methali Kinzani za Kinyankole kuhusu Udhalilishaji wa Wanawake ........................................................................................................ 269
Jedwali 50: Methali Kinzani kuhusu Suala la Ndoa......................................... 272
Jedwali 51: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Ndoa za Mitala.................. 275
Jedwali 52: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Kuzaa................................ 276
Jedwali 53: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Malezi............................... 278
Jedwali 54: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Uongozi na Mamlaka......... 280
Jedwali 55: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Maslahi ya Mume na Mke. 282
Jedwali 56: Methali kuhusu Itikadi Kinzani kuhusu Wakwe............................ 284
Jedwali 57: Methali Kinzani za Kiswahili kuhusu Uwajibikiaji wa Majukumu ........................................................................................................ 286

**C. Orodha ya methali za Kinyankole zilizotumika.**

1. Nyina omwe niwe nyina busha.

   Mama wa mtoto mmoja ni sawa na  mama asiye na mtoto
2. Omwana omwe tamara nyina obugumba.

   Mtoto mmoja haondolei mamake utasa.
3. Omwana omwe n’oruhu rutakuhikire.

   Mtoto mmoja ni ngozi ndogo isiyokuafiki.
4. Abaana nibahwa omumukazi tibahwa mu mushaija

   Watoto huisha tumboni mwa mke siyo kwa mume.
5. Okuzaara kwita abakazi

   Kuzaa huua wanawake.
6. Ou otazaire omutuma orotami.

   Mtoto usiyemzaa unatuma ukiwa umechutama.
7. Omukazi owoyesiga takuzarira mwoja.

   Mke unayeamini hakuzalii mtoto wa kiume.
8. Omuzaire arangwa engozi

   Mzazi hutambuka kwa mbeleko
9. Akaana keiba kajumisa nyinako

   Mtoto mwizi husababisha kutukanwa kwa mama yake
10. Omwana mubi ajumisa nyina

    Mtoto mbaya husababisha kutukanwa kwa mama yake
11. Egabo yabaana eigusya banyinabo.

    Huduma nzuri kwa watoto hushibisha mama zao.
12. Ebihande ni nyoko obunono ni mukasho.

    Unga mbaya ni kwa mamako ihali unga safi ni kwa mamako wa kambo.
13. Enaku yotagambiire nyoko tetuuba.

    Shida usizoambia mama yako hazipunguki.
14. Ku ota nyoko endugu totayo rumuri.

    Ukimkabidhi mama yako dhamana, usiwe na wasiwasi.
15. Ebijumo bya nyoko obinaga nibikwezingirira.

    Matusi ya mama yoko unayepa yakikuandama
16. Owashwera abuuza

    Atakaye kuoa hudadisi

17. Omwishiki ku akura ashwerwa

    Msichana akishakuwa huolewa

18. Enyamwonyo ku ekura eribwa; omwishiki ku akura ashwerwa

    Ndizi ikiwa tayari huliwa; msichana akikua huolewa

19. Nkunda taata na maawe hona tashwerwa nabo.

    Nawapenda baba na mama’ haolewi nao.

20. Emwe y’owibanye ekira igana ry’owa tata

    Ng’ombe mmoja wa mume wangu ni bora kuliko mia wa baba

21. Otamanya ekimutungire eyeiba agikwatisa omukono gumwe.

    Asiyejua kinachommudu, hushika uume wa mumewe kwa mkono mmoja.

22. Omukazi ahangaza obushwere ti rugamba.

    Mke hudumisha ndoa siyo ugomvi

23. Ku oshwera tintegyekwa ozaara tintumwa

    Ukioa mke mbishi utazaa mtoto mkaidi

24. Omukazi wamaryo tahungurwa

    Mke mwenye ubishi harithiwi.

25. Omukazi ne birenje byo’ruhu waba otabizungire tibikworoba.

    Mwanamke ni kama sehemu ngumu za ngozi ya mnyama usipoikamua hailaniki.

26. Omukazi aba empene esibikwa heihi namatojo.

    Mwanamke ni mbuzi afungwa karibu na majani yenye miiba.

27. Omukazi wo’muhuuru tagira matu

    Mke wa kapera hawi na masikio.

28. Akashaija kakye okagaira nseeri.

    Mwanaume mdogo unamdharaulia ngambo.

29. Omukazi hakiri akwangye ebifu kwonka arekye kukugaya.

    Afadhali mkeo asikutosheleze kuliko kukudharau.

30. Abashija tibagaywa.

    Wanaume hawadharauliwi.

31. Omukazi atatina iba ashwererwaki?

    Mke asiyetii mumewe aolewani?

32. Omukazi omira ekiniga amira engundu yeiba.

    Mwanamke amezaye ghadhabu humeza pandikizi la mume wake.

33. Omukazi otaine bwengye asheka iba aine ekiniga.
    Mwanamke mjinga hucheka mumewe akiwa amekasirika.
34. Embu yo'kugaya omushaija omukyenga.
    Heri kumwelewa mumeo kuliko kundharau.
35. Omukazi mubi amaraho iba enyama.
    Mwanamke mwenye tabia mbaya hukondesha mumewe.
36. Omukazi mubi akwijutsya nyoko
    Mke mwenye tabia mbaya, hukukumbusha mama yako.
37. Omukazi kyemirire tamanya gabo yeiba
    Mwanamke mroho hajali mlo wa mume wake
38. Akari ahamahega, karinda nyineeka
    Chakula kitamu mekoni, husubiri mwenye boma.
39. Omukazi ozenga ashombera abaana ekihinzi.
    Mwanamke mzururaji husombea watoto mafua.
40. Omukazi atarikumanya iba ku ariremu arara omumaarwa.
    Mwanamke asiyejua kwamba mumewe yumo hulala katika baa akinywa pombe.
41. Owamaka abiri tarara kwo.
    Mwenye wake wawili halali njaa.
42. Abakazi bashweirwe hamwe nigo mahari.
    Uke wenza haukosi wivu.
43. Eihari ringi rikujumisa ekituuro.
    Wivu mwingi hukufanya kutusi kaburi.
44. Enkoni eteire mukabaro kwogireeba ogirenzya irembo
    Fimbo itumiwayo kupiga mkemwenza uipatapo unaitupa mbali.
45. Omwana aine mukaishe tahwa bunaku.
    Mtoto anayeishi na mama wa kambo haachi kulia.
46. Oteekyerwa muka ishe niwe arya munonga.
    Apikiwaye na mama wa kambo ndiye hula sana.

47. Ku ogaya obukono bukye bwa nyoko ebikono ebihango bya mukasho bikweshumba ohendeka.

    Unapodharau mikono midogo ya mamako, mikubwa ya mama wa kambo itakuepa na utaanguka chini.

48. Mukasho ku akugaburira aha ngata ogimuteera.

    Mama wa kambo akikuwekea chakula kwenye mzingo unaumtupia.

49. Omwana ayonka mukeishe buri aba abuzire nyina.

    Mtoto anyonyeshwaye na mama wa kambo huwa amekosa mamake.

50. Ebihande ni nyoko obunono ni mukasho

    Unga wa chenga chenga ni kwa mama yako unga safi ni mama wa kambo.

51. Mukasho akuha omubazi obu mureire kwo.

    Mama wa kabo hukupatia dawa ikiwa umelala njaa

52. Nyineeka ku ashitamira orurimi entaama zirara omushondi

    Mwenye boma akikalia ulimi, kondoo hulala pachafu.

53. Nyineka ku aba atagiire mukisibo, eze ziitwa engoha

    Mwenye boma asipoenda zizini, ng'ombe wake hushambuliwa na kupe.

54. Nyineeka yaba atarimu zibyamira eshaabo

    Mwenye boma asipokuwepo ng,ombe hulala pachafu.

55. Nyineeka ku ashutamira orurimi entama zirara omushondi.

    Mwenye boma akifyata ulimi, kondoo hulala pachafu.

56. Nyineeka ku ainika amabega eka emarwa amayonjo.

    Mwenye boma akiinamisha mabega familia nzima humalizwa na vibyongo.

57. Nyineeka yaba atarimu ebicere bitemba enju.

    Mkuu wa familia akificha mkono wake kwenye ngozi, familia huugua scabbies

58. Omushaija ahatari omukazi acwa orubanza.

    Pasipo na mwanamume, mwanamke huamua kesi.

59. Omukazi tatiiza ngundu ya iba

    Mwanamke haazimi fahali wa mumewe.

60. Omushaija tahinduka aharurimi, ahinduka ahakitanda

    Mwanamume hageuki kwa ulimi, hugeuka kitandani.

61. Nyineeka ateera enanga yarikwenda

    Mwenye boma hucheza kinanda atakacho.

62. Omushaija omuhango ayeha omwanya muhango

    Mwanamume mnene hujipatia kiti kikubwa

63. Omushaija ku ashoberwa aretsa, omukazi ku ashoberwa arira

    Mwanamume akizidiwa na changamoto huvuta sigara, mwanamke yeye hulia.

64. Omukazi ku ayikarira tayimuka.

    Mwanamke atupapo mweleka hainuki.

65. Omukazi ku aita takurura

    Mwanamke anapoua habururi mzoga.

66. Omukazi tayeihira nyama ahabugamba.

    Mwanamke hajitolei nyama kwenye uchaga.

67. Emburabure yamukazi ati kuri nabeire omushaija

    Mwanamke mzembe, laiti ningekuwa mwanamume

68. Ebibahingire baine enda nibyo barya bazaire.

    Chakula wanacholima wakiwa wajawazito ndicho huliwa wajifunguapo.

69. Omukazi taba mugyenyi

    Mwanamke hawi mgeni

70. Omukazi omuhingi atega eiguru entabire.

    Mwanamke mkulima hugema shamba mbingu

71. Omukazi omugara ayesiima yaazaara.

    Mwanamke mvivu hufurahi anapozaa watoto.

72. Omukazi oine iba taba mworo.

    Mwanamke aliye na mume hawi maskini.

73. Kankore nsiimwe akasa ahekire iba amaguru gayata esaano.

    ‘Nifanye kazi nisifiwe’alisaga mtama akibeba mume wake mgongoni miguu ya mume ikamwaga unga.

74. Emirimo nokukwatanisa, omukazi ku aba nayara, iba aba nahanika enkindi

    Kazi ni kusaidiana, mke akiwa anatandika kitanda, mumewe anaweka nguo fupi za ndani juu.

75. Omukazi ohinga hamwe neiba taba mugara

    Mwanamke afanyaye kazi (kulima) na mumewe hawi mvivu.

76. Omukazi mubi n'otajwaire

    Mwanamke asovutia ni yule asiyejikwatuwa

77. Ekiriho nikimara, amaisho marungi ni garoga enjara.

    Kipatikanacho hutosha: macho mazuri huroga njaa.

78. Omukazi aba amate ayerinda ebitakoozi.

    Mwanamke ni maziwa, anajihadhari na uchafu.

79. Omukazi omurofa bamureebera ahabyokuzwara.

    Mwanamke mchafu hutambulishwa kwa mavazi yake.

80. Otakareebaga kabi ka nyinazaara ati "ninza owa maawe"

    Asiyejua ubaya wa mama mkwe eti "naenda kwa mama"

81. Tocwa gwa muhara wawe mukwe wawe atakaizire.

    Usiamue kesi ya binti yako kabla mkwe wako kufika

82. Omufakazi taijuka kitara.

    Mjane hakumbuki ghala.

83. Omukazi iba ku afa arya enkoko.

    Mke anakula kuku mume wake anapofariki.

84. Omufakazi tagaya nfuni.

    Mjane hadharau uume mdogo/ mfupi.

85. Eyi abakazi bashagire abandi babahindura abazaana.

    Ambapo wanawake ni wangi, wengine hugeuzwa kuwa watumwa.

86. Abakazi ne'ndeere tizihwa murutookye.

    Wanawake ni majani ya migomba hayamaliziki shambani.

87. Ayatwarwa omukazi ku afa empitsi imunuga.

    Aolewaye na mwanamke, afaapo hata na fisi hawamli.

88. Oshwerwa ayoroba

    Aolewaye huwa mtiifu

89. Omukazi mpuguuki ashereka ekibi.
    Mwanamke mwerevu huficha maovu
90. Omukazi mubi ahita “boojo ni mwaare”
    Bora mwanamke asiyevutia kuliko “Wavulana tandikeni tulale”
91. Omukazi akateera enduru ati ka ngiteere nkaagira ebyokuruga omuri egi ka”.
    Mwanamke alipiga nduru eti “ebu niipige huenda nikagundua siri za nymba hii”.
92. Ekibanju okitega nyoko kizarwa mukasho.
    Unayotarajia kutoka kwa mama yako unayapata kutoka kwa mama wa kambo.


## D. Orodha ya methali za Kiswahili zilizotumika

1. Kuku akiacha wana ana mayai tumboni.
2. Nyumba ya mgumba haina matanga.
3. Mcha mke ndugu hazai
4. Kupendana kuzaana
5. Jogoo halei mwana.
6. Kuku mwenye watoto halengwi jiwe.
7. Kuku havunji yai lake
8. Mwana hufuata kisogo cha nina.
9. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
10. Akosaye la mama hata la mbwa yuamwa.
11. Mkono mmoja haulei mwana.
12. Baba n'kanye mwanawe.
13. Kuzaa ni shani (kupenda kwake) ya Mungu , malezi ni wajibu wetu.
14. Mtoto ni wa mama, kwa baba huenda nasaba
15. Pepo i chini ya nyayo za mama.
16. Kulea mimba si kazi kazi kulea mwana
17. Kinyesi cha mtoto hakinuki kwa mama.
18. Kila kitu kina mama dawa yake na salama
19. Mwenye kupata watoto hakosi mbeleko.
20. Pendo za mama zi matakoni mwa nina.
21. Asiye na mke yu uchi.
22. Mwanamke kipofu huangaza nyumba.
23. Mke bila mume ni kama shamba lisilolimwa.
24. Aliwatani wa mwanamke ni kwa mumewe.
25. Talaka ni kuvuliwa nguo
26. Uganga haumweki mume.
27. Ndoa ni kutia mkono kizani.
28. Arusi ni jambo la heri
29. Mke hulia kabla ya kuolewa na mume hulia baada ya kuoa.

30. Atabaki mtoto wa kiume mwanao mpaka umwozeshe, wa kike atabaki mwanao mpaka kufa kwake.
31. Ndoa ni nguo inayochanika.
32. Nikufungie usutu nikusitirie, kila mvuli ayaye nasema siye ya kutu nikutindiye.
    Mke ni dada mdogo.
33. Mke akikwambia 'niwache' nawe ridhia na mwingine kimbilia.
34. Ndoa ni ukumbi wa ngoma
35. Pambo la nyuma ni mwanamke asiyenung'unika.
36. Kosa moja haliachishi mke
37. Kuoa ni harusi kuishi wawili ni ngoma
38. Mke hulia kabla ya kuolewa na mume hulia baada ya kuoa
39. Kuoa ni kuona mengi
40. Kuoa bibi mzuri ni kupanda mdimu kando ya njia
41. Ndoa ya furaha ni muungano.
42. Aliye na wake wawili kabeba mzegamzega.
43. Mke wa kwanza ni kama mama.
44. Akataye kula humwongezea mke mwenziwe.
45. Mama wa kambo si mama
46. Baba wa kambo si baba kunichukuza mikoba na ufunguo wa shaba.
47. Mama ni mamake kwa kambo ni mahali pa kukaa.
48. Cheko la mke kwa mume ni kheri ya nyumbani
49. Jicho la mume ni mkewe.
50. Ametoa nguo jogoi (Jogoo), mkewe hakuzipata.
51. Mke wa kwanza ni kama mama
52. Anayenyimwa ugali na mkewe huvunja nyumba.
53. Amefanya mumewe ng'ombe ya shemere
54. Udhaifu wa mume humpa mke kiburi.
55. Mwanamke hukunjwa na mwanamume huvunjwa.
56. Kichwa cha nyumba ni mume na shingo yake ni mkewe.
57. Kuku jike hawiki penye jogoo.
58. Pasipo na mwanamume nguzo ya nyumba, nyumba itavunjika.
59. Kinywa cha bibi kisipite cha bwana

60. Aloanza ni Aziza, Kamali kaoleza na Kupona kamaliza.
61. Mwanaharamu  ni wa kwamza wa pili ni kukusudia.
62. Mama msaji baba msonobari.
63. Kutembea ni baba kukaa ni mama.
64. Kuishi wawili ni kuvumiliana
65. Ndoa ya furaha ni muungano.
66. Mke ni nguo ya mume na mume ni nguo ya mke.
67. Ndoa huandikwa mbinguni.
68. Nyege ni kunyegezana, mapenzi ya upande mmoja hayanogi.
69. Mzaa mume hakufa wala mzaa mke.
70. Mke ni nguo mgomba kupalilia
71. Adhabu ya juu ya mwanamke ni kumfungia katika kasri lisilokuwa na kioo.
72. Chui naye ana mkwe.
73. Asemaye mengi hajui amemtukana mkwe.
74. Kijicho cha mkwe hakiachishi mume.
75. Mtu msi mke sahibuye shemeji.
76. Kupendwa na mke ni kuchukiwa na wazazi.
77. Mwanamke ni bidhaa mbovu.
78. Mume si babe kwa mkewe.
79. Mwanamke hupewa nyama ya ulimi na mwanamume hupewa nyama ya paja.
80. Buibui ni mke.
81. Eda ya mke hakuna eda ya mume.
82. Mume kazi mke kazi

## E. Cheti cha ruhusu kufanya utafiti



THIS IS TO CERTIFY THAT:
MR. LUBUUKA YUNUSU
of KENYATTA UNIVERSITY, 43844-100
NAIROBI,has been permitted to conduct
research in Kilifi , Lamu , Mombasa
Counties

on the topic: ITIKADI ZA KIUANA KAMA
ZINAVYOBAINIKA KATIKA METHALI ZA
KINYANKOLE NA KISWAHILI

for the period ending:
24th May,2019

Permit No : NACOSTI/P/18/20781/22996
Date Of Issue : 25th May,2018
Fee Recieved :Ksh 2000

Applicant's
Signature

Director General
National Commission for Scie[nce,]
Technology & Innovation

## F. Barua ya ruhusa wa kufanya utafiti

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone:+254-20-2213471,
2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website : www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref. No. **NACOSTI/P/18/20781/22996**

Date: **25th May, 2018**

Lubuuka Yunusu
Kenyatta University
P.O. Box 43844-00100
**NAIROBI**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Itikadi za kiuana kama zinavyobainika katika methali za kinyankole na kiswahili,"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kilifi, Lamu and Mombasa Counties** for the period ending **24th May, 2019.**

You are advised to report to **the County Commissioners and the County Directors of Education, Kilifi, Lamu and Mombasa Counties** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

GKalerwa

**GODFREY P. KALERWA MSc., MBA, MKIM**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Kilifi County.

The County Director of Education
Kilifi County.

National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO9001: 2008 Certified